

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Ishirini na Mbili - Terehe 6 Juni, 2015

(Kikao Kilanza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MHE. ESTHER N. MATIKO (k.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA NISHATI NA MADINI):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2015/2016
Wizara ya Nishati na Madini**

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji ya Mwaka 2014/2015 na

Nakala ya Mlando (Online Document)

kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini na Taasisi zake kwa Mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kutekeleza majukumu ya Kitaifa. Kwa namna ya pekee namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini na tarehe 24 Januari 2015 kunituea kuwa Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi huo umenipa fursa ya kujifunza na kutoa mchango wangu katika kusimamia uendelezaji wa Sekta ya Nishati na Madini ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya Wananchi na Taifa kwa ujumla. Aidha, nawapongeza kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuliongoza vyema Taifa letu. Pia nawapongeza Makamu wa Rais - Mheshimiwa Dkt. Mohammed Gharib Bilal na Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, ambao kwa pamoja wameniongoza vyema katika kusimamia majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika kipindi cha kuliongoza Bunge hili ambalo linakua kwa kasi, lina vijana wengi, lakini bado Mheshimiwa Spika na Wenyeviti mmeonesha umahiri na ukomavu mkubwa katika kusimamia shughuli za Bunge; nawapongeza sana. Vilevile, nawapongeza Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuongoza Kamati zao kwa hekima, busara na ujasiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini - Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Makamu Mwenyekiti - Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi na Wajumbe wote wa Kamati hiyo, kwa ushirikiano na ushauri waliotupa katika Wizara katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru familia yangu akiwepo mke wangu Mariana na ndugu zangu Wanafamilia ya Kibakwe, kwa ushirikiano na umoja na moyo waliokuwa wanani pa katika kipindi hiki ambacho nilikuwa na majukumu ya kuliongoza Jimbo lakini pia Wizara ya Nishati na Madini. Niwaambie tu watu wa Kibakwe, pamoja sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kutoa pole kwa familia ya wenzetu ambao Mwenyezi Mungu imempendeza kuwachukua akiwemo Kapteni Mstaafu John Damiano Komba, aliyekuwa Mbunge wa Mbinga Magharibi na Marehemu Salmin Awadh Salmin, aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni Zanzibar na Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, aliyekuwa Mbunge wa Ukonga. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi; Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya ya awali, sasa nawasilisha Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2014/2015 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ninayosoma ni muhtasari tu wa hotuba niliyoasilisha Mezani leo asubuhi. Hivyo, naomba hotuba yangu yote pamoja na vielelezo vyake vyote iwekwe kwenye Hansard ya Bunge kama ilivyo.

Nakala ya Mlando (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 20 Mei 2015, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi bilioni 375.76, sawa na asilimia 35 ya Bajeti ya Shilingi triliuni 1.07 iliyo tengwa kwa Mwaka 2014/2015. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, Shilingi bilioni 302.54 zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na Shilingi bilioni 73.22 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali, hadi kufikia tarehe 20 Mei 2015, jumla ya Shilingi bilioni 167.92 zilikuwa zilikusanya kutoka Sekta za Nishati na Madini, sawa na asilimia 62.3 ya lengo la Shilingi bilioni 269.39 katika Mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini iliyofanywa na Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (PPRA) mwezi Aprili 2015, imeonyesha kwamba usimamizi wa shughuli za ununuzi na uzingatioji wa sheria na taratibu katika Wizara ya Nishati na Madini umeimarika. Kufuatia tathmini hiyo, Wizara imepata asilimia 93.61 kwa mwaka 2013/2014, ikilinganishwa na asilimia 83 kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mradi wa Kinyerezi I, megawatt 150 Jijini Dar es Salaam, umefikia asilimia 90. Aidha, ufungaji wa mitambo ya kufua umeme kwa kutumia gesi asilia umekamilika na ujenzi wa kituo cha kupozea umeme cha kilovolt 220/132 unaendelea.

Kazi nyingine zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovolt 220 kutoka Kinyerezi hadi Kimara yenye umbali wa kilomita saba na ujenzi wa njia ya kilomita tatu ya msongo wa kilovolt 132 hadi Gongo la Mboto. Gharama za Mradi ni Dola za Kimarekani milioni 183 na hadi sasa Serikali imetoa Dola za Kimarekani milioni 168. Mradi huu unatarajiwaa kukamilika Mwezi Agosti 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kukua kwa mahitaji ya umeme, katika mwaka 2015/2016 Serikali imeamua kuongeza mitambo mingine ya kuzalisha umeme wa megawatt 185 katika Mradi wa Kinyerezi I (*Kinyerezi I Expansion*). Kazi zitakazofanyika ni kukamilisha usanifu wa Mradi wa Megawatt 185 na kuajiri Mshauri wa Mradi. Fedha za ndani Shilingi bilioni 40 zimetengwa katika Mwaka 2015/2016 kwa ajili ya kuanza kutekeleza kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Rusumo megawatt 80 unahusu ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu za maji. Mradi unatekelezwa kwa ushirikiano wa nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi, ambapo kila nchi itapata megawatt 26.6. Katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, Serikali ilisaini makubaliano ya mkopo na Benki ya Dunia kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme. Serikali pia ilisaini makubaliano ya mkopo na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovolt 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi. Vilevile tathmini ya eneo ambalo mkuza utapita kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha umeme kutoka Rusumo hadi Nyakanazi imeanza. Gharama za Mradi huo zinakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 164.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutekeleza Miradi mbalimbali kutoka vyanzo vya gesi asilia, makaa ya mawe na nishati jadidifu, ikiwemo nguvu ya maji, hydro, tungamo taka, joro ardhi, umeme wa jua na umeme wa upopo ili kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini. Miradi hiyo itatekelezwa kwa kuzingatia Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Iringa – Shinyanga kV 400 (*backbone*), unahusisha upanuzi wa vituo vikuu vya kupozea umeme wa gridi ya kV 400/220 katika Miji ya Iringa, Dodoma, Singida na Shinyanga.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 Serikali imekamilisha malipo ya fidia kwa Wananchi walioathiriwa na Mradi. Wakandarasi wa Mradi ni Kampuni ya KEC International Limited ya India na Kampuni ya Jyoti Structures Limited ya India na Kampuni za M/S GSE & C na Hyosung za kutoka Korea Kusini, ambapo utekelezaji kwa sasa umefikia wastani wa asilimia 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/16, kazi zitakazoendelea ni pamoja na upanuzi wa vituo vya kupozea umeme; usimikaji wa nguzo; na utandazaji wa nyaya za kupertisha umeme. Mradi huo unaghanrimiwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Maendeleo la Japani, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) na Shirika la Maendeleo la Korea. Gharama za Mradi ni Dola za Marekani milioni 224, sawa na Shilingi bilioni 387.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Makambako – Songea ni moja ya Mradi muhimu wa kuunganisha Gridi ya Taifa na Mikoa ya Kusini. Kampuni ya Isolux ya Hispania imekamilisha usanifu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme na kuunganisha wateja. Pia, Shirika la Maendeleo na Ushirikiano wa Kimataifa la Sweden (SIDA), limetoa kibali (No Objection), kwa ajili ya ujenzi wa njia ya usafirishaji umeme wa KV 220. Aidha, Serikali imekamilisha ulipaji wa fidia kwa Wananchi watakaopisha ujenzi wa njia kuu ya usafirishaji wa umeme, ambapo shilingi bilioni 4.07 zimelipwa kwa Wananchi 1,042 katи ya 1,063 katika Mkoa wa Njombe. Serikali pia imelipa fidia ya Shilingi bilioni 2.59 kwa wananchi 767 katи ya 770 wa Mkoa wa Ruvuma. Mradi huu utaghanrimiwa kwa msaada wa Serikali ya Sweden wa Krona za Sweden milioni 500. Serikali pia itachangia Dola za Marekani milioni 20, sawa na Shilingi bilioni 34.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi mwingine unaofadhiliwa na Serikali ni North – East Grid ambaa unahusisha ujenzi wa njia ya usafirishaji wa umeme yenye urefu wa kilomita 664 na Msongo wa Kv 400 kutoka Dar-es-Salaam kuptitia Tanga hadi Arusha. Pia vituo vikubwa vya kupoozea umeme vitajengwa Bagamoyo, Chalinze, Segera na Tanga. Kazi za kutathmini athari za kijamii na kimazingira na upimaji wa awali wa ardhi katika sehemu za Dar-es-Salaam, Kinyerezi hadi Chalinze zimekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zitakazofanyika katika Mwaka 2015/2016 ni ulipaji wa fidia kwa watakaopisha Mradi katika Awamu ya Kwanza ya Dar-es-Salaam - Kinyerezi hadi Chalinze na kupata mshauri wa kusimamia ujenzi na utekelezaji wa Mradi. Mradi huo unaghanrimiwa kwa mkopo wa Dola za Marekani milioni 693 kutoka Benki ya EXIM ya China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia inatekeleza Mradi wa Kuboresha Upatikanaji Umeme katika Wilaya ya Ngara, Bihamulo na Mpanda (ORIO), kwa ushirikiano na Serikali ya Tanzania na Serikali ya Ufalme wa Uhlanzi. Serikali ya Ufalme wa Uhlanzi imeidhinisha msaada wa Shilingi bilioni 22 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huo ambaa lengo lake ni kuongeza uzalishaji na usambazaji wa umeme katika wilaya husika. Aidha, Serikali imetoa Shilingi bilioni 10.5 katи ya Shilingi bilioni kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa Mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza Ibara ya 63(c) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 – 2015, inayoelekeza kuongeza idadi ya Wananchi walionganishiwa umeme mijini na vijiji. Katika kutekeleza azma hiyo, Awamu ya Pili ya Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijiji chini ya Wakala wa Nishati Vijiji umeendelea kutekelezwa, ambapo umeme umepelekwa katika Makao Makuu ya Wilaya za Busega, Chemba, Itilima, Kalambo, Kyerwa, Mkalama, Mlele na Nanyumbu. Katika Mwaka 2014/2015, jumla ya wateja 5,210 wameunganishiwa umeme kwenye Wilaya hizo.

Mheshimiwa Spika, Mradi pia umewezesha upelekaji umeme katika maeneo mbalimbali nchini ambapo hadi kufikia mwezi Aprili 2015, wateja wapya walionganishiwa umeme kupitia

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mradi huo wamefikia 8,078 katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Geita, Iringa, Kagera, Katavi, Kilimanjaro, Lindi, Mtwara, Mara, Njombe, Simiyu, Singida na Tanga. Idadi hii inafanya jumla ya wateja wote waliounganishiwa umeme chini ya Mradi wa REA na TANESCO kuanzia Julai 2014 hadi Aprili 2015 kufikia 241,401. Idadi hiyo ni sawa na ongezeko la asilimia 68 ikilinganishwa na wateja 143,113 waliounganishwa mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi vilevile umewezesha utekelezaji wa jumla ya Miradi 52 ya Kusambaza Umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Hadi kufikia mwezi Machi 2015, wateja 2,270 waliunganishiwa umeme. Kati ya hao wateja 1,038 ni wa Mkoa wa Lindi na wateja 1,232 ni wa Mkoa wa Mtwara. Miradi hiyo imegharimu Serikali jumla ya Shilingi bilioni 6.1. Serikali imeongeza wigo wa utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini kwa Mikoa hiyo, ambapo Shilingi bilioni 48 zitahitajika. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Serikali kupitia REA itaendelea kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Kupeleka Umeme Vijijini. Napenda kutumia nafasi hii kuwahimiza Waheshimiwa Wabunge na Viongozi walioko kwenye maeneo yao, kuwahamasisha Wananchi kuunganishiwa umeme kwenye nyumba zao pamoja na kutumia umeme huo katika shughuli za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Juni 2014, Serikali iliidhinisha Mkakati na Mwelekeo wa Kuboresha Sekta Ndogo ya Umeme ya Mwaka 2014 – 2025. Mkakati huo utatekelezwa kwa vipindi vyaa muda mfupi, kati na mrefu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi. Utekelezaji wa mkakati unaoendelea, ambapo ukusanyaji wa mapato ya TANESCO umeongezeka kutoka Shilingi bilioni 893.3 mwaka 2013 hadi kufikia Shilingi trilioni 1.14, sawa na ongezeko la asilimia 22. Shirika pia limegatua madaraka ya ununuzi wa baadhi ya vifaa kutoka Makao Makuu kwenda Ofisi za Kanda ili kuboresha utoaji huduma kwa haraka.

Katika mwaka 2015/2016 kazi zitakazofanyika ni pamoja na kuendelea kuboresha hali ya kifedha na kiutendaji wa TANESCO; kuongeza uwekezaji katika Sekta Ndogo ya Umeme kwa kushirikisha sekta binafsi; kuongeza uunganishaji wateja wapya katika maeneo ya mijini na vijijini; na kujenga uwezo wa kiutendaji kwa watumishi katika Sekta Ndogo ya Umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta Ndogo ya Nishati Jadidifu; Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini iliendelea kuhamasisha uendelezaji wa Sekta ya Upopo kwa ajili ya kuzalisha umeme katika maeneo mbalimbali. Kampuni zilizonesha nia ya kuwekeza ni pamoja na Wind East Africa Ltd - Singida, Geowind Power Company - Singida na Sino-Tan Renewable Energy Ltd - Makambako. Kampuni hizo zinatarajiwa kuwekeza katika Miradi yenye uwezo wa kuzalisha umeme kati ya MW 50 na MW 200. Majadiliano kati ya TANESCO na Kampuni husika yanatarajiwa kukamilika katika mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na SIDA, Taasisi ya Serikali ya Ujerumani (GIZ) na Taasisi ya Maendeleo ya Korea Kusini (KEMCO), iliandaa Mpango wa Matumizi Bora ya Nishati. Mpango huo unahuvi Viwango vya Matumizi Bora ya Nishati na Ukaguzi wa Matumizi ya Nishati. TANESCO pia itaendelea na juhudzi za kupunguza upotevu wa umeme ambao umepungua kutoka asilimia 24 mwaka 2012 hadi asilimia 19 mwaka 2014 pamoja na kusimamia matumizi bora ya umeme. Katika Mwaka 2015/2016 Serikali itaendelea kusimamia matumizi bora ya nishati ikiwemo kupunguza upotevu wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka 2014/2015, shughuli za utafutaji mafuta na gesi asilia ziliendelea katika maeneo mbalimbali nchini. Kutokana na shughuli hizo, kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa nchini kimeongezeka kutoka futi za ujazo trilioni (TCF) 46.5 mwezi Juni 2014 hadi TCF 55.08 mwezi Aprili 2015. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 18 kwa mwaka mmoja tu. Gesi hiyo iligunduliwa katika kina kirefu cha bahari kwenye visima vya Gilgilani – 1, Mdalsini – 1

na Piri – 1, vilivyochorongwa na Kampuni za Statoil na Exxon Mobil; na visima vyatyaachui – 1 na Kamba – 1, vilivyochorongwa na Kampuni za BG na Ophir.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Dodsal imegundua gesi asilia katika Kisima cha Mambakofi – 1 kwenye Kitalu cha Ruvu, ambapo tathmini ya kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa katika eneo hilo inaendelea, maeneo ya Chalinze. Katika Mwaka 2015/2016 Serikali itaendelea kusimamia na kuhamasisha shughuli za utafutaji mafuta na gesi asilia nchini. Aidha, baada ya TPDC kupewa jukumu la kuendeleza vitalu Na. 4 – 1B na 4 – 1C itaendelea kutathmini takwimu za mitetemo ili kubainisha rasilimali zilizopo katika vitalu hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za utafutaji mafuta katika maeneo ya mipakani, hususan katika Ziwa Tanganyika zinaendelea. Ili kuhakikisha shughuli za utafutaji katika maeneo ya mipakani zinazofanyika kwa amani, Serikali imeendelea na majadiliano na nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Malawi, Msumbiji na Zambia kwa lengo la kuweka mipaka katika Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. Serikali kuititia TPDC imeanza majadiliano na Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Msumbiji, kwa lengo la kufanya kwa pamoja tafiti za jiojia katika maeneo ya mipakani. Katika Mwaka 2015/2016, Serikali itaendelea kuratibu majadiliano na nchi jirani kuhusu shughuli za utafutaji mafuta na gesi asilia mipakani ili kuepusha migogoro baada ya kugundulika kwa rasilimali hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Bomba la Gesi Asilia kutoka Mtwara kuititia Lindi hadi Dar es Salaam umekamilika. Aidha, ujenzi wa mitambo ya kusafisha gesi asilia katika eneo la Madimba, Mtwara umefikia asilimia 99 na mitambo ya Songo Songo, Lindi umefikia asilimia 97. Vilevile, ujenzi wa nyumba 16 zenye uwezo wa kuhudumia wafanyakazi 86 katika maeneo ya Madimba na Songo Songo umekamilika. Mitambo na bomba hilo vinatarajiwa kuanza kufanya kazi ifikapo mwezi Septemba 2015. Haya ni matokeo ya utekelezaji wa mionganoni mwa Miradi iliyoinishwa kwenye Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016). Matumizi ya gesi asilia yatachochea ukuaji wa viwanda, utunzaji wa mazingira kwa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa, kuongeza ajira na hatimaye kuleta maendeleo ya uchumi na kijamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hesabu za mwaka 2013 kukamilika, TIPER ilitoa gawio la Shilingi bilioni 1.27 kwa Serikali kutokana na umiliki wa hisa asilimia 50. Serikali inamiliki hisa asilimia 50 katika Kampuni ya Puma Energy Tanzania Ltd na imepata gawio la Shilingi bilioni 3.28 za mwaka 2013. Katika mwaka 2015/2016, Serikali inatarajia kupata gawio kutoka kampuni hizo baada ya kukamilisha hesabu za mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, EWURA iliendelea kusimamia bei za mafuta katika soko la ndani ili kuhakikisha bei hizo zinaendana na mabadiliko katika Soko la Dunia na kuwianisha thamani ya Shilingi ya Tanzania na Dola ya Marekani. Pia, bei ya mafuta ghafi katika Soko la Dunia ilishuka kutoka Dola za Marekani 109 kwa pipa mwezi Julai 2014 hadi Dola za Marekani 64 kwa pipa mwezi Desemba 2014, sawa na punguzo la asilimia 41. Punguzo hili la bei ya mafuta katika Soko la Dunia liliwezesha EWURA kupunguza bei ya umeme kwa wastani wa asilimia 2.5. Serikali kuititia EWURA iliendelea kuhakikisha kuwa, Wananchi wananaufaika na punguzo hilo la bei hiyo katika Soko la Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha udhibiti wa vilainishi vyatya mitambo (*lubricants*), EWURA imeanza kutoa leseni za biashara ya vilainishi na imetunga kanuni kuhusu usimamizi wa bidhaa hiyo. EWURA itaendelea kuhakikisha ujenzi wa miundombinu na biashara ya bidhaa ya mafuta ya petroli nchini vinazingatia usalama na utunzaji wa mazingira. Serikali inafanya tathmini ya miundombinu ya kupoolea mafuta katika Bandari ya Tanga ili sehemu ya shehena

ya mafuta kupitia mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja yaweze kushushwa kwenye bandari hiyo kuanzia mwezi Julai mwaka huu 2015. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huo unalenga kuondoa utegemezi wa Bandari ya Dar es Salaam, kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za petroli nchini, kupunguza gharama za usafirishaji na msongamano wa meli katika Bandari ya Dar es Salaam na gharama na msongamano wa magari yanayosafirisha mafuta kutoka Dar es Salaam. Katika mwaka 2015/2016, Serikali itaendelea kuboresha shughuli za udhibiti wa bidhaa za petroli na Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja nchini ikiwemo kubadilisha muundo wa kampuni inayoratibu mfumo huo. Kuanza kutumika kwa bandari hiyo kutahamasisha shughuli za uchumi katika Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Serikali imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2013 na kuandaa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015. Pamoja na mambo mengine, Sera hiyo imeweka mkazo kuhusu kuongezeka kwa uzalishaji umeme kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo nishati jadidifu, kuimarisha usimamizi wa shughuli za mafuta na gesi asilia na kuongeza ushiriki wa Watanzania kwenye rasilimali hizo. Serikali pia imeandaa Rasimu ya Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015 na Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania (*The Tanzania Extractive Industries Transparency and Accountability Act, 2015*). Lengo la kutunga na kuboresha Sera na Sheria hizo ni kuimarisha usimamizi katika Sekta ya Nishati. Katika Mwaka 2015/2016, mikakati ya utekelezaji wa Sera husika itakamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliendelea kufuatilia ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na shughuli za madini nchini ili kuhakikisha kuwa mapato stahiki yanalipwa Serikalini. Katika Mwaka 2014/2015 Wizara ililenga kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 209.96 kutoka Sekta ya Madini. Hadi kufikia tarehe 20 Mei 2015, jumla ya Shilingi bilioni 137.55 ziliikuwa zilikusanya, sawa na asilimia 65.5 ya lengo la makusanyo. Katika Mwaka 2015/2016 Serikali inategemea kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 211.96 kutoka katika Sekta ya Madini. Ili kufikia lengo hilo, ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Sekta ya Madini utaimarishwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa mapato stahiki kutokana na shughuli za madini yanalipwa na wachimbaji na wafanyabiashara wa madini nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Nishati na Madini imekamilisha majadiliano na Kampuni yenyeye mikataba ya madini kuhusu ulipaji wa asilimia 0.3 ya mapato ya turnover, yaani service levy, ikiwa ni ushuru wa huduma kwa Halmashauri husika badala ya Dola za Marekani 200,000 kwa mwaka. Hivyo, Migodi ya Geita, Bulyanhulu, Buzwagi na North Mara imelipa jumla ya Shilingi bilioni 4.1 kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2014. Kati ya fedha hizo, Mgodi wa Geita umelipa kiasi cha Shilingi bilioni 1.65 kwa Halmashauri ya Mji wa Geita; Mgodi wa Bulyanhulu Shilingi milioni 749.5 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala; Mgodi wa North Mara Shilingi milioni 863.3 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime; na Mgodi wa Buzwagi Shilingi milioni 843.2 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama. Malipo hayo yataendelea kufanya kila baada ya miezi sita. Katika Mwaka 2015/2016, Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha zitakazokuwa zinalipwa na migodi kwa Halmashauri husika ili zitekeleze Miradi ya Maendeleo kulingana na vipaumbele vya maeneo husika vya Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitenga maeneo mapya sita kwa ajili ya uchimbaji mdogo chini ya utaratibu wa ushirikiano kati ya Serikali na Kampuni kubwa za utafutaji na uchimbaji madini ambazo zilikubali kuachia maeneo hayo. Maeneo hayo yana jumla ya hekta 22,970 na yapo Buzwagi (Kahama), Ibologelo (Igunga), Kinamiyuba (Shinyanga) na Mumba, Selewi na Ukene (Nzega). Katika maeneo hayo, takribani leseni 2,297 zilipatikana ambazo

Nakala ya Mtandao (Online Document)

zilitolewa kwa wachimbaji wadogo. Hadi sasa jumla ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo ni 31, aidha mitambo miwili ya kuchoronga miamba imenunuliwa kwa ajili ya kuwezesha utambuzi wa mashapo katika maeneo ya wachimbaji wadogo. Shughuli hizi ni katika kutekeleza lbara ya 56(d) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 – 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka 2015/2016, Wizara itatenga maeneo yasiyopungua matano kwa ajili ya uchimbaji mdogo baada ya kufanyiwa utafiti wa jiolojia ili kubaini mashapo yanayoweza kuchimbwa kwa faida na wachimbaji wadogo. Wizara itaendeleza huduma za ugani na utoaji wa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa wachimbaji wadogo na Viongozi wa Wilaya wapatao 1,000 na kusambaza nakala 4,000 za mwongozo elekezi kwa wachimbaji wadogo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Kampuni za AngloGold Ashanti na Acacia, zitaanzisha migodi ya mfano na mafunzo kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu katika Wilaya za Geita na Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya tathmini ya utekelezaji wa mpango wa utoaji wa mikopo kwa wachimbaji wadogo. Tathmini hiyo imeonesha kuwa wachimbaji wadogo walio wengi wameshindwa kukidhi masharti ya kupata mikopo hiyo. Kutokana na hali hiyo, Serikali kuitia Wizara ya Nishati na Madini imeendeleza utaratibu mpya wa utoaji ruzuku kwa wachimbaji wadogo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya uchimbaji. Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo kwa kutoa ruzuku, ambapo Serikali imetenga Shilingi bilioni tatu na Benki ya Dunia imekubali kutoa Dola za Marekani milioni tatu kuitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuboresha mfumo wa utoaji leseni kwa kuanzisha huduma za kupokea maombi ya leseni kwa njia ya mtandao utakaozinduliwa rasmi tarehe 8 Juni 2015. Mfumo huo unawezesha wateja kutuma maombi na kufanya malipo kwa njia ya mtandao. Kufikia mwezi Mei 2015, jumla ya leseni 1,514 kati ya leseni 4,200 zimesajiliwa kwenye mfumo huo. Hata hivyo, pamoja na malengo mazuri ya uanzishwaji wa mfumo huo, kumekuwepo na mwitikio mdogo wa wateja kujisajili, ambapo hadi sasa wamiliki wa leseni 140 kati ya 400 wamesajiliwa. Natoa wito kwa wamiliki wote wa leseni za madini kujisajili kwa njia ya mtandao ili kurahisisha utoaji wa huduma. Pamoja na kuboresha mfumo huo wa utoaji leseni, Wizara imekamilisha ujenzi wa jengo la Kituo Maalum cha Kuhifadhi Takwimu Mjini Morogoro. Kwa mwaka 2015/2016 Wizara itakamilisha ufungaji wa mitambo katika Kituo hicho.

Katika Mwaka 2014/2015, Wizara imekamilisha ukarabati wa Kituo cha Jimolojia (Gemological Centre – TGC) cha Arusha ambacho kilizinduliwa rasmi mwezi Aprili, 2015. Kupitia Mfuko wa Kuwaendeleza na Kuwajengea Uwezo Wanawake wa Tanzania ulioanzishwa Jijini Arusha, kituo kimetoa mafunzo ya ukataji na usanifu wa madini ya vito kwa vitendo kwa wanawake 15. Mfuko huo ulianzishwa Mwaka 2012 kwa ushirikiano kati ya Wizara na Tanzania Mineral Dealers Association (TAMIDA) na unasimamiwa na Kamati ya Maonesho ya Kimataifa ya Vito ya Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliratibu Maonesho ya Vito na Usonara yaliyofanyika Mwezi Novemba 2014 Jijini Arusha, ambapo washiriki 465 kutoka nchi 29 walihuduria. Katika Maonesho hayo, madini yenye thamani ya Shilingi bilioni 3.4 yaliuzwa na kuiwezesha Serikali kukusanya mrabaha wa Shilingi milioni 113.8. Maonesho mengine yaliyofanyika mwezi Aprili 2015, ambapo washiriki 960 walihuduria kutoka nchi 30. Katika maonesho hayo, madini yenye thamani ya Shilingi bilioni 7.2 yaliuzwa na kuiwezesha Serikali kukusanya mrabaha wa Shilingi milioni 279.8. Washiriki katika maonesho hayo walitoka Afrika ya Kati na maeneo mengine. Natoa wito kwa wadau wa madini ya vito waendelee kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini ili kufanikisha maonyesho hayo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 56(d) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 – 2015, ambayo pamoja na mambo mengine ilisisitiza uimarishaji wa miundombinu ikiwemo ofisi na vitendea kazi, Wizara ilianzisha Ofisi mpya za Madini za Bariadi, Moshi, Nachingwea na Njombe na kununua majengo na kukarabati baadhi ya majengo na kujenga majengo mapya katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka 2014/2015, TANSORT ilithaminisha na kusimamia uuwaji wa karati 183,165.12 za almasi zenyet thamani ya Dola za Marekani milioni 56.7. Mauzo hayo yaliingizia Serikali mrabaha wa Dola za Marekani milioni 2.8. Mapato hayo ni ongezeko la asilimia 68 ikilinganishwa na kipindi cha mwaka 2013/2014. TANSORT pia ilithaminisha tani 2,938.68 za madini ya mapambo; gramu milioni 1.65 za vito; na karati 319,000 za madini ya vito yanayochorongwa na kusanifiwa yenyet thamani ya Dola za Marekani milioni 36.52. Katika mwaka 2015/2016, Serikali itaendelea kuiimarisha TANSORT ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti; katika mwaka 2014/2015, Serikali imeandaa Rasimu ya Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia ya Mwaka 2015. Sheria hiyo pamoja na mambo mengine, itaweka utaratibu wa upatikanaji kwa wakati wa taarifa za malipo, mapato, mauzo na gharama za uwekezaji kutokana na shughuli za madini, mafuta na gesi asilia. Aidha, Sheria hiyo inaipa Kamati ya Utekelezaji ya TEITI uwezo wa kisheria wa kufanya uchunguzi endapo kutakuwa na tofauti katika taarifa za usuluhishi wa malipo na mapato yanayotokana na rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Serikali itaendelea kuiwezesha TEITI, kuelimisha kampuni na taasisi husika za Serikali, kuzijengea uwezo asasi za kiraia na vyombo vya habari kuhusu uwekezaji katika shughuli za madini, mafuta na gesi na ukokotoaji wa mapato ya Serikali na kukamilisha Taarifa za Ulinganishi wa Malipo na Mapato ya Mwaka 2012/2013 na 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tuzo ya Rais ya Huduma ya Jamii na Uwezeshwaji kwa Miradi ya Tasnia ya Uziduaji ilitolewa na Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 28 Februari 2012. Lengo la Tuzo hiyo ni kutambua mchango wa kampuni za madini, mafuta na gesi asilia kwa Wananchi na kwa Pato la Taifa. Natoa wito kwa makampuni yote yanayojihusisha katika shughuli za madini, mafuta na gesi, kuungeza ushiriki wao katika Miradi ya Kijamii, ili shughuli hizo zilete manufaa stahiki kwa kampuni na jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 Wakala wa Jiolojia Tanzania ulikusanya Taarifa zinazowezesha kuchorwa kwa ramani nne za Jiolojia kwa mfano wa Quarter Degree Sheet kwenye maeneo yaliyoko katika Wilaya za Kilwa, Liwale, Nachingwea na Ruangwa na ramani mbili za Kikemia katika Wilaya za Liwale na Ruangwa. Katika mwaka 2015/2016 Wakala utaendelea kukusanya Taarifa za Jiosayansi na kuchoronga ramani kwa ajili ya kuvutia wawekezaji katika sekta hiyo katika maeneo mbalimbali, yakiwemo maeneo ya Songea na Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mpango wa bajeti wa mwaka 2014/2015, Serikali kupitia Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA), iliendelea kufuatilia ulipaji wa kodi ya mapato wa migodi mikubwa. Ukaguzi uliofanywa na TMAA kwa kushirikiana na TRA umeiwezesha Kampuni ya Geita Gold Mining kulipa kodi ya mapato ya shilingi bilioni 68.5 katika kipindi cha Julai 2014/2015. Aidha, Wakala ulifanya ukaguzi kwenye migodi mikubwa na ya katika kuhusu ulipaji wa mrabaha, ushuru wa huduma, ada ya mwaka ya leseni na kodi za zuvio na kufanikiwa kuiwezesha Serikali kukusanya jumla ya shilingi bilioni 4.94.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala uliendelea kukagua madini yaliyozaalishwa na kuuzwa kutoka katika migodi yote mikubwa nchini. Mrabaha wa Dola za Marekani milioni 57.3 ulilipwa Serikalini kutoka kwenye migodi hiyo katika kipindi cha kuanzia Julai 2014 hadi Aprili 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Madini la Taifa STAMICO na Kampuni ya Tanzanite One Mining Limited imeendelea kusimamia shughuli za uchimbaji wa madini katika Mgodi wa Tanzanite uliopo Mererani Wilayani Simanjiro. Ushiriki wa STAMICO katika kusimamia shughuli za kila siku za mgodi huo umeimarika, ambapo hadi mwezi Machi 2015, Shirika limelipwa ada ya usimamizi Dola za Marekani 331,660. Idadi ya Watanzania walioajiriwa katika mgodi huo pia imeongezeka kutoka 608 hadi 1,186.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na usimamizi huo pia ushirikiano kati ya Mgodi huo na Chama cha Wachimbaji Wadogo wa Mkao wa Manyara – MAREMA umeimarika; hivyo, kusaidia katika utatuzi wa migogoro iliyokuwa ikijitokeza. Pamoja na kusimamia hisa za Serikali katika miradi ya kimkakati iliyoelezwa hapo juu, STAMICO iliendelea kutoa huduma za utafiti wa madini na uchorongaji miamba kwa wadau. Hadi kufikia mwezi Mei, Shirika limefanikiwa kupata zabuni nne za uchorongaji na zabuni tatu za utafiti kwa ujumla za thamani ya Dola za Marekani milioni 1.01.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la STAMICO kuitia Kampuni yake ya STAMIGOLD limeanza uchimbaji wa dhahabu kwenye Mgodi wa STAMIGOLD ulioko Biharamulo. Wakia 13,099 zimepatikana, zimewenza kuzalishwa hadi Mei 2015 na kuuza nje wakia 11,613 zenye thamani ya Shilingi milioni 14.082. Katika Mwaka 2015/2016 Serikali itaendelea kuiwezesha STAMICO ili kuweza kusimamia ipasavyo masilahi ya Taifa katika Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015 Wizara iliandaa Establishment Order kwa ajili ya kukibadili Chuo cha Madini Dodoma kuwa Polytechnic na kuiwasilisha kwenye mamlaka husika. Vilevile, kufuatia hatua ya Kampuni ya Resolute kuikabidhi Serikali eneo lilitokuwa chini ya Mgodi wa Golden Pride mwezi Disemba 2014, Chuo kimefanikiwa kuanzisha mafunzo katika eneo hilo. Serikali itaendelea kukiwezesha Chuo hiki ili kuweza kutoa mafunzo yake ya nadharia na vitendo kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka 2014/2015, jumla ya watumishi 412 walioajiriwa katika Wizara ya Nishati na Madini. Mpango Mkakati wa Mwaka 2011 Wizara ya Nishati na Madini, watumishi wameendelea kujengewa uwezo kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Nishati na Madini inaendelea kushirikiana na wadau katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali. Kwa niaba ya Serikali, napenda kutoa shukrani kwa Serikali ya Algeria, Brazil, Canada, Finland, Jamhuri ya Watu wa China, Jamhuri ya Korea, Marekani, Norway, Sweden, Uhlanzi, Ujeruman, Urusi na Uturuki. Pia, natumia fursa hii kutoa shukrani kwa Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Exim ya China, Benki ya BADEA, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya na Umoja wa Ulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru Naibu Mawaziri wa Wizara ya Nishati na Madini; Mheshimo Charles Muhangwa Kitwanga, Mbunge wa Misungwi, anayesimamia masuala ya Madini; na Mheshimiwa Charles Mwijage, Mbunge wa Jimbo la Muleba Kaskazini, anayesimamia masuala ya Nishati kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa, siyo tu kama Waziri wao, lakini kama mdogo wao. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Mhandisi Ngosi Mwihava, kwa ushirikiano anaonipa katika kuwezesha shughuli za Wizara. Aidha, nawashukuru Kamishna wa Nishati wa Masuala ya Petroli na Makamishna wote na Wafanyakazi wote wa Taasisi zote zikiwemo EWURA, PICL, PUMA, REA, STAMICO, TANESCO, TIPER, TPDC na Wenyeviti wote wa Bodii za Ushauri za GST, MRI, TMAA pamoja na Mwenyekiti wa Bodii ya Ushauri wa Madini, kwa ushirikiano wanaonipa katika kuongoza Wizara. Nawashukuru pia Wakuu wa Taasisi hizo chini ya Wizara na Watumishi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa nakushukuru sana wewe mwenyewe Mheshimiwa Mwenyekiti Zungu, kwa ushirikiano unaonipa moja kwa moja katika kufanya majukumu yangu ya Uwaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe Bajeti ya jumla ya Shilingi 536,960,436,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini na Taasisi zake kama ifuatavyo: Shilingi 365,346,938,000 ni Bajeti ya Maendeleo, ambapo Shilingi milioni 280 ni fedha za ndani na Shilingi 85,346,938,000 ni fedha za nje. Shilingi 171,613,498,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida; kati ya fedha hizo, Shilingi 137,813,703,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi 33,799,795,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (Makofij)

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI NA MADINI MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2015/16 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji ya Mwaka 2014/15 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini na Taasisi zake kwa Mwaka 2015/16.
2. Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kutekeleza majukumu ya kitaifa. Kwa namna ya kipekee namshukuru sana Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na tarehe 24 Januari, 2015 kunithea kuwa Waziri wa Nishati na Madini.
3. Mheshimiwa Spika, uteuzi huo umenipa fursa ya kujifunza na kutoa mchango wangu katika kusimamia uendelezaji wa Sekta za Nishati na Madini ambazo ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Aidha, nawapongeza kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa na Mhe. Rais katika kipindi hicho, akiwemo Mhe. Charles John Mwjjage, Mbunge wa Jimbo la Muleba Kaskazini, anayenisaidia katika kusimamia masuala ya nishati.

Nakala ya Mlango (Online Document)

4. Mheshimiwa Spika, misingi ya Mipango, Sera na Sheria katika Sekta za Nishati na Madini imenipa miongozo ya kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi na hatimaye leo nawasilisha Hotuba yangu kwa mara ya kwanza katika Bunge hili.
5. Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Mwaka 2015/16 ni ya kipekee kwa Taifa letu kwa sababu mbalimbali. Kwanza ni Hotuba ambayo inahitimisha Awamu ya Nne ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Pili, kipindi hiki kinahitimisha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mpango Mkakati wa Wizara ya Nishati na Madini, mipango ambayo ilianza kutekelezwa Mwaka 2011/12. Mpango hii pamoja na ubunifu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yake imekuwa chachu ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Nne.
6. Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kumpongeza Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza vema Taifa letu. Pia, nawapongeza Makamu wa Rais, Mhe. Dkt. Mohammed Gharib Bilal na Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb.), ambao kwa pamoja wameniongoza vema katika kusimamia majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini.
7. Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika kipindi cha kuliongoza Bunge hili, umeonesha umahiri na ukomavu mkubwa katika kusimamia shughuli za Bunge, nakupongeza sana. Vilevile, nawapongeza Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuliongoza Bunge hili kwa hekima, busara na ujasiri.
8. Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mhe. Richard Mganga Ndassa (Mb.), Makamu Mwenyekiti Mhe. Jerome Dismas Bwanausi (Mb.) na wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushirikiano wanaonipa na ushauri wao katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini. Pia, nawapongeza Mhe. Dkt. Grace Khwaya Puja (Mb.) na Mhe. Innocent Rwabushajja Sebba (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
9. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki pia tumewapoteza wenzetu waliokuwa katika Bunge hili ambao ni Marehemu Kapteni Mstaafu John Damiano Komba aliyekuwa Mbunge wa Mbinga Magharibi na Marehemu Salmin Awadh Salmin, aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni- Zanzibar. Tunaomba Mwenyezi Mungu aendelee kutufariji, hususan ndugu na marafiki wa marehemu.
10. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ya awali, sasa nawasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2014/15 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2015/16.

B.TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA YA NISHATI NA MADINI KWA MWAKA 2014/15 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2015/16

11. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/15 Wizara iliendelea kusimamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika Sekta ya Nishati kwa kuzingatia vipaumbele vilivyowekwa ambavyo ni pamoja na: utekelezaji wa miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme; upelekaji umeme vijiji; ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia; utafutaji wa mafuta na gesi asilia na kuandaa rasimu za sera na sheria katika Sekta ya Nishati; uendelezaji wa nishati jadidifu; na matumizi bora ya nishati.
12. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Madini vipaumbele vilikuwa ni: kuongeza fungamanisho la Sekta ya Madini na sekta nydingine; utafutaji na uchimbaji madini; kuboresha mfumo

wa utoaji leseni za madini; kuendeleza uchimbaji mdogo wa madini na kuboresha sera na sheria katika Sekta ya Madini.

13. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia utekelezaji wa vipaumbele viliwyotajwa, hadi kufikia tarehe 20 Mei, 2015 Wizara ilipokeajumla ya Shilingi bilioni 375.76, sawa na asilimia 35 ya Bajeti ya Shilingi trilioni 1.07 iliyotengwa kwa Mwaka 2014/15. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, Shilingi bilioni 302.54 zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na Shilingi bilioni 73.22 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

14. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali, hadi kufikia tarehe 20 Mei, 2015 jumla ya Shilingi bilioni 167.92 zilikuwa zimekusanya kutoka Sekta za Nishati na Madini. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 62.3 ya lengo la mapato ya Shilingi bilioni 269.39 yaliyokadiriwa kukusanya katika Mwaka 2014/15. Kutofikiwa kwa malengo hayo kumechangiwa zaidi na kushuka kwa bei ya dhahabu na vito katika soko la dunia. Katika Mwaka 2015/16, lengo la makusanyo ya mapato ni Shilingi bilioni 291.98. Ili kufikia lengo hilo, Wizara imeweka mipango mbalimbali ikwemo: kuboresha mfumo wa utoaji na usimamizi wa leseni za madini; kuongeza udhibiti katika kukusanya mapato yatokanayo na madini ya ujenzi na ya viwandani; shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia; na kuongeza uzalishaji na matumizi ya gesi asilia.

15. Mheshimiwa Spika, tathmini iliyofanywa na Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (PPRA) Mwezi Aprili, 2015 imeonesha kwamba usimamizi wa shughuli za ununuzi na uzingatiji wa sheria na taratibu katika Wizara ya Nishati na Madini umeimarika. Kufuatia tathmini hiyo, Wizara imepata asilimia 93.61 Mwaka 2013/14 ikilunganishwa na asilimia 83 kwa Mwaka 2012/13.

SEKTA YA NISHATI

Mafanikio katika Sekta ya Nishati

16. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka 2014/15 mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Nishati ni pamoja na: kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya nane (8) za Busega, Chemba, Itlima, Kalambo, Kyerwa, Mkalama, Mlele na Nanyumbu; kuongeza idadi ya wateja waliounganishiwa umeme kutoka 143,113 Mwaka 2013 hadi kufikia 241,401, sawa na ongezeko la asilimia 68; kukamilika kwamiradi minne (4) ya uzalishaji na usambazaji umeme ya Mwenga, Mawengi, Awamu ya Kwanza ya Sustainable Solar Market Packages (SSMP - I) na Kisanga (TAZAMA fuel pump) iliyoratibiwa chini ya Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (Big Results Now Initiative - BRN); na kukamilika kwa ufungaji wa mitambo (turbines) minne (4) yenye uwezo wa MW 150 kwa Mradi wa Kinyerezi - I, ambao upo katika hatua za mwisho kukamilishwa.

17. Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni: kuongezeka kwa kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa kutoka futi za ujazo trilioni 46.5 Mwaka 2013/14 hadi futi za ujazo trilioni 55.08; kukamilika kwa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Mtware na Lindi hadi Dar es Salaam; kuanzishwa kwa Kampuni tanzu za TPDC ambazo ni GASCO na COPEC; kukamilika kwa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015; kukamilika kwa Rasimu ya Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015; na Rasimu ya Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasimimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania.

SEKTA NDONGO YA UMEME

(i) Hali ya Uzalishaji wa Umeme

18. Mheshimiwa Spika, umeme uliozalishwa nchini uliongezeka kutoka Gigawatt hour (GWh) 5,997.41 Mwaka 2013 hadi kufikia GWh 6,285.03 Mwaka 2014, sawa na ongezeko la asilimia 48. Umeme uliozalishwa kwenye mitambo iliyounganishwa kwenye Gridi ya Taifa ni GWh 6,033.98 na GWh 251.05 zilitalishwa nje ya Gridi. Kati ya umeme huo, GWh 4,073.26 zilitalishwa na mitambo inayomilikiwa na TANESCO, ambazo ni sawa na asilimia 64.8 ya umeme wote uliozalishwa. Umeme ulionunuliwa kutoka nchi jirani za Kenya, Uganda na Zambia ulikuwa GWh 59.29.

(ii) Miradi ya Uzalishaji wa Umeme

19. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mradi wa Kinyerezi I, MW 150 Jijini Dar es Salaam umefikia asilimia 90. Aidha, ufungaji wa mitambo ya kufua umeme kwa kutumia gesi asilia umekamilika na ujenzi wa kituo cha kupozea umeme cha KV 220/132 unaendelea. Kazi nyingine zinazoendelea ni pamoja na: ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa KV 220 kutoka Kinyerezi hadi Kimara yenye umbali wa kilomita saba (7); na ujenzi wa njia ya kilomita tatu (3) ya msongo wa KV 132 hadi Gongo la Mboto. Gharama za mradi ni Dola za Marekani milioni 183 na hadi sasa Serikali imetoa Dola za Marekani milioni 168, sawa na Shilingi bilioni 290.64. Mradi huu unatarajwa kukamilika Mwezi Agosti, 2015.

20. Mheshimiwa Spika, kutokana na kukua kwa kasi ya mahitaji ya umeme, katika Mwaka 2015/16, Serikali imeamua kuongeza mitambo mingine ya kuzalisha umeme kwa kiasi cha MW 185 katika Mradi wa Kinyerezi - I (Kinyerezi I -Expansion). Mitambo hiyo itasaidia kupunguza utegemezi wa mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu za maji ambayo huathiriwa na ukame, pamoja na mafuta ambayo ni ghali. Kazi zitakazofanyika ni kukamilisha usanifu wa mradi wa MW 185 na kuajiri mshauri wa mradi. Fedha za ndani Shilingi bilioni 40 zimetengwa katika Mwaka 2015/16 kwa ajili ya kuanza kutekeleza kazi hizo.

21. Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa Kinyerezi II - MW 240, Serikali katika Mwaka 2015/16 itaanza utekelezaji wa shughuli za awali za mradi huo ikiwemo ujenzi wa misingi, ambapo mitambo hiyo itafungwa. Gharama za mradi ni Dola za Marekani milioni 344, sawa na Shilingi bilioni 564.16. Asilimia 85 ya għarama za Mradi zitatolewa na Benki za Sumitomo Mitsui Banking Corporation (SMBC) na Japan Bank for International Cooperation (JBIC) za Japani ikiwa ni mkopo. Aidha, asilimia 15 zilzbaki zitagharamiwa na Serikali ambapo Shilingi bilioni 6 zimetengwa kwa Mwaka 2015/16.

22. Mheshimiwa Spika, Mradi wa Rusumo - MW 80 unahusu ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu za maji. Mradi unatekelezwa kwa ushirikiano wa nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi ambapo kila nchi itakuwa na fursa ya kupata MW 26.6. Katika Mwaka 2014/15, Serikali ilisaini makubaliano ya mkopo na Benki ya Dunia kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme. Serikali pia ilisaini makubaliano ya mkopo na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa KV 220.

23. Mheshimiwa Spika, vilevile, tathmini ya eneo ambalo mkuza utapita kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha umeme kutoka Rusumo hadi Nyakanazi imeanza. Aidha, chombo madlum (Special Purpose Vehicle) cha kusimamia utekelezaji wa mradi huo kimeundwa. Gharama za mradi huo zinakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 164.

24. Mheshimiwa Spika, Mradi wa Mtwara - MW 600 ni wa ujenzi wa mtambo wa kufua umeme kwa kutumia gesi asilia pamoja na ujenzi wa njia ya usafirishaji umeme wa msongo wa KV 400 kutoka Mtwara hadi Songea. Mradi huo utatekelezwa kwa njia ya ubia kati ya TANESCO na Kampuni ya Symbion Power Ltd. Kwa sasa Rasimu ya Taarifa ya Upembusi Yakinifu ya mradi inaboreshwu kwa kuzingatia maoni ya TANESCO. Katika Mwaka 2015/16 hatua za awali za utekelezaji wa mradi zitaanza.

25. Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na TANESCO wamepitia upya bei ya ununuzi wa umeme ambayo itawezesha Mradi wa kufua umeme kwa kutumia Makaa ya Mawe Kiwira kuendeshwa kwa faida. Aidha, STAMICO imekamilisha Tathmini ya Athari ya Mazingira na Kijamii (Environmental and Social Impact Assessment - ESIA) ya mradi wa MW 200 ambayo itawasilishwa Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC) kwa ajili ya kupata kibali kabla ya kuanza kutekeleza mradi.

26. Mheshimiwa Spika, STAMICO pia iko kwenye hatua za mwisho za kumpata mbia kwa ajili ya kuendeleza mradi wa Kiwira kwa ajili ya kuzalisha MW 200 za umeme. Gharama za mradi huo zinakadirwa kuwa Dola za Marekani milioni 500. Katika Mwaka 2015/16 kazi zitakazofanyika ni pamoja na kumpata mshauri kwa ajili ya kufanya tathmini ya fidia kwa watakaopisha mradi wa usafirishaji umeme wa njia ya msongo wa KV 400 kutoka Kiwira hadi Mwakibete (Uyole), ambapo Shilingi bilioni 2 zimetengwa kwa ajili hiyo.

(iii) Miradi ya Usafirishaji Umeme

27. Mheshimiwa Spika, Mradi wa Iringa - Shinyanga KV 400 (backbone): mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa KV 400 kutoka Iringa hadi Shinyanga na upanuzi wa vituo vikuu vya kupozea umeme wa gridi KV 400/220 katika mijji ya Iringa, Dodoma, Singida na Shinyanga.

28. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/15 Serikali imekamilisha malipo ya fidia kwa wananchi walioathiriwa na mradi. Wakandarasi wa mradi wapo katika sehemu (lot) nne (4) kama ifuatavyo: Sehemu ya Kwanza kutoka Iringa hadi Dodoma inajengwa na Kampuni ya KEC International Limited ya India; Sehemu ya Pili ni kutoka Dodoma hadi Singida inajengwa na Kampuni ya Jyoti Structures Limited ya India; Sehemu ya Tatu inajengwa na KEC International Limited ya India; na Sehemu ya Nne inahusisha ujenzi wa vituo vinne vya kupozea umeme katika maeneo ya Iringa, Dodoma, Singida na Shinyanga vinavyojengwa na Kampuni za M/S GSE & C na Hyosung za kutoka Korea Kusini. Wakandarasi wako katika maeneo husika ya mradi na utekelezaji umefikia asilimia 45.

29. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16, kazi zitakazoendelea ni pamoja na: upanuzi wa vituo vya kupozea umeme; usimikaji wa nguzo; na utandazaji wa nyaya za kupitisha umeme. Mradi huo unagharamiwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Maendeleo la Japan (JICA), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) na Shirika la Maendeleo la Korea (EDCF). Gharama za mradi ni Dola za Marekani milioni 224, sawa na Shilingi bilioni 387.5.

30. Mheshimiwa Spika, Mradi wa Makambako - Songea KV 220 ni moja ya mradi muhimu wa kuunganisha Gridi ya Taifa na mikoa ya kusini. Kampuni ya Isolux ya Hispania imekamilisha usanifu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme na kuunganisha wateja. Pia, Shirika la Maendeleo na Ushirkiano wa Kimataifa la Sweden (Sida) limetoa kibali (No Objection) kwa ajili ya ujenzi wa njia ya usafirishaji umeme wa KV 220.

31. Mheshimiwa Spika, Serikali pia imekamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi, ambapo Shilingi bilioni 4.07 zimelipwa kwa wananchi 1,042 kati ya 1,063 katika Mkao wa Njombe. Pia, Serikali imelipa fidia ya Shilingi bilioni 2.59 kwa wananchi 767 kati ya 770 wa Mkao wa Ruvuma. Wananchi wachache (24) wa mikoa hiyo hawajalipwa kutokana na kutokukamilisha vielelezo vyao.

32. Mheshimiwa Spika, mradi huu unagharamiwa kwa msaada wa Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Sida kwa kiasi cha Krona za Sweden milioni 500, sawa na Shilingi bilioni 112. Serikali pia itachangia Dola za Marekani milioni 20, sawa na takriban Shilingi bilioni 34. Hata hivyo, mradi huo haukuanza kutekeleza kama

ilivyopangwa kutokana na kuchelewa kukamilika kwa majadiliano ya makubaliano ya mkopo kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Sweden ya AB-SEK. Hivyo, utekelezaji wa mradi utaanza Mwaka 2015/16.

33. Mheshimiwa Spika, Mradi wa North - West Grid KV 400 unahu ujenzi wa njia ya umeme kutoka Mbeya - Sumbawanga - Mpanda - Kigoma - Nyakanazi yenyen urefu wa kilomita 1,148. Mradi huu utatekelezwa katika awamu tatu kama ifuatavyo: awamu ya kwanza (Mbeya - Sumbawanga) itahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa KV 400 yenyen urefu wa kilomita 340 kutoka Mbeya hadi Sumbawanga, na vituo vikubwa vijipa vya kupozea umeme vya Uyole - Mbeya na Sumbawanga.

34. Mheshimiwa Spika, kazi ya upimaji wa njia ya umeme imekamilika na Mshauri amepatikana kwa ajili ya usanifu (upgrading) wa njia ya msongo wa KV 220 ili kuwiana na mahitaji ya sasa ya kujenga njia ya msongo wa KV 400 kwa awamu ya kwanza ya mradi. Gharama za mradi wa North - West Grid ni Dola za Marekani milioni 664, ambapo awamu ya kwanza itagharimu Dola za Marekani milioni 136.25.

35. Mheshimiwa Spika, ili kuunganisha Mradi wa North - West Grid na mikoa ya Kanda ya Ziwa Viktoria, Serikali pia inatekeleza mradi wa Geita - Nyakanazi. Mradi huo unahu: ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa KV 220 yenyen urefu wa kilomita 133; ujenzi wa kituo cha kupozea umeme cha Nyakanazi chenye uwezo wa MVA 20, KV 220/33; upanuzi wa kituo cha kupozea umeme cha Geita pamoja na usambazaji wa umeme kwenye viji vinavyopitisha na mradi huo. Gharama za mradi wa Geita - Nyakanazi ni Shilingi bilioni 81.48.

36. Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kufanyika katika Mwaka 2015/16 ni: kukamilisha upembusi yakinifu; kufanya tathmini ya mazingira; kulipa fidia kwa watakaopisha mradi; kupata mkandarasi wa ujenzi wa mradi; na kuanza ujenzi. Mradi unagharamiwa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) na Umoja wa Ulaya (EU), ambapo fedha za nje Shilingi bilioni 4.6 zimetengwa kutekeleza kazi hizo.

37. Mheshimiwa Spika, katika jijihada za kuongeza njia za usafirishaji umeme ambazo zinaunganishwa na Mradi wa North - West Grid, Serikali pia inatekeleza Mradi wa Bulyanhulu - Geita KV 220. Kazi zitakazofanyika Mwaka 2015/16 ni: kukamilisha Tathmini ya Athari za Kijamii na Kimazingira; na kufanya upembusi yakinifu. Mradi unagharamiwa na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA) kwa mkopo wenye thamani ya Shilingi bilioni 41.

38. Mheshimiwa Spika, mradi mwininge unaosimamiwa na Serikali ni North - East Grid, ambao unahu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme yenyen urefu wa kilomita 664 na msongo wa KV 400. Njia hiyo itajengwa kutoka Kinyerezi (Dar es Salaam) kuititia Chalinze (Pwani) na Segera (Tanga) hadi Arusha. Mradi pia utahusisha ujenzi wa vituo vikubwa vya kupozea umeme vitakavyojengwa Bagamoyo, Chalinze, Segera na Tanga. Kazi za upimaji wa athari za Kijamii na Kimazingira na Dar es Salaam (Kinyerezi) hadi Chalinze zimekamilika.

39. Mheshimiwa Spika, kazi ya ulipaji fidia kwa watakaopisha mradi katika awamu ya kwanza ya Dar es Salaam (Kinyerezi) hadi Chalinze na kazi ya tathmini ya fidia kwa wananchi watakaopisha mradi kwa sehemu iliyobaki zitaanza Mwaka 2015/16. Kazi nyingine itakayofanyika ni kumpata mshauri mwelekezi kwa ajili ya kusimamia ujenzi na utekelezaji wa mradi. Mradi huo unagharamiwa kwa mkopo wa Dola za Marekani milioni 693 kutoka Benki ya EXIM ya China.

40. Mheshimiwa Spika, ili kuwa na umeme wa uhakika nchini na kuwezesha biashara ya umeme nje ya nchi, Serikali inashiriki katika programu na mradi mbalimbali ya kikanda. Mionganini mwa mradi

inayotekelawa ni ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa KV 400 kutoka Zambia kupitia Tanzania hadi Kenya (ZTK Interconnector). Kwa upande wa Tanzania, Serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa KV 400 yenye urefu wa kilomita 414 kutoka Singida kupitia Arusha hadi Namanga.

41. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/15 majadiliano ya mkopo kati ya Serikali, Benki ya Maendeleo ya Afrika na Serikali ya Japani kupitia Shirika lake la maendeleo la JICA ya kamilika. Aidha, TANESCO na Kampuni ya Kusafirisha Umeme ya Kenya (KETRACO) wamekamilisha uandaaji wa zabuni kwa ajili ya kumpata mshauri wa mradi. Gharama ya sehemu hii ya mradi ni Dola za Marekani milioni 258.82.

42. Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kufanyika Mwaka 2015/16 ni: kukamilisha tathmini ya mali na kulipa fidia kwa wananchi watakapoisha mradi; kuajiri mshauri wa mradi nawakandarasi wa ujenzi wa vituo na njia ya umeme; na kuanza maandalizi ya usambazaji umeme kwa vijiji vilivypo kando kando ya njia ya umeme. Mradi unagharamiwa kwa mkopo kutoka AfDB na JICA. Katika Bajeti ya Mwaka 2015/16, jumla ya Shillingi bilioni 1.5 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

43. Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ya mradi wa ZTK inayotekelawa kwa upande wa Tanzania ni ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa KV 400 yenye urefu wa kilomita 292 kutoka Iringa hadi Mbeya. Kazi ya upembuzi yakinifu imekamilika na gharama za mradi ni Dola za Marekani milioni 182.54.

(iv) Miradi ya Usambazaji Umeme

44. Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kusimamia uboreshaji wa miundombinu ya umeme katika Jiji la Dar es Salaam. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na: kupatikana kwa vibali vyakupitisha njia za umeme kutoka TANROADS, Dar es Salaam Institute of Technology (DIT), Mahakama ya Kisutu na Manispaa ya Ilala. Vifaa vyakupitisha njia za usambazaji umeme chini ya ardhi na switch gears tayari vimewasilii Dar es Salaam na ufungaji wa vifaa hivyo unaendelea. Jumla ya Shillingi bilioni 1.2 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo na zitatolewa na Serikali ya Finland.

45. Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine iliyofanyika ni kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha Ilala na kuanza ujenzi wa kituo cha Sokoine chini ya Mradi wa Electricity V. Mradi huo pia unatekeleza katika Wilaya za Kwimba, Magu, Misungwi, Sengerema, Mbogwe na Bukombe, ambapo kazi ya kuwaunganishia umeme wateja inaendelea. Katika Mwaka 2015/16, kazi ya ukarabati wa vituo vyakupitisha njia za usambazaji umeme chini ya ardhi na switch gears tayari vimewasilii Dar es Salaam na ufungaji wa vifaa hivyo unaendelea. Jumla ya Shillingi bilioni 1.25 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha kazi hizo.

46. Mheshimiwa Spika, Serikali pia inatekeleza Mradi wa Kuboresha Upatikanaji Umeme katika Miji ya Ngara, Biharamulo na Mpanda (ORIO) kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Ufalme wa Uhulanzi. Serikali ya Ufalme wa Uhulanzi imeidhinisha msaada wa Shillingi bilioni 22 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo ambaeo lengo lake ni kuongeza uzalishaji na usambazaji umeme katika wilaya husika. Aidha, Serikali imetoa Shillingi bilioni 10.5 kati ya Shillingi bilioni 22 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi. Mradi huo haukuweza kutekeleza kwa wakati kutokana na changamoto za upatikanaji wa fedha kwa upande wa Serikali.

(v) Miradi ya Umeme Vijiji

47. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza lbara ya 63 (c) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 - 2015 inayoelekeza kuongeza idadi ya wananchi waliounganishiwa umeme mijini na vijiji. Katika kutekeleza azma hiyo, Awamu ya Pili ya Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijiji chini ya Wakala wa Nishati Vijiji (REA - Turnkey Project Phase II) umeendelea kutekeleza, ambapo Makao Makuu

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ya Wilaya za Busega, Chemba, Itilima, Kalambo, Kyerwa, Mkalama, Mlele na Nanyumbu zimefikishiwa umeme. Katika Mwaka 2014/15, jumla ya wateja 5,210 wameunganishiwa umeme kwenye wilaya hizo.

48. Mheshimiwa Spika, mradi pia umewezesha upelekaji umeme katika maeneo mbalimbali nchini ambapo hadi kufikia Mwezi Aprili, 2015 wateja wapya waliouanganishiwa umeme kupitia mradi huo wamefikia 8,078 katika mikoa ya Arusha (1,333); Dodoma (389); Geita (55); Iringa (73); Kagera (1,437); Katavi (73); Kilimanjaro (1,778); Lindi (114); Mtwara (213); Mara (315); Njombe (42); Simiyu (750); Singida (1,030) na Tanga (476). Idadi hii inafanya jumla ya wateja wote waliouanganishiwa umeme chini ya miradi ya REA na TANESCO kuanzia Julai, 2014 hadi Aprili, 2015 kufikia 241,401. Idadi hiyo ni sawa na ongezeko la asilimia 68 ikilinganishwa na wateja 143,113 waliouanganishwa Mwaka 2013.

49. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia REA imewezesha utekelezaji wa jumla ya miradi 52 ya kusambaza umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2015 wateja 2,270 waliouanganishiwa umeme. Kati ya hao wateja 1,038 ni wa Mkoa wa Lindi na wateja 1,232 ni wa Mkoa wa Mtwara. Miradi hiyo imegharimu Serikali jumla ya Shillingi bilioni 6.1.

50. Mheshimiwa Spika, Serikali imeongeza wigo wa utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijiji kwa mikoa hiyo. REA kwa kushirikiana na TANESCO imefanya tathmini ya garama za kutekeleza mradi wa kusambaza umeme katika vijiji vya Mikoa hiyo, pamoja na vijiji vilivyo kandokando ya bomba la gesi asilia kutoka Mtwara hadi Somanga Fungu, ambapo Shillingi bilioni 48 zilahitajika. REA itaendelea kutekeleza miradi hiyo kupitia Kampuni ya Namis Corporate Ltd kwa Mkoa wa Mtwara na Kampuni ya OK Electrical and Electronics kwa upande wa Mkoa wa Lindi.

51. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16, Serikali kupitia REA itaendelea kusimamia utekelezaji wa mradi. Napenda kutumia nafasi hii kuwahimiza Waheshimiwa Wabunge na viongozi walioko kwenye maeneo husika kuwahamasisha wananchi kuunganishiwa umeme kwenye nyumba zao pamoja na kutumia umeme huo katika shughuli za kiuchumina kijamii. Katika Mwaka 2015/16, Shillingi bilioni 191.96 zimetengwa, kati ya fedha hizo, Shillingi bilioni 21 zitatolewa na Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD).

52. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/15, Serikali iliendelea kutekeleza mradi wa usambazaji umeme nje ya gridi (off-grid) kupitia Tanzania Energy Development and Access Expansion Project (TEDAP). Chini ya mradi huo, utekelezaji wa programu ya Awamu ya Kwanza ya Sustainable Solar Market Packages - I (SSMP - I) katika Wilaya ya Sumbawanga Vijiji (Rukwa) umekamiliika.

53. Mheshimiwa Spika, mradi umewezesha kufungwa jumla ya mifumo 285 kwenye maeneo ya huduma za kijamii ambazo ni zahanati 35, shule za sekondari 9, vituo vya afya 6, nyumba za walimu na watumishi wa afya 71, vituo vya polisi pamoja na taa za barabarani 240. Kupitia TEDAP mifumo ya umeme wa jua imefungwa katika vituo (centres) 50 vya huduma za jamii ambazo ni shule, zahanati, vituo vya afya na nyumba za watumishi katika Wilaya za Tarime, Bunda na Chemba.

54. Mheshimiwa Spika, baada ya kukamiliika kwa SSMP - I, REA imekamiliha taratibu za kuwapata wakandarasi wa kutekeleza awamu ya pili ya mradi huo (SSMP - II). Wakandarasi hao ni Kampuni za Rex Investment Ltd. na Sinotec Co. Ltd., ambao watatekeleza mradi katika Wilaya nane (8) za mikoa mitano (5) ambayo ni Geita (Bukombe), Kagera (Biharamulo na Chato), Kigoma (Kibondo na Kasulu), Ruvuma (Tunduru na Namtumbo) na Tabora (Sikonge).

55. Mheshimiwa Spika, mradi huo utawezesha jumla ya mifumo 596 kufungwa kwenye huduma za kijamii ambazo ni zahanati 165, vituo vya afya 18, hospitali moja (1), shule za sekondari 97, vituo vya polisi 17, nyumba za wafanyakazi 924 na taa za barabarani 2,260 kwenye vijiji 455. Ufungaji wa mifumo ya awali utaanza Mwaka 2015/16.

56. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/15, Serikali ilahidi kufunga makontena 14 ya jenereta za Umeme wa Jua (Photovoltaic Generators). Ahadi hiyo imetekelizwa, ambapo makontena hayo

yamefungwa katika vijji 10 kwenye Wilaya za Kongwa (Dodoma), Mlele (Katavi) na Uyui (Tabora). Kupitia mradi huo, mifumo ya umeme wa jua imefungwa kwenye nyumba za makazi 812, nyumba za ibada 27, shule sita (6), zahanati nane (8) na taa za barabarani 200.

Uboreshaji wa Sekta Ndogo ya Umeme

57. Mheshimiwa Spika, Mwezi Juni, 2014 Serikali iilidhinisha Mkakati na Mwelekeo wa Kuboresha Sekta Ndogo ya Umeme ya Mwaka 2014 - 2025 (Electricity Supply Industry Reform Strategy and Roadmap). Mkakati huo utatekelezwa kwa vipindi nya muda mfupi, kati na mrefu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi. Utekelezaji wa mkakati huo unaendelea, ambapo ukusanyaji wa mapato ya TANESCO umeongezeka kutoka Shilingi bilioni 893.3 Mwaka 2013 hadi kufikia Shilingi trillioni 1.14, sawa na ongezeko la asilimia 22. Shirika pia limegatua madaraka ya ununuzi wa baadhi ya vifaa kutoka Makao Makuu kwenda Ofisi za Kanda ili kuboresha utoaji huduma.

58. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine iiyofanyika ni kuandaa Rasimu ya Mikataba Kifani ya Kuuziana Umeme (Model Power Purchase Agreements). Mikataba hiyo inahusisha vyanzo nya uzalishaji umeme kutokana na nguvu ya maji, gesi asilia, makaa ya mawe, upepo, jua na mafuta. Lengo la mikataba hiyo ni kupunguza muda wa majadiliano kati ya wazalishaji umeme (power producers) na wanunuzi wa umeme (off-takers) na hivyo kuharakisha taratibu za uwekezaji katika sekta.

59. Mheshimiwa Spika, kazi zitakazofanyika Mwaka 2015/16 ni pamoja na: kuendelea kuboresha halii ya kifedha na kiutendaji wa TANESCO; kuongeza uwekezaji katika Sekta Ndogo ya Umeme kwa kushirikisha sekta binafsi; kuongeza uunganishaji wateja wapya katika maeneo ya mijini na vijijini; na kujenga uwezo wa kiutendaji kwa watumishi katika Sekta Ndogo ya Umeme.

Uendelezaji wa Miradi Midogo ya Umeme

60. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusaidia wawekezaji wadogo kuyatambua maeneo yaliyo na vyanzo nya kuzalisha umeme nchini kwa miradi isiyozidi MW 10. Kwa sasa uwezo wa uzalishaji umeme kutoka miradi midogo ni MW 16. Kuanzia Mwezi Julai, 2014 hadi Aprili, 2015 EWURA imetoa leseni za awali (provisional license) kwa kampuni tatu (3) zitakazozalisha jumla ya MW 12.6. Kampuni hizo ni Bwelui (Ileje, Mbeya) - MW 4.7, Ulaya (Sumbawanga, Rukwa) - MW 2.9 na Twiga Cement (Kinondoni, Dar es Salaam) - MW 5. Serikali itaendelea kuhamasisha wawekezaji katika miradi midogo ya kuzalisha umeme ili kuongeza kasi ya kuwapatia huduma ya umeme wananchi wengi zaidi, hususan maeneo ya vijijini.

SEKTA NDOGO YA NISHATI JADIDIFU

61. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia msaada wa European Union Energy Initiative Partnership Dialogue Facility imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Nishati ya Tungamotaka (Biomass Energy Strategy) na Mpango Kazi. Lengo la mkakati huo ni kuhamasisha matumizi bora na endelevu ya tungamotaka nchini. Aidha, kupitia Programu ya Kitaifa ya Uendelezaji Bayogesi (Tanzania Domestic Biogas Programme), Serikali kupitia Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijiijini (CARMATEC) iijengwa mitambo 12,000 katika mikoa 22 ya Tanzania Bara.

62. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mitambo hiyo, ni ongezeko la asilimia 33 kutoka mitambo 9,000 iiyokuwepo Mwaka 2013/14. Vilevile, mitambo 50 ya mfano ya bayogesi iijengwa katika Wilaya za Tarime na Serengeti. Katika Mwaka 2015/16, kupitia Programu ya Kitaifa ya Uendelezaji Bayogesi, Serikali itaendelea kutekeleza Awamu ya Pili ya Programu hiyo kwa kujenga mitambo 20,700 ifikapo Mwaka 2017.

63. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini iliendelea kuhamasisha uendelezaji wa nishati ya upepo kwa ajili ya kuzalisha umeme katika maeneo mbalimbali nchini yakiwemo Makambako

(Njombe) na Kititimo (Singida). Kampuni zilizonesha nia ya kuwekeza ni pamoja na Geowind Power, Wind East Africa Ltd. na Sino-Tan Renewable Energy Ltd. Kampuni hizo zinatarajiwa kuwekeza katika miradi yenyewe uwezo wa kuzalisha umeme kati ya MW 50 na MW 200. Majadiliano kati ya TANESCO na Kampuni husika yanatarajiwa kukamilika katika Mwaka 2015/16.

64. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika nishati ya jotoardhi (Geothermal) kupitia mikutano na makongamano nje na ndani ya nchi. Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Kongamano la Tano la Jotoardhi katika Kanda ya Afrika Mashariki ilifanyika kuanzia tarehe 27 Oktoba hadi tarehe 4 Novemba, 2014 Jijini Arusha.

65. Mheshimiwa Spika, kongamano hilo ilifunguliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Gharib Mohammed Bilal na washiriki takriban 600 kutoka sehemu mbalimbali duniani walihuduria. Kongamano hilo limesaidia kuitangaza Tanzania kuhusu masuala ya jotoardhi pamoja na kubadilishana uzoefu. Katika kipindi cha Mwaka 2015/16, Serikali kupitia Tanzania Geothermal Development Company (TGDC) itaendelea na maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya jotoardhi.

Matumizi Bora ya Nishati

66. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirkiana na Sida, Taasisi ya Serikali ya Ujeruman (GIZ) na Taasisi ya Maendeleo ya Korea Kusini (KEMCO) iliandaa Mpango wa Matumizi Bora ya Nishati (Energy Efficiency Programme). Mpango huo unahusu Viwango vya Matumizi Bora ya Nishati,(Energy Efficiency Standards), Labelling and Code of Practice na Ukaguzi wa Nishati (Energy Audit).

67. Mheshimiwa Spika, TANESCO pia inaendelea na juhudzi za kupunguza upotevu wa umeme ambao kwa sasa umefikia asilimia 19 pamoja na kusimamia matumizi ya umeme (Demand Side Management). Katika Mwaka 2015/16 Serikali itaendelea kuhamasisha matumizi bora ya nishati ikiwemo kupunguza upotevu wa umeme.

SEKTA NDOGO YA MAFUTA NAGESI

68. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/15 shughuli za utafutaji zilendelea katika maeneo mbalimbali nchini. Kutokana na shughuli hizo kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa nchini kimeongezeka kutoka futi za ujazo trilioni (TCF) 46.5 Mwezi Juni, 2014 hadi 55.08 Mwezi Aprili, 2015 sawa na ongezekola asilimia 18. Gesi hiyo iligunduliwa katika visima viuuatavyo: Gilgilani - 1 (TCF 1.7), Mdalasini - 1 (TCF 1.8) na Piri - 1 (TCF 3), vilivyochorongwa na Kampuni za Statoil na Exxon Mobil; Taachui - 1(TCF 1) na Kamba - 1 (TCF 1.03) vilivyochorongwa na Kampuni za BG na Ophir.

69. Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Dodsal imegundua gesi asilia katika kisima cha Mambakofi - 1 kwenye Kitalu cha Ruvu, ambapo tathmini ya kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa katika eneo hilo inaendelea. Katika Mwaka 2015/16 Serikali itaendelea kusimamia na kuhamasisha shughuli za utafutaji mafuta na gesi asilia nchini. Aidha, baada ya TPDC kupewa jukumu la kuendeleza vitalu Na. 4 - 1B na 4 -1C itaendelea na kazi ya kutathmini takwimu za mitetemo.

70. Mheshimiwa Spika, shughuli za utafutaji mafuta katika maeneo ya mipakani, hususan kitalu cha kusini mwa Ziwa Tanganyika zinaendelea. Ili kuhakikisha shughuli za utafutaji katika maeneo ya mipakani zinafanyika kwa amani, Serikali imeendelea na majadiliano na nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Malawi, Msambiji na Zambia kwa lengo la kuweka mipaka katika Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa.

71. Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia TPDC imeanza majadiliano na Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Msumbiji (NIP) kwa lengo la kufanya kwa pamoja tafiti za joloja maeneo ya mipakani. Katika Mwaka 2015/16, Serikali itaendelea kuratibu majadiliano na nchi jirani kuhusu shughuli za utafutaji mafuta na gesi asilia mipakani.

Miundombinu ya Kusafisha na Kusafirisha Gesi Asilia

72. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Bomba la Gesi Asilia kutoka Mtwara kuitia Lindi hadi Dar es Salaam umekamilika. Aidha, ujenzi wa mitambo ya kusafisha gesi asilia katika eneo la Madimba, Mtwara umefikia asilimia 99 na mitambo ya Songo Songo, Lindi umefikia asilimia 97. Vilevile, ujenzi wa nyumba 16 zenyne uwezo wa kuhudumia wafanyakazi 86 katika maeneo ya Madimba na Songo Songo umekamilika.

73. Mheshimiwa Spika, mitambo na bomba hilo vitaanza kufanya kazi rasmi (Commercial Operational Date) Mwezi Septemba, 2015. Haya ni matokeo ya utekelezaji wa miongoni mwa miradi iliyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 -2015/16). Matumizi ya gesi asilia yatachochea ukuaji wa viwanda, utunzaji wa mazingira kwa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa, kuongeza ajira na hatimaye kuleta maendeleo ya uchumi na kijamii kwa ujumla.

Miundombinu ya Usambazaji wa Gesi Asilia

74. Mheshimiwa Spika, kazi za upembuzi yakinifu, Tathmini ya Athari ya Mazingira na usanifu wa miundombinu ya kuunganisha gesi asilia kwenye mitambo ya kuzalisha umeme na Kiwanda cha Saruji (Wazo Hill) zimekamilika. Aidha, Rasimu za Taarifa za Upembuzi Yakinifu na Tathmini ya Athari ya Mazingira kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika miji ya Mtwara, Lindi na Kilwa zimeandaliwa. Katika Mwaka 2015/16, kazi ya ujenzi wa miundombinu kwa awamu ya kwanza itahusisha kuwaunganisha wateja wakubwa wakiwemo TANESCO na IPTL. Fedha zilitotengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hiyo ni Shilingi bilioni 25.

Hifadhi ya Taifa ya Mafuta

75. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/15 Serikali ilikamilisha maandalizi ya Kanuni za Uratibu wa Hifadhi ya Taifa ya Mafuta (National Strategic Petroleum Reserve Regulations, 2014) kwa kutangaza kwenye Gazeti la Serikali Na. 233 ya tarehe 11 Julai, 2014. Serikali kuitia TPDC pia imekamilisha majadiliano na Kampuni ya Oman Trading International (OTI) kwa ajili ya kuiuzia TPDC mafuta yatakayotumika kwenye Hifadhi ya Taifa ya Mafuta. Aidha, EWURA inakamilisha maandalizi ya Kanuni zitakazotumika kukokotoa bei ya mafuta kutoka kwenye Hifadhi ya Taifa. Baada ya kukamilisha taratibu zote, uendeshaji wa hifadhi hiyo utaanza Mwaka 2015/16.

Uanzishwaji wa Kampuni Tanzu za TPDC

76. Mheshimiwa Spika, Mwezi Septemba, 2014 TPDC ilianzisha Kampuni Tanzu za GASCO na COPEC. Kampuni hizo zimeanza kutekeleza majukumu yake baada ya Kaimu Meneja Wakuu kuteuliwa. Kampuni ya GASCO itahusika na usimamizi wa miundombinu ya gesi asilia ikiwemo mitambo ya kusafisha gesi asilia ya Madimba (Mtwara) na Songo Songo (Lindi) pamoja na bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam. Kampuni ya COPEC itakuwa na jukumu la kusimamia Hifadhi ya Mafuta ya Taifa na kushiriki katika biashara ya mafuta nchini.

77. Mheshimiwa Spika, Kampuni ya COPEC imekamilisha uaandaji wa usanifu wa vituo saba (7) vya mafuta (Petrol stations). Vituo hivyo ni Geita mkoani Geita, Makuyuni (Arusha), Muheza na Segera (Tanga), Musoma na Tarime (Mara) na Singida mkoani Singida. Kazi ya ukarabati na ujenzi wa vituo hivyo itaanza Mwaka 2015/16. Kukamilika kwa vituo hivyo kutaimarisha upatikanaji wa mafuta na ushindani wa kibiashara katika maeneo husika.

Hisa za Serikali katika Kampuni za TIPER, Puma Energy Tanzania Ltd na TAZAMA

78. Mheshimiwa Spika, baada ya hesabu za Mwaka 2013 kukamilika, TIPER iitao gawio la Shilingi bilioni 1.27 kwa Serikali kutokana na umilki wa hisa asilimia 50. Vilevile, Serikali inamili ki hisa asilimia 50 katika Kampuni ya Puma Energy Tanzania Ltd na imepata gawio la Shilingi bilioni 3.28 za Mwaka 2013. Aidha, Serikali hajapata gawio kutokana na hisa asilimia 30 inazomiliki katika Kampuni ya TAZAMA. Katika Mwaka 2015/16, Serikali itapata gawio baada kampuni hizo kukamilisha hesabu za Mwaka 2014.

Shughuli za Udhibiti wa Mafuta

79. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Petroleum Importation Coordinator Limited (PICL) iliendelea kusimamia Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (Bulk Procurement System - BPS). Aidha, EWURA imeendelea kudhibiti na kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa za petroli nchini. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2014 jumla ya lita bilioni 4.41 za aina mbalimbali za mafuta ziliingizwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam. Kati ya kiasi hicho, lita bilioni 2.8 sawa na asilimia 65 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya ndani na lita bilioni 1.56 sawa na asilimia 35 zilikuwa ni kwa ajili ya nchi jirani. Aidha, uagizaji wa mafuta kwa Mwaka 2014 kupitia Bandari ya Dar es Salaam umepungua kwa asilimia 6 ikililinganishwa na lita bilioni 4.68 ziliingizwa nchini Mwaka 2013.

80. Mheshimiwa spika, katika Mwaka 2014/15, EWURA iliendelea kusimamia bei za mafuta katika soko la ndani ili kuhakikisha bei hizo zinaendana na mabadiliko katika soko la dunia na kuwanisha thamani ya Shilingi ya Tanzania na Dola ya Marekani. Bei ya mafuta ghafi katika soko la dunia ilishuka kutoka Dola za Marekani 109 kwa pipa Mwezi Julai, 2014 hadi Dola za Marekani 64 kwa pipa Mwezi Desemba, 2014 sawa na punguzo la asilimia 41.

81. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho bei ya mafuta yaliyosafishwa katika soko la dunia ilishuka kama ifuatavyo: petroli kutoka Dola za Marekani 1,004 kwa tani hadi kufikia Dola za Marekani 573; dizeli kutoka Dola za Marekani 825 kwa tani hadi Dola za Marekani 551; mafuta ya taa/ndege kutoka Dola za Marekani 890 kwa tani hadi Dola za Marekani 605. Aidha, punguzo hilo la bei ya mafuta katika soko la dunia liliwezesha EWURA kupunguza bei ya umeme kwa wastani wa asilimia 2.5. Serikali kupitia EWURA iliendelea kuhakikisha kuwa, wananchi wananzaika na punguzo hilo la bei katika soko la dunia.

82. Mheshimiwa Spika, EWURA imeendelea kudhibiti ubora wa bidhaa za mafuta ya petroli nchini kwa kuwachukulia hatua za kisheria waliothibitika kuza mafuta chini ya viwango vilivyowekwa. Aidha, ili kuimarishe udhibiti wa vilainishi vya mitambo (lubricants), Mamlaka hiyo imeanza kutoa leseni za biashara ya vilainishi na imetunga Kanuni kuhusu usimamizi wa bidhaa hiyo. EWURA itaendelea kuhakikisha ujenzi wa miundombinu na biashara ya mafuta ya petroli nchini vinazingatia usalama na utunzaji wa mazingira.

83. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma ya mafuta kwa njia salama hasa maeneo ya vijiji, EWURA imeandaa Kanuni kuhusu ujenzi wa vituo vya mafuta katika maeneo ya vijiji - The Petroleum (Village and Township Retail Outlet Operations) Rules, 2014. Kanuni hizo pamoja na mambo mengine zinaweka viwango tofauti vya ujenzi wa vituo vya kuuzia mafuta kati ya vijiji na mijini. Aidha, ili kuboresha usambazaji wa bidhaa za petroli hapa nchini, EWURA inaendelea na tathmini ya kuanzisha mfumo mpya wa usambazaji mafuta kwa kutumia magari (mobile dispensers) na vituo vidogo vinavyohamishika.

84. Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya tathmini ya miundombinu ya kupokelea mafuta katika Bandari ya Tanga ili sehemu ya shehena ya mafuta kupitia BPS yaweze kushushwa kwenye bandari hiyo. Mpango huo unalenga kuondoa utegemezi wa Bandari ya Dar es Salaam pekee, kuimarishe upatikanaji wa bidhaa za petroli nchini, kupunguza msongamano wa meli katika Bandari ya Dar es Salaam na gharama za usafirishaji. Katika Mwaka 2015/16, Serikali itaendelea kuboresha

shughuli za udhibiti wa bidhaa za petroli na Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja nchini ikiwemo kubadilisha muundo wa PICL.

Mradi wa Uzalishaji Mbola kwa Kutumia Gesi Asilia

85. Mheshimiwa Spika, TPDC imekamilisha taratibu za kumpata mwekezaji kwenye kiwanda cha mbola kitakachoengwa Mkoani Mtware. Baada ya uchambuzi wa zabuni, Kampuni ya Ferrostaal ya Ujerumanii lishinda. Mradi huo utatekelezwa kwa njia ya ubia, ambapo Kampuni ya Ferrostaal itamili asilimia 60 na Serikali kupitia TPDC asilimia 40. Kiwanda hicho kitahitaji futi za ujazo milioni 104 za gesi asilia kwa siku ili kuzalisha takriban tani 4,000 za mbola kwa siku, sawa na tani milioni 1.3 kwa mwaka. Katika Mwaka 2015/16, wabia wataendelea na maandalizi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

Sera na Sheria katika Sekta ya Nishati

86. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/15, Serikali iilkamiliisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2003 na kuandaa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015. Pamoja na mambo mengine, Sera hiyo imeweka mkazo kuhusu: kuongeza uzalishaji umeme kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo nishati jadidifu; kuimarisha usimamizi wa shughuli za mafuta na gesi asilia; na kuongeza ushiriki wa Watanzania kwenye rasilimali hizo.

87. Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeandaa Rasimu ya Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015 na Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania (The Tanzania Extractive Industries Transparency and Accountability Act, 2015). Lengo la kutunga na kuboresha Sera na Sheria hizo ni kuimarisha usimamizi katika Sekta ya Nishati. Katika Mwaka 2015/16, mikakati ya utekelezaji wa Sera husika itakamiliishwa.

SEKTA YA MADINI

Mafanikio katika Sekta ya Madini

88. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/15, mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Madini ni pamoja na: kuendelea kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Madini ambapo wastani wa Dola za Marekani milioni 460 ziliwekezwa ikiwa ni mtaji kutoka nje ya nchi; na kulipwa kwa ushuru wa huduma (service levy) jumla ya Shilingi bilioni 4.1 kutoka kwa Kampuni za Madini za Acacia (iliyokuwa ikijulikana kwa jina la African Barrick Gold) na Geita Gold Mine ikiwa ni asilimia 0.3 ya mapato (turnover) kwa Halmashauri husika.

89. Mheshimiwa Spika, Wizara pia iilwezesha kununuliwa kwa mitambo miwili ya kuchoronga miamba (drilling rigs) itakayotumika katika utafiti wa jiolojia kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo; kukamiliika kwa asilimia 92 ya uchoraji wa ramani za upatikanaji wa madini katika nchi kavu ya Tanzania Bara; na kutengwa kwa maeneo sita (6) kwa ajili ya wachimbaji wadogo ambayo ni Buzwagi (Kahama), Ibologelo (Igunga), Kinamiyuba (Shinyanga) na Mumba, Selemi na Ukene (Nzega).

90. Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni: kuandalila kwa Mpango Kifani wa Utunzaji Mazingira (Model Environmental Protection Plan - EPP) kwa ajili ya wachimbaji wadogo; kupatikana kwa majengo ya kudumu ya Ofisi za Madinizi Moshi, Bariadi, Njombe, Tabora, Kigoma, Nachingwea na Songea; kulipwa Serikalini jumla ya Shilingi bilioni 415.23 ikiwa ni kodi na mrabaha kwa Mwaka 2014 ikilanganishwa na Shilingi bilioni 327.35 zilizolipwa Mwaka 2013 na kampuni zinazomiliki migodi mikubwa; na kusajiliwa kwa maabara ya TMAA na Shirika la Viwango vya Kimataifa (ISO/IEC 17025) iilikutoa huduma za uchunguzi na utambuzi wa sampuli za madini.

91. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16, Serikali itaendelea kutekeleza vipaumbele katika Sekta ya Madini vikiwemo: kuimarisha makusanyo ya maduhuli yatokanayo na shughuli za madini; kuendeleza uchimbaji mdogo; kuboresha utoaji na usimamizi wa leseni za madini; kuimarisha usimamizi wa afya, usalama na utunzaji wa mazingira migodini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; na kuendelea kuboresha mazingira ya kazi katika Ofisi za Madini nchini.

Thamani ya Madini yaliyouzwa Nje ya Nchi

92. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014 jumla ya wakia milioni 1.27 za dhahabu, wakia 469,027 za fedha na ratili milioni 13.8 za shaba zilizalishwa na kusafirishwa nje ya nchi kutoka migodi mikubwa ya Biharamulo, Bulyanhulu, Buzwagi, Geita, New Luika na North Mara. Jumla ya thamani ya madini hayo ni Dola za Marekani bilioni 1.66 ikilinanishwa na Dola za Marekani bilioni 1.79 kwa Mwaka 2013, sawa na pungufu kwa asilimia 7.3.

93. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, jumla ya karati 203,786 za almasi na karati milioni 3.8 za Tanzanite (Grade A - I) zilizalishwa na Migodi ya Mwadui na TanzaniteOne sawia katika Mwaka 2014 ikilinanishwa na karati 158,562 za almasi na karati milioni 3.2 za Tanzanite kutoka katika migodi hiyo Mwaka 2013. Mrabaha uliolipwa Serikalini na wamiiiki wote wa migodi mikubwa nchini kwa Mwaka 2014 ni Dola za Marekani milioni 70.16 ikilinanishwa na Dola za Marekani milioni 72.90 zilizolipwa Mwaka 2013.

94. Mheshimiwa Spika, mauzo ya madini nje ya nchi na mrabaha uliolipwa Serikalini vilipungua kutokana na m dororo wa kuchumi duniani. Kutokana na hali hiyo, bei za madini mbalimbali zilishuka katika soko la dunia, hususan dhahabu inayoongoza kuchimbwa hapa nchini. Kwa mfano, wastani wa bei ya dhahabu kwa Mwaka 2013 ilikuwa Dola za Marekani 1,411 kwa wakia wakati wastani wa bei ya dhahabu Mwaka 2014 ilikuwa Dola za Marekani 1,266 kwa wakia, sawa na bei kushuka kwa asilimia 10. Hali hii imeendelea kuathiri uwekezaji katika Sekta ya Madini. Katika Mwaka 2015/16, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa shughuli za uzalishaji na biashara ya madini ili kuongeza mchango wa Sekta ya Madini katika maendeleo ya Taifa.

Kuimarisha Makusanyo ya Maduhuli yatokanayo na Madini

95. Mheshimiwa Spika, Wizara ilendelea kufuatilia ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na shughuli za madini nchini ili kuhakikisha kuwa mapato stahiki yanaliipwa Serikalini. Katika Mwaka 2014/15 Wizara ilenga kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 209.96 kutoka Sekta ya Madini. Hadi kufikia tarehe 20 Mei, 2015 jumla ya Shilingi bilioni 137.55 zilikuwa zimekusanywa, sawa na asilimia 65.5 ya lengo la makusanyo. Sababu za kushindwa kufikia lengo la makusanyo kwa kipindi husika ni pamoja na: kuendelea kushuka kwa bei ya madini katika soko la dunia, hususan dhahabu; na kushindwa kufunguliwa migodi mipya iliyotarajiwa kufunguliwa katika kipindi husika ikiwemo Migodi ya Buckreef na Busolwa.

96. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16 Serikali inategemea kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 211.96 kutoka katika Sekta ya Madini. Ili kufikia lengo hilo, ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Sekta ya Madini utaimarishwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa malipo stahiki ya ada na mrabaha wa madini yanaliipwa na wachimbaji na wafanyabiashara wa madini nchini.

97. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuzuia utoroshaji wa madini, Wizara imeanzisha mpango maalum wa kutoa motisha kwa watu watakaotoa taarifa zitakazowezesha kukamatwa kwa watoroshaji madini; kuimarisha Ofisi za Madini kwa kuzipatia rasilimali zinazohitajika katika kufuatilia maduhuli kwenye maeneo ya uchimbaji; na kuongeza udhibiti na usimamizi wa sehemu za uzalishaji wa madini ya dhahabu, vito pamoja na madini ya ujenzi na ya viwandani.

Majadiliano na Kampuni za Madini

Nakala ya Mtandao (Online Document)

98. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini imekamilisha majadiliano na Kampuni zenyе mikataba ya madini (MDAs), kuhusu ulipaji wa asilimia 0.3 ya mapato (turnover) yakiwa ni ushuru wa huduma kwa Halmashauri husika badala ya Dola za Marekani 200,000 kwa mwaka. Hivyo, Migodi ya Geita, Bulyanhulu, Buzwagi na North Mara imelipa jumla ya Shillingi bilioni 4.1 kwa kipindi cha Mwezi Julai hadi Desemba, 2014.

99. Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo, Mgodi wa Geita umelipa kiasi cha Shilingi bilioni 1.65 kwa Halmashauri ya Mji wa Geita; Mgodi wa Bulyanhulu Shilingi milioni 749.5 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala; Mgodi wa North Mara Shilingi milioni 863.3 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime; na Mgodi wa Buzwagi Shilingi milioni 843.2 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama. Malipo hayo yataendelea kufanyika kila baada ya miezi sita (6). Katika Mwaka 2015/16, Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha zitakazokuwa zinalipwa na migodi kwa Halmashauri husika ili zitekeleze miradi ya maendeleo kulingana na vipaumbele vya maeneo husika.

100. Mheshimiwa Spika, Wizara iikamilisha majadiliano na Kampuni ya Acacia kuhusu ulipaji wa kodi ya mapato kwenye Migodi ya Bulyanhulu, Buzwagi na North Mara. Katika Mwaka 2015/16, Kampuni hiyo itaanza kulipa kodi ya mapato kwa migodi yake hapa nchini. Hatua hii itafanya migodi yote yenye MDAs kuwa walipaji wa kodi ya mapato. Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa makubaliano yaliyofanyika katika yake na Kampuni husika.

101. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka 2014/15 Serikali imekamilisha majadiliano na Kampuni ya Mantra kuhusu Mkataba wa Kuendeleza Uchimbaji wa Madini (MDA) ya Urani katika eneo la Mto Mkuru wilayani Namtumbo. Hata hivyo, kushuka kwa bei ya madini ya urani katika soko la dunia kumeathiri shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini hayo katika mradi wa Bahi unaotekelizwa na Kampuni ya Uranex na Mto Mkuru unaotekelizwa na Kampuni ya Mantra.

Kuendeleza Uchimbaji Mdogo wa Madini

102. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/15 Serikali imefanya tathmini katika maeneo 25 yaliyotengwa kwa ajili ya uchimbaji mdogo katika wilaya mbalimbali nchini. Maeneo hayo yana jumla ya ukubwa wa kilomita za mraba 2,047 na yana leseni 8,800 za uchimbaji mdogo wa madini. Tathmini hiyo imesaidia kubaini changamoto zinazotokana na utengaji wa maeneo ya wachimboji wadoqo na kubuni mbinu za kutatua changamoto hizo.

103. Mheshimiwa Spika, Serikali iitenga maeneo mapya sita (6) kwa ajili ya uchimbaji mdogo chini ya utaratibu wa ushirikiano kati ya Serikali na Kampuni kubwa za utafutaji na uchimbaji madini ambazo zilikubali kuachia baadhi ya maeneo. Maeneo hayo yana jumla ya hekta 22,970 na yapo Buzwagi, (Kahama), Ibologelo (Igunga), Kinamiyuba (Shinyanga) na Mumba, Selemi na Ukene (Nzega). Katika maeneo hayo, takriban leseni 2,297 zitapatikana ambazo zitatolewa kwa wachimbaji wadogo.

104. Mheshimiwa Spika, kama iivyoahidiwa na Serikali katika Hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini ya Mwaka 2014/15, mitambo miwili (2) ya kuchoronga miamba imenunuliwa kwa ajili ya kuwezesha utambuzi wa mashapo katika maeneo ya wachimbaji wadogo. Shughuli hizi ni katika kutekeleza Ibara ya 56 (d) ya llani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 - 2015.

105. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16, Wizara itatenga maeneo yasiyopungua matano (5) kwa ajili ya uchimbaji mdogo baada ya kufanyiwa utafiti wa jilojia ili kubaini mashapo yanayoweza kuchimbwa kwa faida na wachimbaji wadogo. Wizara itaendeleza huduma za ugani na utoaji wa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa wachimbaji wadogo na Viongozi wa Wilaya wapatao 1,000 na kusambaza nakala 4,000 za mwongozo elekezi kwa wachimbaji wadogo.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Kampuni za AngloGold Ashanti na Acacia zitaanzisha migodi ya mfano na mafunzo kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu katika Wilaya za Geita na Tarime.

106. Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanya tathmini ya utekelezaji wa mpango wa utoaji wa mikopo kwa wachimbaji wadogo. Tathmini hiyo imeonesha kuwa wachimbaji wadogo walio wengi wameshindwa kukidhi masharti ya kupata mikopo hiyo. Kutokana na halii hiyo, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini imeandaa utaratibu mpya wa utoaji ruzuku kwa wachimbaji wadogo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya uchimbaji. Katika Mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo kwa kutoa ruzuku, ambapo Serikali imetenga Shilingi bilioni 3 na Benki ya Dunia imekubali kutoa Dola za Marekani milioni 3 kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP).

Kuboresha Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini

107. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha mfumo wa utoaji leseni kwa kuanzisha huduma za kupokea maombi ya leseni kwa njia ya mtandao (Online Mining Cadastre Transactional Portal). Mfumo huo unawezesha wateja kutuma maombi na kufanya malipo kwa njia ya mtandao. Kufikia Mwezi Mei, 2015 jumla ya leseni 1,514 kati ya leseni 4,200 zimesajiliwa kwenye mfumo huo.

108. Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pamoja na malengo mazuri ya uanzishwaji wa mfumo huo, kumekuwepo na mwitikio mdogo wa wateja kujisajili, ambapo hadi sasa wamiliki wa leseni 140 kati ya 400 wamesajiliwa. Natoa wito kwa wamiliki wote wa leseni za madini kujisajili kwa njia ya mtandao ili kurahisisha utoaji wa huduma. Huduma hiyo itazinduliwa rasmi tarehe 8 Juni, 2015. Pamoja na kuboresha mfumo wa utoaji leseni, Wizara imekamilisha ujenzi wa jengo la Kituo Maalum cha Kuhifadhi Takwimu (Data Recovery Centre) Mjini Morogoro. Kwa Mwaka 2015/16 Wizara itakamilisha ufungaji wa mitambo katika Kituo hicho.

109. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwezi Julai, 2014 hadi Machi, 2015 jumla ya maombi ya leseni 7,966 ya utafutaji na uchimbaji madini yalipokelewa na kuingizwa kwenye Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini. Baada ya uchambuzi wa kina, maombi 111 ya leseni yalikataliwa kwa kutokidhi vigezo vya masharti ya leseni. Katika kipindi hicho, jumla ya leseni 4,506 zilitolewa, kati ya hizo 750 ni kwa ajili ya utafutaji mkubwa wa madini; 27 za uchimbaji wa kati; na 3,729 kwa ajili ya uchimbaji mdogo. Aidha, leseni 248 za biashara ya madini na leseni 232 za wanunuzi wa kati zimetolewa. Maombi 3,349 yanaendelea kufanyiwa uchambuzi.

110. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kisheria kwa wamiliki wa leseni wasiotimiza masharti ya leseni. Katika kipindi hicho, jumla ya leseni 2,461 zilifutwa, kati ya hizo 557 zilikuwa ni za utafutaji madini na 1,904 ni za uchimbaji mdogo wa madini. Aidha, kati ya Mwezi Julai, 2014 na Machi, 2015 Hati za Makosa 609 zilitolewa kwa leseni 533 za utafutaji madini na 76 za uchimbaji wa kati.

111. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16, Wizara itafanya uchambuzi wa kina wa leseni za uchimbaji mdogo katika maeneo mbalimbali nchini (PML resurveying) ili kuhakikisha kuwa leseni zote zimeingizwa kwenye mfumo wa utoaji leseni. Hatua hii itasaidia kupunguza migogoro ya umilikaji wa leseni.

Kuimarisha Usimamizi wa Masuala ya Baruti Nchini

112. Mheshimiwa Spika, matumizi ya baruti nchini yameendelea kuongezeka hasa kutokana na ongezeko la shughuli za uchimbaji wa madini, utafiti wa mafuta, gesi asilia na miradi mingine ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali. Katika Mwaka 2014/15 tani 24,308 za baruti ziliingizwa nchini ikilinganishwa na tani 15,628.8 Mwaka 2013/14, sawa na ongezeko la asilimia 55. Katika kipindi hicho vipande 3,046,497 vya fataki vilivyoingizwa nchini ikilinganishwa na vipande 2,177,062 vilivyoingizwa Mwaka 2013/14, ikiwa ni ongezeko la asilimia 40.

113. Mheshimiwa Spika, Wizara pia ilitoa vibali 133 vya kuingiza baruti nchini (import permits), vibali 117 vya kulipua baruti (blasting certificates) na leseni 5 za maghala ya kuhifadzia baruti (magazine licenses). Aidha,

Nakala ya Mtandao (Online Document)

mafunzo yalitolewa kwa wachimbaji wadogo wa madini 259 katika Wilaya ya Bunda mkoni Mara. Mafunzo hayo yalilenga kuwaelimisha wachimbaji hao kuhusu taratibu za upatikanaji, utunzaji, usafirishaji na matumizi sahihi ya baruti katika uchimbaji wa madini. Wizara pia ilifanya ukaguzi katika maghala 44 ya kuhifadhiya baruti.

114. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sheria ya Baruti ya Mwaka 1963 na marekebisho yake ya Mwaka 2002 umekuwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kiusalama; kiteknolojia; ongezeko la matumizi ya baruti katika shughuli za utafiti wa mafuta na gesi asilia; ujenzi wa miundombinu; na kuibuka kwa vitendo vinavyohusu matumizi haramu ya baruti.

115. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imeandaa Rasimu ya Sheria Mpya ya Baruti ya Mwaka 2015 ili kuboresha usimamizi wa upatikanaji, usafirishaji, utunzaji, utumiaji na biashara ya baruti nchini. Muswada wa Sheria ya Baruti utawasilishwa Bungeni katika Mwaka 2015/16. Vilevile, Wizara itaendelea kushirikiana na taasisi nyingine katika kudhibiti matumizi haramu ya baruti nchini na kutoa mafunzo kwa wadau kuhusu matumizi bora na salama ya baruti.

Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini

116. Mheshimiwa Spika, kazi ya ukaguzi wa shughuli za uongezaji thamani madini ulifanyika katika Kanda ya Kaskazini (Arusha na Mererani) na Mashariki (Dar es Salaam, Morogoro na Tanga) ambapo jumla ya mashine 436 za uchongaji na 430 za ukataji zilikaguliwa kutoka kwa wafanyabiashara 78 wa madini.

117. Mheshimiwa Spika, ukaguzi huo umesaidia ukusanyaji wa takwimu kuhusu wataalamu wa kusanifu vito na idadi ya mitambo ya uchongaji wa madini. Katika kipindi hicho, leseni 46 za uchenjuaji madini ya dhahabu na moja (1) ya madini ya viwandani zilitolewa, hivyo kuongeza idadi ya leseni za uchenjuaji madini kufikia leseni 142. Aidha, Rasimu ya Sheria Mpya ya Uongezaji Thamani Madini (The Draft Mineral Value Addition Act) imeandaliwa kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa shughuli hizo ili kuongeza mapato ya Serikali.

118. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/15 Wizara imekamilisha ukarabati wa Kituo cha Jimolojia (Tanzania Gemological Centre - TGC) cha Arusha ambacho kilizinduliwa rasmi Mwezi Aprili, 2015. Kupitia Mfuko wa Kuwaendeleza na Kuwajengea Uwezo Wanawake wa Kitanzania ulioanzishwa Jijini Arusha (Arusha Gem Fair Women Foundation Fund), kituo kimetoa mafunzo ya ukataji na usanifu wa madini ya vito kwa vitendo kwa wanawake 15. Mfuko huo ulianzishwa Mwaka 2012 kwa ushirikiano kati ya Wizara na Tanzania Mineral Dealers Association (TAMIDA) na unasi mamiwa na Kamati ya Maonesho ya Kimataifa ya Vito ya Arusha.

119. Mheshimiwa Spika, fedha za Mfuko huo zinatokana na michango ya wafanyabiashara wa madini ya vito wakati wa Maonesho ya Vito ya Arusha. Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wadau wa tasnia ya vito kwa kuendelea kuchangia katika Mfuko huo. Katika kipindi cha Mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini na kukagua mitambo ya uchenjuaji na vituo vya ukataji na usanifu wa madini ya vito.

Kuvutia Uwekezaji Katika Sekta ya Madini

120. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/15, Wizara ilishiriki katika mikutano na maonesho mbalimbali ya kimataifa ili kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Madini. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara ilishiriki kwenye Maonesho ya INDABA (Afrika Kusini), PDAC (Canada) na ADUC (Australia) yanayokutanisha wawekezaji katika Sekta ya Madini. Kupitia fursa hii, Serikali imetoa taarifa mbalimbali kuhusu mazingira wezeshi ya uwekezaji katika Sekta ya Madini hapa nchini ikiwa ni pamoja na taarifa za jiolojia ili kuvutia wawekezaji.

121. Mheshimiwa Spika, Wizara pia iliratibu Maonesho ya Vito na Usonara yaliyofanyika Mwezi Novemba, 2014 Jijini Arusha, ambapo washiriki 465 kutoka nchi 29 walihudhuria. Katika Maonesho hayo, madini yenye thamani ya Shilingi bilioni 3.4 yaliuzwa na kuiwezesha Serikali kukusanya mrabaha wa Shilingi milioni 113.8. Maonesho mengine yaliyofanyika Mwezi Aprili, 2015 ambapo washiriki 960 walihudhuria kutoka nchi 30. Katika maonesho hayo, madini yenye thamani ya Shilingi bilioni 7.2 yaliuzwa na kuiwezesha Serikali kukusanya mrabaha wa Shilingi milioni 279.8. Washiriki wa maonesho hayo walitoka Afrika Mashariki na Kati, Asia, Amerika na Ulaya.

122. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kushiriki katika maonesho mbalimbali ya kimataifa yakiwemo ya Arusha kwa lengo la kuvutia wawekezaji katika Sekta ya Madini. Natoa wito kwa wadau wa madini ya vito waendelee kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini ili kufanikisha maonesho hayo kwa lengo la kukuza masoko ya ndani na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini.

Kuimarisha Usimamizi wa Afya, Usalama na Utunzaji wa Mazingira Migodini

123. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwezi Julai, 2014 hadi Machi, 2015 jumla ya migodi 1,322 ilikaguliwa ili kuhakikisha kuwa Kanuni za Afya, Usalama na Utunzaji wa Mazingira zinazingatiwa. Kati ya hiyo: sita (6) ilikuwa ni migodi mikubwa ya Buzwagi, Bulyanhulu, Geita, Mwadui, New Luika na North Mara; 84 migodi ya kati; na 1,232 migodi midogo.

124. Mheshimiwa Spika, ukaguzi huo umesaidia kuimarisha hali ya afya na usalama kwa wachimbaji wa migodi husika. Vilevile, Wizara imeidhinisha Mpango wa Utunzaji Mazingira (Environmental Protection Plan) kwa migodi 25 ya wachimbaji wadogo. Katika Mwaka 2015/16 Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo juu ya kuandaa Mpango wa Utunzaji Mazingira kwa kuzingatia Sheria ya Madini ya Mwaka 2010.

125. Mheshimiwa pika, katika kusimamia utunzaji wa mazingira migodini, Wizara imefikia makubaliano na migodi ya Bulyanhulu, Buzwagi na North Mara kuhusu utaratibu wa uwekaji wa Hati Fungani za ufungaji wa migodi. Aidha, Mgodi wa Dhahabu wa Golden Pride uliokuwa unamiliika na Kampuni ya Resolute Tanzania Limited Wilayani Nzega ulikamilisha shughuli za ukarabati wa mazingira Mwezi Novemba, 2014 kulingana na Mpango wa Ufungaji wa Mgodi.

126. Mheshimiwa Spika, eneo la Mgodi wa Golden Pride ilikabidhiwa kwa Serikali Mwezi Desemba, 2014 ili litumiwe na Chuo cha Madini Dodoma kutoa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa wanafunzi. Pia, Kampuni ya Resolute ilikabidhi Serikali nyumba 35 na mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 316 na nyumba 15 kwa ajili ya walimu; mabasi madogo matatu; vifaa vya maabara na vifaa vya kompyuta. Mwezi Februari, 2015 Chuo cha Madini kilianza kutoa mafunzo katika eneo hilo.

127. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka 2015/16 Wizara itaendelea kusimamia uboreshaji wa Afya, Usalama na Mazingira Migodini ili kuendana na matakwa ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Kanuni zake. Aidha, Wizara itaendelea kufuatilia uhuishaji wa Mpango wa Ufungaji Mgodi wa Dhahabu wa Tulawaka (ambao kwa sasa unajulikana kama Biharamulo) kufuatia makabidhiano kati ya Kampuni ya Pangea Minerals Limited na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) Mwaka 2013.

Kuimarisha Mazingira ya Kazi Katika Ofisi za Madini

128. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Ibara ya 56 (b) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 - 2015, ambayo pamoja na mambo mengine inasitisiza uimarisaji wa miundombinu ikiwemo ofisi na vitendea kazi, Mwaka 2014/15 Wizara ilianzisha Ofisi mpya za Madini za Bariadi, Moshi,

Nakala ya Mtando (Online Document)

Nachingwea na Njombe na kununua majengo kwa ajili ya Ofisi hizo. Wizara pia ilinunua majengo kwa ajili ya Ofisi za Kigoma, Songea na Tabora pamoja na kuanza kujenga majengo ya Ofisi za Madini za Dodoma na Morogoro. Vilevile, Ofisi hizo zilipatiwa vitendea kazi muhimu yakiwemo magari na kompyuta.

129. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16, Wizara itakamilisha ujenzi wa majengo ya Ofisi za Morogoro na Dodoma na kuendelea kuzimarisha Ofisi za Madini za Kanda na za Maafisa Madini Wakazi ili kuongeza ufanisi katika usimamiaji wa Sekta ya Madini.

Uchambuzi na Uthaminishaji wa Madini ya Vito Kupitia TANSORT

130. Mhesimiwa Spika, katika Mwaka 2014/15 TANSORT ilithaminisha na kusimamia uuzwajî wa karati 183,165.12 za almasi zenyé thamani ya Dola za Marekani milioni 56.7. Mauzo hayo yaliingizia Serikali mrabaha wa Dola za Marekani milioni 2.8. Mapato hayo ni ongezeko la asilimia 68 ikilinganishwa na kipindi kama hicho katika Mwaka 2013/14. TANSORT pia ilithaminisha tani 2,938.68 za madini ya mapambo; gramu milioni 1.65 za vito ghafi; na karati 319,090 za madini ya vito yaliyochongwa na kusanifiwa yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 36.52. Katika Mwaka 2015/16, Serikali itaendelea kuimarisha TANSORT ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP)

131. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP) unaendelea vizuri ambapo shughuli zilizotekelze wa ni pamoja na: kukamilisha ukarabati wa maabara na Ofisi za Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST), majengo ya kituo cha Tanzania Gemmological Centre (TGC), majengo ya Chuo cha Madini Dodoma (MRI) na ujenzi wa Kituo cha Kutunza Takwimu Morogoro. Vilevile, mradi umefanikisha kuanza kwa ukarabati wa majengo ya Ofisi za Madini za Baridi, Kigoma, Moshi, Mtwara, Nachingwea, Njombe, Songea na Tunduru. Aidha, Mradi umeendelea kuziimarisha maabara za GST na TMAA kwa kuzipatia vifaa wa kisasa.

132. Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka 2015/16 kuititia mradi huo kazi zifuatazo zitatekelezwa: kukamilisha ukarabati wa Ofisi za Madini za Bariadi, Kigoma, Moshi, Mtwaro, Nachingwea, Njombe, Songea na Tunduru; ukarabati na upanuzi wa ofisi za Mpanda, Songea, Geita na Kahama ili kuziwezesha kuwa vituo vya ufundishaji kwa wachimbaji wadogo.

133. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zitakazofanyika ni: ujenzi wa vituo vya mafunzo kwa wachimbaji wadogo vya Kapalambsenga, Mbesa, Rwanagasa, Kyerwa na Katente; kuandaa miongozo ya uendeshaji wa vituo wa

mafunzo kwa wachimbaji wadogo; kuiwezesha
GST kuandaa ramani mbalimbali za jiosayansi
katika maeneo saba (7) yaliyotengwa kwa wachimbaji wadogo; kuiwezesha STAMICO kutoa mafunzo
kwa wachimbaji wadogo; na kuendelea kuwajengea maafisa uwezo wa kusimamia Sekta ya Madini.

134. Mheshimiwa Spika, mradi huu ulikuwa umalizike mwezi Juni, 2015. Hata hivyo, kutokana na utekelezaji mzuri wa shughuli za mradi, Benki ya Dunia baada ya majadiliano na Serikali, imeridhia maombi yaliyowasilishwa na Serikali ya kuongeza muda wa mradi huo. Hivyo, mradi umeongezewa muda wa miaka mitatu (3) na miezi sita (6) ambapo Benki ya Dunia itatoa mkopo wa nyongeza wa Dola za Marekani milioni 45 ambazo zitaanza kutumika mwezi Agosti, 2015.

Asasi ya Uwazi katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia (Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative - TEITI)

135. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/15 Serikali imeandaa Rasimu ya Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia ya Mwaka 2015. Sheria hiyo pamoja na mambo mengine, itaweka utaratibu wa upatikanaji kwa wakati taarifa za malipo, mapato, mauzo na gharama za uwekezaji kutokana na shughuli za madini, mafuta na gesi asilia. Aidha, Sheria hiyo inaipa Kamati Tekelezi ya TEITI uwezo wa kisheria wa kufanya uchunguzi endapo kutakuwa na tofauti katika taarifa ya usuluhishi wa malipo na mapato yanayotokana na rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia.

136. Mheshimiwa Spika, Kamati Tekelezi ya TEITI imeendelea kufanya maandalizi ya Taarifa za Ulinganishi wa malipo na mapato ya Mwaka 2012/13 na 2013/14. Aidha, Kamati iliendesha warsha kwa vyombo vya habari, asasi za kiraia na wananchi wanaoishi karibu na shughuli za uchimbaji na utafutaji madini, mafuta na gesi asilia. Lengo la mafunzo hayo ilikuwa ni kuwajengea uwezo kuhusu uchambuzi na ukokotoaji wa takwimu za mapato yanayoliwa Serikalini kutoka kampuni za madini, mafuta na gesi asilia zinazotolewa kupitia Taarifa za TEITI. Mafunzo hayo yalifanyika katika Wilaya za Geita, Kahama, Lindi, Mtwara na Tarime.

137. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16, Serikali itawasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya TEITI; itaendelea kuiwezesha TEITI kuelimisha kampuni na taasisi husika za Serikali; kuzijengea uwezo asasi za kiraia na vyombo vya habari kuhusu uwekezaji katika shughuli za madini, mafuta na gesi asilia na ukokotoaji wa mapato ya Serikali; na kumkiliwa Taarifa za Ulinganishi wa Malipo na Mapato ya Mwaka 2012/13 na 2013/14.

Tuzo ya Rais ya Huduma za Jamii na Uvezeshwaji katika Tasnia ya Uziduaji

138. Mheshimiwa Spika, Tuzo ya Rais ya Huduma za Jamii na Uvezeshwaji kwa Miradi ya Tasnia ya Uziduaji nchini (Presidential Award on Corporate Social Responsibility and Empowerment - CSRE in Extractive Industries) ilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa, Dkt. Jakaya Mshiro Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 28 Februari, 2012. Tuzo hiyo inayofanyika kila mwaka ilitolewa kwa mara ya kwanza tarehe 28 Agosti, 2013 ambapo Kampuni ya Williamson Diamonds Limited ilibuka mshindi wa jumla katika kampuni 38 za madini, mafuta na gesi asilia zilitozishiriki katika zoezi la kuwania tuzo hiyo.

139. Mheshimiwa Spika, lengo la Tuzo hii ni kutambua mchango wa kampuni hizo katika miradi mbalimbali na kuzihamasisha kuongeza mchango wake katika maendeleo ya jamii, hususan maeneo yanayozunguka miradi madini, mafuta na gesi asilia. Pia, Tuzo hii imelenga kuiwezesha jamii na Serikali za Mitaa kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi ya jamii katika maeneo yao.

140. Mheshimiwa Spika, Tuzo hii ilitolewa kwa mara ya pili tarehe 21 Aprili, 2015 ambapo Mgodi wa North Mara unaoendesha shughuli zake Wilayani Tarime ilibuka Mshindi wa jumla. Katika awamu hii ya pili, jumla ya Kampuni 59 zilitindanishwa kwa kutathmini miradi ya huduma za jamii iliyotekelzeza na Kampuni hizo kuanzia Januari, 2013 hadi Juni, 2014.

141. Mheshimiwa Spika, tathmini hiyo ilhusisha miradi ya elimu, maji, afya, ujenzi wa miundombinu na uvezeshaji wa mitaji kwa vikundi ndani ya jamii inayozunguka migodi. Jumla ya fedha iliyotumiwa na Kampuni hizo 59 kutekeleza miradi ya kijamii ilikuwa ni Shilingi bilioni 42.8. Natoa wito kwa Kampuni zote zinazojihusisha katika shughuli za madini, mafuta na gesi kuongeza ushiriki wao kwenye miradi ya kijamii ili shughuli hizo zilete manufaa stahiki (win-win benefits) kwa Kampuni na Jamii husika.

Wakala wa Jiolojia Tanzania - GST

142. Mheshimiwa Spika, Wakala uliendelea kukusanya na kuchambua takwimu za jiosayansi na kutoa huduma mbalimbali za jiolojia. Wakala huo ulikusanya taarifa zilitowezesha kuchorwa kwa

ramani nne (4) za joloja kwa mfumo wa QDS kwenye maeneo yaliyo katika Wilaya za Kilwa, Liwale, Nachingwea na Ruangwa; na ramani mbili (2) za jokemia katika Wilaya za Liwale na Ruangwa.

143. Mheshimiwa Spika, Wakala ulifanya kazi za ugani wa jokemia katika maeneo ya Handeni na Kilindi pamoja na kufanya tafiti juu ya upatikanaji wa nishati ya jotoardhi mkoani Mbeya, gesi ya helium mkoani Mara; na madini yanayohimili joto kali (refractory minerals) katika mikoa ya Dodoma na Morogoro. Wakala pia ulikusanya takwimu vituo 8 vya kudumu vya kupimia matetemeko vilivypo Dodoma, Kibaya, Babati, Manyoni, Geita, Mtwara, Mbeya na Longido na vituo vingine 25 vya muda vilivypo katika mikoa ya Mbeya, Njombe na Ruvuma.

144. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha Wakala wa Jiolojia ili uweze kutoa huduma za kisasa za jiosayansi. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali imewezesha Wakala huo kuanzisha maabara mpya ya jioteknoloja (geotechnical laboratory) yenye vifaa mbalimbali vya kutathmini ubora wa udongo, miamba na kokoto kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu.

145. Mheshimiwa Spika, maabara ya Kemiaimeboreshwa kwa kununua vifaa vya kisasa ikiwa ni pamoja na AAS, ICP-OES, XRF na vifaa vya kuratibu uchafuzi wa mazingira. Kazi nyininge zilizofanyika ni kuanzisha mfumo

mpya wa kutunza na kusambaza taarifa na takwimu za upatikanaji wa madini unaotwa Geological and Mineral Information System (GMIS); na mfumo wa kutangaza taarifa kwa njia ya mtandao (web-portal: www.gmis-tanzania.com) ambao ulizinduliwa Mwezi Machi, 2015.

146. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16 Wakala utaendelea kukusanya taarifa za jiosayansi na kuchora ramani kwa ajili ya kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Madini. Aidha, GST itaendelea kufanya utafiti na kukusanya taarifa za jiosayansi katika Wilaya za Songea Vijiji na Ludewa.

147. Mheshimiwa Spika, Wakala pia utaendeleza utafiti wa jotoardhi chini ya Mradi wa Geo-Power Africa unaofadhiwa na Serikali ya Marekani; na utafiti wa upatikanaji wa madini katika Wilaya ya Nachingwea chini ya ufadhili wa Serikali ya Finland. Chini ya ufadhili huo, sampuli za udongo za nchi nzima zitafanyiwa uchunguzi wa kimaabara na ramani za jokemia za nchi nzima zitachorwa. GST pia itaendelea kutoa huduma za ugani kwa wachimbaji wadogo wa madini.

Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania - TMAA

148. Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2014/15, Serikali kupitia Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania iliendelea kufuatilia ulipaji wa kodi ya mapato katika migodi mikubwa. Ukaguzi ulifanywa na TMAA kwa kushirikiana na TRA umewezesha Kampuni ya Geita Gold Mining Limited kulipa kodi ya mapato ya Shilingi bilioni 68.5 katika kipindi cha Julai, 2014 hadi Aprili, 2015. Aidha, Wakala ulifanya ukaguzi kwenye migodi mikubwa na ya kati kuhusu ulipaji wa mrabaha, ushuru wa huduma, ada ya mwaka ya zuio na kufanikiwa kuiwezesha Serikali kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 4.94.

149. Mheshimiwa Spika, Wakala uliendeleza ukaguzi na uhakiki wa madini yaliyozalishwa na kuuzwa na migodi mikubwa ya Bulyanhulu, Buzwagi, Geita, North Mara, New Luika, Mwadui na TanzaniteOne. Ukaguzi huo ulilenga kuiwezesha Serikali kujua kiasi na thamani halisi ya madini yaliyozalishwa na kuuzwa, ambapo mrabaha wa Dola za Marekani milioni 57.3 ulilipa Serikalini kutoka kwenye migodi hiyo katika kipindi cha kuanzia Julai, 2014 hadi Aprili, 2015.

150. Mheshimiwa Spika, pamoja na ukaguzi wa migodi mikubwa na ya kati, Wakala uliendeleza ukaguzi wa kimkakati kwa madini ya ujenzi na ya viwandani. Ukaguzi huo ulifanyika katika Kanda za Kaskazini, Kati, Kusini, Kusini Magharibi, Magharibi, Mashariki, Ziwa Nyasa, Ziwa Viktoria Magharibi

na Ziwa Viktoria Mashariki na kuwezesha mrabaha wa Shilingi bilioni 4.7 kulipwa Serikalini. Makusanyo hayo ni ongezeko la asilimia 173 zilizokusanywa kuanzia Julai, 2014 hadi Aprili, 2015 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 1.72 zilizokusanywa kwa kipindi kama hicho kwa Mwaka 2013/14.

151. Mheshimiwa Spika, Wakala pia uliwezesha mrabaha wa Shilingi bilioni 2.24 kulipwa Serikalini kutoka kwa wazalishaji wanaotumia teknolojia ya "vat leaching" katika Mikoa ya Mwanza, Geita na Mbeya. Kiasi hicho cha mrabaha ni sawa na ongezeko la asilimia 111 ikilinganishwa na mrabaha wa Shilingi bilioni 1.06 zilizolipwa kwa Mwaka 2013/14. Kwa kutumia teknolojia hiyo, jumla ya kilo 1,031 za dhahabu zenye thamani ya Shilingi bilioni 55.92 zilizalishwa kutokana na uhakiki ulofanywa na Wakala.

152. Mheshimiwa Spika, katika juhudzi za kudhibiti biashara haramu na utoroshaji wa madini, Wakala uliendelea kuimarisha Madawati Maalum ya ukaguzi yaliyo kwenye viwanja vya ndege. Kwa kipindi cha Julai, 2014 hadi Aprili, 2015 ukaguzi huo umewezesha kukamatwa kwa watoroshaji wa madini katika matukio 20 yaliyopotiwa katika viwanja hivyo. Matukio hayo yanahusu utoroshaji nje wa madini yenye thamani ya Shilingi milioni 12 na Dola za Marekani 86,722.31.

153. Mheshimiwa Spika, hatua za kisheria zimechukuliwa kwa wahusika kufikishwa mahakamani, kutozwa faini na madini yao kutaifishwa. Aidha, Wakala umefanikiwa kusajili maabarayake katika Shirika la Viwango vya Kimataifa vya ISO/IEC 17025 ili kuweza kutoa huduma za uchunguzi na utambuzi wa sampuli za madini kwa uhakika na kwa viwango vinavyotambulika duniani. Katika Mwaka 2015/16 Wizara itaendelea kuimarisha ukaguzi wa biashara ya madini na kupambana na vitendo vya udanganyifu vinavyoikosesha Serikali mapato.

Shirika la Madini la Taifa - STAMICO

154. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/15, Serikali iliendelea kuiwezesha STAMICO kushiriki katika umiliki wa migodi mikubwa na ya katì. Kwa upande wa Mgodi wa Buckreef uliopo wilayani Geita, STAMICO kwa kushirkiana na TANZAM 2000 wameanza ujenzi wa mitambo ya uchimbaji na uchenjuaji madini pamoja na miundombinu ya mgodi. Aidha, Shirika linaendelea na taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata mbia mpya wa kuendeleza Mgodi wa Dhahabu Buhemba.

155. Mheshimiwa Spika, STAMICO na Kampuni ya TanzaniteOne Mining Ltd, imeendelea kusimamia shughuli za uchimbaji katika Mgodi wa Tanzanite uliopo Merelani wilayani Simanjiro. Uzalishaji wa Tanzanite kwenye mgodi huo unaendelea kuongezeka; na ushiriki wa STAMICO katika kusimamia shughuli za kila siku za mgodi huo umeimarika, ambapo hadi Mwezi Machi, 2015 Shirika limelipwa ada ya usimamizi ya Dola za Marekani 331,660.

156. Mheshimiwa Spika, idadi ya Watanzania walioajiriwa kwenye mgodi huo imeongezeka kutoka 608 Mwezi Mei, 2014 hadi kufikia 1,189 Mwezi Mei, 2015. Aidha, ushirikiano katì ya mgodi huo na Chama cha Wachimbaji Wadogo wa Mkoa wa Manyara (MAREMA) umeimarika, hivyo kusaidia katika utatuzi wa migogoro.

157. Mheshimiwa Spika, pamoja na kusimamia hisa za Serikali katika miradi ya kimkakati iyo echezwa hapo juu, STAMICO iliendelea kutoa huduma za utafiti wa madini na uchorongaji wa miamba kwa wadau. Hadi kufikia Mwezi Mei, 2015 Shirika limefanikiwa kupata zabuni nne (4) za uchorongaji miamba na zabuni tatu (3) za utafiti madini zenye jumla ya thamani ya Dola za Marekani milioni 1.02.

158. Mheshimiwa Spika, Shirika kupitia Kampuni yake tanzu ya STAMIGOLD limeanza uchimbaji wa dhahabu kwenye mgodi wa STAMIGOLD Biharamulo ulikuwa ukijulikana kama Mgodi wa Tulawaka ambaou ulikuwa unamilikiwa na Kampuni ya Pangea Minerals Limited. Hadi Mwezi Mei, 2015 Kampuni ya STAMIGOLD imezalisha wakia 13,099 na kuuza nje wakia 11,613 zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 14.082 na hivyo Shirika linatarajia kupata Shilingi milioni 609.05 kama ada ya usimamizi.

159. Mheshimiwa Spika, Mwezi Julai, 2014 STAMICO ilianza shughuli za ununuzi na uchenjuaji wa madini ya bati (tin ore) katika eneo la Kyerwa mkoani Kagera kuititia Kampuni yake Tanzu ya Kyerwa Tin Company Limited (KTCL). Aidha, Shirika limesaini Mkataba na Kampuni ya Dar Gold DMCC ya Dubai kwa ajili ya kununua madini ya bati. Biashara hii itapunguza utoroshaji wa madini hayo kwenda nchi jirani na kuongezea Serikali mapato.

160. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16 Serikali itaendelea kuiwezesha STAMICO iliweze kusimamia ipasavyo maslahi ya Taifa katika migodi ambayo Serikali ina hisa. Shirika pia litakamilisha uanzishwaji wa Mfumo wa Mtandao wa Uchimbaji Mdogo (Small Scale Mining Portal) ambao utawawezesha wachimbaji wadogo kupata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu bei ya vifaa vya uchimbaji na uchenjuaji pamoja na masoko.

Chuo Cha Madini - MRI

161. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/15 Wizara liiandaa Establishment Order kwa ajili ya kukibadili Chuo cha Madini Dodoma kuwa Polytechnic na kuiwasilisha kwenye mamlaka husika. Vilevile, kufuatia hatua ya Kampuni ya Resolute kuikebadili Serikali eneo liilokuwa chini ya Mgodi wa Golden Pride Mwezi Desemba, 2014 Chuo kimefanikiwa kuanzisha mafunzo katika eneo hilo ambapo jumla ya wanafunzi 240 wanaendelea na mafunzo ya nadharia na vitendo. Mahafali ya kwanza chini ya mfumo wa ngazi ya National Technical Award (NTA) yalifanyika ambapo wanafunzi 368 walihitimu, kati ya hao 68 ni wanawake na 300 ni wanaume.

162. Mheshimiwa Spika, kazi nyiningine zilitofanyika katika Chuo hicho ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa madarasa mawili (2), mfumo wa majitaka na mtandao wa mawasiliano chuoni (Optical Fibre Network). Kutokana na uimarishaji wa miundombinu ya Chuo, udahili wa wanafunzi katika fani mbalimbali umeongezeka kutoka wanafunzi 197 Mwaka 2010/11 hadi kufikia 668 Mwaka 2014/15.

163. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kukiwezesha Chuo kuendesha mafunzo ya nadharia na vitendo kwa wanafunzi katika Kampasi za Dodoma na Nzega. Pia, wanafunzi watapelekwa kwenye baadhi ya migodi mikubwa na ya kati ili kujifunza teknolojia ya uchimbaji wa madini, usimamizi wa mazingira, uchenjuaji wa madini, utafutaji na uvunaji wa mafuta na gesi asilia. Aidha, mafunzo mapya katika ngazi ya Astashahada na Stashahada yataanzishwa katika fani za Mine Surveying, Small Scale Mining na Gemology. Serikali pia itaendelea kukiwezesha Chuo kuanza ujenzi wa jengo la taaluma lenye ofisi 40, ambapo Shilingi bilioni 1.5 zimetengwa.

C. AJIRA NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU

164. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/15, jumla ya watumishi 412 walajiriwa na Wizara ya Nishati na Madini pamoja na Taasisi zake. Kati ya watumishi hao, 108 ni wa Wizara ya Nishati na Madini, 37 GST, 7 REA, 5 STAMICO, 29 TMAA na 226 TPDC. Katika Mwaka 2015/16, Wizara na Taasisi zake inatarajia kuajiri jumla ya watumishi 338 katika kada mbalimbali, kati ya hao, 153 ni wa Wizara; 43 STAMICO; 38 GST; 90 TPDC na 14 REA.

165. Mheshimiwa Spika, Wizara pia liwapandisha vyeo watumishi 139, kuwathibitisha kazini watumishi 30 na kuwabadilisha kazi watumishi 10 katika fani mbalimbali. Katika Mwaka 2015/16, Wizara inatarajia kuwapandisha vyeo watumishi 76 ambao wamepata sifa za kitaaluma na wenye utendaji mzuri wa kazi kulingana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 1999.

166. Mheshimiwa Spika, kuititia Mpango Mkakati wa Mwaka 2011/12 - 2015/16 wa Wizara ya Nishati na Madini, watumishi wameendelea kujengewa uwezo kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yao. Katika Mwaka 2014/15 Wizara liipeleka watumishi 44 katika mafunzo ya muda mfupi na watumishi 30 katika

mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi. Aidha, kutokana na ukuaji wa Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia, Wizara kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo imeendelea kutoa fursa za mafunzo kwa Watanzania katika ngazi za Shahada za Uzamili na Uzamivu. Vilevile, Watanzania 22 walipata ufadhili wa masomo kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China na wengine wawili (2) kupitia Serikali ya Brazil.

167. Mheshimiwa Spika, kupitia Mpango wa Kuendeleza Rasilimali Watu katika Sekta ya Nishati chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia na CIDA, Wizara ya Nishati na Madini iliwezesha mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 47 wa Taasisi za Serikali (4 MEM, 12 NEMC, 2 OSHA, 2 REA, 1 STAMICO, 11 TANESCO, 1 TEITI, 1 TMAA, 8 TPDC na 4 VETA). Hadi kufikia Aprili, 2015 Serikali imetoa ufadhili kwa Watanzania 229, kati ya hao 8 Chuo Kikuu cha Dodoma, Shahada ya Uhandisi wa mafuta na gesi asilia; 40 VETA - Lindi, Ufundis stadi kuhusu uzalishaji wa mafuta na gesi asilia; na 181 Chuo cha Madini Dodoma, Stashahada ya Sayansi ya mafuta na gesi asilia.

168. Mheshimiwa Spika, ili kuwa na uwezo wa kuendesha miradi katika Sekta za Nishati na Madini, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini inatekeleza Mradi wa Capacity Development in Energy Sector and Extractive industries (CADESE) unaofadhiliwa na UNDP. Wadau wengine katika mradi huo ni REA, Uongozi Institute na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

169. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2014/15 mradi umejenga uwezo wa wataalamu 71 wa Wizara, EWURA, TPDC na TANESCO katika maeneo mbalimbali yakiwepo Negotiation Skills katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia, uandishi wa mapendekezo ya miradi, uandaaji wa sera na usimamiaji wa miradi. Katika Mwaka 2015/16 Serikali itaendelea kutekeleza Mradi wa CADESE ili kuwajengea uwezo wataalamu kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Sekta za Nishati na Madini.

170. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini imeendelea kuwahudumia watumishi wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU) na wenyewe Ukimwi waliojitokeza kwa kuwapa lishe na dawa, kwa kuzingatia miongozo husika.

Katika Mwaka 2015/16, Wizara itaendelea kutoa huduma hizo pamoja na elimu mahali pa kazi ili kuzuia maambukizi mapya. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha watumishi kupima afya zao mara kwa mara.

Elimu kwa Umma kuhusu Sekta za Nishati na Madini

171. Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa ikitoa taarifa kuhusu shughuli zake kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo Jarida la Wizara (Newsbulletin) linalotolewa kila wiki. Pia, Wizara imeanzisha utaratibu wa kutumia gari la matangazo kutoa elimu kwa umma katika mikoa mbalimbali kuhusu Sekta za Nishati na Madini. Aidha, Rasimu ya Mkakati wa Mawasiliano kuhusu masuala ya Mafuta na Gesi Asilia imeandaliwa na Mkakati utakamilishwa Mwaka 2015/16 baada ya kupata maoni ya wadau.

D. USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

172. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini inaendelea kushirikiana na wadau katika utekelezaji wa shughuli zake. Kwa niaba ya Serikali napenda kutoa shukrani kwa Serikali za Algeria, Brazil, Canada, Finland, Jamhuri ya Watu wa China, Jamhuri ya Korea, Marekani, Norway, Sweden, Uhlanzi, Ujeruman, Urusi na Uturuki. Pia, natumia fursa hii kutoa shukrani kwa Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Exim ya China, Benki ya BADEA, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Umoja wa Ulaya (EU), pamoja na Taasisi na Mashirika ya AFD (Ufaransa), CIDA (Canada), ECDF (Korea Kusini), FINIDA (Finland), JICA (Japan), NORAD (Norway), OFID (Saudi Arabia), ORIO (Uhlanzi), Sida (Sweden), UNDP, USAID (Marekani) na JBIC (Japan).

E. SHUKRANI

173. Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru Naibu Mawaziri wa Wizara ya Nishati na Madini, Mhe. Charles Muhangwa Kitwanga, Mbunge wa Jimbo la Misungwi, anayesimamia masuala ya Madini; na Mhe. Charles John Mwijage, Mbunge wa Jimbo la Muleba Kaskazini, anayesimamia masuala ya Nishati kwa ushirikiano wao walionipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

174. Mheshimiwa Spika, nawashukuru Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Mhandisi Ngosi C. X. Mwiava kwa ushirikiano anaonipa katika utekelezaji wa shughuli za Wizara. Aidha, nawashukuru Kamishna wa Nishati na Masuala ya Petroli; Kamishna wa Madini; Wakuu wa Idara, Sehemu na Vitengo kwa utendaji wao uliovezesha kupatikana kwa mafanikio mbalimbali katika Wizara ya Nishati na Madini.

175. Mheshimiwa Spika, vilevile, ninatoa shukurani zangu kwa Wenyeviti wa Bodii za Wakurugenzi za TANESCO, TPDC, REA, STAMICO, EWURA, PICL, PUMA, na TIPER; na Wenyeviti wa Bodii za Ushauri za GST, MRI na TMAA pamoja na Mwenyekiti wa Bodii ya Ushauri ya Madini (MAB) kwa ushirikiano wanaonipa katika kuongoza Wizara. Nawashukuru pia Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara; na watumishi wote kwa ujumla kwa utendaji wao mzuri.

176. Mheshimiwa Spika, kwa dharti kabisa naishukuru familia yangu, ndugu, marafiki na wananchi, hususan wa Jimbo langu la Kibakwe kwa imani yao kwangu na ushirikiano wao katika shughuli za maendeleo za jumbe letu.

F. HITIMISHO

177. Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2015/16, imeelekezwa katika maeneo machache yatakayoleta matokeo makubwa. Maeneo yatakayopewa kipaumbele ni: kuongeza kasi ya kuwaunganisha wateja umeme, hususan viijini; kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kwa ajili ya matumizi viwandani, majumbani, kwenye magari na katika kuzalisha umeme; kuimarisha makusanyo ya mapato kutoka Sekta ya Madini; na kuendeleza uchimbaji mdogo wa madini.

178. Mheshimiwa Spika, naomba sasa Bunge lako iidhinishe Bajeti ya jumla ya Shilingi 536,960,436,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini na Taasisi zake kama ifuatavyo:

- (i) Shilingi 365,346,938,000 ni Bajeti ya Maendeleo ambapo Shilingi 280,000,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 85,346,938,000 ni fedha za nje; na
- (ii) Shilingi 171,613,498,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi 137,813,703,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi 33,799,795,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

179. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati, Mheshimiwa Ndassa!

MHE. RICHARD M. NDASSA – MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nikushukuru sana kwa nafasi hii.

Awali ya yote, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kusimama hapa. Naomba kutoa pole nyingi kwa msiba uliotokea wa Mbunge mwenzetu, Mungu ailaze Roho ya Marehemu mahali Pema Peponi; Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu niwashukuru sana Wanasumve kwa kuendelea kuniamini. Nami natoa ahadi kwao kwamba, sitawaangusha.

Naomba vilevile niishukuru sana familia yangu; mama yangu mzazi Mwanang'osha Ng'ombe na mke wangu Grace, kwa kuendelea kunivumilia katika majukumu yangu haya mapya niliyonayo. Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanikisha yote haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Fungu Namba 58 kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Kamati ilikutana katika Vikao vyake na Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa George Simbachawene, akiwa na Manaibu wake wawili; Mheshimiwa Kitwanga na Mheshimiwa Mwijage, Kaimu Injinia Ngosha, ambaye ni Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji Wakuu na Viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara. Pamoja na kutoa ufanuzi palipohitajika katika vikao hivyo, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa zifuatazo; Taarifa ya TANESCO, Taarifa ya REA, Taarifa ya TPDC, Taarifa ya TMAA, STAMICO, Wakala wa Jiolojia na Chuo cha Madini kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa matakwa ya Kanuni 98(1), Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Dar-es-Salaam, Dodoma, Singida, Arusha na Kilimanjaro, kwa lengo la kukagua utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo. Kamati ilikagua Miradi ya Umeme Vijijini (REA), gesi asilia ya kuzalisha umeme wa Kinyerezi megawatt 150 na megawatts 240 na Mradi wa Iringa, Singida, Shinyanga Backbone Transmission wa KV 400. Mradi wa Umeme wa Upopo Singida, Mradi wa Tanzania Energy Development na Access Expansion Project (TEDAP) pamoja na Mradi wa Umeme wa Njiro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha zilizotengwa katika Miradi ya REA. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa, Wizara pamoja na Hazina wanaendelea kutafuta ufumbuzi wa changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo katika maeneo ya umeme, gesi asilia, biashara ya mafuta, utendaji wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, baadhi ya ushauri uliotolewa na Kamati haukizingatiwa na kufanyiwa kazi na Serikali ipasavyo kama ifuatavyo:-

Kubwa zaidi ni Serikali kutochukua hatua za kutosha katika kuhakikisha vinapatikana vyanzo mbadala vya umeme vyenye bei nafuu na rafiki wa mazingira kama vile umeme wa joto ardhi na umeme wa upopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili 2015 kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kilikuwa shilingi 63.8 bilioni, sawa na 52%. Fedha za Ndani za Maendeleo zilizotengwa (Exchequer Release) zilikuwa shilingi bilioni 284, sawa na 43.6% ya bajeti ya ndani. Fedha taslimu za ndani za maendeleo zilipokelewa shilingi bilioni 264.04, sawa na 40% ya bajeti ya fedha za ndani. Aidha, fedha za maendeleo zilizopokelewa zilielekezwa kwénye Miradi mitano mikubwa, yaani BRN. Miradi hiyo ni Mradi wa Kufua Umeme wa Kinyerezi –

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kinyerezi I, Mradi wa Kuongeza Ufanisi wa Shirika la Umeme – TANESCO na Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijiini Awamu ya pili, Mradi wa kuboresha miundombinu katika Wilaya ya Mpanda, Bihamalo na Ngara (ORIO), Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta la Gesi kutoka Mtwara hadi Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefanikiwa kutekeleza majukumu mbalimbali katika Sekta ya Nishati na Madini kama ifuatavyo:-

TANESCO, imesemwa na Mheshimiwa Waziri wa Nishati ni kuunganisha wateja wapya 241,401, ambayo ni 59%, tofauti na wateja 143,113 kwa mwaka wa fedha uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Nishati na Madini Vijijiini; Wilaya 17 zimeunganishiwa huduma ya umeme na kufanya Makao Makuu ya Wilaya zipatazo 120 kati ya Wilaya 130 ambazo ziliikuwa hazina umeme. Vilevile vijiji vipatavyo 3,734 vimeunganishiwa umeme, shule za sekondari 1,445, zahanati na vituo vya afya 898 na hospitali 96 zimepatiwa umeme kupitia REA.

REA Awamu ya Pili; hadi kufikia mwezi Aprili 2015, wateja wapya waliounganishiwa umeme kupitia Mradi huu walifikia 2,629 katika Mikoa ya Singida, Kilimanjaro, Kagera, Simiyu, Katavi na Iringa. Wateja wapya waliounganishiwa umeme vijijiini nchi nzima kuanzia Julai 2014 hadi kufikia 2015 ni 11,286, sawa na 64.33%. Hadi Machi 2015, 36% ya Watanzania wote walikuwa wameunganishiwa umeme Tanzania. Tunaipongeza sana REA pamoja na TANESCO kwa kazi nzuri sana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania limeweza kutekeleza mipango yake ya maendeleo kama ifuatavyo; kubwa ni kukamilisha kwa bomba la gesi ambalo limekamilika kwa 97%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2015 Sekta ya Madini ilipata mafanikio yafuatayo; kubwa ni kukagua jumla ya migodi 1,109 ya madini ambayo ilikaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, STAMICO. Mnamo tarehe 30 Januari 2015, Wizara ya Nishati na Madini iliridhia kampuni ya Sky Associate Group ya Afrika Kusini kununua hisa za Tanzanite One, ambayo nayo ni ya Afrika Kusini kwa 50%. Pamoja na Serikali kulipwa Dola za Kimarekani 331,660, sawa na shilingi 570,456,000,000 kwa wakati huo kama ada ya usimamizi (*Management Fee*), Kamati kupitia Bunge lako Tukufu inaitaka Serikali kutekeleza yafuatayo; moja, kuainisha na kuweka mikakati ya kumaliza migogoro ya muda mrefu kwenye mgodi huo, hilo ndiyo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA), ulibaini upotevu wa kiasi cha Dola za Marekani 100,047.84 na shilingi bilioni 4.97 kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kutokana na kasoro mbalimbali katika ukokotoaji wa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio ya Wizara, Wizara inakabiliwa na changamoto kubwa zifuatazo; moja, changamoto hizo ni pamoja na kutokupatikana fedha kwa wakati hasa kwa Wakala wa REA na TANESCO zile zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fedha za Miradi ya Umeme Vijijiini (REA), zilizopitishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya Mfuko wa Nishati Vijijiini kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 ziliikuwa shilingi bilioni 292.6. Shilingi 271.6 ya fedha hizo ni fedha za vyanzo vya ndani. Shilingi bilioni 21 ni kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Taarifa za REA kiasi cha shilingi bilioni 111.95, sawa na 41% ya kiasi cha fedha kilichopitishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, hadi ninaposoma taarifa hii hakijapokelewa kwenye Mfuko wa Nishati na Madini, ndiyo maana Miradi yetu mingi imesimama. Kiasi cha shilingi bilioni 64.5 kutoka kwenye hiyo bakaa ambazo ni fedha za tozo ya mafuta, mpaka leo hazijapelekwa kwenye Mfuko huu, ndiyo maana Miradi yote imesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hazina imekuwa chanzo kikubwa cha ukwamishaji wa utekelezaji wa Miradi ya REA kwa wakati kwa kushindwa kupeleka fedha za tozo zilizokusanywa kwa mujibu wa Sheria za Bunge lako Tukufu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea Miradi mingi ya REA na kujionea jinsi ambavyo Miradi hiyo imekwama. Wabunge wenywewe ni mashahidi kwenye maeneo yenu, hali ya utekelezaji wa Miradi ya REA ni mbaya na kwa pamoja ninaomba tuibane Serikali ili Miradi hiyo iweze kutekelezwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini - Fungu 58 kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 ni Shilingi bilioni 536.96, ambayo ni pungufu ya asilimia 50.2 ya bajeti ya mwaka 2014/2015. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 365.35, ambayo ni sawa na asilimia 68 ya bajeti yote ya Wizara, zimetengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na Shilingi bilioni 171.61, sawa na asilimia 32 ni Bajeti kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 58, mwaka 2015 fedha za ndani za maendeleo zimepungua kutoka shilingi bilioni 653 hadi shilingi bilioni 280 na fedha za nje zimepungua kutoka shilingi bilioni 304 hadi shilingi bilioni 85. Kamati iliagiza Wizara kufanya maboresho kwenye bajeti ya Miradi ya Maendeleo kipaumbele. Kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 Miradi ya kipaumbele ni ifuatayo: REA, Miradi ya Kinyerezi I, North-East Grid 400kv na Mradi wa Bomba la Gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya nyongeza ya fedha ya shilingi bilioni 586.86 yataifanya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kuongezeka kutoka shilingi bilioni 536.96 hadi kufika shilingi bilioni 923.84. Tunaomba ongezeko hilo kwa mambo makubwa mawili. Moja, kutokurudisha nyuma juhudhi za Serikali za usambazaji wa umeme vijijini; na pili, upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa kujenga mitambo na njia za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naomba niweke angalizo; kama mambo haya hayatakelezwa, hadi kufikia Juni 2015, uwezo wa kufua umeme kwa mitambo iliyopo katika mfumo wa Gridi ya Taifa umepungua kutoka megawatts 1226.24 hadi kufikia megawatts 943.5 za umeme kutokana na upungufu wa vina vya maji katika mabwawa. Hali hii ni hatari sana kwani mahitaji ya umeme nchi nzima ni megawatts 934.64, ambapo kwa sasa tuna ziada ya megawatts 8.86 ya kiasi cha umeme ambacho kinahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo ziada ya megawatts 8.6 na hali ya Bwawa la Mtera kwa sasa siyo nzuri hata kidogo. Kamati inaomba kupitia Bunge lako Tukufu, liitake Serikali ione umuhimu na ilazimike kuongeza fedha za Miradi ya Kimkakati ili mradi hiyo ya kipaumbele iweze kutekelezwa ndani ya wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto zilizojitokeza katika Taasisi pamoja na Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

Moja, tozo ya umeme iongezwe kutoka asilimia tatu kwenda asilimia tano, lakini pia tozo ya mafuta iongezwe kutoka shilingi hamsini kwenda shilingi mia moja ya lita ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za REA zinazokusanya kutoka kwenye tozo ziwasilishwe moja kwa moja kwenye Mfuko wa Nishati tofauti na utaratibu wa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kuishauri Serikali ikamilishe miundombinu ya bomba la gesi ili TANESCO iachane na kukodisha mitambo yenyе kutumia mafuta ya makampuni, hatua ambayo itaipelekea TANESCO kujarendesha kwa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, naomba taarifa yangu yote iingie kwenye Hansard.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote leo tuibane Serikali ili itoe fedha zote za Mfuko wa Nishati Vijijiini zikakwamue Miradi iliyokwama. Vinginevyo, tutabaki na nguzo na nyaya kwa sababu hivi sasa wakandarasi hawana fedha. Kwa hiyo, niliombe sana Bunge lako tuibane Serikali iweze kutoa fedha hizo haraka iwezekanavyo. Aidha, Serikali iachane na tabia ya kuwa...

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuliongoza Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano walionipa wakati wa kujadili na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya fedha za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 katika utumishi wangu kama Mwenyekiti wa Kamati. Naomba majina ya Wajumbe wenzangu yaingizwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Kashililah.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi kwa Fungu Namba 58 kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, ambayo ni shilingi bilioni 536.96 na mapendekezo ya nyongeza kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naunga mkono hoja. (Makof)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA

**MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA NISHATI NA MADINI KWA MWAKA
WA FEDHA WA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117(11), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na kuitia Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, katika vikao hivyo Waziri wa Nishati na Madini Mhe. George Simbachawene, (Mb) akiwa na Manaibu wake Mhe. Charles N. Kitwanga, (Mb) na Mhe. Charles Mwijage, (Mb), Kaimu Katibu Mkuu Eng. Ngosi X. Mwihana pamoja na Watendaji wakuu na viongozi wa taasisi zilizo chini ya Wizara walifika mbele ya Kamati kwa ajili ya uwasilishaji wa Taarifa pamoja na kutoa ufanuzi pale palipohitajika.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na majukumu ya Wizara, Mheshimiwa Waziri alieleza **Dira na Dhima** ya Wizara na masuala yaliyotekelawa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na maombi ya fedha kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Katika vikao hivyo, Kamati ilipokea na kujadili taarifa zifuatazo:-

- i. Taarifa ya hali ya fedha na utekelezaji wa Shirika la Umeme (TANESCO), Wakala wa Umeme Vijiji (REA) pamoja na hali ya upatikanaji wa Fedha za mfuko wa Nishati vijiji (REF) kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kwa kubainisha mafanikio na changamoto zake.
- ii. Taarifa ya hali ya fedha na utekelezaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.
- iii. Taarifa ya hali ya fedha na utekelezaji wa bajeti za Taasisi nyingine chini ya Wizara ambazo ni **TMAA, STAMICO, WAKALA WA JILOJIA (GST), CHUO CHA MADINI (MRI)**, kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.
- iv. Taarifa ya utekelezaji wa malengo ya Bajeti **Fungu 58** kwa Mwaka wa Fedha 2014/15.
- v. Randama ya Wizara ya Nishati na Madini (**Fungu 58**) kuhusu makadirio ya mapato, matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa Mwaka 2015/16.

1.1 Yaliyojitokeza kwenye Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Nishati na Madini ilitekeleza matakwa ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Aprili, 2013 kwa kufanya ziara katika Mikoa ya Dar Es salaam, Dodoma, Singida, Arusha na Kilimanjaro kwa lengo la kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ilio chini ya Wizara ya Nishati na Madini iliyotengewa fedha kwa Mwaka 2014/2015. Kamati ilikagua miradi ya Umeme Vijiji-(REA), Miradi ya Gesi asilia ya Kuzalisha umeme ya Kinyerezi ya MW 150 na MW 240, Miradi wa **Iringa-Singida/Shinyanga Backbone Transmission (BTIP) wa kv 400**, Miradi wa umeme wa upepo Singida, Miradi wa **Tanzania Energy Development and Access Project (TEDAP)** pamoja na Miradi wa umeme wa **NJIRO**.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha zilizotengwa hasa katika miradi ya REA. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa Wizara pamoja na Hazina wanaendelea kutafuta ufumbuzi wa changamoto hiyo.

2.0 UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2014/2015

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo katika maeneo ya **umeme, gesi asilia, biashara**

ya mafuta, utendaji wa Wizara na taasisi chini ya Wizara. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa baadhi ya Ushauri uliotolewa na Kamati haukuzingatiwa na kufanyiwa kazi na Serikali ipasavyo kama ifuatavyo:-

(i) Tatizo la upatikanaji wa vibali vya kuajiri kwa Taasisi za Wizara ya Nishati na Madini, bado kuna tatizo la kukaimisha watendaji wasaidizi kwa muda mrefu bila kuwapatia mamlaka kamili ya kiutendaji. Tatizo hili lipo STAMICO na Chuo cha Madini. Hali hii inaendelea kukwamisha utekelezaji bora wa mipango ya maendeleo.

(ii) Serikali haijachukua hatua za kutosha katika kuhakikisha kunapatikana vyanzo mbadala vya Umeme wenye bei nafuu na rafiki wa mazingira kama vile Umeme wa Joto ardhi na Umeme wa Upopo. Kwa kushindwa kufanya maamuzi stahiki kwa wakati upo uwezekano wa nchi kukumbwa na tatizo la mgao wa umeme hasa ikizingatiwa kuwa vyanzo vingine kama maji havina uwezo wa kutosha na gesi bado miradi yake haujakamilika,na

(iii) Kamati haikuridhishwa na kasi ya EWURA katika kuwasimamia wajenzi na wamiliki wa vituo vya mafuta hasa katika maeneo ya vijijini.

2.1 Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015;

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 Wizara ya Nishati na Madini iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,077,692,347,000/=** kati ya fedha hizo **Shilingi 957,177,170,000/=** sawa na **asilimia 88.8** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo **shilingi 652,805,000,000** sawa na **asilimia 68.2** ya fedha za maendeleo ziliikuwa fedha za ndani na **Shilingi 304,372,170,000** sawa na **asilimia 31.8** ya bajeti ya maendeleo ni fedha za nje. Bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ilikuwa **Shilingi 125,378,452,000** sawa na **asilimia 11.2** ya bajeti yote ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2015, kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kilikuwa ni **Shilingi 63,834,069,098.31** sawa na **asilimia 52.97 tu.**

Kwa upande wa miradi ya maendeleo, kiasi cha fedha za ndani kilichotolewa (Exchequer Release) ni **Shilingi 284,526,000,000** sawa na **asilimia 43.6** ya bajeti ya fedha za ndani. Hata hivyo, fedha halisi/taslimu za ndani za maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi 264,035,000,000** sawa na **asilimia 40.4** ya bajeti ya fedha ya ndani. Fedha za nje zilizopokelewa ni jumla ya **Shilingi 7,530,621,842** sawa na **asilimia 2.47** ya bajeti ya fedha za nje. Fedha za nje zilizopokelewa ziliikuwa ni kwa ajili ya mradi wa kuongeza ufanisi wa Shirika la Umeme-TANESCO(Transfers to TANESCO).

Mheshimiwa Spika, jedwali **namba 1** linafafanua zaidi mchanganuo wa kibajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kama ifuatavyo:-

Jedwali Na.1

Bajeti Iliyopitishwa 2014/2015 (TZS)	Fedha ya maendeleo Iliyotengwa 2014/2015 (TZS)	Asilimia %	Fedha iliyotolewa hadi Aprili, 2015 (TZS)	Asilimia %
Triliioni 1.08	Bilioni 957.18	88.8%	Bilioni 271.57	28.4%
	Fedha ya matumizi ya kawaida iliyo tengwa 2014/2015 (TZS)	Asilimia %	Fedha iliyotolewa hadi Aprili, 2015	Asilimia %
	Bilioni 125.38	11.2%	Bilioni 63.80	52.97%

Aidha, fedha za maendeleo zilizopokelewa zimeelekezwa kwenye miradi mitano (5) chini ya mfumo wa Tekeleza sasa kwa Matokeo Makubwa(BRN) ambayo ni:-

- i) **Mradi wa kufua Umeme wa Kinyerezi 1(MW 150),**
- ii) **Mradi wa kuongeza ufanisi wa Shirika la Umeme-TANESCO,**
- iii) **Mradi wa kupeleka Umeme Vijijini awamu ya Pili**
- v) **Mradi wa kuboresha miundombinu katika Wilaya za Biharamulo, Mpanda na Ngara-Orio,**
- v) **Mradi wa ujenzi wa Bomba la kusafirisha gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam.**

Aidha, Wizara imeendelea kutekeleza miradi mingine ambayo haipo chini ya mfumo wa BRN kwa fedha za ndani na za Wafadhili.

2.2 MAFANIKIO

Mheshimiwa Spika,Wizara imefanikiwa kutekeleza majukumu mbalimbali katika Sekta za Nishati na Madini kama ifuatavyo:

2.2.1 SEKTA YA NISHATI

a) Shirika la Umeme TANESCO

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa fedha 2014/2015 Shirika limefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

- Kupunguzwa kwa mgawo wa umeme.
- Kuunganisha wateja wapya ambapo hadi kufikia machi, 2015 TANESCO ilikuwa imeunganisha wateja wapya **241,401** sawa na ongezeko la **asilimia 59.3** ikilinganishwa na wateja **143,113** waliounganishwa kwa mwaka 2013/2014.
- Mapato ya makusanyo yameongezeka kutoka **Shilingi Bilioni 735.4** kwa Mwaka 2011 hadi **Shilingi Triliioni 1.13** kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015,na

- Kutekeleza mradi wa **Kinyerezi-1 MW150** wa kuzalisha gesi asilia kufikia **asilimia 84**.
- Serikali imesaini mkataba wa kutekeleza mradi wa kufufua Umeme kutoka mto **Rusumo** utakaozalisha **MW 80** ili kuyapatia umeme wa uhakika maeneo ya Mikoa ya Kagera na Kigoma yaliyo nje ya gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya yametokana na kupungua kwa upotevu wa umeme katika miundombinu, ongezeko la matumizi ya LUKU, na ongezeko la bei za umeme na kasi ya kukusanya mapato. Hata hivyo ,mapato ya Shirika bado siyo yakuridhisha sana kutokana na taasisi za Serikali kushindwa kulipa ankara zao za matumizi ya umeme kwa wakati.

b) Wakala wa Nishati Vijijini-REA

i. **REA awamu ya kwanza:**

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa REA awamu ya kwanza umewezesha **Wilaya 17** kuunganishiwa huduma za umeme na kufanya makao makuu ya Wilaya zilizopata umeme **kufikia 120** kati ya **Wilaya 133** zilizopo. Aidha, maeneo mbalimbali ya uzalishaji mali na huduma za jamii na **vijiji vipatavyo 3,734** yameunganishiwa umeme. Jumla ya Shule za **Sekondari 1,845**, zahanati na **vituo vya afya 898** na **hospiteli 96** zimepatiwa umeme wa REA.

ii. **REA awamu ya Pili:**

Mheshimiwa Spika, REA awamu ya pili ni mradi wa kusambaza umeme vijijini ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2015 Wateja wapya waliouanganishiwa umeme kupitia mradi huu walifikia **2,629** katika mikoa ya **Singida, Kilimanjaro, Kagera, Simiyu, Arusha, Katavi na Iringa**. Aidha, idadi ya wateja wapya waliouanganishiwa umeme vijijini nchi nzima kuanzia Julai 2014 hadi Aprili, 2015 waliongezeka kufikia **11,286** ambalo ni ongezeko la **asilimia 64.33** ikilinganishwa na idadi iliyouanganishwa Mwaka 2013/2014.

Kupungua kwa gharama za kuunganishiwa Umeme: Mheshimiwa Spika, Serikali imepunguza gharama kutoka **shilingi 455,108/=** hadi **Shilingi 177,000/=** wanaouanganishwa kwa miradi ya **REA** na kwa maeneo ya mijini gharama zimepunguzwa kutoka **Shilingi 455,108/=** hadi **Shilingi 320,960/=** kwa Wateja wa Single phase na kwa umbali usiozidi mita 30 bila mahitaji ya nguzo.

Mheshimiwa Spika, kwa hatua hiyo ya utekelezaji hadi Machi, 2015 **asilimia 36** ya Watanzania wote wameunganishiwa umeme.

c) Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania-TPDC

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 TPDC ilitengewa **Shilingi bilioni 164,811,600,000** ambapo **Shilingi bilioni 138.0** zilitengwa kwa ajili ya maendeleo.

Hadi kufikia Machi, 2015 kiasi cha **Shilingi bilioni 123.6** sawa **asilimia 75** ya bajeti yote ilikuwa imepokelewa na TPDC. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, fedha ya maendeleo ilikuwa **Shilingi bilioni 61.32** sawa na **asilimia 44.43 tu** ya bajeti ya maendeleo kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Shirika liliweza kutekeleza mipango yake ya maendeleo kama ifuatavyo:-

- Kutekeleza mradi wa ujenzi wa bomba la kusafirisha Gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar Es Salaam na mradi huo umekamilika **kwa asilimia 97**, pia maendeleo ya ujenzi wa mitambo ya

kusafisha gesi yamekamilika kwa **asilimia 93.81**. Mradi wote unatarajiwa kukabidhiwa kwa TPDC ifikapo Novemba, 2015.

- Kuongeza ugunduzi wa gesi asilia nchini ambapo hadi mwezi Aprili, 2015 jumla ya futi za ujazo **Trillioni (TFC) 55.08** zilikuwa zimegunduliwa.
- Kuandaa Sera ya ushiriki wa Watanzania kwenye raslimali za mafuta na gesi asilia (Local Content Policy) na Rasimu ya Sheria ya Gesi asilia na Petroli 2015.
- Kuanzisha kampuni tanzu chini ya TPDC ambazo ni: **GASCO** yenyeye wajibu wa kusimamia shughuli za uendeshaji wa miundombinu mipy ya gesi asilia inayojengwa na Serikali na kampuni ya **PETROTAN** yenyeye jukumu la kusimamia shughuli za hifadhi ya mafuta (SPR) pamoja na uuzaji mafuta.

2.2.2 SEKTA YA MADINI

Mhesimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015 serikali ilipata mafanikio yafuatayo:-

- Kwa kipindi cha mwezi Julai, 2014 hadi Machi, 2015 jumla ya leseni 3,449 zilitolewa kwa wachimbaji wa madini ya aina mbalimbali. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini imeanzisha Ofisi mbili za Kanda ya ziwa nyasa (Songea) na kanda ya ziwa (Tarime).
- Kuwezesha wachimbaji wadogo kwa kutenga **Shilingi Bilioni 2.3** kwa ajili ya mikopo ya Wachimbaji Wadogo. Kamati inashauri fedha hizo ambazo hazijatolewa zitolewe kabla ya Julai, 2015.
- Kukamilika kwa Rasimu ya Sheria ya Kusimamia shughuli za Mpango wa Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Tasnia ya Uziduaji (TEITI)
- Kwa Mwaka wa fedha 2014/2015 jumla ya **migodi 1,109** ya madini imekaguliwa ambapo mgodi wa dhahabu wa **Golden Pride** wilayani Nzega na miundo mbinu yake kwa Chuo cha Madini Dodoma mwezi Desemba, 2014.

(a) Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

Mhesimiwa Spika, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya shirika la STAMICO kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 ilikuwa ni Shilingi bilioni **20,841,937,586**. Shilingi bilioni **11,506,720,000** ya bajeti hiyo zilitakiwa kutolewa na Serikali kama ruzuku na shilingi bilioni **9,335, 217,586** ya bajeti ni kutokana na vyanzo vya ndani vya Shirika.

Mhesimiwa Spika, hadi machi, 2015 Shirika lilikuwa limepokea Shilingi bilioni **5,582,556,233** sawa na asilimia 26.9 ya bajeti yote.

Mhesimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) lina leseni 50 za utafutaji na uchimbaji wa madini nchini. Kati ya leseni hizo, kumi na nne(14) zipo kwenye ubia (Buckreef 13 na TML 1), kumi na moja (11) zipo kwenye kampuni tanzu ya STAMIGOLD inayomilikiwa na STAMICO kwa 100%. Aidha, shirika linaendelea kukamilisha tafiti mbalimbali katika Wilaya mbalimbali nchini.

Mhesimiwa Spika, STAMICO imeongeza mapato yake kutoka **Shilingi Milioni 281** kwa Mwaka 2013/2014 hadi **Shilingi bilioni 1.7** kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mhesimiwa Spika, STAMICO imeanza uzalishaji wa dhahabu kupitia kampuni tanzu ya **STAMIGOLD Biharamulo Mine**.

Mheshimiwa Spika, STAMICO inamiliki mgogi wa makaa yam awe Kiwira ambapo katika mgodi huo wafanyakazi wapatao **1682** wanaidai Serikali mapunjo ya mishahara kabla ya kubin afsishwa kuwa mgodi wa kampuni ya **TANPOWER RESOURCE**. Mwaka 2008 Serikali ilimwagiza CAG kwenda kufanya ukaguzi ili kujiridhisha na madai hayo ya mapunjo ya stahili zao. Mbali na Serikali kumtuma CAG hadi leo hakuna taarifa ye yote ya kuwa madai yao ni halali au siyo halali.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako tukufu kwa niaba ya wafanyakazi hao tunaomba kupata majibu ya madai yao kama yalikuwa halali au siyo halali.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 30 Januari, 2015 Wizara ya Nishati na Madini ililiridhia Kampuni ya **Sky Associates Group Ltd** ya Afrika ya Kusini kununua hisa za **Tanzanite One (SA) Proprietary Ltd** ya Afrika ya Kusini na hivyo kumiliki asilimia 50 ya mgodi wa Tanzanite kwa ubia na STAMICO.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kulipwa **Dola za Marekani 331,660.20** sawa na **shilingi Bilioni 570.456** kama ada ya usimamizi (Management fees), Kamati kupitia Bunge lako tukufu inaitaka Serikali kutekeleza yafuatayo:-

- Kuainisha na kuweka mikakati ya kumaliza migogoro ya muda mrefu kwenye mgodi huo,
- Kuainisha maslai ya Wachimbaji wadogo na wafanyakazi kwenye mgodi kwa kuwapatia haki zao na kuzilinda,
- Kuainisha malipo stahiki ya Serikali kwa mujibu wa Sheria na kuhakikisha zimelipwa kwa wakati, na
- Kuimarisha ulinzi, usalama wa watu na raslimali zao kwenye mgodi na eneo lote la Mererani.

(b) Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA)

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Julai 2014 hadi Machi, 2015 Wakala ulitekeleza vizuri majukumu yake kwa kukagua ulipaji kodi katika Makampuni mbalimbali. Wakala ulibaini na kutekeleza mambo yafuatayo:

- Kukamata watoroshaji wa Madini katika **matukio 17** kupitia madawati yaliyopo katika viawanja vya ndege ambapo madini yenye thamani ya **Shilingi milioni 135** yalikamatwa, na
- Kubaini upotevu wa fedha kiasi cha **Dola za Marekani 147.87** na **Shilingi bilioni 4.97** kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kuto kana na kasoro mbalimbali katika ukokotoaji wa kodi za madini.

Mheshimiwa Spika, kamati haikuridhishwa na mchango wa sekta ya madini katika pato la Taifa. Serikali iongeze usimamizi ili pato liendane na madini yanayozalishwa. Hapa uwazi na ukweli katika sekta hii haupo.

(c) Chuo cha Madini (MRI)

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Madini kilitengewa jumla ya **Shilingi Bilioni 7.8** kwa Mwaka wa fedha 2014/2015. **Shilingi billioni 3.2** zilitengwa kwa ajili ya maendeleo na **Shilingi billioni 4.6** zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, hadi nawasilisha taarifa hii Chuo kilikuwa kimepokea **shilingi billioni 2.25** kwa matumizi ya kawaida na hakuna fedha yoyote ya maendeleo imetolewa .Kiasi hicho kilichotolewa ni sawa na **asilimia 28.85** ya bajeti yote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukosefu wa fedha za kutosha, Kamati imeridhishwa na utendaji wa Chuo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, kwakuweza kudahili **wanafunzi 668** katika fani mbalimbali na kuendelea kuboresha miundombinu ya mazingira ya kitaaluma.

(d) Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST)

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Wakala uliidhinishwa jumla ya **Shilingi billioni 8,033,482,000**. **Shilingi Bilioni 7,033,482,000** zilikuwa fedha za matumizi ya kawaida, na **shilingi billioni 1.0** zilikuwa fedha za maendeleo. Hadi Aprili, 2015 Wakala ulikuwa umepokea **shilingi billioni 1.6** kwa matumizi ya kawaida na kwa upande wa fedha za maendeleo wakala haujapkea fedha yoyote isipokuwa **Shilingi milioni 125.5** zilizokusanywa kwenye maduhuli.

2.4 Changamoto zilizokwamisha utekelezaji wa Bajeti Mwaka wa Fedha 2014/2015

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio, Wizara imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali katika Sekta ya Nishati na Madini wakati wa utekelezaji wa bajeti yake kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Changamoto hizo ni pamoja na kutopatikana kwa wakati fedha za miradi ya **REA** na **TANESCO** zilizo idhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, fedha za miradi ya umeme vijijini-**REA** zilizopitishwa na Bunge lako tukufu kwa ajili ya Mfuko wa Nishati Vijijini kwa Mwaka 2014/2015 zilikuwa **Shilingi Bilioni 292.6**. **Shilingi Bilioni 271.6** kutoka kwenye bajeti ya Serikali na vyanzo vya ndani, **shilingi Bilioni 21.0** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa mujibu wa taarifa ya REA , kiasi cha **shilingi Bilioni 111.95** sawa na **asilimia 41** ya kiasi cha fedha kilichopitishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015,hadi ninaposoma taarifa hii hakijapelekwa kwenye **Mfuko wa Nishati Vijijini – REF.**

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa **kifungu 32** cha sheria ya Mafuta ya Mwaka 2008 Waziri wa Nishati na Madini kwa kushauriana na Waziri Wa Fedha, walianzisha Tozo ya **shilingi 50** kwa lita ya mafuta ya Petroli kwa ajili ya Mfuko wa Nishati Vijijini, pia sehemu ya **Customs processing Fees(0.4%)** ilielekezwa kwenye Mfuko wa Nishati Vijijini. Hata hivyo, bado kuna bakaa ya kiasi cha **Shilingi Bilioni 52.75** ambayo ni tozo ya mafuta na **Shilingi Bilioni 12.0** ambayo ni tozo ya Customs Processing Fee ambazo jumla yake ni **Shilingi Bilioni 64.75** zilizokusanywa nazo hazijawasilishwa REA. Kwa ufanuzi zaidi wa mchanganuo wa kibajeti kuhusu fedha za REA ni kama ilivyofafanuliwa kwenye **jedwali na.2** lifuatalo:-

Jedwali na.2

BAJETI ILIOPIISHWA 2014/2015	KIASI KILICHO TOLEWA	KIASI KILICHO BAKI	ASILIMIA ILIOBAKI
Bilioni 292.6	Bilioni 159.65	Bilioni 111.95	41%
TOZO YA MAFUTA ILIOKUSANYWA (2013-March,2015)	ILIO TOLEWA	ILIO BAKI	ASILIMIA ILIO BAKI
Bilioni 218.1	Bilioni 165.34	52.75	24%
TOZO YA CUSTOMS PROCESSING FEES	ILIO TOLEWA	ILIO BAKI	ASILIMIA ILIO BAKI
Bilioni 24.2	Bilioni 12.2	Bilioni 12.0	49.6%

Mheshimiwa Spika, Hazina imekuwa chanzo kikubwa cha ukwamishaji wa utekelezaji wa miradi ya REA kwa wakati kutokana na kushindwa kupeleka REA fedha za tozo zilizokusanywa kwa mujibu wa sheria za Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, kutokupelekwa kwa fedha za REA kwa wakati kumesababisha miradi mingi ya umeme vijijini inayotekelwa na REA kuchelewa kukamilika. Wakandarasi kwenye maeneo mengi wamesimamisha kazi na kuchelewesha kukamilika kwa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea miradi mingi ya REA na kujionea jinsi ambavyo miradi hiyo imekwama, na Wabunge mmejionea kwenye maeneo yenu hali ya utekelezaji wa miradi ya REA ni mbaya. Kwa pamoja tuibane serikali ipeleke fedha kwenye miradi hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Muungano na taasisi zake pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeshindwa kulipa madeni ya TANESCO kwa wakati. Hadi kufikia Aprili, 2015 TANESCO inawadai wateja wake **Shilingi Bilioni 332.5** ambapo **Shilingi Bilioni 216.63** ni deni la taasisi mbalimbali za Serikali na **Shilingi Bilioni 115.84** kwa wateja binafsi.

Mheshimiwa Spika, hazina wamekuwa wakisurasua kuridhia mikataba yakuzalisha umeme mbadala kama vile Geo-wind (Umeme wa upopo) hata kama taratibu zmekamilika.

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kwa ufunguzi wa mradi wa bomba la gesi na kupatikana kwa gesi kwa wakati ambapo pamoja na sababu nyingine za kiutaalam, tishio la uharibifu wa miundombinu ya bomba la gesi huko Mnazibay-Mtware kutokana na kumommonyoka kwa kingo za Bahari uliosababishwa na kimbunga, ni changamoto kubwa iliyoikabili serikali na imechelewesha kwa kiasi kikubwa maendeleo ya sekta ndogo ya gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa mpango mkakati wa ujenzi wa mabomba ya kusafirisha mafuta kutoka Dar Es salaam kwenda Mikoani ili kupunguza gharama za bei ya mafuta, kulinda miundo mbinu ya barabara pamoja na kupunguza msongamano wa magari ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, chanagamoto nyingine ni kutokuwepo udhibiti wa kutosha kwa mafuta yanayosafirishwa nje ya nchi (*On transit*) kupitia Bandari ya Dar es Salaam hali inayopelekea kupoteza mapato ya Serikali kwani mafuta hayo hurejeshwa nchini kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Spika, wizara kutosimamia mafuta yanayosafirishwa nje (*transit*) kwa kuiachia TRA kuyahalalisha (*Localization*) bila Wizara kujua.

Mheshimiwa Spika, kutokuwa na mpango wa kuweka Uzio na mfumo wa ulinzi endelevu kuzunguka mgodi wa Tanzanite kumeongeza utoroshwaji wa Madini ya Tanzanite nje ya nchi na hivyo kuendelea kupoteza mapato ya Serikali kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kamati inaendelea kuishauri serikaliitekeleze mara moja kanuni zivu za eneo la Mererani za mwaka 2001 (**The mining Mererani controlled area regulatory, 2001**). Kanuni hizi zinaitaka Serikali iweke uzio kuzunguka eneo lote la Mererani, imetambua na kuwapa vitambulisho wakazi na wachimbaji wa Mererani, kuweka utawala unaojitegemea na kuyatambua na kuyapa thamani madini yote yanayotoka katika mgodi huo (**Mwarobaini**).

Mheshimiwa Spika, hali ya muundo wa Shirika la Mandeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) katika masuala ya kiutawala na ukosefu wa fedha za kutosha siyo nzuri. Hali hii inalikwamisha shirika kuijendesha lenyewe ili kuhimili ushindani kwenye sekta ya gesi na mafuta ndani na nje ya nchi. Kamati inaitaka wizara itafakari upya na kulitafutia ufumbuzi suala la watumishi (wataalam) waliohamishwa kutoka TPDC ili kuondoa manunguniko yanayoendelea hivi sasa.

3.0 UCHAMBUZI, MAOMBI YA FEDHA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI NA MADINI (FUNGU 58) KWA MWAKA WA FEDHA WA 2015/2016

Mheshimiwa Spika, Kamati kwa pamoja imepitia **Fungu 58** kifungu kwa kifungu, kwa kujadili, kuchambua, kuhoji na hatimaye kupitisha bajeti ya Wizara kama ilivyopendekezwa. Mapendeleko ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini **Fungu 58** kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ni **Shilingi Bilioni 536.96** ambayo ni **pungufu ya asilimia 50.2** ya bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015. Kati ya fedha hizo **shilingi Bilioni 365.35** ambayo ni sawa na **asilimia 68** ya bajeti yote ya Wizara zimetengwa kwa ajili ya Miradi ya maendeleo na **Shilingi Bilioni 171.61** sawa na **asilimia 32** ya Bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, ikilinganishwa na Mwaka 2014/2015, fedha za ndani za maendeleo zimepungua kutoka **shilingi bilioni 653** hadi **shilingi bilioni 280**, na fedha za nje zimepungua kutoka **shilingi bilioni 304** hadi **shilingi bilioni 85**.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2014/2015 fedha za maendeleo za **fungu 58** katika Wizara 10 ilikuwa ni kipaumbele namba moja, katika bajeti hii ni **kipaumbele namba 6**. Vivyo hivyo kwa fedha za nje sekta ya nishati na madini Mwaka 2014/2015 ilipewa **kipaumbele namba moja** lakini Mwaka 2015/2016 imepewa **kipaumbele namba 7**.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa uchambuzi wa bajeti na kwa mujibu wa maelezo ya Wizara kunahitajika fedha za nyongeza kwenye bajeti ya miradi ya maendeleo kutoka kiasi cha **Shilingi Bilioni 365** kinachopendekezwa hadi kufikia **Shilingi Bilioni 663.6** ambacho kitasaidia kulipa gharama za miradi inayoendelea kutekelezwa na kuikamilisha ndani ya wakati. Ukokotoaji wa jumla ya fedha zinazoombwa kuongezwa kwenye miradi ya vipaumbele ni kama ifuatavyo:-

Jedwali na.3

No.	Jina la Mradi	Bajeti Iliyotengwa Mwaka 2015/2016 (Sh.Bilion ni)	Fedha zinazoombwa kuongezwa (Sh.Bilion ni)	Jumla (Sh.Bilion ni)
01	Miradi ya umeme vijiji REA	250	290	540
02	Ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia kwa ajili ya mitambo ya kuzalisha umeme	25	10	35
03	Njia ya kusafirisha Kv400U meme - Dar - Tanga - Arusha (North/East Grid)	1.74	86.86	88.6
JUMLA		276.74	386.86	663.6

Mheshimiwa Spika, maombi ya nyongeza ya **Shilingi Bilioni 386.86**, yataifanya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kuongezeka kutoka **Shilingi 536, 960, 436,000** hadi Shilingi **923, 820, 436,000**. Kati ya Bajeti hiyo ya Wizara, **Shilingi Bilioni 752, 206, 938,000** ni fedha za maendeleo ambazo ni sawa na **asilimia 81.42** ya bajeti yote, ambapo **shilingi 666, 860,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 85, 346, 938,000** ni fedha za nje. Matumizi ya kawaida ni **Shilingi 171,613,498,000** ambayo ni sawa na **asilimia 18.58** ya bajeti yote .

Mheshimiwa Spika, Fedha za ziada zinazoombwa na Wizara ni kwa sababu kuu mbili:-

- kutokurudisha nyuma juhudzi za Serikali za usambazaji umeme vijiji, na
- upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa kujenga mitambo na njia za umeme.

Mheshimiwa Spika, hadi Juni, 2015 uwezo wa kufua umeme kwa mitambo iliyopo katika mfumo wa gridi ya Taifa umepungua kutoka **MW 1,226.24** hadi **MW 943.5** za umeme kutokana na kupungua kwa vina vya maji katika mabwawa.Hali hii ni hatari kwani mahitaji ya umeme nchini ni **MW 934.64, ambayo ni ziada ya MW 8.86 ya kiasi cha umeme kinachohitajika nchini. Kiasi hiki ni kidogo sana hasa ukilinganisha na ongezeko la wateja wapya wa umeme wa REA.**

Mheshimiwa Spika, kamati inaomba kuititia Bunge lako tukufu liitake Serikali ione umuhimu na ilazimike kuongeza fedha kwa miradi ya kimkakati ili miradi hiyo ya vipaumbele iweze kutekelezwa ndani ya wakati kama ilivyooneshwaa kwenye **jedwali na 3**. Miradi hiyo ni:-

- REA,
- Miradi ya Kinyerezi One,
- North-East Grid 400kv,
- Mradi wa Bomba la Gesi

3.1 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kutokana na changamoto zilizojitokeza katika taasisi pamoja na Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

3.1.1 Utendaji wa Taasisi za Wizara na Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, taasisi na mashirika yatengewe fedha za kutosha ili yaweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo, fedha zitolewe kwa wakati na zitolewe zote kama zitakavyo idhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, tozo ya Umeme iongezwe kutoka **asilimia 3** ya sasa hadi **asilimia 5** kiwango cha juu kilichoainishwa kwenye Sheria ya Nishati Vijijini, lakini pia tozo ya mafuta iongezwe kutoka **Shilingi 50** hadi kufikia kiasi cha **Shilingi 100** kwa lita ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, fedha za REA zinazokusanywa kutoka kwenye tozo ziwasilishwe moja kwa moja kwenye Mfuko wa Nishati Vijijini tofauti na utaratibu wa sasa wa kuzipeleka Hazina ambako zinacheleweshwa kupelekwa REA na kukwamisha utekelezaji haraka wa miradi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kutoa kipaumbele kutafuta fedha kugharimia miradi ilivoainishwa katika mpango wa matokeo makubwa sasa (BRN) ili kuondokana na upungufu wa Umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, TANESCO iweke mpango maalum wa muda mfupi, kati na wa muda mrefu wa kukusanya madeni yote wanayowadai watu binafsi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, madeni ya matumizi ya umeme ya Wizara na taasisi za Serikali yaanzee kulipwa moja kwa moja kwa TANESCO kujitilia Hazina.

Mheshimiwa Spika, kamati inaendelea kuishaur serikali ikamilishe miundombinu ya bomba la gesi ili TANESCO iachane na kukodisha mitambo yenyе kutumia mafuta ya Makampuni binafsi, hatua ambayo itapelekea TANESCO kujidhesha kwa faida.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kutenga kiasi cha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi wa Kinyerezi I, Kamati bado inaona kuna umuhimu mkubwa wa kutafuta fedha zaidi kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Kinyerezi II, III, na IV ambayo itazalisha jumla ya Megawati 870. Miradi hii itasaidia upatikanaji wa Umeme wa uhakika na haraka kwani ni ukweli ulio wazi kuwa katika maeneo ambayo Umeme umepita tumejionea ukuaji wa kimaendeleo wa kasi sana.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri serikali kuona umuhimu wa kuwekeza zaidi kwenye miradi ya vipaumbele kama ilivyoainishwa ili kuondoa uwezekano wa nchi kuingia kwenye mgao wa umeme na kuendelea kukodi mitambo ya Makampuni ambayo huiuzia umeme TANESCO kwa bei za juu.

Mheshimiwa Spika, kamati inaliomba Bunge lako tukufu kuitaka Serikali kutoa takwimu sahihi za mahitaji na matumizi ya umeme kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilieleze Bunge lako tukufu na jamii kwa ujumla kuhusu hali ya mikataba baina ya TANESCO

na Makampuni ya,IPTL, AGGREKKO , SYMBION ,IPTL, na SONGAS ili tujuue mkataba upi umekwisha, upi unaendelea na lini utakwisha.

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe maelezo ya kinakuhusu utekelezaji wa mradi wau meme wa **kv 220** kutoka Makambako hadi Songea kutohana na kusucasua kwa mradi huo.

3.1.2 Sekta Ndogo ya Gesi

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekezasSera mpya ya Gesi Asilia na Sheria yake (zinazopendekezwa) ziwekwe wazi na zitafsiriwe katika lugha ya kiswahili ili Wananchi na Wadau wote wazisome na kuzielewa kwa lengo la kutoa maoni yao katika kuziboresha.

Mheshimiwa Spika, aidha matumizi ya gesi asilia katika kuzalishia umeme yalenge kupunguza gharama za umeme na Serikali iangalie upya ushirikishwaji wa Sekta binafsi (*Private Sector*).

Mheshimiwa Spika, Serikali itatue haraka migogoro mbalimbali kwenye maeneo yote yanayozunguka miundombinu ya bomba la gesi ikiwemo kutoa fidia kwa wananchi wanaostahili kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

3.1.3 Vyanzo Mbadala vya Nishati nchini

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali ikamilishe mkataba baina ya TANESCO na NDC katika kuanzisha mradi wa umeme utokanao na upopo huko Singida ili kuongeza umeme kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri serikali ili kupunguza utegemezi wa vyanzo vya nishati vya kutegemea chanzo cha maji, serikali iendelee na mpango wake wa kuendeleza nsiahati mbadala ya joto ardhi (**Geo-thermal**) kwa kutupa sera na sheria ya joto ardhi ya kuzisimamia.

3.1.4 Sekta ya Mafuta Nchini:

- Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine ihakikishe inadhibiti udanganyifu unaofanywa na Makampuni yanayosafirisha mafuta nje ya nchi (*transit*) kwa kuyarudisha mafuta hayo ndani kinyume cha Sheria na hivyo kuikosesha Serikali mapato.
- EWURA iongeze usimamizi katika usafi wa ghalia (**Depo**) za mafuta kwa kushirikisha Sekta binafsi ili kudhibiti ubora wa mafuta nchini.
- Serikali itekeleze haraka mpango wake wa kuboresha bandari ya Tanga ili bandari hiyo ianze kupokea meli za mafuta, hali ambayo itapunguza kero mbalimbali kwenye bandari ya Dar es Salaam.

3.1.5 MAONI YA JUMLA

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na utendaji wa REA na TANESCO katika kusimamia utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Nishati Vijiji chini ya Uongozi wa Wizara ya Nishati na Madini. Hata hivyo kamati inaishauri Serikali kuharakisha upatikanaji wa Fedha za wazabuni ili vijiji ambavyo havijapata umeme viweze kuunganishwa. Hii ni pamoja kuvunganisha vijiji vyote vilivyorukwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaliomba Bunge lako tukufu liitake Serikali kutekeleza maagizo yafuatayo:

- Warrant of Fund ya makusanyo ya **tozo** za mafuta na umeme na 'Customs Processing Fees' ambayo imepokelewa na Wizara , fedha zake zipelekwe haraka kwenye Mfuko wa Nishati Vijijini , na
- Serikali itafute bakaa ya bajeti ya REA na kuipeleka kwenye mfuko wa Nishati Vijijini ili kukwamua Miradi ya REA iliyokwama kwa kukosa fedha.

Mheshimiwa Spika, niwaombe Waheshimiwa wabunge wote leo tuibane Serikali ili izitoe fedha zote za mfuko wa Nishati vijijini ili zikakwamue miradi iliyokwama.

Mheshimiwa Spika, kupatikana kwa gesi asilia ni kichocheo cha ukuaji wa uchumi wetu, Kamati imeridhishwa na hatua za umalizajji wa ujenzi wa bomba la gesi na miundombinu yote kwa ujumla . Hata hivyo , tunaiomba Serikali kuhakikisha fedha zinazohitajika kukamilisha mradi huo zitolewe kwa wakati na pia Serikali ihakikishe **Sera na Sheria Mpya ya Gesi na Mafuta** inawalenga na kuwanufaisha Watanzania.

Mheshimiwa Spika,Kamati inaendelea kutoa ushauri kwa Serikali kuhakikisha Makampuni yote ya madini yanalipa kodi ya mapato (corporate tax) pamoja na mrabaha kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, aidha serikali iachane na tabia ya kuwakaimisha kwa muda mrefu watendaji wasaidizi katika taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika,Kamati inaendelea kuishauri Serikali iandae na kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu (ndani ya Wakati) mpango maalum kuhusu mageuzi katika Sekta ya Madini ambapo pamoja na mambo mengine muhimu, mpango huo uzingatie mambo yafuatayo:

- Ujenzi wa uzio kuzunguka machimbo ya Tanzanite huko Mererani kwa lengo la kudhibiti utoroshwaji wa Madini hayo nje ya nchi na hivyo kupoteza pato kubwa kwa Taifa, na
- Uanzishwaji wa kituo maalum cha Kitaifa cha utalii na uuzwaji wa vito vya Madini yanayochimbwa hapa nchini ikiwemo Tanzanite. Hatua hii italisaidia Bunge lako tukufu kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kuishauri na kuisimamia Serikali katika kuboresha sekta hii muhimu kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Mheshimiwa spika, kwa mwaka huu wa bajeti 2015/2016 Kamati inaishauri serikali ihakikishe inasimamia kwa umakini wa hali ya juu ukamilishaji wa miradi ya vipaumbele ya kuzalisha umeme wa uhakika ambayo ni , **REA, Miradi ya Kinyerezi One, North-East Grid 400kv ,na kukamilisha mfumo mzima wa Mradi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara hadi Dar Es Salaam.**

Mheshimiwa Spika, ni matumaini ya Kamati na wananchi kwa ujumla kuwa ukamilishaji wa miradi hiyo utatuwezesha kupata umeme kwa wingi, umeme wa uhakika na umeme wa bei nafuu.

4.0 SHUKRANI

Mheshimiwa Spika, nakupongeza pamoja na Naibu Spika, na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa tuliowakabidhi.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano walionipa wakati wa kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 na katika utumishi wangu kama Mwenyekiti wa Kamati hii. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1.Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb	-	Mwenyekiti
2.Mhe. Jerome Dismas Bwanausi, Mb	-	M/Mwenyekiti
3.Mhe. Josephine Tabitha Chagulla, Mb	-	Mjumbe
4.Mhe. David Ernest Silinde, Mb	-	Mjumbe
5.Mhe. Martha Moses Mlata, Mb	-	Mjumbe
6.Mhe. Devotha Mkuwa Likokola, Mb	-	Mjumbe
7.Mhe. Raya Ibrahim Khamis, Mb	-	Mjumbe
8.Mhe. Mariam Nassor Kisangi, Mb	-	Mjumbe
9.Mhe. Murtaza Ally Mangungu, Mb	-	Mjumbe
10.Mhe. Juma Abdallah Njwayo, Mb	-	Mjumbe
11.Mhe. Herbert James Mntangi, Mb	-	Mjumbe
12.Mhe. Shaffin Ahmedali Sumar, Mb	-	Mjumbe
13.Mhe. Yussuf Haji Khamis, Mb	-	Mjumbe
14.Mhe. Riziki Saidi Lulida, Mb	-	Mjumbe
15.Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb	-	Mjumbe
16.Mhe. Yussuf Salim Hussein, Mb	-	Mjumbe
17.Mhe. Dkt.John Emmanuel Nchimbi, Mb	-	Mjumbe
18.Mhe. Victor Kiliusile Mwambalaswa,Mb	-	Mjumbe
19.Mhe.Innocent S.Bilakwate, Mb	-	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Didimu Kashilillah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Charles Mloka, makatibu wa Kamati Ndugu Evelyn Shibandiko ,Ndugu Stanslaus Kagisa na Pamela Pallangyo wakisaidiwa na Ndugu Kokuwaisa Joseph Gondo pamoja na Ndugu Halima Laizer, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na kukamilisha Taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu.

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara **Fungu 58** kwa mwaka wa Fedha 2015/2016 ambayo ni Shilingi **Bilioni 536.96 na mapendeleko ya nyongeza kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.**

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Richard Mganga Ndassa, (Mb)
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI
06 Juni, 2015

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Esther Matiko!

MHE. ESTHER N. MATIKO (k.n.y. MHE. JOHN J. MNYIKA - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPIZANI JUU YA WIZARA YA NISHATI NA MADINI): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu. Zaidi, napenda kuchukua fursa hii kuwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa niaba ya Msemaji wa Kambi Ramsi ya

Upinzani Bungeni wa Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa John John Mnyika kuhusu Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2014/2015 na makadirio ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Taarifa hii imetolewa chini ya Kanuni ya 99(9), Toleo la Mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kitabu cha Uongozi Wetu na Hatima ya Tanzania, Mwalimu Nyerere anasema nanukuu: "Anasema akinukuu msemo wa Waingereza katika ukurasa wa 52 wa Kitabu kwa kusema Waingereza wana msemo "Nature abhors a vacuum;" yaani hulka huchukia ombwe, hata siasa huchukia ombwe. Kama uongozi ni mbovu, upo kama haupo au upo kwa masilahi ya wenyewe, watatokea watu waujaze uwazi uliopo; hauwezi kuachwa wazi hivi hivi. Uongozi mbovu ni kama mzoga, una tabia ya kukaribisha mafisi na mainzi. Tusidhani kuwa hulka ya siasa yetu ni tofauti na hulka ya siasa ya watu wengine; kwamba, sisi tunaweza kuvumilia uongozi mbovu na tusivune matunda ya hulka ya uongozi mbovu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere wakati akiandika haya juu ya Rais Mwinyi na Muungano, naomba Wabunge leo tutafakari maneno hayo kwa uongozi wetu wa sasa na sekta tunayoijadili leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufuatao ni ushauri wetu katika masuala mtambuka katika Sekta ya Nishati:-

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilishauri kuwepo kwa mfumo thabit wa kuhakikisha Maoni na Maazimio mbalimbali yaliyotolewa na Kamati Teule za Bunge yanatekelezwa kwa wakati na kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa Serikali imeendelea kupuuza mapendekezo hayo na kutoa ahadi ambazo haikuwa tayari kuzitekeleza; mathalani ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliyoitao wakati akahirisha Bunge la Bajeti 2011/2012 ya kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ili kuongeza pesa ya Wizara ya Nishati na Madini, lakini tofauti na ahadi yake, Serikali ikaamua kuja na mpango wa kukopa fedha katika taasisi za fedha ili kuinurusu TANESCO, ambao nao haujatekelezwa kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea na kuonyesha udhaifu na uwezo mdogo wa Wizara katika kusimamia sheria za nchi, kwa mujibu wa Taarifa ya CAG ya Juni 2012, nchi imepoteza kiasi cha Dola za Marekani 12,634,354.6, sawa na shilingi bilioni 19.71. Hizi ni fedha ambazo hazikukusanya kutoka kwa makampuni ya madini kufuatia Sheria Mpya ya Madini ya Mwaka 2010, kifungu cha 87(1) kuwa mrabaha wa 4% utozwe kabla ya makato na badala yake mrabaha ukawa 3% na kutozwa baada ya makato, kinyume kabisa na sheria za nchi na hakuna hatua zozote ambazo zimechukuliwa kuhusiana na tukio hilo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilihoji kuhusiana na hasara hiyo, tukaishia kubewa na aliyekuwa Waziri aliyeachishwa Uwaziri kutokana na Sakata la Escrow, Mheshimiwa Sospeter Muhongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu gesi asilia, tarehe 15 Julai 2011, Kambi Rasmi ya Upinzani ilieleza kuwa, nchi yetu imejaliwa utajiri wa gesi asilia katikati ya lindi la umaskini wa Wananchi na kwamba, Taifa letu lina fursa ya kuwa nchi kiongozi katika gesi Afrika na kushindana Kimataifa, ikiwa tutaweka mistari wa mbele uzalendo, upeo, umakini na uadilifu katika Sekta ya Nishati ili kuliepusha Taifa kukumbwa na laana ya rasilimali, yaani resource curse kama ambavyo baadhi ya nchi za Africa zimejikuta zikikumbwa na laana hiyo kutokana na kukosekana kwa usimamizi na mipango dhabiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, mapitio ya utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012, yalionyesha Serikali kutochukua hatua thabiti kushughulikia ujisadi na udhaifu wa kiuongozi katika Sekta Ndogo ya Gesi Asili. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliitaka Serikali kuweka wazi kwa Watanzania wote Mikataba hiyo na mingine ambayo Serikali imeisaini inayohusiana na rasilimali za Taifa hili. Hadi sasa Mikataba hiyo haijawekwa wazi na Watanzania kuelewa ni nani anafanya nini na mipaka ya mwekezaji katika rasilimali ni ipi na Mwananchi anashiriki vipi. Kwa kuwa Serikali haitaki kuiweka wazi Mikataba hiyo kutokana na hofu ya kuwa ujisadi unaotokana na Mikataba utajulikana na Watanzania, ni wakati sasa wa Tanzania kuiondoa CCM madarakani na kuweka viongozi waadilifu na ambao wataenda kusimamia rasilimali za Taifa hili kwa uwazi na uadilifu wa hali ya juu. Viongozi hao wanapatikana UKAWA. Kila Mtanzania akajiandikishe ili aweze kutumia haki yake na ili aweze kuwa sehemu ya kulinda na kunufaika na rasilimali za Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uagizaji wa mafuta wa pamoja, yaani *Oil Bulk Procurement*: Ili kuepusha Watanzania kubebeshwa mzigo wa gharama kubwa ya mafuta, katika Kikao cha Arobaini na Mbili, Tarehe 9 Agosti 2011, kulitolewa hoja ya dharura kuhusu uhaba wa mafuta baada ya michango kadhaa ya Waheshimiwa Wabunge na hatimaye Serikali ilitoa kauli yake. Baada ya mjadala huo, Bunge lilifanya uamuzi na hata hivyo hakukuwa na ufuatiliaji wa karibu baada ya Maazimio. Hali hii ni moja katika kasoro kubwa ambayo kuanzia mwaka huu Kambi Rasmi ya Upinzani iliitaka irekebishwe. Katika Kamati zote zilizopo za kisekta, hakuna Kamati ambayo inafuatilia Maazimio yote ya Bunge ili Serikali kusimamiwa kwa zile ahadi au Maazimio tuliyoyapitisha hapa Bungeni na kutoa mrejesho Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhaifu au uzembe huu wa kutokuwepo kwa mwendelezo wa ufuatiliaji wa Maazimio au hoja ambazo Bunge linaazimia na hivyo kuonekana kuwa Bunge ni sawa na maji ya moto tu, lakini kadiri muda unavyopita, basi yanapoa na Serikali inarudi kwenye utendaji kazi wake wa *business as usual*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri aliahidi mbele ya Bunge kuanza kwa mpango wa utekelezaji uingizaji wa mafuta wa pamoja, yaani *Bulk Oil Procurement* mwezi Januari 2012. Wizara ilieleza kuanza kwa utaratibu huu umeokoa kiasi gani cha pesa kilichokuwa kinapotea kabla ya kuanza kutumika kwa utaratibu huu mpya na sababu za mpango huo kushindwa kushusha bei ya mafuta kinyume na ahadi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kauli ya Serikali kuhusu Mgawo wa Umeme: Wakati Waziri wa Nishati na Madini akiwasilisha makadirio ya bajeti ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka 2012/2013, aliliambia Bunge lako Tukufu kuwa, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni 2012, lengo la kuiondoa mgao wa umeme lilifikiwa kwa asilimia 100. Bado kunaendelea kuwepo na utata kuhusu mgawo wa umeme katika maeneo mengine ya nchi huku Serikali ikikanusha kuhusu mgawo wakati Watanzania wakiendelea kupewa nishati hiyo kwa mgawo. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalitaka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wizara ya Nishati na Madini, kuwaambia ukweli Watanzania kuhusu mgawo wa umeme kwa kuzingatia hali mbaya ya Shirika hilo kifedha ambayo imeripotiwa na vyombo vya habari hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo tuliyasema katika Hotuba yetu ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mwaka 2013/2014, lakini hali hiyo ya kukatika kwa umeme bado inaendelea takribani nchi nzima. Huu ni ushahidi wa dhahiri kuwa, Serikali ya CCM haiaminiki kwa ahadi wanazozitoa kwa Wananchi na haiwezi kutekeleza kwani imechoka na inastahili kupumzishwa na kuendelea kuiacha ni kuliingiza Taifa katika janga kuu siku za usoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani iliwahi kusisitiza ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini wa kuitaka Serikali kuiwezesha TANESCO kumiliki mitambo yake

badala ya kutegemea mitambo ya kukodi ambayo inaligharimu shirika hilo fedha nyingi linazolipa kwa makampuni yanayomiliki kama capacity charge. Je, maagizo hayo ya Kamati yametekelawa kwa kiwango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja hii Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba, Kamati ilifanya uchunguzi wa suala hili kabla ya kutoa ushauri kwa Serikali. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa mchanganuo wa gharama ambazo TANESCO itazipata katika kusafirisha mafuta mazito ya mitambo ya kufua umeme inayojengwa Nyakato Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali imejaribu kuelezea jitihada zake za kujenga mitambo mbalimbali ya kufua umeme wa gesi ikiwemo ile ya Kinyerezi, Ubungo na Mwanza. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza bayana namna mitambo hii inayojengwa itakavyokuwa mbadala wa mitambo ya kukodi, kuliko kuendelea kijisifia inajenga mitambo wakati kuna baadhi ya mitambo imekamilika lakini bado mitambo ya kukodi haipungui na TANESCO inazidi kulipa capacity charge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani iliitaka Serikali kutoa kauli kuhusu sababu za ucheleweshaji wa utekelezaji wa Mpango wa Dharura wa Umeme na kushindwa kubadilisha mfumo wa majenereta kutumia gesi badala ya mafuta; na kama kweli dharura iliyokuwepo bado ipo au imekwisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mionganoni mwa Miradi ya dharura iliyotakiwa kuwa imekamilika ni pamoja na Mradi wa Jacobsen Awamu ya Pili, ambao ulitakiwa kutekelezwa kuanzia mwezi Januari hadi Disemba 2012, ambao ungezalisha megawatts 150 na kuendeshwa na fedha za mkopo. Tulipenda kupata ufanuzi kuhusu Miradi hii ya Umeme wa Dharura ni mingapi imekamilika, kiasi gani cha fedha kimetumika na kama Taifa tunadaiwa kiasi gani cha fedha ambazo hadi sasa zimekopwa kwa ajili ya Miradi ya Umeme kwa vile ni mionganoni mwa maeneo ambayo nchi hii imekuwa ikiingia gharama kubwa lakini ikishindwa kumaliza tatizo hili na kuchangia katika Deni la Taifa ambalo kwa wakati huo lilikuwa shilingi trilioni 22, kwa Machi 2014 ilikuwa shilingi trilioni 30.6 na Machi 2015 deni ni shilingi trilioni 35.01.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha unaomalizika mwezi Juni 2015, Wizara ilitengewa na Bunge kiasi cha shilingi 957,177,000,000 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kwa mwaka huu wa fedha, bajeti kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo zimetengwa jumla ya shilingi 365,346,000,000, ikiwa ni pungufu ya shilingi 591,830,000,000, sawa na asilimia 61.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha hizo, asilimia 85 ni shilingi 310,844,000,000 zinakwenda kwenye Miradi ya BRN. Miradi hiyo ya BRN ni 11 ikiwemo REA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ina mashaka makubwa na mgawanyo huo wa fedha kwa Miradi hii ya Maendeleo, kwani mahitaji ya REA kiuhalisia ni shilingi bilioni 552.3, sasa zimetengwa shilingi bilioni 191.96, hii ni sawa na asilimia 34.7 ya mahitaji halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Kambi Rasmi ilisema kwenye Wizara ya Maji kwamba, Serikali hii ya CCM haiwezi kuwalettea Wananchi umeme kwani wanachofanya ni kuwahadaa Watanzania kwa kutandika nguzo chini na siyo kuzichimbia kwa takribani asilimia 80 ya vijiji. Hii ni aina nyingine ya utapeli wa Serikali ya CCM kwa Wananchi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Wananchi wanaoishi maeneo jirani na migodi wamekuwa wakisumbuliwa kupata haki zao hasa wanapotakiwa kuondoka maeneo ya mgodi

Nakala ya Mtandao (Online Document)

ili kupisha shughuli za uchimbaji ziendelee. Kwa mfano, Wananchi wa Kitongoji cha Nyamichele katika Kijiji cha Nyakunguru, ambao walifanyiwa tathmini ya mazao na nyumba zao ili waweze kupisha mgodi uendelee na shughuli za uchimbaji, sasa ni mwaka wa tatu hawajalipwa fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini katika eneo hilo ilifanyika mwezi Aprili 2013 na toka kipindi chote hicho hawajalipwa na wamekuwa wakiishi maisha ya dhiki kutokana na kutofanya shughuli za maendeleo katika maeneo yao. Pamoja na uvumilivu ambao Wananchi wameuonyesha katika kipindi chote hicho, Serikali inataku kuwabagua katika malipo wanayostahili. Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Ndugu Glorius Luoga, tarehe 19 Mei 2015, alimwandikia Mtendaji wa Kijiji akitaka watu walifanyiwa tathmini wachambuliwe ili kubaini wazawa wa eneo hilo na wageni kabla ya malipo kufanyika. Huu unaonekana ni mkakati wa Serikali katika kuwabagua Wananchi wa eneo hilo, kwani hata Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Ndugu Charles Muhangwa Kitwanga, alipofanya ziara katika maeneo hayo tarehe 4 na 5 Mei 2015, alielekeza watu wachambuliwe kabla ya kufanyiwa malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa maeneo hayo wanapinga kabisa hatua hiyo, kwani hailengi kuwatendea haki na wanahoji mambo yafuatayo:-

Kwa nini hoja ya kuwabagua wazawa na wageni haikuletwa kabla au wakati wa tathmini?

Pili, mbona katika tathmini zilizotangulia katika maeneo yanayopakana na eneo hilo hakukuwa na kitu kama hicho?

Tatu, tathmini iliyofuata katika maeneo mengine yanayozunguka mgodi ilifanyika na Wananchi wakalipwa bila kubaguliwa.

Nne, kwa nini Serikali inataku kuwabagua Wananchi wakati mgodi uko tayari kulipa Wananchi wote wanaostahili kulipwa haki zao kulingana na tathimini iliyofanyika?

Tano, iwapo utaratibu wa kulenga kulipa wazawa tu utafuatwa, je, Wananchi wengine ambao ni wakazi wa pale na ambao maeneo yao yalifanyiwa tathmini ni nani atawalipa haki zao?

Sita, je, kuzuwa kufanya shughuli za maendeleo kwa kipindi cha miaka mitatu baada ya tathmini ni haki?

Saba, je, ni kwa nini vikao halali kwa maana ya Mkutano Mkuu wa Kijiji ambao ulikuwa na viongozi halali kwa maana ya Mtendaji, Mwenyekiti wa Kijiji na Vitongoji pamoja na miutasari uliazimia kutochambua Wananchi kwani ni ubaguzi bali walipwe wote walifanyiwa tathmini lakini unakuikwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kufanya shughuli za mgodi ndani ya mita mia mbili. Mgodi wa Acacia unaendelea kufanya shughuli za uchimbaji ilhali kuna watu ndani ya mita hamsini, kitendo hiki kimeendelea kuhatarisha maisha ya Wananchi hao. Wanapata athari za nyumba zao kubomoka, matatizo ya vifua vikuu, mimba kuharibika, watu kulemazwa na madhara mengine mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyoendelea na vikao, kuna Wananchi juzi waliumia wakakimbizwa Hospitali ya Bugando kwa matibabu, ikiwemo mtoto mdogo aliyepigwa kichwani na kipande cha nyumba iliyobomoka kutokana na athari za mlipuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi haithamini maisha ya Wananchi wake, kwani ni katika Mkutano huu wakati wa Bajeti ya Wizara ya Mazingira, Mheshimiwa Matiko alishika Shilingi ya Wizara ili kupata ufumbuzi wa haraka wa Wananchi wanaoishi ndani ya mita mia mbili hasa wa Kitongoji cha Nyabikondo, Nyabichune na Mjini Kati Kata ya Matongo Tarime wahamishwe ili sasa wapishe shughuli za uchimbaji ili kunusuru maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu, kama ilivyo kawaida, Wabunge wa CCM kwa wingi wao walipinga hoja ya Mheshimiwa Matiko na kupitisha mgodi uendelee na uchimbaji hata kama Wananchi wale wanaathirika. Nadhani Wananchi wa Tarime na Watanzania wanaona nani mwenye nia njema na maendeleo yao na jibu ni UKAWA. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Mkaguzi na Ubadhirifu TANESCO: Kwa mujibu wa kifungu cha 54(2)(d) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2004 na Kanuni ya 20(2)(e) ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi ya Umma ya Mwaka 2005, kinyume na matakwa haya, katika ukaguzi wa hesabu za TANESCO, Mkaguzi alibaini ununuzi wa takribani Shilingi za Kitanzania Bilioni 3.2 kupitia zabuni Namba hiyo, bila kuzingatia kiasi kilichotengwa kwenye bajeti, yaani shilingi milioni 400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zabuni nyingine TANESCO waliingga mkataba wa shilingi milioni 340.8 ambayo ni zaidi ya bajeti iliyotengwa, yaani ya shilingi milioni 154. Ukaguzi huu haukuweza kupata ushahidi wa kuwepo kwa marejeo ya bajeti kwa kiasi kilichotumika nje ya makadirio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapata tabu kuelewa ni kwa vipi TANESCO inapata uthubutu wa kutumia hivyo bila kufuata utaratibu uliowekwa kisheria na kama dharura inatokea; je, wakati wa maandalizi ya bajeti yao hadi inapitishwa na Bodi dharura haiwekwi au ni njia nyingine ya wizi unaoendelea katika Shirika hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ucheleweshwaji wa Miradi unapelekea kuongezeka kwa gharama zisizokuwa za lazima. Mapitio ya zabuni namba hiyo, yenye thamani ya Dola za Kimarekani 34,848,390 kwa ajili ya ujenzi wa mtandao wa umeme kiwango cha 132 kV, Mradi huo ulipangwa kumalizika ndani ya miezi 18, yaani Septemba 2011. Hata hivyo, Mradi huo ulichelewa kukamilika hadi Juni 2013 kutokana na ugumu uliojitokeza kwa kupata eneo la Mradi. Hii ni aibu kwani haiwezekani ukasaini Mkataba bila ya kuwa na eneo la utekelezaji wa Mradi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ucheleweshwaji huu, Mkandarasi na Mshauri Mwelekezi walianza kazi bila kuwa na Mkataba halali; hivyo, kupelekea TANESCO kutakiwa kulipa gharama za kusubiria kuanza kazi kiasi cha Euro 981,831, Dola za Kimarekani 1,423,098 pamoja na adhabu ya Dola za Kimarekani 682,940.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili ni dhahiri kabisa kwa Kambi Rasmi ya Upinzani kusema kuwa, TANESCO inafanya kazi zake kiubabaishaji, jambo ambalo linatia hasara walipa kodi wa nchi hii. Je, ubabaishaji huu utaendelea hadi lini kwani Mikataba ya kiujanaujanja ndiyo inafilisi Shirika hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Usambazaji Umeme Vijijini ulianzishwa kwa Sheria Na. 8 ya Mwaka 2005 na uliana kazi rasmi Oktoba 2007, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2003; lengo likiwa ni kuwapatia Wananchi waishio vijijini nishati bora.

Pamoja na umuhimu wa Wakala huu, bado Serikali haijaonyesha kwa vitendo kuwa ina nia ya kusaidia wakala huu ili uweze kutimiza majukumu yake kikamilifu na hasa linapokuja suala la kuupatia fedha kama zinavyoombwa na zinavyopitishwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Wakala ulihitaji kiasi cha shilingi bilioni 366.9 kwa ajili ya kutekeleza Miradi sita ya Nishati vijijini, lakini kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 203/2014, tayari Bunge hili limeambiwa kuwa fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo iliyotolewa ni asilimia 42.3 tu. Kwa mwaka 2014/2015 bajeti iliyokuwa imetengwa ni shilingi bilioni 292.6, lakini hadi mwezi Machi 2015, kiasi kilichopokelewa kutoka Hazina ni shilingi bilioni 100.5, sawa na asilimia 37 tu. Kama ilivyo kwa Wizara ya Ujenzi hadi kufikia mwezi Machi 2015, REA inadaiwa na wakandarasi kiasi cha shilingi bilioni 124. Je, hapa ni kweli kuna usambazaji wa umeme vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za Mdhibiti wa Maji na Mafuta zinaonyesha kuwa, kuanzia Januari 2011 hadi Desemba 2014, mafuta yaliyoingizwa nchini ni meta za ujazo 8,660,160, ambazo ni sawa na lita 8,660,160,400. Kwa mujibu wa Sheria za Tozo ya Mafuta kwa lita moja ni shilingi 50. Hivyo basi, kwa kipindi hicho REA ilitakiwa kupata jumla ya shilingi bilioni 433 kama tozo ya mafuta tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na takwimu hizi kama Serikali haikupeleka fedha hizo REA ina sababu gani za msingi? Taarifa ya REA inaonyesha hadi Machi 2015 kiasi kilichopokelewa ni shilingi bilioni 144.2 tu na bakaa ambayo haijapokelewa na REA hadi mwezi Novemba 2014 ni shilingi bilioni 36.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mfano mmojawapo kuwa, Serikali ya CCM haiheshimu sheria zilizopo, kwani tozo ya mafuta imelipwa na TRA inazo fedha hizo. Sasa ni kwa nini fedha hizo hazina haizipeleki sehemu husika kwa mujibu wa sheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa fedha mahitaji halisi ya Wakala kwa ajili ya kutekeleza Miradi katika Mpango wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Pili ni takribani shilingi bilioni 881na kwa Miradi inayoendelea kutekelezwa kwa Awamu ya Kwanza na ya Pili zinahitajika shilingi milioni 552.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla ili Wakala ufanye kazi zake na kufikia malengo yaliyowekwa wanahitaji shilingi bilioni 1,433.3. Hoja ni je, Serikali ya CCM inaweza kutoa kiasi hicho cha fedha?

Kwa kuwa kiasi hicho hakiwezi kupatikana, kinachofanyika sasa ni kuwatapeli Wananchi kwa kusambaza nguzo tu na sehemu zingine wazisimika tu na sehemu zingine wanaunganisha nguzo tatu au nne kwa waya ili Wananchi waamini kuwa umeme unaletwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kitu kibaya kama kutoa matumaini kwa watu wakati unajua kabisa hauna uwezo wa kutekeleza mambo ulyiowaahidi. Hiki ndicho kitakachopelekea kifo cha Serikali ya CCM, kutoa matumaini ya uongo wakati wanaelewa kabisa kuwa REA haipewi fedha za kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkataba ambao Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) iliingia na Kampuni ya Tanzania American International Corporation (2000) Limited ili kuendeleza mgodi wa Buck Reef Gold Mine, ilikubalika kwamba uzalishaji utaanza ndani ya miezi 30 toka siku ya kutiliana saini makubaliano na endapo muda wa kuanza uzalishaji utachelewa, Tanzania American International Corporation (2000) Limited, ilianzishwa tarehe 24 Oktoba 2011 kwa

madhumuni ya kuendeleza Mgodi huo. Ilikubalika kuwa kucheleweshwa kokote ingeili pa STAMICO fidia ya ucheleweshaji kiasi cha Dola za Kimarekani 500,000 kama Mradi utasogezwa mbele mara ya kwanza, Dola za Kimarekani 625,000 kwa mara ya pili na Dola la Kimarekani 750,000 kwa vipindi vyovyote vitakavyofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Waziri alieleze Bunge lako hadi sasa Mradi huo umeanza au bado na kama bado kwa mujibu wa Mkataba STAMICO inatakiwa kulipwa toka mshirika wake kwa mujibu wa matakwa ya Mkataba husika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), ndilo liliilo na jukumu la msingi la kuhakikisha kuwa rasilimali ya mafuta na gesi iliyopo nchini inajulikana ilipo na inajulikana kiasi cha hazina kilichopo na inavunwa na nani na Watanzania watanufaika vipi na rasilimali hizo. Katika kutekeleza hayo yote, inatakiwa kuwa na fedha za kutosha pale uhitaji wa TPDC kuwekeza unapokuwepo. Pale ambapo Mikataba inayoingiwa kutafuta watu wenye utaalim wa ziada kwenye fani hii ili kutoziuzia nchi kwa Mikataba kama ile ilioingiwa na Serikali na Kampuni ya Kiholanzi ya MSI wakati wa kubinafsisha Kampuni ya simu TTCL. Aibu hiyo sasa hivi inakuwa ni aibu ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahenga wanasema mchuma janga hula na wa kwao. Hilo la Mikataba ya Ubinafsishaji hadi sasa Watanzania wanalipia. Sasa ili kuondokana na uchafu uliotokea kipindi hicho, ndiyo maana tunaitaka TPDC kuwa na taaluma inayotakiwa katika kuhakikisha uwekezaji wa rasilimali zetu za mafuta na gesi zinakuwa na manufaa kwa kizazi kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo haliwezi kufanikiwa ikiwa Bajeti ya Maendeleo ambayo inapangwa haitolewi. Mwaka wa Fedha 2014/2015, kwa fedha za maendeleo zilitengwa jumla ya shilingi bilioni 138, hadi mwezi Machi TPDC ilitarajia kupokea jumla ya shilingi bilioni 103, lakini ilipokea shilingi bilioni 53.2 tu. Hivi ni kweli kampuni inaweza kuwa na *burgaining power*, uwezo wa kibiashara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unyonge wa fedha unaolikumba Shirika hili ndiyo unapelekea mapato ya gesi kutokusanya kwa kadiri Mikataba na Sheria zinavyosema.

Kwa mujibu wa Taarifa ya TPDC inaonyesha kuwa SONGAS na Pan African Energy zinadaiwa jumla ya shilingi bilioni 69.2. Je, kwa mwendo huu gesi hii inaweza kuwa na manufaa kwa Wananchi kama madeni yanashindwa kudaiwa kwa kusimamia Mikataba iliyopo?

Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA) ni Wakala wa Serikali ulioanzishwa tarehe 2 Novemba 2009 chini ya Sheria ya Wakala wa Serikali (Sura 245). Lengo kuu la Wakala ikiwa ni kuhakikisha kwamba, Serikali inapata mapato stahiki kutoka kwenye shughuli za uzalishaji na biashara za madini nchini kuitia usimamizi na ukaguzi makini wa shughuli hizo na kuhakikisha kuwa shughuli hizo zinafanyika kwa kuzingatia uhifadhi na utunzaji thabiti wa mazingira katika maeneo ya migodi. Taarifa ya Wakala inasema kuwa, ili kujuua thamani halisi ya madini yaliyozalishwa na kuuzwa nje, jumla ya sampuli 1,976 za madini zilizozalishwa na migodi mikubwa ya dhahabu zilichukuliwa na kufanyiwa uchunguzi kwenye Maabara ya wakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hiyo ya Wakala ni kiini macho kwa Waheshimiwa Wabunge, kwani kwa uelewa wa kawaida tu haiwezekani sampuli zikakuwezesha kuelewa thamani halisi ya madini yaliyozalishwa na kusafirishwa nje ya nchi. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri kulitolea kauli suala hili ili kutoa uelewa mzuri kwa Waheshimiwa Wabunge. kitendo cha kuweka wakaguzi kila mgodi ni sawa na kitendo cha Mkaguzi Mkuu wa Ndani kuweka wakaguzi kwenye halmashauri na mwisho wa siku wakaguzi

hao wanakuwa ni sehemu ya Menejimenti ya Halmashauri. Jambo hili nalo ndiyo linalopelekea Taarifa ya Wakala kuwa kama inavyonukuliwa na Kambi Rasmi ya Upinzani ili kuleta ufanisi unaokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, naomba taarifa hii iingie kwenye Hansard na baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (Makofii)

**HOTUBA YA MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WIZARA YA NISHATI NA MADINI
JOHN JOHN MNYIKA (MB) KUHUSU MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA MAPITIO YA
UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2014/2015 NA MAKADIRIO YA MATUMIZI
YA WIZARA YA NISHATI NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

(Inatolewa chini ya kanuni ya 99(9) toleo la mwaka 2013)

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere katika kitabu chake cha **TUJISAHIHISHE** katika ukurasa wa pili anasema maneno yafuatayo naomba kumnungu ‘*ukweli una tabia moja nzuri sana. Haujali mkubwa wala mdogo; haujali adui wala rafiki. Kwake wote ni sawa. Pia ukweli unayo tabia ya kujilipiza kisasi kama ukipuuzwa. Ukiniona na taka kulipiga teke jiwe kwa kuwa nafikiri kuwa ni dongo au mpira, natumaini utanionya. Lakini nikilipuza onyo lako kwa sababu eti wewe ni mdogo au kwa sababu sikupendi, nitalipiga teke, basi litanivunja dole japo ningekuwa nani. Ukwelihaupendi kupuuzwapuuzwa.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katikakitabu cha **UONGOZI WETU NA HATIMA YA TANZANIA** Mwalimu Nyerere anasema “ananukuu msemo wa waingeereza katika ukurasa wa 52 wa kitabu kwa kusema “Waingereza wana msemo “Nature abhors vacuum”, “hulka huchukia ombwe”. Hata siasa huchukia ombwe. Kama uongozi ni mbovu, upo kama haupo au upo kwa masilahi ya wenyewe, watatokea watu waujaze uwazi uliopo; hauwezi kuachwa wazi hivi hivi. Lakini uongozi mbovu ni kama mzoga, unatabia ya kukaribisha mafisi na mainzi. Tusidhani kuwa hulka ya siasa yetu ni tofauti na hulka ya siasa ya watu wengine; kwamba sisi tunaweza kuvumilia uongozi mbovu na tusivune matunda ya hulka ya uongozi mbovu”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakati Mwalimu Nyerere akiandika haya juu ya Rais Mwinyi na Muungano, naomba wabunge leo tutafakari maneno hayo kwa uongozi wetu wa sasa na sekta tunayojadili leo.

2. USHAURI WETU KATIKA MASUALA MTAMBUKA KATIKA SEKTA YA NISHATI

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilishauri kuwepo kwa mfumo thabiti wa kuhakikisha maoni na maazimio mbalimbali yaliyotolewa na Kamati teule za Bunge yanatekelezwa kwa wakati na kwa ukamilifu.

Lakini hadi sasa Serikali imeendelea kupuua mapendekezo hayo na kutoa ahadi ambazo haikuwa tayari kuzitekeleza, mathalani ahadi ya Mhe Waziri Mkuu aliyotoa wakati akiahirisha bunge la bajeti 2011/2012 ya kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ili kuongeza pesa wizara ya Nishati na Madini lakini tofauti na ahadi yake, Serikali ikaamua kuja na mpango wa kukopa fedha katika taasisi za fedha ili kulinusuru shirika la umeme Tanzania TANESCO, ambaao nao haujatekelezwa kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kuendelea kuonyesha udhaifu na uwezo mdogo wa wizara katika kusimamia sheria za nchi, kwa mujibu wa taarifa ya CAG ya Juni 2012 nchi imepoteza kiasi cha dola za kimarekani 12,634,354.61 sawa na shilingi bilioni 19.71 , hizi ni fedha ambazo hazikukusanywa kutoka kwa makampuni ya madini kwa kufuata sheria mpya ya madini ya mwaka 2010, kifungu cha 87(1) kuwa mrahaba wa 4% utozwe kabla ya makato na badala yake mrahaba ukawa ni 3% na kutozwa baada ya makato kinyume kabisa na sheria za nchi na hakuna hatua zozote ambazo zimechukuliwa kuhusiana na tukio hilo.. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni ilihoji kuhusiana na hasara hiyo ila tukaishiakubezwa na aliyekuwa Waziri aliyeachishwa uwaziri kutokana na sakata la Escrow Mheshimiwa Sospeter Mhongo.

3. UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KAMATI TEULE YA BUNGE KUHUSU RICHMOND

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa mbili za serikali kuhusu utekelezwaji wa maazimio haya ziliwasilishwa Bungeni na Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Pinda, tarehe 28 Agosti, 2008 na tarehe 11 Februari, 2009. Taarifa moja ilikabidhiwa na kujadiliwa na Kamati, ambazo zilitaaarifu Bunge kuwa utekelezaji wa Maazimio 10 kati ya 23 yaliyotolewa na Bunge, yafaniyiwa kazi hadi mwezi Februari, 2009 na Maazimio 13 bado yalikuwa hayajakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lilazimia kwamba taarifa za utekelezaji wa maazimio yaliyobaki ziwasilishwe kwa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambayo hata hivyo katika mwaka 2011, 2012 na mpaka mabadiliko ya muundo wa Kamati yalipofanyika kamati hiyo haikuwasilisha taarifa yoyote bungeni ya kueleza kukamilika kwa utekelezaji wa maazimio husika hali ambayo inahitaji bunge kuingilia kati kuweza kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Nchi Ibara ya 63 (2) na (3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kufuatilia maazimio ya Bunge kuhusu Kashfa ya RICHMOND ilishauriwa kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama iliopewa dhamana na Bunge kufuatilia utekelezaji wa maazimio kuhusu mkataba kati ya TANESCO na Richmond. Katika hali hiyo, haishangazi kwamba kwa miaka miwili toka wakati huo, mpaka mabadiliko ya kamati za Bunge yalipofanyika, kamati hiyo katika taarifa zake zote bunge haijawahi kuisimamia Serikali kuhakikisha maazimio husika ya Bunge yanatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani illitaka Wizara ya Nishati na Madini na Serikali kwa ujumla kutoa majibu bungeni juu ya hatma ya maazimio 10 yaliyobaki: Azimio Namba 3, 5, 7, 8, 9, 10, 11, 13, 14 na 18 ili bunge liweze kuishauri na kuisimamia serikali kuhakikisha maazimio husika yanatekelezwa kwa ukamilifu na kwa haraka. Lakini hadi sasa tunaposoma hotuba hii maazimio hayo ya Bunge bado hayajatekelezwa na Bunge kupata mrejesho rasmi.

4. SEKTA NDOGO YA GESI ASILIA

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu gesi asilia, tarehe 15 Julai, 2011 Kambi Rasmi ya Upinzani ilieleza kuwa, nchi yetu imejaliwa utajiri wa gesi asilia katikati ya lindi la umaskini wa wananchi na kwamba Taifa letu lina fursa ya kuwa nchi kiongozi katika gesi Afrika na kushindana Kimataifa ikiwa tutaweka mstari wa mbele uzalendo, upeo, umakini na uadilifu katika sekta ya nishati ili kuliepusha Taifa kukumbwa na laana ya rasilimali, (resource curse) kama ambavyo baadhi ya nchi za Africa zimejikuta zikikumbwa na laana hiyo kutokana na kukosekana kwa usimamizi na mipango dhabiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hata hivyo, mapitio ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2011/2012, yalionesha Serikali kutochukua hatua thabiti kushughulikia ufisadi na udhaifu wa kiuongozi katika sekta ndogo ya gesi asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushahidi wa hili ulipatikana katika ushauri ambao Serikali ilipewa kwa nyakati mbili tofauti lakini ikashindwa kuzuia vurugu za Lindi na Mtwara. Tarehe 27 Julai 2012 nikiwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu mapitio na makadirio ya mapato na matumizi ya wizara ya nishati na madini nilishauri "**Mapitio ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2011/2012, yanaonekana bado serikali haichukui hatua thabiti kushughulikia ujisadi na udhaifu wa kiuongozi katika sekta ndogo ya gesi asili hivyo hatua za haraka zisipochukuliwa katika mwaka 2012/2013 na kuendelea rasilimali inaweza kuwa chanzo cha migogoro na kuhatarisha pia usalama wa nchi**". Lakini pamoja na angalizo hili serikali haikuchukua hatua yoyote na matokeo yake sote tunayafahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani iliitaka Wizara ya Nishati na Madini kutoa kwa Bunge taarifa ya uchunguzi wa mikataba hiyo iliyokamilika toka mwaka 2012 lakini imeendelea kufanywa kuwa siri mpaka hivi sasa.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliitaka serikali kuweka wazi kwa watanzania wote mikataba hiyo na mingine ambayo serikali imeisaini inayohusu rasilimali za Taifa hili. Hadi sasa mikataba hiyo haijawekwa wazina watanzania kuelewa ni nani anafanya nini na mipaka ya mwekezaji katika rasilimali ni ipi na mwananchi anashiriki viyi.

Kwa kuwa serikali haitaki kuiweka wazi mikataba hiyo kutokana na hofu ya kuwa ujisadi unaotokana na mikataba utajulikana kwa watanzania, ni wakati sasa wa watanzania kuiondoa CCM madarakani na kuweka viongozi waadilifu na ambao wataenda kusimamia rasilimali za taifa hili kwa uwazi na uadilifu wa hali ya juu, viongozi hao wanapatikana UKAWA!Kila mtanzania akajandikishe ili aweze kutumia haki yake na ili aweze kuwasehemu ya kulinda na kunufaika na rasilimali za taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani iliyahi kusema kuwa, Katibu Mkuu wa CCM Abdurahaman Kinana amewahi kuwa Mjumbe wa Bodi ya wakurugenzi ya kampuni ya Artumas ambayo iliingia mkataba na Serikali wa kuzalisha Mega Watt- 300 za umeme Mtwara. Mkataba huo ulikuwa wa misingi ya mabadilishano ya gesi kwa nishati ya umeme (gas for power). Kwamba Artumas ingechimba na kuuza gesi asilia na kuilipa serikali kwa pamoja na mambo mengine kuizalishia umeme wa 300MW. Baadae mwaka 2010 Artumas baada ya kufaidika vya kutosha kutokana na uvunaji na uuzaji iliachaka kuendeleza mradi huo kwa kisingizio cha madai ya m dororo wa Uchumi mwaka 2009 na kuuza hisa zake kwa kampuni ya **Wentworth ya Ufaransa**.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushiriki huo wa viongozi waandamizi wa Chama Cha Mapinduzi kwenye shughuli ambazo zinaitia hasara serikali ni uthibitisho tosha kwamba CCM inawanyonya watanzania maskini, na hivyo ni dhahiri si mwafaka kwao kuendelea kuongoza nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pamoja na ujenzi wa mitambo miwili ya kusafishia gesi asili Mnazi Bay na Songo Songo kama sehemu ya mradi huo, Kambi Rasmi ya Upinzani iliitaka Serikali kueleza ni miradi ipi iliyotengewa fedha inayoambatana na mradi huo ambayo imepangwa kuwanufaisha wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara na imetengewa kiasi gani cha fedha katika mwaka wa fedha 2013/2014 ili kuharakisha msukumo wa maendeleo kwa mikoa hiyo ya Kusini ambayo imesahaulika kwa siku nyingi na hivyo siyo tu kuharakisha maendeleo kwa mikoa ya Kusini bali pia kuhakikisha usalama wa mradi huo mkubwa kwa manufaa mapana ya jamii ya kitanzania. Aidha, tunarudia tena kuitaka Serikali kueleza katika bajeti 2015/16 ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa miradi hiyo nani ipi?

5. UAGIZAJI WA MAFUTA WA PAMOJA (Oil Bulk Procurement)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuепusha watanzania kubebeshwa mzigo wa gharama kubwa ya mafuta katika **Kikao cha Arobaini na Mbili – Tarehe 9 Agosti, 2011**, **kulitolewa hoja ya dharura kuhusu uhaba wa mafuta baada ya michango kadhaa ya waheshimiwa wabunge na hatimae Serikali ilitoa kauli yake. Baada ya mjadala huo Bunge lilifanya uamuvi, hata hivyo hakukuwa na ufuatiliaji wa karibu baada ya maazimio.** Halihii ni moja katika kasoro kubwa ambayo kuanzia mwaka huu Kambi Rasmi ya Upinzani ilitaka irekebishwe. Katika Kamati zote zilizopo za sekta hakuna Kamati ambayo inafuatilia maazimio yote ya Bunge ili Serikali kusimamiwa kwa zile ahadi au maazimio tuliyoyapitisha hapa Bungeni na kutoa mrejesho Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhaifu au uzembe huu wa kutokuwepo kwa muendelezo wa ufuatiliaji wa maazimio ya maazimio au hoja ambazo Bunge linazisimamia na hivyo kuonekana kuwa Bunge ni sawa na maji ya moto tu lakini kadri muda unavyopita basi yanapoa na Serikali inarudi kwenye utendajikazi wake wa BUSINESS AS USUAL.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Nishati na Madini ya Bunge la Tisa iliwahi kupendekeza kwa Serikali mara nyingi sana kuhusu suala la TPDC kuitia kampuni tanzu ya COPEC kuanzisha biashara ya mafuta. Kamati ya Nishati ya Bunge la Tisa ikazungumzia pia Bulk Procurement pia Strategic Reserve. Masuala yote haya yamehojiwa na Kambi Rasmi ya Upinzani mwaka 2011 na 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mwaka 2011/2012 wa fedha Wizara ya Nishati na Madini, COPEC ilikuwa imepangiwa shilingi milioni 20 tu kwa ajili ya kampuni hiyo kuanza kufanya biashara. Ukweli ni kwamba kampuni hiyo haikuwa na miundombinu yoyote ya kuiwezesha kufanyabiashara kama Serikali ilivyaoagiza.

Kambi Rasmi ya Upinzani ilitaka Serikali ilieleze Bunge toka ilipopatiwa leseni ya biashara hadi sasa COPEC imeongeza tija ipi katika biashara ya mafuta kwa watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri aliahidi mbele ya bunge kuanza kwa mpango wa utekelezaji uingizaji wa mafuta wa pamoja (Bulk procurement) mwezi January 2012. Wizara ieleze kuanza kwa utaratibu huu umeokoa kiasi gani cha pesa kilichokuwa kinapotea kabla ya kuanza kutumika kwa utaratibu huu mpya na sababu za mpango huo kushindwa kushusha bei ya mafuta kinyume na ahadi za Serikali.

6. KAULI YA SERIKALI KUHUSU MGAWO WA UMEME

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini akiwasilisha makadirio ya Bajeti ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka 2012/2013 aliliambia bunge lako tukufu kuwa **“hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni 2012 lengo la kuondoa mgao wa umeme lilifikiwa kwa asilimia 100”**. Bado kunaendelea kuwepo na utata kuhusu mgawo wa umeme katika maeneo mengine ya nchi huku serikali ikikanusha kuhusu mgawo wakati watanzania wakiendelea kupewa nishati hiyo kwa mgawo. Aidha Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni inalitaka shirika la umeme Tanzania (TANESCO) na Wizara ya Nishati na Madini kuwaambia ukweli watanzania kuhusu mgawo wa umeme kwa kuzingatia hali mbaya ya shirika hilo kifedha ambayo imeripotiwa na vyombo vya habari hivi karibuni.

Hayo tuliyasema katika hotuba yetu ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mwaka **2013/2014**, **lakini hali hiyo ya kukatika kwa umeme bado kunaendelea takriban nchi nzima. Huu ni ushahidi wa dhahiri kuwa Serikali ya CCM haiaminiki kwa ahadi wanazozitoa kwa wananchina haiwezi**

kutekeleza kwani imechoka na inastahili kupumzishwa kwani kuendelea kuiacha ni kuliingiza taifa katika janga kuu siku za usoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani iliwayi kusitiza ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini wa kuitaka serikali kuiwezesha TANESCO kumiliki mitambo yake badala ya kutegemea mitambo ya kukodi ambayo inaligharimu shirika hilo fedha nyingi linazolipa kwa makampuni yanayomiliki kama capacity charge. Je, maagizo hayo ya Kamati yametekelawa kwa kiwango gani?

Katika hoja hii Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni inaamini kwamba kamati ilifanya uchunguzi wa swala hili kabla ya kutoa ushauri kwa serikali. Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kutoa mchanganuo wa gharama ambazo TANESCO itazipata katika kusafirisha mafuta mazito ya mitambo ya kufua umeme inayo jengwa Nyakato Mwanza.

Katika hoja hii serikali imejaribu kueleza jitihada yake ya kujenga mitambo mbalimbali ya kufua umeme wa gesi ikiwemo ile ya Kinyerezi, Ubungo na Mwanza.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliitaka serikali kueleza bayana namna mitambo hii inayojengwa itakavyokuwa mbadala wa mitambo ya kukodi kuliko kuendelea kijisifia inajenga mitambo wakati kuna baadhi ya mitambo imekamilika lakini bado mitambo ya kukodi haipungui na TANESCO inazidi kulipa capacity charge.

7. MPANGO WA UMEME WA DHARURA

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani iliitaka serikali kutoa kauli kuhusu sababu za ucheleweshaji katika utekelezaji wa mpango wa dharura wa umeme na kushindwa kubadilisha mfumo wa majenereta kutumia gesi badala ya mafuta, na kama kweli dharura iliyokuwepo bado ipo au imekwisha?

Miongoni mwa miradi ya dharura iliyotakiwa kuwa imekamilika ni pamoja na mradi wa Jacobsen awamu ya pili ambao ultakiwa kutekelezwa kuanzia mwezi Januari hadi disemba 2012 ambao ungezalisha mega-watt 150 na kuendeshwa na fedha za mkopo. Tulipenda kupata ufanuzi kuhusu miradi hii ya umeme wa dharura miradi mingapi imekamilika, kiasi gani cha pesa kimetumika na kama taifa tunadaiwa kiasi gani cha fedha ambazo hadi sasa zimekopwa kwa ajili ya miradi ya umeme kwa vile ni miongoni mwa maeneo ambayo nchi hii imekuwa ikiingia gharama kubwa lakini ikishindwa kumaliza tatizo hili na kuchangia katika deni la Taifa ambalo kwa wakati huo lilikuwa trilioni 22, kwa machi 2014 ilikuwa shilingi trilioni 30.6 na machi 2015 deni ni shilingi trilioni 35.01.

8. MAPITIO YA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2014/15 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2015/16

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha unaomalizika mwezi Juni, 2015 wizara ilitengewa na Bunge kiasi cha shilingi 957,177,170,000/- kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kwa mwaka huu wa fedha bajeti kwa ajili ya miradi ya maendeleo zimetengwa jumla ya shilingi 365,346,938,000/- ikiwa ni pungufu ya shilingi 591,830,232,000/- sawa na asilimia 61.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha hizo asilimia 85 ambazo ni shilingi 310,844,393,000 zinakwenda kwenye miradi ya BRN. Miradi hiyo ya BRN ni kama ifuatavyo;

- I. Ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia.
- II. Ujenzi wa mradi wa kinyerezi-I
- III. Ujenzi wa mtambo wa kinyerezi-II
- IV. Mradi kambambe wa kupelekea umeme vijiji awamu ya pili na miradi mingine ya umeme vijiji
- V. 220Kv Makambako-Songea TransmissionLine
- VI. Iringa-Shinyanga 400kV-backbone Transimission Investment Project
- VII. North West Grid Kv 220(Geita-Nyakanazi)
- VIII. Bulyanhulu-Geita KV220
- IX. North-East Grid (Dar -Tanga-Arusha)
- X. Singida-Arusha-Namanga KV400
- XI. Emergency repair project-Hydro-power plants

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ina mashaka makubwa na mgawanyo huo wa fedha kwa miradi hii ya maendeleo, kwani mahitaji ya REA kiuhalisia shilingi bilioni 552.3. Sasa zimetengwa shilingi bilioni 191.96 tu, hii ni sawa na asilimia 34.756 ya mahitaji halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kama ambavyo Kambi Rasmi ilivyosema kwenye wizara ya maji kwamba Serikali hii ya CCM haiwezi kuwalettea wananchi umeme kwani wanachofanya ni kuwahadaa watanzania kwa kutandika nguzo chini na sio kuzichimbia kwa takribani asilimia 80 ya vijiji. Hii ni aina nyingine ya utapeli wa Serikali ya CCM kwa wananchi.

9. FIDIA KWA WANANCHI WANAOISHI KUZUNGUKA MIGODI

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bado wananchi wanaoishi maeneo jirani na migodi wamekuwa wakisumbuliwa kupata haki zao, hasa anapotakiwa kuondoka maeneo ya mgodi ili kupisha shughuli za uchimbaji ziendelee. Wananchi wa Kitongoji cha Nyamichele katika Kijiji cha Nyakunguru, ambao walifanyiwa tathmini ya mazao na nyumba zao ili waweze kupisha mgodi uendeleee na shughuli za uchimbaji, sasa ni mwaka wa tatu hawajalipwa fedha zao.

Tathmini katika eneo hilo ilifanyika mwezi Aprili 2013 na toka kipindi chote hicho hawajalipwa na wamekuwa wakiishi maisha ya dhiki kutokana na kutofanya shughuli za maendeleo katika maeneo yao.

Pamoja na uvumilivu ambao wameunesha wananchi katika kipindi chote hicho, Serikali inataka kuwabagua katika malipo wanayostahili. Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Ndugu Glorius Luoga tarehe 19 Mei, 2015 aliuandikia Uongozi wa Kijiji (Mtendaji wa Kijiji) akitaka watu walifanyiwa tathmini wachambuliwe ili kubaini wazawa wa eneo hilo na wageni kabla ya malipo kufanyika. Huu unaonekana ni mkakati wa Serikali katika kuwabagua Wananchi wa eneo hilo, kwani hata Naibu Waziri wa Nishati na Madini (Charles Muhangwa Kitwanga) alipofanya ziara katika maeneo hayo tarehe 04 na 05 Mei, 2015 alielekeza watu wachambuliwe kabla ya kufanyiwa malipo.

Wananchi wa maeneo hayo, wanapinga kabisa hatua hiyo kwani hailengi kuwatendea haki na wanahoji mambo yafuatayo:-

- i. Ni kwa nini hoja ya kuwabagua (Wazawa na Wageni) haikuletwa kabla au wakati wa tathmini?
- ii. Mbona katika tathmini zilizotangulia katika maeneo yanayopakana na eneo hilo hakukuwa na kitu kama hicho?

- iii. Mbona tathmini iliyofuata katika maeneo mengine yanayozunguka mgodi ilifanyika na Wananchi wakalipwa bila kubaguliwa?
- iv. Ni kwanini Serikali ndiyo inataka kuwabagua Wananchi wakati mgodi uko tayari kulipa Wananchi wote wanaostahili kulipwa haki zao kulingana na tathmini iliyofanyika?
- v. Iwapo utaratibu wa kulenga kulipa Wazawa utafuatwa, je, wananchi wengine ambao ni wakazi wa pale na ambao maeneo yao yalifanyiwa tathmini ni nani atawalipa haki zao?
- vi. Je, kuzuiwa kufanya shughuli za maendeleo kwa kipindi cha miaka 3 baada ya tathmini ni haki?

vii. Je, ni kwanini vikao halali kwa maana ya mkutano mkuu wa kijiji ambao ulikuwa na viongozi halali kwa maana ya mtendaji, mwenyekiti wa kijiji na vitongoji pamoja na mihutasari umeazimia kutochambua wananchi kwani ni ubaguzi bali walipwe wote waliofanyiwa tathimni?

10. KUFANYA SHUGHULI ZA MGODI NDANI YA MITA MIA MBILI

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgodi wa Acacia unaendelea kufanya shughuli za uchimbaji ilihari kuna watu ndani ya mita hamsini, kitendo hiki kimeendelea kuatarisha maisha ya wananchi hawa. Wanapata athari za nyumba zao kubomoka, matatizo ya vifua vikuu, mimba kuharibika, watu kulemazwa na madhara mengine mengi.

Hivi tunavyoendelea na vikao kuna wananchi juzi waliumia na wakakimbizwa hospitali ya Bugando kwa matibabu ikiwemo mtoto mdogo aliepigwa kichwani na kipande cha nyumba iliyobomoka kutohana na athari za mlipuko. Ni dhahiri serikali hii ya chama cha mapinduzi haithamini maisha wa wananchi wake. Kwani ni mkutano wakati wa bajeti ya wizara ya Mazingira mhe. Matiko alishika shilingi ya waziri ili kupata ufumbuzi wa haraka kwa wananchi wanaoishi ndani ya mita mia mbili hasa wa kitongoji cha Nyabikondo, Nyabichune na mijini kati kata ya matongo Tarime wahamishwe ili sasa wapishe shughuli za uchimbaji ili kunusuru maisha yao, cha ajabu kama ilivyokawaida wabunge wa ccm kwa wingi wao walipinga hoja ya Mhe. Matiko na kuitisha mgodi uendelee na uchimbaji hata kama wananchi wale wanaathirika. Nadhani wananchi wa tarime na watanzania wanaona nani mwenye nia njema na maendeleo yao Jibu ni ukawa na mwaka huu ndo

11. KUNYANYAPAA WAWEKEZAJI WA NDANI

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kuonesha kutokuwa tayari kwa Serikali katika kuwasaidiawatanza kumiliki rasilimali za taifa hili, serikali kuitia kwawaziri aliyekuwa na dhamana ya nishati na madini Profesa Muhongo alisikika akiwaambia watanza kwamba; "Kampuni za Mengi zimeshikilia vitalu 59 vya madini vyenye ukubwa wa mita za mraba 3,752.37 (sq km) sawa na Dar es salaam tatu, amevishikilia, ameshindwa kuvienda. Watanzania wanakosa mapato na ajira! Sasa anataka vitalu vya gesi na mafuta. Je, huu ndio uzawa... tutaoa orodha ya vitalu vya madini vilivyoko mikononi mwa Mengi ambavyo anafanya ulangazi. Ukweli utaonyesha ubabaishaji na ulangazi wa Mengi wa genge lake."

Tunaamini kuwa hatua ya kwanza kwa wazalendo kuwekeza na kunufaika na rasilimali za nchi, kwanza ni kumiliki rasilimali husika na kwa kuwa wanakosa mitaji, basi hatua ya pili ni kutafuta wabia katika uvunaji wa rasilimali hizo. Hii ndio "**best practice**" duniani kote. Haiwezekani wazawa wakanufaika bila ya kwanza kuwa na umiliki wa rasilimali husika. Haiwezekani kuingia ubia kama mzawa kwa kitu ambacho hauna umiliki nacho.

Kambi Rasmi ya Upinzani inahitaji kuelewa kama huo ndio msimamo wa Serikali hadi sasa au ulikuwa ni msimamo binafsi wa Mhe Prof. Sospeter Muhongo?

12. TAARIFA YA MKAGUZI NA UBADHIRIFU TANESCO

Kwa mujibu wa kifungu Na. 54(2(d)) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 na Kanuni Na. 20(2 (e)) ya Kanuni za Sheria ya Ununuzi ya Umma ya mwaka 2005. Kinyume na matakwa haya, katika ukaguzi wa hesabu za Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO) mkaguzi alibaini ununuzi wa takribani Shilingi za Kitanzania Bilioni 3.2 kupitia zabuni Na.PA/001/13/HQ/H/106 bila kuzingatia kiasi kilichotengwa kwenye bajeti yaani Shilingi za Kitanzania Milioni 400.

Katika zabuni nyingine Na.PA/001/13/HQ/H/G/106 TANESCO waliingia mkataba wa Shilingi za Kitanzania milioni 340.8 ambayo ni zaidi ya bajeti iliyotengwa ya Shilingi za Kitanzania milioni 154. Ukaguzi huu haukuweza kupata ushahidi wa kuwepo kwa marejeo ya bajeti kwa kiasi kilichotumika nje ya makisio.

Kambi Rasmi ya Upinzani inapata taabu kuelewa ni kwa vipi TANESCO inapata udhubutu wa kutumia hivyo bila kufuata utaratibu uliowekwa kisheria, na kama dharura inatokea, je wakati wa maandalizi ya bajeti yao na hadi inapitishwa na bodi dharura haiwekwi? Au ni njia nyingine ya wizi unaendelea katika shirika hili?

Aidha,kulikuwa naucheleweshwaji wa miradi uliopelekeea kuongezeka kwa gharama zisizokuba za lazima. Mapitio ya zabuni Na.PA/001/08/HQ/W/46 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 34,848,390.78 kwa ajili ya ujenzi wa mtando wa umeme kiwango cha 132KV, mradi huu ulipangwa kumalizika ndani ya miezi 18 yaani Septemba 2011. Hata hivyo, mradi huu ulichelewa kukamilika hadi Juni 2013 kutokana na ugumu uliojitokeza wa kupata eneo la mradi. Hii ni aibu kwani haiwezekani ukasaini mkataba bila ya kuwa na eneo la utekelezaji wa mradi husika.

Kwa ucheleweshwaji huu Mkandarasi na Mshauri Mwelekezi walianza kazi bila kuwa na mkataba halali hivyo kupelekeea TANESCO kutakiwa kulipa gharama za kusubiria kuanza kazi kiasi cha Euro 981,831, Dola za Kimarekani 1,423,098.60 pamoja na adhabu ya Dola za Kimarekani 682,940.09.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hili ni dhahiri kabisa kwa Kambi Rasmi ya Upinzani kusema kuwa TANESCO inafanyakazi zake "ki-ubabaishaji" jambo ambalo linatia hasara walipa kodi wanchi hii. Je,ubabaishaji huu utaendelea hadi lini? Kwani mikataba ya kiujaunja ndiyo inalifilisi shirika hilo.

13. WAKALA WA USAMBAZAJI UMEME VIJJINI-REA

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakala huyu alianzishwa kwa sheria Na 8 ya mwaka 2005 na alianza kazi rasmi oktoba mwaka 2007, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa sera ya Taifa ya Nishat i ya mwaka 2003. Lengo likiwa ni kuwapat ia wananchi waishio vijijini nishati bora. Pamoja na umuhimu wa wakala huyu bado serikali haijaonyesha kwa vitendo kuwa ina nia ya kusaidia wakala huyu ili aweze kut imiza majukumu yake kikamilifu na hasa linapokuja suala la kuupat ia fedha kama zinavyoombwa na zinavyopitishwa na Bunge hili.

Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 wakala alihitaji kiasi cha shilingi **bilioni 366.9** kwa ajili ya kutekeleza miradi sita ya nishati vijijini. lakini kwa kipindi cha mwaka wa fedha 203/2014 tayari bunge hili limeambiwa kuwa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ilitolewa asilimia 42.32 tu.

Kwa mwaka 2014/15 bajeti iliyokuwa imetengwa kwa ni shilingi bilioni 292.6 lakini hadi mwezi Machi 2015 kiasi kilichokwuwa kimepokelewa toka hazina ni shilingi bilioni 100.56 sawa na asilimia 37 tu. Kama ilivyo kwa wizara ya Ujenzi hadi kufikia mwezi Machi 2015 REA inadaiwa na wakandarasi kiasi cha shilingi bilioni 124. Je hapa ni kweli kuna kusambaza umeme vijiji?

Kwa mujibu wa takwimu za Mdhibiti wa maji na mafuta zinaonesha kuwa kuanzia Januari 2011 hadi Desemba 2014 mafuta yaliyoingizwa nchini ni meta za ujazo 8,660,160.40 ambazo ni sawa na lita 8,660,160,400. Kwa mujibu wa sheria tozo ya mafuta kwa lita moja ni shilingi 50. Hivyo basi kwa kipindi hicho REA ilitakiwa kupata jumla ya shilingi bilioni 433.01 kama tozo ya mafuta tu. Kulingana na takwimu hizi kama Serikali haikupeleka fedha hizo REA, ni sababu gani za msingi? Taarifa ya REA inaonesha hadi Machi 2015 kiasi kilichopokelewa ni shilingi bilioni 144.2 tu na bakaa ambayo haijapokelewa na REA hadi mwezi Novemba 2014 ni shilingi bilioni 36.5.

Huu ni mfano mmoja wapo kuwa Serikali ya CCM haiheshimu sheria zilizopo. Kwani tozo ya mafuta imelipwa na TRA inazo fedha hizo, sasa ni kwanini fedha hizo hazina haizipeleki sehemu husika kwa mujibu wa sheria?

Kwa mwaka huu wa fedha mahitaji halisi ya wakala kwa ajili ya kutekeleza miradi katika mpango wa kusambaza umeme vijiji awamu ya pili ni takribu shilingi bilioni 881, na kwa miradi inayoendelea kutekelezwa ya awamu ya kawanza naya pili zinahitajika shilingi bilioni 552.3.

Kwa ujumla wake ili wakala ufanye kazi zake na kufikia malengo yaliyowekwa wanahitaji shilingi bilioni 1,433.3. Hoja ni je Serikali ya CCM inaweza kutoa kiasi hicho cha fedha? Kwa kuwa kiasi hicho hakiwezi kupatikana, kinachofanyika sasa ni kuwatapeli wananchi kwa kusambaza nguzo tu na sehemu ziingine wazisimika tu na sehemu zingine wanaunganisha nguzo tatu au nne kwa waya ili wananchi waamini kuwa umeme unaletwa.

Hakuna kitu kibaya kama kutoamatumaini kwa watu wakati unajua kabisa hauna uwezo wa kutekeleza yale yanayoahidiwa. Hii ndicho kitakachopelekea kifo cha Serikali ya CCM kutoa matumaini ya uongo, kwani wanaelewa kabisa kuwa REA haipewi hela za kufanya kazi hiyo.

14. SHIRIKA LA MADINI LA TAIFA- STAMICO

Mheshimiwa Mwenyekiti, STATE MINING CORPORATION (STAMICO) ni shirika la umma lililo chini ya wizara lilianzishwa chini ya sheria ya makampuni sura 257 ya mwaka 1972 na pia sheria hiyo ikafanyiwa marejeo au marekebisho 2014. Sheria mpya ya madini ya mwaka 2009 ambayo iliifuta sera ya madini ya mwaka 1997, lengo kuu la sera hiyo mpya ilikuwa na kuifanya serikali kushiriki katika uwekezaji wa madini kwa kuititia taasisi zaka kama sera hiyo inavyosema.

Ili kwenda sambamba na sera hiyo ya madini ya mwaka 2009, Bunge lilitunga sheria mpya ya madini ya mwaka 2010 ambayo iliweka kifungu ambacho kinaipa haki Serikali kuititia taasisi zake kujihusisha na uwekezaji katika madini. Katika kuifanya hivyo, STAMICO ikawa ndio taasisi ya Serikali inayoendesha jukumu hilo na likafanyiwa maboresho ya kimuundo.

Toka uboreshwaji huo wa kimuundo wa STAMICO, shirika hilo limejitatidi kujiweka kiushindani lakini kutokana na kutokuwa na mtaji wa kutosha ni dhahiri haliwezi kuwa shindani na tija yake kwa nchi haiwezi kupatikana kwa miaka ya hivi karibuni.

Licha ya kutokuwa na mtaji wa kutosha wa kufuanya kazi, lakini bado shirika hili limeshindwa kukusanya fedha ambazo washirika wake walioingia Mkataba nalo wameshindwa kutimiza matakwa ya mkataba husika.

Katika mkataba ambao STAMICO iliingia na Kampuni ya **Tanzania American International Corporation (2000) Limited** ili kuendeleza mgodi wa 'Buck Reef Gold Mine'. Katika mkataba huu ilikubalika kwamba uzalishaji utaanza ndani ya miezi 30 toka siku ya kutiliana saini makubaliano na endapo muda wa kuanza uzalishaji utachelewa, "**Tanzania American International Corporation (2000) Limited**", ilianzishwa tarehe 24 Oktoba, 2011 kwa madhumuni ya kuendeleza mgodi huo, ilikubalika kuwa kucheleweshwa kokoteingellipa STAMICO fidia ya ucheleweshaji kiasi cha Dola za Kimarekani 500,000 kama mradi utasogezwa mbelekwa mara ya kwanza, Dola za Kimarekani 625,000 kwa mara ya pili na Dola la Kimarekani 750,000 kwa vipindi vyovoyote vitakavyofuata.

Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Waziri alieleza Bunge hadi sasa mradi huo umeanza au bado na kama bado kwa mujibu wa Mkataba STAMICO inatakiwa kulipwa toka kwa Mshirika wake kwa mujibu wa matakwa ya mkataba husika.

15. SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA-TPDC

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika hili la mafuta ndilo lililo na jukumu la msingi la kuhakikisha kuwa raslimali ya mafuta na gesi iliyo hapa nchini inajulikana ilipo na inajulikana kiasi cha hazina kilichopo na inavunwa na nani na watanzania watanufaika vipi na raslimali hizo. Katika kutekeleza hayo yote inatakiwa kuwa na fedha za kutosha kwa pale uhitaji wa TPDC kuwekeza unakuwepo, pale ambapo mikataba inayoingiwa kutafuta watu wenye utaalam wa ziada kwenye fani ili kutokuiiza nchi kwa mikataba kama ile iliyoingiwa na Serikali na Kiholanzi ya MSI wakati wa kuibinafsia Kampuni ya simu TTCL. Aibu hiyo sasa hivi inakuwa ni aibu ya watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wahenga wanasema "**mchuma janga hula na wakwao**" hilo la mkataba wa ubinafsishaji hadi sasa watanzania wanalipia. Sasa ili kuondokana na uchafu uliotokea kipindi hicho, ndio maana tunaitaka TPDC kuwa na taaluma inayotakiwa katika kuhakikisha uwekezaji wa rasilimali zetu za mafuta na gesi zinakuwa na manufaa kwa kizazi kijacho.

Hilo haliwezi kufanikiwa ikiwa bajeti ya maendeleo ambayo inapangwa haitolewi, mwaka wa fedha 2014/15 kwa fedha za maendeleo zilitengwa jumla ya shilingi bilioni 138, na hadi mwezi machi TPDC ilitarajia kupokea jumla ya shilingi bilioni 103.5 lakini ilipokea shilingi bilioni 53.295 tu. Hivini kweli kampuni inaweza kuwa na "**burgaining power**" uwezo wa kibashara?

Unyonge wa fedha unaolikumba shirika hili ndio unaopelekea mapato ya gesi kutokukusanywa kwa kadri mikataba na sheria zinavyosema. Kwa mujibu wa taarifa ya TPDC inaonesha kuwa Songas na Pan African Energy zinadaiwa jumla ya shilingi bilioni 69.285. Je, kwa mwendo huu gesi hii inaweza kuwa na manufaa kwa wananchi, Kama madeni yanashindwa kudaiwa kwa kusimamia mikataba iliyopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2014/15 kambi Rasmi ya Upinzani ilihoji yafuatayo katika eneo hili la TPDC lakini haikupata majibu toka Serikalini.

Waziri wa Nishati na Madini alipokuwa anazindua Bodi mpya ya Shirika la Maendeleo ya Pet rol alitoa maagizo ya kuiti ia mikataba yote ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta kupitiwa upya baada ya kuonekana ya kuwa ilikuwa na hisia za rushwa na haina maslahi kwa nchi. Aidha maelezo kuwa Muundo ulishirikisha wafanyakazi wote management, TUICO na Bodi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Inasema kuwa huo sio ukweli kwasababu muundo uliotengenezwa ambao ulishirikisha hao hapo juu ulipelekwa Wizara ya Nishati na hadi leo haujawahi kujibiwa. Muundo unotelekelezwa sasa ni muundo uliotengenezwa na Wizara na Bodi kwa siri. Kuna vitengo vimefutwa, na kuna kazi zilizofutwa na wanaozishikilia hawajaelezwa hatima yao.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kupata majibu katika masuala yafuatayo kutoka kwa Waziri waNishati na Madini;

(i) Ni hatua gani zimechukuliwa kwa waliobainika kuwa walihusika katika kuingia mikataba mibovu?

(ii) Mikataba yote ya PSA na hususan ile ambayo inakaribia uzalishaji imeongezewa "Addendum" za kifisadi zenye vipengele ambavyo havina masilahi kwa nchi ila vinamnufaisha zaidi mwekezaji?

Mikataba iliyoongezewa "addendum" ni ya STATOI L ambao wapom pamoja nja EXONMOBIL na ile ya BG wakiwa pamoja na OPHIR. Kwa sasa OPHIL wameuza baadhi ya nhisa kwa Kampuni moja kutoka Singapore. Tunaomba Rais wetu aingilie kati kwani Wizara imethbit isha kutokuwa na uwezo wa kurekebisha hali iliyopo. Serikali ilishakiri ya kuwa mikataba upande wa madini haikuwa kwa maslahi ya nchi. Tunaomba Serikali iangalie kwa upana hii mikataba ya utafutaji na uchimbaji wa gesi kwani kuna kila dalili ya kwamba nchi haitaweza epuka laana ya gesi kutokana na mikataba iliyopo.

(iii) Badala ya bodi kutekeleza majukumu iliyopewa, kazi yake ni kusafiri nje ya nchi kila kukicha. Mwenyekiti i wake amefanya safari sita nje ya nchi kuanzia Januari mpaka May 2014 tu. Inatisha!!!!!!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Utoaji wa Vitalu Bila Kufuata Taratibu, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania lilitoa vitalu kwa Kampuni ya OPHIR bila kutangaza Tenda, tunaomba maafisa wote walioshiriki kutoa vitalu kwa Kampuni ya OPHIR wachukuliwe hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyejewa Mkurugenzi wa Utafutaji na Uzalishaji wa mafuta na gesi amejiunga na kampuni ya Ophir. Kampuni hii ilipewa kitalu bila kufuata sheria za manunuzi, leo mkurugenzi huyu amestaafu amejiunga nayo na kupewa wadhifa mkubwa. Nchi yetu kweli tutafika!

Alieshindwa Kuendeleza Kitalu cha GesiAnalindwa. Kampuni ya HYDROTANZ inayomilikiwa na Bwana SING (SINGASINGA) ambae ndiye aliyenunua IPTL kuiti ia kampuni yaPAP ndiye mmiliki wa kampuni ya HYDROTANZ ameshindwakuendeleza kitatu alichokuwa amepewa kwa mujibu wa Mkataba. Alistahili kunyang'anywa kitalu husika kutokana na kushindwakukiendeleza ila kutokana na kulindwa na wizara badoameendelea kumiliki kitalu husika.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inajua kuwakuhusu Viongozi Walioshiriki Katika Mikataba Mibovu Kama Wa Songo Songo. Cha kushangaza ni kwamba Katibu Mkuu aliyejewo wakati wa utiaji saini mikataba inayosemekana nimibovu ya Songo Songo na PAN AFRIKA Mhe. Rutabanzibwa ndiye kwa sasa ni Mwenyekiti wa Kampuni ya Pan Afrika Tanzania.

Hivi sasa anafanya mbinu waziwazi za kuisafisha Kampuni hiyoambayo imeonekana kuwa na dosari lukuki za kiutendaji nakimaadili. Kampuni ya PAN AFRICAN ENERGY inafanya jitihada zamakusudi "ku-sabotage" mradi wa bomba la gesi asiliaunaoendelea kwa kutotekeleza majukumu yao ya kuongezakiwango cha gesi asilia kinachoweza kuzalishwa kwa ajili ya mradi huu mkubwa wa serikali.

16. WAKALA WA UKAGUZI WA MADINI TANZANIA-TMAA

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (Tanzania Minerals Audit Agency-TMAA) ni wakaashara wa Serikali ulioanzishwa tarehe 2 Novemba 2009 chini ya sheria ya Wakala wa Serikali, Sura ya 245. Lengo kuu la Wakala ikiwa ni kuhakikisha kwamba, Serikali inapata mapato stahiki kutoka kwenye shughuli za uzalishaji na biashara ya madini nchini

kupitia usimamizi na ukaguzi makini wa shughuli hizo, na kuhakikisha kuwa shughuli hizo zinafanyika kwa kuzingatia uhifadhi na utunzaji thabiti wa mazingira katika maeneo ya migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Wakala inasema kuwa;

"ilikujuu thamani halisi ya madini yaliyozaalishwa na kuuzwa nje, jumla ya sampuli 1,976 za madini yaliyozaalishwa na migodi mikubwa ya dhahabu zilichukuliwa na kufanyiwa uchunguzi kwenye maabara ya wakala".

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo ya wakala ni kiini macho kwa waheshimiwa wabunge kwani kwa uelewa wa kawaida tu haiwezekani sampuli zikakuwezesha kuelewa thamani halisi ya madini yaliyozaalishwa na kusafirishwa nje ya nchi. Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mhe Waziri kulitolea kauli suala hili ili kutoa uelewa mzuri kwa waheshimiwa wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kuweka wakaguzi kila mgodi ni sawa na kitendo cha Mkaguzi Mkuu wa Ndani kuweka wakaguzi kwenye halmashauri na mwisho wa siku wakaguzi hao wanakuwa ni sehemu ya Menejimenti za Halmashauri. Jambo hili nalo ndilo linalopelekea taarifa ya wakala kuwa kama ilivyonukuliwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema ili Wakala utele ufanisi uliokusudiwa na sheria ni lazima kubadilishwa kwa mbinu za ukaguzi wa migodi mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo inaonesha kuwa kulikuwa na kasoro zilizoipotezea Serikali stahili zake za mapato, kwa mujibu wa sheria kwa migodi mikubwa na migodi ya kati. Kwa kuwa wakala huyu majukumu yake ni kuhakikisha kile ambacho Serikali inastahili basi kinapatikana. Sasa inakuwaje tena anasema mapungufu hayo anayapeleka kwa taasisi husika za Serikali kwa hatua zaidi na nyingine zimepelekwa kwa wamiliki wa migodi? Kambi Rasmi ya Upinzani ingetarajia kuelezwu ni hatua gani wakala amechukua ili Serikali kupata kile inachostahili kupata. Aidha kuhusu ukaguzi wa shughuli za ukarabati na utunzaji wa mazingira migodini, taarifa inaonesha kuwa kasoro zilizobainika wakati wa ukaguzi wa migodi mikubwa ni:

- a. Uhifadhi na matumizi ya kemikali mbalimbali usiofaa
- b. Usomamizi mbovu wa makapi yatokanayo na uchenjuaji wa madini
- c. Uchafuzi wa mazingira utokanao na utupaji wa vifusi taka usiozingatia kanuni na taratibu na,
- d. Uchafuzi wa mazingira utokanao na uvujaji na utiririshaji wa oil chafu kutoka kwenye mashine na vyombo mbalimbali;

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ya wakala inakubaliana kabisa na hoja za wakazi hasa wa Nyamongo –Tarime na kijiji cha Katoma na vitongoji vingine vya karibu vya Nyakabale na Mgusu - Geita vinavyozunguka migodi mikubwa ya madini kuwa walipata madhara makubwa ya wao kuathirika binafsi na pia kupoteza mifugo yao kutokana na maji yenye sumu yatokanayo na uchenjuaji wa madini na kutiririka kwenye vyanzo vya maji wanayotumia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kuwa KAMATI MAALUM YA BUNGE katika Bunge la Tisa, ilikwenda Nyamongo kuangalia madhara wanayopata wananchi kutokana na taka sumu zinazotoka kwenye mgodi wa North Mara ulipo TARIME, lakini hadi leo hii taarifa hiyo haijawahi kuleta katika Bunge hili. Hili linatupa wasi wasi zaidi kwa ufuatiliaji wa Bunge kwa masuala makubwa ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo inatueleza kuwa mgodi mkubwa wa Golden Pride uliofungwa kuna mapungufu mengi sana yaliyojitekeza kwani hayakufanyiwa ukarabati wa mazingira kama inavyotakiwa. Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuangalia haya mapungufu yaliyotolewa na

wakala ni dhahiri kwamba Serikali ya CCM haiku "**coordinated**" kwani Kama bunge ilitakiwa kupokea taarifa ya utekelezaji wa Wakala kwa kushirikiana na NEMC kuhusiana na **KAMPUNI YA GOLDEN PRIDE** iliyokuwa inafanya shughuli zake Wilaya ya Nzegabadala ya kutoa taarifa ya kulalamika tu. Ni muda mwafaka sasa kuwa Serikali isiyowajibika kukaa pembedi na kuwapisha wengine waoneshe kwa vitendo uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

Esther N.Matiko (Mb)
K.n.y Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upizani-Wizara ya Nishati na Madini
06.06.2015

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, sasa nitatambua wageni ambao wapo ndani ya Ukumbi.

Wageni wa Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nishati na Madini, ambao ni familia yake; Ndugu Mariano Nano, mke wake; Karita Simbachawene, mtoto wake; Renatha Simbachawene, dada yake; Dominican William Nau, shemeji yake; na Ndugu Yusuph Semguruka, shemeji yake. (Makofii)

Wageni wengine wa Mheshimiwa Simbachawene, Waziri wa Nishati na Madini kutoka Wizarani ni Ndugu Ngosi Mwihava, Kaimu Katibu Mkuu; Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi wa Taasisi na Mashirika ya Wizara; Wakuu wa Idara na Vitengo; na Wakuu wa Taasisi; Makamishna Wasaidizi; Wakurugenzi na Mameneja Wakuu wa Miradi; Wakaguzi wa Nje; Wadau kutoka Sekta ya Madini; Wahisani na Washirika wa Maendeleo; Wadau kutoka Sekta ya Nishati; na Maafisa kutoka Taasisi za Wizara; karibuni Dodoma. Vilevile wapo wageni 16 kutoka Jimboni kwa Waziri Kibakwe. Karibuni sana, Waziri wenu anafanya kazi nzuri sana. (Makofii)

Wageni wa Mheshimiwa Charles Kitwanga, Naibu Waziri wa Nishati na Madini ambao ni Ndugu Amir Lugendo, rafiki yake; Maafisa kutoka Chuo cha Madini wakiongozwa na Ndugu Ramadhan Singano, Makamu Mkuu wa Chuo; na Umoja wa Wachimba Madini wa Marema Manyara; karibuni Dodoma.

Wageni saba wa Mheshimiwa Charles Mwijage, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, ambao ni Wafanyakazi wa Kiwanda cha Dodoma Wine. (Makofii)

Wageni wa Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, mbao ni Ndugu Benjamin Mpamo na Ndugu Tumaini Magori; karibuni. (Makofii)

Wageni sita wa Mheshimiwa Magalle Shibuda, wakiongozwa na Ndugu Joseph Paroko, Katibu wa Chama cha Wafugaji Kanda ya Magharibi; karibuni. (Makofii)

Mgeni wa Mheshimiwa Salum Halfan Barwany, ambaye ni Dkt. Zuberi Sigar, Mshauri wa Chama cha Wazalishaji wa Chumvi Tanzania. (Makofii)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Richard Ndassa, ambao ni Ndugu Zabron Kisendi Gagayi, Mwenyekiti wa Vijana CCM Kwimba; na Ndugu Pendo Gavana Machiru, Katibu wa Vijana CCM Kwimba. (Makofii)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Wageni 12 wa Mheshimiwa Josephine Chagula, ambao ni Wanachuo kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma; karibuni Dodoma. (Makofi)

Wageni wa Mheshimiwa John Cheyo, ambao ni Waheshimiwa Madiwani 11 kutoka Bariadi; wamekosa nafasi Ukumbini.

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni Wanafunzi 60 wa Chuo cha Saint John Dodoma; Wanafunzi 12 kutoa chuo cha Ustawi wa Jamii Dar es Salaam; na Wanafunzi 57 kutoka Chuo cha Uhasibu (TIA) Dar es Salaam.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Deo Sanga!

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii ya kukushukuru kwa kunipa nafasi niwe na mimi mionganoni mwa wachangiaji wa Wizara hii ya Nishati na Madini. Kabla sijashukuru, kwa niaba ya Wananchi wangu wa Jimbo la Njombe Kaskazini, naomba niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza Hotuba ya Waziri, Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati na Hotuba ya upande wa pili wa Kambi Rasmi ya Upinzani. Jambo ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani wamelisema hapa, nadhani wameanza Waheshimiwa Wabunge wenzangu kama ambavyo tulipaonza Serikali hii ya Awamu ya Nne ya Jakaya Mrisho Kikwete, ilipoanza kujenga Shule za Sekondari kila Kata walisema yeboyebo, imeanza tena hii kazi ya nishati na madini. Hivi kweli Waheshimiwa Wabunge umeme wa REA unakwenda vijiji wanasema tunawahadaa Watanzania; ni kweli? (Makofi)

Jamani tuwe wakweli hapa, tunawahadaa Watanzania kwa kazi nzuri ambazo zinayofanya. Mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kazi nzuri anayofanya. Nimpongeze Waziri pamoja na Manaibu wake, Makatibu wake na Watendaji wake, kwa kazi nzuri wanayofanya. (Makofi)

Leo tunahadaa kuna nguzo kule; ndiyo pale niliposema tulipoanza kujenga sekondari wakasema shule za yeboyebo! Hivi unaanza kuweka nguzo ardhini au unaanza kuweka waya; si unaweka nguzo kwanza? Sasa nguzo zinawekwa kule na kazi inafanyika nzuri. Kwangu pale Wananchi wangu wa pale Kijiji cha Maguvani umeme umewashwa wanawahadaa? Umeme umeshawashwa. Ukitoka Makambako kuja Jimbo la ndugu yangu pale wa Mfindi, Kigola, ukitoka Makambako barabara hii ya Mbeya unakuja vijiji vya barabarani vyote mpaka Malangali Shuleni kule Sekondari umeme upo. Umewashwa tayari; sasa hiyo ni kuwahadaa Watanzania? (Makofi)

Mheshimiwa Mrema, uko Upinzani, ndiyo haya mliyokwenda kujadili mambo ya kwamba tunawahadaa Watanzania? Mrema, kwako kule umeme umewekwa pale ni kuwahadaa Watanzania kweli! Hapana, nakushukuru sana Mrema. Serikali ya Awamu ya Nne imefanya kazi nzuri na shughuli inakwenda vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia juu ya Mradi mkubwa wa kutoka Makambako...

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hebu vumilieni, kila mtu hapa atasema ya kwake atajibiwa humu humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru hotuba ya Mheshimiwa Waziri juu ya mradi mkubwa wa kutoka Makambako kwenda Songea kuitia Kata mbalimbali katika Jimbo langu. Nashukuru hotuba imeeleza vizuri, Serikali imelipa fidia kwa wananchi, ni kweli wameshalipa fidia. Ombi langu kwa Serikali, hawajaniambia sasa na hela zimetengwa juu za mradi huu mkubwa wa kutoka Makambako kwenda Songea. Naiomba Serikali, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha aniambie, kwa sababu amesema hela zipo tayari, mradi huu utaanza lini? (Kicheko)

MBUNGE FULANI: Aaaah! (Kicheko)

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji ambavyo vitapitiwa na mradi huu mkubwa ni vizuri nikataja Kata zifuatazo: kuna Kata ya Liamkena pamoja na vijiji vyake, vinapitiwa na mradi huu mkubwa, kuna Kata ya Igongolo inapitiwa na vijiji vyake, kuna Kata ya Kichiwa inapitiwa pamoja na vijiji vyake ambapo fidia hizo zimeshalipwa, kuna Kata ya Matembwe Kijiji cha Wanginyi na Kata ya Idamba. Kwa hiyo, maadam fedha zipo, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha, aniambe ni lini mradi huo utaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena. Lazima tuishukuru Serikali ya awamu ya nne kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kufanya katika shughuli hizi za umeme wa REA. Ukipita humu njiani umeme upo na sehemu nyingine zimeshawashwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Lakini niseme, Jakaya Mrisho Kikwete kwa kazi aliyoifanya; hata Yesu alipofanya kazi kubwa, wapo wanaume walisema asulubiwe! Asulubiwe! Baadaye waliona kazi ambayo anaifanya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete amefanya kazi nzuri pamoja na Mawaziri wake kama nilivyosema, ni lazima tupongeze. Wewe Mheshimiwa Simbachawene pamoja na timu yako songa mbele. Unapoona watu wanasema hujafanya, wewe songa mbele na kazi inaonekana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda nimalizie, kuna vijiji viwili ambavyo nilileta maombi maalum. Katika vijiji hivyo ambavyo vinapakana na mradi ambao unaendelea ni Kijiji cha Mlowa ambacho kinapakana na kazi ambayo mmemalizia hivi juzi; kuna kijiji cha Mawande nacho nilileta ombi maalum, ambapo Naibu Waziri alipokuja katika Jimbo langu alitembelea vijiji hivyo. Naomba katika maombi maalum tuwape umeme ili wawe sawa na wenzao wa vijiji vinavyopakana. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, kuna Jimbo la Njombe Kusini kwa Mheshimiwa Spika; vijiji hivi ambavyo Kata zake zinapata umeme huu mkubwa kama nilivyosema wa kutoka Makambako kwenda Songea ni pamoja na Kata ya Kifanya pamoja na vijiji vyake, Kata ya Kobi pamoja na vijiji vyake na Kata nyingine zinazozunguka katika eneo lile ambalo linapata umeme huu wa gridi ya Taifa kutoka Makambako kwenda Songea. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niseme maneno yafuatayo: namshukuru sana Mheshimiwa Mrema kwa kusema ukweli kwamba umeme ambao wananchi wana mategemeo makubwa sana kule vijijini, na kwake Mheshimiwa Mrema hapa anakiri kwamba baadhi ya vijiji ame...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Gervas Mbassa, ajiandae Mheshimiwa Susan Kiwanga.

TAARIFA

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa! Samahani, taarifa!

MWENYEKITI: Taarifa!

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilitaka tu tuweke sawa lile la Mheshimiwa aliyetoka kuzungumza, namheshimu sana. Ni kwamba taarifa ya Kambi ya Upinzani ukurasa wa 22, 23, 24 na 25 kuhusu Wakala wa Usambazaji Umeme (REA) hakuna mahali ambapo Kambi ya Upinzani imesema Serikali inawahadaa wananchi, isipokuwa kilichoandikwa (naomba usikilize. Hii ndiyo taarifa. Kimeandikwa kwenye taarifa! Soma kwenye taarifa) kwenye taarifa ni kwamba Serikali haipeleki fedha REA. Sijui kama mmenielewa!

Kwa hiyo, Kambi ya Upinzani tunataka Serikali ipeleke fedha kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili wananchi wapate umeme inavyotakiwa. Tunaitakia mema REA, *tusi-manipulate language* kana kwamba sisi hatutaki umeme. REA wamefanya kwangu na wameendelea kufanya maeneo mengine. Ni fedha za Watanzania na tunataka Serikali ipeleke fedha, na huo... (Makofii)

MWENYEKITI: Ahsante, inatosha. Mheshimiwa Mbassa!

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia asubuhi ya leo, lakini kabla sijaanza mchango wangu, naomba watu watambue Kambi ya Upinzani tunapoongelea, hatuongelei sehemu moja moja, ni maeneo yote. Kubwa tunalolihitaji ni miradi hii itekelezwe kama vile Bunge tunavyokuwa tumezimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 20 kuhusu miradi hii ya Umeme vijijini. Ni kweli katika Jimbo langu la Biharamulo ni mojawapo ya sehemu ambako miradi hii imetekelezwa na imekwenda vizuri. Nashukuru kwa kazi ambayo imefanyika katika Kata ambazo tumeanza nazo; Kata ya Kabindi, Runazi, Nyarubungo, Nyamahanga, Rusaunga na Nyakahula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwa na tatizo kubwa sana kwamba kuna kata nydingine ambazo zingeweza kupata, hajizapata. Naomba REA wanapokuja katika awamu ifuatayo; Kata za Nyamigogo, Nyabusozi, Inemba, Nyantakala, Kaniha, Kalenge Bisibo na Ruziba nazo ziwekwe katika mpango ili kusudi wananchi wapate umeme na waweze kufanya uzalishaji ili kujikwamua kimapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mradi huu, kumekuwa na matatizo kidogo. Kuna baadhi ya wananchi ambao walikuwa wameomba kuunganishiwa, lakini imefika mahali hawaunganishiwi. Sasa unashindwa kumbada Mkandarasi au TANESCO. Naomba tafadhali Wizara inapokuja ituwekee bayana hawa wanaohitaji kuunganishiwa ambao tayari umeme ulishapita maeneo yao, wanaziona nyaya zinapita na ilhali wanahitaji kuunganishiwa umeme, wanapatiwaje huduma hiyo ili kusudi nao waweze kufaidika na huduma hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika kitabu chake ukurasa wa 22, ni mradi mzima wa umeme katika Wilaya ya Biharamulo na Chato kwa maana ya mradi wa ORION.

Napenda kwanza kumshukuru Mheshimiwa Mwijage kwa jitihada zake, umeme umewaka juzi angalau kwa jenereta mbili zilizokuwepo, imeongezeka moja. Lakini bado kwa mahitaji ya Wilaya hizi mbili za Chato na Biharamulo unahitajika umeme mwingine. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila uchao Taifa linaongezeka, watu wanabuni miradi mbalimbali na mahitaji makubwa ya umeme yanahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujuu na Wizara watuambie, jenereta zetu hizi mbili za Mradi wa ORION ambazo nazo zilikuwa ni suluhisho kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya umeme, zitapatikana lini? Maana miradi imepangwa ya muda mrefu sana, lakini mpaka sasa utekelezaji wake umekuwa ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili tunaomba tafadhali jenereta hizi mbili ziletwe haraka sana kwani hizi zilizopo zimechoka na pamoja na hivyo, mahitaji bado ni makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 67 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kuhusu malipo ya mrahaba; tunashukuru kwamba yamekuwa yakifanyika huko, nyuma lakini mpaka sasa tumepata tatizo kubwa sana. Tangu Kampuni hii ya Tulawaka walivyokabidhiana na STAMIGOLD, Mheshimiwa Waziri umekiri kabisa kwamba wameweza kuchimba na kuzalisha wakia karibia 13,099 na kuza nje wakia 11,613 lakini bado kuna matatizo ya msingi sana ambayo tunahitaji kama Wilaya mtuletee majibu na mtusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tulawaka walipowauzia STAMIGOLD, kulikuwa na mrahaba ambaa ulikuwa unapashwa ulipwe, lakini mpaka sasa imekuwa ni danadana hatujui ni nini kinachoendelea katika mkataba wao. Kwa maana ya kwamba Tulawaka walisema wao mkataba huo wamewapa STAMIGOLD, STAMIGOLD wanapaswa walipe na STAMIGOLD wanasesma hapana, hili deni ni la huko nyuma. Sasa hivi kuna Bodi mpya, tunaomba hilo mlifanyie kazi, tujue nini hatima ya Halmashauri ya Biharamulo kupata mrahaba huo.

Vile vile kulikuwa na cess asilimia tano ya ujenzi. Eneo jipya limechimbwa, wameweza kupata hizo wakia mlizozitaja hapo juu, ni baada ya STAMIGOLD kuanza. Lakini ni kwamba hizo asilimia tano mpaka sasa hivi bado, kama Halmashauri yangu, haijapata. Hii ingeweza kutusaidia angalau hata kuinua mapato ya ndani ili kuweza kuweza kutekeleza yale yaliyopo. Tunaomba mtusaidie ili kusudi tuweze kupata kiasi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na suala zima la malipo haya ya service levy, yamelipwa tangu mwezi Julai na Septemba, 2014. Sasa sijui hapa katikati kumekuwa na nini kiasi kwamba kunakuwa ni mgogoro. Pindi tunapokosa pesa hizi katika Halmashauri, hakika uendeshaji wa shughuli unakuwa ni mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie suala zima la huduma ambazo mgodi unapaswa kuzitimiza kwa wananchi. Nashukuru kwa kazi iliyofanyika kwa Kata ya Mavota. Kata ya Mavota pale tumejengewa kituo cha kutolea huduma, kwa maana ya dispensary, shule, madawati yamepelekwa shulen na barabara ya kutoka Mavota mpaka Mbaba imetengenezwa. Lakini kuna shida ya wale watu ambaa wanapakana na lile bwawa lililojengwa na mgodi. Wanadai fidia na mpaka sasa hawajui watalipwa wapi na wamekuwa wakinipigia simu mara kwa mara. Naomba tafadhali Wizara ilifanyie kazi suala hili ili kusudi watu hawa wajue hatima yao ni ipi waweze kupata stahiki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba tunapoelekea, suala la upatikanaji wa umeme na uboreshaji wa Kituo cha Nyakanazi kwa maana ya kupokelea umeme; tumeshafanya mpango mkakati wa kupima maeneo haya. Kwa hiyo, wananchi ambaa

Nakala ya Mtandao (Online Document)

watakuwa kwenye hayo maeneo tafadhali wapewe fidia yao haraka ili kusudi kusiwepo tena na masuala ya kuzungushana na kuanza kunyoosheana vidole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (Makof)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Suzan Kiwanga, halafu Mheshimiwa Mansoor ajiandae.

MHE. SUSAN L. A. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Dah, muda mchache!

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja; kwanza naunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani. Vile vile nina mambo mawili makubwa kuhusu Wizara hii ya Nishati na Madini. Jambo la kwanza swali langu liliuja hapa Bungeni na Mheshimiwa Naibu Waziri aliniita ili aniambie ni maswali gani ya nyongeza ninayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nauliza kuhusu gesi. Kule Kilombero Kata ya Mofu kuna magari nami mwenyewe niliyashuhudia siyo chini ya mia yanakwenda kutafiti gesi, lakini mpaka leo wananchi wa Kilombero hawajui. Nyie Wizara vipi? Kwa nini hamwaambii wananchi wale? Huko huko wanasema kuna Mkusa, Ramsa, Site, mara ooh Selous lakini mnawaweka watu kule wanakwenda kutafiti gesi. Mbona wananchi hamjawaambia? Wanatega tega mambo yao kule, wananchi wanakwenda kule labda wanalima au wanakwenda kutafuta samaki mtoni, wakienda wakipambana na milipuko wakipata athari! Kwa nini hamwendi kutoa elimu kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tupate majibu, ni lini mtawaambia wananchi wa Kilombero kuhusu gesi inayopatikana ndani ya ile Wilaya na ni kiasi gani na iko maeneo gani na wao wafanye vipi? Mengine mnakwenda kutafiti kwenye mashamba yao. Au mnataka kutuibia? Au kwa sababu wananchi wa Kilombero sio wakali kama wa Mtwara? Nasema hata kule haitoki. Hiyo moja. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema, Wilaya ya Kilombero hapa kila siku hapa nauliza maswali kuhusu umeme. Ina kata 35, ina vijiji 110 na vitongoji kibao, lakini mmesema kule kuna mradi maalum, sawa. Nami nilishamnong'oneza Waziri pemberi maana nilifanya ziara kule, maana unamwona Mteketa hayupo hapa, sasa hivi amekumbuka shuka yaani kumekucha. Mimi kule nilishamaliza kazi! Hakuna kijiji wala kitongoji kule sijafika! (Kicheko/Makof)

Kwa hiyo, kuna maeneo Kilombero ambayo ina vyanzo vikubwa vyatuhu; Kihansi na Kidatu, lakini kama huyu mtu wa mradi yuko hapa, nakwambia wewe uje uzungumze name. Kwa sababu gani? Kuna kata kama ya Mchombe, Ching'anda, kule eti nguzo zimepita lakini katika vijiji haijaingia. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo ya taasisi ya shule, misikiti na makanisa hakuna nguzo zilizopita. Walifanyiwa tathmini mwaka 2011, lakini cha kushangaza, (naomba mnisikilize), huko Kata ya Mngeta kuna jamaa, huyu ndugu yangu anaitwa Beno Ndulu, yuko kule. Mwaka 2011 hajafanyiwa tathmini, leo wananchi wameachwa kuingiziwa nguzo hizo katika vijiji eti wamepeleka transfoma na nguzo kule Ndulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi, tutaonana wabaya mwaka huu! Haki ya Mungu! Tena aende haraka! Kule hajafanyiwa tathmini, leo mmepeleka transfoma na nguzo; lakini leo nimepata malalamiko mwananchi wa kawaida anaambwa hivi nguzo walipie Sh. 450,000/=. Kuingiza umeme ni Sh. 117,000/=, mbona Mtwara ambako gesi walikokatalia haitoki mmewapa

kwa Sh. 27,000/=? Sisi tuna vyanzo viwili vya umeme, mnatuambia kuingiza umeme Sh. 450,000/=, sijui Sh. 117,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi, kule kwa Ndulu wananchi wanasema umeme usiwake. Mkiwasha, imekula kwenu! Nguzo watalamba! Hiyo ndiyo habari ya mjini. Ninyi si mmezoea wananchi wa Kilombero ni wapole, sasa hivi hawakubali! (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wanataka mambo mawili mwajibu kuhusu umeme katika vijiji na katika Shule za Sekondari, mtapeleka lini? Kama mkataba wenu mliongia una mashaka, nendeni mkakae na wananchi, wana uwezo wa kuchangia, watauza mipunga yao, wanataka umeme. Hawataki kitu kingine! Nendeni! Hatutaki awamu ya pili wala awamu ya tatu; tumesasubiri sana sasa inatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme umetoka Kilombero umekwenda mpaka Zanzibar, Dar es Salaam na Mwanza. Mnatuone kwa sababu gani? Tunataka umeme, hatutaki kitu kingine. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shinyanga, nimetoka huko juzi. Shinyanga mjini yaani Kata ya Mwamanza, Mwamalili na baadhi ya vijiji, Kata ya Kuzimbu katika Manispaa ya Shinyanga, umeme hakuna. Shinyanga wanakozalisha madini, dhahabu kila kitu, leo mnaacha kuwapelekea umeme, kwa sababu gani? Nendeni mkafanye tathmini, pelekeni umeme Shinyanga na Kilombero. Haki ya Mungu mwaka huu, tunakula na ninyi sahani moja! Ninyi wenyewe mnajua kwamba Kilombero hakuna kitu, Shinyanga hamna kitu. Mwaka ule si mliiba? Safari hii watu wamejipanga, tunachukua kila kitu. Hiyo ndiyo habari yenyewe! Mkichelewa, tunachukua wenyewe, tunaweka umeme mpaka kwenye migomba kama ilivyo Kilimanjaro, tuko pamoja ndugu zangu? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiyo gesi na mafuta nataka mlete majibu hapa maana maswali yangu mmeyarudisha mara nydingi. Sasa leo nataka majibu hapa wakati mnakuja kurewind. Ahsante, mimi naenda zangu. (Makofii)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mansoor na Mheshimiwa Dkt. Kafumu ajiandae.

MHE. MANSOOR SHANIF HIRAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru umenipa nafasi na mimi nichangie hoja hii ambayo iko mbele yetu. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri sana aliyoisoma hapa. Naomba nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri na Manaibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza pia Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini Mheshimiwa Richard Ndassa kwa hotuba nzuri. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni-declare interest, mimi ni mdau wa mafuta, ni vizuri ni-declare interest ili mchango wangu ueleweke vizuri zaidi. Ni mtu ambaye nahusika moja kwa moja na shughuli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii pia kuwapongeza EWURA kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya. Sasa hivi ukifika EWURA kwa kweli pamebadilika, moja kwa moja wanakuhudumia vizuri ipasavyo, nawapongeza sana kwa hilo.

Pia nachukua nafasi hii kuwapongeza EWURA kwa kuandaa kanuni mpya kuhusu ujenzi wa vituo vijijini ambayo imeandikwa kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwenye aya namba 83. Naomba njue tu kama kanuni hiyo ambayo wameandaa mpya zimeanza kutumika au

bado? Kwa sababu tatizo la vituo vijijini lilikuwa ni tatizo kubwa, kwa sababu vituo vijijini huwezi kuvinganisha na vituo vya mjini.

Kwa hiyo, ukiweka masharti ambayo yanafanana kwa kweli unakuwa umemwonea mwananchi wa kijijini au mfanyakibashara ambaye anatoa huaduma kwa kuuza kerosene labda vijijini pale. Ukimwekeea masharti yanayofanana na ya mijini hapa kwa kweli unakuwa hujamtendea haki. Naomba kujua tu kama kanuni hiyo imeanza kutumika Mheshimiwa Waziri atatupa majibu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwengine naomba kutoa kwa EWURA kwamba kanuni na taratibu zao zilizoandaliwa zimepitwa na wakati kwa sababu kanuni hizo ambazo wanazitumia, zilikuwa zimeandaliwa wakati bulk procurement system ilikuwa haijaaanza ndani ya nchi yetu. Pia GFI haikuwepo. GFI ni ile ambayo wanaoweka dawa kwenye mafuta.

Kwa hiyo, nashauri kwamba hizo kanuni za EWURA ziangaliwe upya kwa sababu wakati ule ilikuwa siyo *single importation*, ilikuwa ni *importation* ambayo kila mtu anaweza akaleta mafuta kutoka sehemu yoyote anakotaka. Lakini sasa hivi tuna taratibu ya *bulk procurement*. Kwa hiyo, nashauri Wizara isimamie, EWURA waanze kuzitengeneza upya kanuni ili ziende na wakati kwa sababu biashara ya mafuta ni very dynamic, inabadilika. Kwa hiyo, nashauri pia kanuni hizo ziende na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalopenda kugusia hapa ni suala la *template* ya EWURA ambayo inatao bei elekezi kwenye soko, nayo inatakiwa iangaliwe kwa upya haraka sana kwa sababu hiyo *template* inakuwa na taratibu ya *formula* ambayo inasema M - 2. Maana yake, faida ya bei inaposhuka duniani, hupati moja kwa moja. Unasubiri kupata baada ya miezi miwili. Hiyo kwa kweli inanyima fursa kwa wananchi kupata mafuta kwa bei nafuu wakati bei imeshuka duniani.

Pia, hiyo *template* inayotumia exchange rate ya dola inayotumika kwenye hiyo *template* nayo ni muhimu sana iangaliwe upya kwa sababu haiendani na soko lilivyo sasa hivi. Kwa mfano, *template* ya juzi waliyoitoa EWURA, wametoa dollar rate 2,025 wakati sokoni Dola leo inauzwa sh. 2,155/=. Kwa hiyo, inakuwa inanyima haki kwa kampuni za mafuta kufanya biashara vizuri kwa sababu hiyo *template* inaumiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoshauri ni kwamba hiyo *template* iangaliwe upya ili iwe na faida kwa mfanyakibasha na kwa mwananchi pia. Sasa hivi kila sehemu inaumiza. Bei ikishuka, mwananchi hapati faida moja kwa moja. Kwa hiyo, ni vizuri *template* iangaliwe upya ili tuone tunawezaje kuiboresha vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la dola kupatikana sokoni imekuwa ni tatizo. BoT huwa wanatoa dola kwenye makampuni ya mafuta kwa kupitia benki lakini hizo dola hazifiki kwa makampuni kama inavyotakiwa. Dola zinazotolewa zote hazifiki kwa makampuni na bei wanazozitoa ni tofauti na benki zinavyotuuzia makampuni ya mafuta. Naomba na kushauri, kwa sababu ya taratibu za sasa hivi EWURA wana takwimu sahihi kwa mfano mwisho wa mwezi wa tano kampuni fulani imeuza lita ngapi na bei yake ni Shilingi ngapi. Kwa hiyo, naomba hilo liangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kupongeza Bulky Procurement System ambayo inasimamiwa na P/C, wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye Jimbo langu la Kwimba, wananchi mwaka 2010 waliponichagua walinituma kutatua kero ya umeme na maji na mengine. Maji nimesema

jana, lakini nina kata 15 lakini nina umeme kwenye Kata moja mwaka 2010. Sasa hivi naishukuru Serikali kwani nimepata umeme kwenye kata 10 nyingine. Nawashukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na Ginnery ya Mwalijo na Sangu Ginnery ambazo zilifungwa kwa sababu ya kutokuwa na umeme lakini sasa hivi zote zimepata umeme, kwa hiyo, nawashukuru sana kwani ajira itaongezeka kwa wananchi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme umepita kwenye Kata 10 lakini changamoto iliyopo ni Shule za Sekondari na Msingi hazijaunganishwa umeme ambao wanaona nguzo za umeme zinapita karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba kwenye Jimbo langu naomba kwenye Shule za Sekondari na Msingi, pia nyumba za Walimu waziunganishe umeme, lakini pia Zahanati, nguzo zinapita karibu sana karibu mbili au tatu; naomba watuletee umeme. Pia kwenye Zahanati, waganga wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Hawana umeme wa REA wala Solar, wana shida, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kusema ni kwamba nina Kata nne ambazo bado zina changamoto za umeme ambazo ni Kata za Shilembo, Ilula, Mwakilambiti na Mwankulwe. Naomba REA wajipange awamu hii angalau basi na hizo Kata nne zipate umeme kwa sababu hata umeme wa REA hawana na pia mradi huu wa TANESCO ambao umepatikana kwenye Kata zangu 10 hawana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme kwangu siyo kwamba ni nguzo tu, umeshawaka! Nawashukuru sana kwa hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, naomba TANESCO wafungue ofisi kwenye Kata ya Hungumaro ambayo ni Kata ya katikati ili wananchi wapate huduma kwa karibu, kwani sasa hivi wanakuja pale kwa muda tu, wanafanya shughuli wanaondoka. Naomba ofisi ifunguliwe pale ili wananchi wapeleke malalamiko na maoni yao pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Kafumu na Mheshimiwa Bungara na Mheshimiwa Murtaza Mangungu, wajiandae.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hoja ilioopo mbele yetu. Lakini kwanza namshukuru Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama kwenye Bunge lako hili niseme. Nitakuwa na mambo machache tu ya kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Madini ni sekta ambayo inaweze kuwa ni kihamasisho kikubwa cha kujenga uchumi katika Taifa lolote, inaweza kuwa engine ya uchumi kama ilivyo Sekta ya Mafuta na Gesi. Naishukuru Serikali ya Awamu ya Tatu kwanza, kwani ilichukua jambo hili kwa ukubwa wake. Lakini siku za karibuni tumeacha kidogo temple hiyo na tumeiacha hii sekta ianze kuangalia mwelekeo wa kushindwa kuwa engine ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hayo kwa sababu miaka miwili iliyopita kulikuwa na maamuzi yalitokea Wizarani ambayo yameifanya sekta hii isihamasike kutafuta madini. Utafutaji wa madini ndiyo engine halisi ya kupata migodi katika taifa lolote. Kwa hiyo, kuliongezwa tozo ambazo zimefanya leseni nyingi za wachimbaji wadogo za utafutaji ziachwe na wenyewe kwa sababu wameshindwa kulipa tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema humu Bungeni miaka miwili yote tunaiomba Serikali iangalie hizi tozo yaani izipunguze ili tuweze kuhamasisha utafutaji wa madini tuwasaidie wachimbaji wadogo ili wafanye shughuli zao. Sasa hivi wachimbaji wadogo wengi wameacha leseni wanachimba bila leseni, ni wachimbaji haramu kwa sababu tumewaruhusu wafanye hivyo, hawawezi kulipia leseni zao. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, tumeshawahi kuongea, hebu kupunguza hizi tozo. Shirikianeni na wadau au watafutaji wakubwa pamoja na wachimbaji wadogo ili mpunguze tozo ili tuhamasishe kutafuta madini na baada ya miaka kadhaa tuwe na migodi minge. Hatujafungua migodi kwa kipindi cha miaka minne, hakuna mgodi mpya unaofunguliwa ni kwa sababu tumeshindwa kuwahamasisha. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba wakati tunatengeneza sheria ya VAT hapa, nilisema sana humu ndani lakini hakuna aliyenielewa. Kwamba ukiweka VAT kwa vifaa vya mtu anayetaka kuja kutafuta mafuta au gesi au madini unamfukuza. Naomba tena Serikali, tazameni hilo jambo. VAT kwa vifaa vya utafutaji, wasamehewe. Mkifanya kama vile wanazalisha, hatutapata wawekezaji katika shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili naomba nizungumzie matumizi ya mrabaha. Mrabaha siyo kodi, ni tozo maalum inayotolewa kwa ajili ya mtu anayechimba madini, raslimali tuliyopewa na Mungu. Sasa sisi Serikali yetu tumeona mrabaha kama kodi na inachukuliwa na Serikali Kuu. Kwa kawaida Mrabaha unatakiwa ubaki kwenye maeneo yale ambayo madini yanachimbwa, kwa sababu kuchimba madini kunaharibu mazingira na maisha ya watu kwa hiyo ni lazima urudishie. Hii ni kama adhabu ya mchimbaji; na hata kama hapati faida, analipa hiyo tozo ya royalty.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyngi duniani kama Ghana, wanapewa Wafalme wale. Machifu ndio wanapewa huo mrabaha. Australia, zile Serikali za Majimbo ndiyo zinachukua mrabaha, siyo Serikali Kuu. Hata Canada, *Aboriginal Communities* ndiyo wanachukua mrabaha, lakini sisi tunapeleka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka mmoja uliopita nilimwandikia Barua Waziri Mkuu nikamwomba watazame namna ya kubadilisha sheria ya madini ili mrabaha sasa hata kipande kidogo au sehemu ndogo ya mrabaha ibaki kwenye maeneo, ili yale maeneo yafanye maendeleo yaweze kuona kwamba kwa kweli madini yanawanufaisha badala ya kuweka kwenye Mfuko Mkuu. Naomba sana Serikali mliangalie hili. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunarekebisha sheria, kuna marekebisho ya sheria mtaleta ya madini, wekeni kipengele ambacho sehemu ya mrabaha ipelekwe kwenye maeneo yanayohusika, vinginevyo tunawanyima haki wananchi wetu.

Jambo la mwisho kwenye madini ambalo nataka kusema ni fidia ya wananchi wa Kijiji cha Ntobo ambako kuna mradi wa Kampuni ya NMDC kutoka India. Ni miaka miwili sasa wanasubiri fidia. Najua jambo hili lipo Wizara ya Ardhi. Namwomba Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini utusaidie. Wasiliana na Waziri yule ili tupate hizi fidia kwa hawa wananchi. Sasa hivi wanaona kama tumewaaacha na yule mwekezaji ameshindwa kuendeleza kwa sababu fidia hajjatolewa, najua ni mchakato tu ndiyo unaharibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye nishati. Uvunaji wa nishati ya gesi na mafuta una changamoto kubwa sana katika nchi za Afrika kwa sababu ni biashara ya Kimataifa, hatuwezi tukafanya peke yetu, tunafanya pamoja na wenzetu.

Kwa hiyo, lazima tuwe na sheria na sera ambazo zinatuhamasisha sisi wenyewe kufanya hii shughuli. Nashukuru sasa hivi mmeleta sheria hii, mlitupa semina juzi ikaonekana kwamba mnafanya vizuri. Ni lazima tuanzishe Kampuni ya Mafuta na Gesi ya Taifa. TPDC ibadilisheni iwe Kampuni ya Mafuta na Gesi ya Taifa isiwe shirika namna ile, ili iweze kushindana na makampuni mengine kutoka nje kuwekeza katika shughuli hii. (Makofi)

Pia makampuni ya wazawa wa Tanzania na wenyewe yapani priority yafanye kazi. Hii shughuli tukiweza kuifanya hapa Tanzania kutakuwa na uwezekano wa kunufaika vizuri zaidi. Tusipofanya hivyo, tutakuwa sawasawa tu na nchi nyingine kama Nigeria na nchi nyingine kwa sababu jambo hili la raslimali linatumika na wenzetu kuendelea kutukandamiza. Wote mnajua kwamba raslimali hizi, wengi wanasema ni *resource scarce*; ni kwa sababu inatumika na wenzetu kutukandamiza na kututawala. Ni lazima tuwe wajanja!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kusema wawekezaji waondoke, tutakosea kwa sababu ni lazima iwe hivyo. Lakini tufanye kazi tuwaruhusu wananchi wetu na makampuni yetu na tujiruhusu wenyewe kushiriki kwenye jambo hili na baadaye wanaweza kujikuta hayo makampuni makubwa yakaondoka kwa sababu tumeweza tumeshika uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema tena nawashukuru sana Serikali kwa kuwapa wananchi wa Igunga wale walipitiwa na *Back Burn Project* kwa kuwalipa fedha zao ambazo walikuwa wamepunjwa. Kuna watu waliiba pale Igunga, Serikali imewarudishia wananchi wale lakini pia kuna watu wana kesi. Naomba basi hizi kesi za watu hawa walioiba hizi fedha kwa ajili ya wananchi wetu washughulikiwe. (Makofi)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Ni zamu sasa ya Mheshimiwa Bungara; Mheshimiwa Mangungu na Mheshimiwa Devotha Likokola wajiandae.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa kutusaidia sisi watu wa Kilwa kupata gesi na kujulikana katika nchi hii, bila kuwa na gesi basi nchi hii tusingejulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nanukuu.

MHE. ISMAIL A. RAGE: (*Aliongea nje ya microphone*)

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Kaa kimya wewe Rage! Umeshindwa Simba, unakuja hapa! (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawaomba Watanzania, tumaini la Tanzania ni Chama cha Wananchi CUF na Umoja wa UKAWA, hilo ndiyo tumaini la wanyonge wa Tanzania. Ukimsikia mtu ye yeyote anasema yeye ni tumaini kutoka CCM, basi ujue ni longolongo hiyo, lakini tumaini ni UKAWA kwa wanyonge wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi watakapowatambua viongozi waongo na wakazidi kuwachagua viongozi hao waongo, basi wasitegemee kupata rehema kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu utakapomchagua mwongo halafu ukamlaumu Mwenyezi Mungu, basi unamwonea Mwenyezi Mungu, wakati wewe mwenyewe umemchagua mwongo. Wamandhara banafsi layabuki! Anayejipiga mwenyewe, asilie. (Makofi)

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Waheshimiwa tumaini letu ni UKAWA na ninawaomba viongozi wa UKAWA msiwe wanafiki. Kama hamkuweza kuungana, basi ninyi na CCM, kaba-kahusain, ni kama mshale na upinde. Sawasawa tu mtakuwa! Lazima tushirikiane na tuungane. Mkishindwa, Watanzania tutajua ninyi na CCM, kaba-kahusain, mnawadaganya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuchangia kuhusu Wizara ya rafiki yangu Mheshimiwa Simbachawene, almaarufu Mesi! Nilikwambia Mheshimiwa Simbachawene, wewe ni Mesi unashambulia, defense huna. Wakati ulipokuwa Wizara ya Ardhi na umeona defense yako imeanguka, Waziri wako kaanguka na wewe upo Mesi unashambulia zaidi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla Mheshimiwa Simbachawene kuingia katika Wizara ya Ardhi alikuwa Wizara hii Naibu Waziri. Nilimwambia katika Jimbo langu la Kilwa Kusini Mradi wa REA una Kijiji kimoja tu cha Matandu katika Jimbo lote la Kilwa Kusini. Jimbo ambalo ndiyo inatoka Gesi Asilia katika nchi ya Tanzania, mwaka 2004 Songosongo Jimbo la Kilwa Kusini ndiyo iliyokuwa inatoa gesi, lakini ndiyo Jimbo ambalo katika mradi wa REA ni Kijiji kimoja tu cha Matandu ndiyo kimepata mradi huo. Ukaniambia ni kweli na uandike barua maalum ya kuomba Jimbo la Kilwa Kusini lipatiwe miradi ya REA.

Tarehe 13/2/2014 Mkurugenzi wa Wilaya ya Kilwa Mheshimiwa Mapunda nikamwambia hoja yako na akaandika barua kumbukumbu namba, nanuuu; KDC1016678 ya tarehe 13/02/2014 kupeleka kwa Katibu Mkuu wa Nishati, maombi maalum ya kuwekewa umeme katika vijiji kupitia Wakala wa Umeme wa REA. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barua iliandikwa na ilifika kwa katibu tarehe 13/02/2014, vijiji vilivyoombewa ni Nanjilinji, Likawage, Mandawa, Pande Plot, Mikoma, Limalyao, Kisongo, Hotelitatu, Kilanjelande, Mavuji, Mbwemkulu na Kikole. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barua hiyo ilipotumwa haikujibiwa tangu mwaka 2014 na nakala ya barua hiyo mimi nikapewa. Tarehe 22 Desemba, 2014 mimi nilianidika barua kupeleka kwa Katibu Mkuu; "Maombi Maalum ya Kuwekewa Umeme." Tukasemaa, nikaandikaa ikapokelewa. Nanukuu. (Kicheko/Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taabu yenu ninyi watu wa CCM, mnaondoka, basi akili yetu kidogo tayari! Nikajibiwa tarehe 21 Januari, 2015, "Maombi Maalum ya Umeme." Katika majibu hayo, Wizara inakiri kupokea barua ya tarehe hiyo. "Aidha, tunapenda kukutaarifa kuwa maombi yako yatafanyiwa kazi na utajulishwa hatua ya utekelezaji baada ya kuwasiliana mambo hayo kwa Wakala wa REA."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Januari nimejibiwa! Basi mpaka leo sijajua chochote! Sasa sisi Kilwa Kusini ndiyo tunaotoa gesi. Sisi hatufaidiki na gesi hiyo! Nilimsikia jana Mheshimiwa aliyetangaza urais nani huyu?

WABUNGE FULANI: Huyo huyo!

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mbona mna wasiwasi Waheshimiwa? Mheshimiwa Ngeleja anasema asiliimia 80 ya Jimbo lake mradi wa REA. Sisi Kilwa ambao tunatoa gesi, hatujapata!

Nakupenda sana Mheshimiwa Simbachawene na ninaamini kabisa katika watu safi katika CCM ni wewe, Mesi tu peke yako. Wengine wote ni mapakacha mabovu! (Kicheko/Makofii)

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Sasa leo uniambie, katika barua yangu, vijiji nilivyovitaja vitapata umeme au havipati? Kama havipati na livunde tugawane mbao. Kwa kuwa gesi

inapitia Kilwa, nawaambia haitoki na tutapambana na sisi hatuwezi kulinda bomba la gesi ilhali manufaa ya gesi hiyo yanaonekana sehemu nyingine. (Makofi/Kicheko)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mangungu, kisha jiandae Mheshimiwa Devotha.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa kifungu kinachozungumzia Kanuni za majadiliano, kifungu cha 64. Nitakisoma.

“Mbunge aliyeo Bungeni wakati wa mjadala atatakiwa; basi yameelezwa mambo yasiyo ruhusiwa Bungeni. Kanuni ya 64(g): “hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kwa heshima na taadhima, ndugu yangu, mtani wangu na mijukuu wangu, aliyealiza kuongea sasa; naturahi anatambua kwamba tuna Waziri makini maana amemsifu. Lakini amesema, ndani ya CCM yuko yeye peke yake, wengine wote mapakacha mabovu. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pamoja na kwamba wanashangilia, unaposhangilia lugha kama hii unajionesha wewe ni mtu wa aina gani. Naomba Watanzania mnaotusikiliza mwelewe kwamba, hivi ndivyo walivyo.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Hata mwaka 2014 niliposema Hospitali ya Kivinje haina maji, wewe ukasema maji yapo. Wewe ni mnafiki vilevile!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bungara, tafadhali kaa chini. Mheshimiwa Waziri, nafikiri wamekuelewa. Nakuomba ukae. Mheshimiwa Mangungu! (Makofi)

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu niliposema Hospitali ya Kilwa Kivinje...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bungala, kuna utaratibu wa kuzungumza Bungeni. Hatuko kwenye viwanja vya mpira, wala kantini. Unapopewa nafasi ya kusema, utasema. Kama hupewi, unatakiwa ukae chini. Nakuomba sana. Mheshimiwa, kaa chini! Acha mikwara yako, kaa chini! (Kicheko)

Mheshimiwa Mangungu!

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tunaelekea mwisho wa Bunge hili ni heri nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kilwa Kaskazini ambao wamekuwa wakinunga mkono kwa kipindi chote. Lakini mwisho wa jambo moja ni kuashiria kuanza kwa jambo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni zetu tulizonazo Mbunge ama Serikali itawasilisha hoja Bungeni na itajadiliwa. Sasa nadhani kwenye marekebisho ya Kanuni kwa

Bunge linalokuja, turuhusu kuwe na hoja lakini kuwe na vioja vilevile. Kwa sababu kwa taarifa hizi ambazo zimekuwa zikiwasilishwa kutoka upande wa pili, nyingi ni za vioja. Lakini kwa kuwa sisi ni Waswahili, tunaelewa mtu akidanganya kusema, basi na wewe mdanganye kumsikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri wana CCM, wananchi na Serikali; kwa kuwa wao wanadanganya kusema, nasi tuwadanganye kuwasikiliza, basi yapite hayo yaendelee mengine. Maana imekuwa ni ajabu sana, wanasema kwamba sisi ni lazima tuingie. Hivi mmeshawahi kutoa mfano wa jambo moja tu jema ambalo mmewahi kufanya mpaka kusema wenzenyu kuwa ni wabaya zaidi na ninyi mna uzuri? Ni uzuri na ukweli gani ambaao mmewahi kuusema? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie kwenye hoja. Tukianza na umeme, kwanza sisi ambaao tunaishi kwa kuamini na Quran imetufundisha kwamba kama usipoweza kumshukuru mwanadamu mwenzio, basi hata Mungu mwenyewe huwezi kumshukuru. (Makofii)

MBUNGE FULANI: Kabisa!

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mimi nawashukuru sana Wizara ya Nishati na Madini, Wakala wa Umeme Vijini REA, mmenisaidia katika Jimbo la Kilwa Kaskazini ninaweza kufikia kiwango cha asilimia 75 kama siyo 80 kupata umeme. Mradi wa umeme kutoka Njia Nne hadi Kipatimu, lakini mradi wa umeme kutoka Nangurukulu hadi kufika Miguruwe. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kumtaarifu Mbunge wa Kilwa Kusini kwamba vijiji vya Jimbo la Kilwa Kusini pia vitanufaika kikiwemo Migelegele, Kikole, pamoja na pale Mbate, vitapata umeme kupitia mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mradi ambaao kwa kukosa umakini tu, labda imeainishwa humu, ni mradi ambaao utachukua njia ya umeme kutoka Mtwara ambapo bomba linapita mpaka kufikia Mikoa ya Lindi, Dar es Salaam na Pwani; na ni vijiji hivyo ambavyo vimikuwa vikitajwa. Kwa hiyo, hilo lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la upelekaji umeme vijijini, tozo ambayo imekuwa ikitozwa nawashauri sana, Serikali ni lazima mlete mapendekezo, tukubaliane na Wabunge wote tuongeze hizi fedha kwa sababu nchi hii hatutaweza kukuza uchumi kama hatutaweza kuongeza nishati na vilevile kama hatutafanya miradi ya kushusha gharama ya nishati kuwa chini. Hiyo, ndiyo njia pekee ambayo tunaweza tukakuza uchumi. Kwa hiyo, ni lazima tukubaliane tuongeze tozo tupeleke umeme zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini na Waheshimiwa Wabunge wengine waliochangia, kumekuwa natatizo kubwa sana la upelekaji wa fedha ambazo zinakusanywa. Ni kwanini Hazina wanasita kupeleka fedha katika miradi hii ya umeme vijijini? Sasa ni lazima tuweke mfumo ambaao utasaidia upatikanaji wa fedha hizi kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hazina pia wanasita sana kwenye kuidhinisha na kukubaliana na mikataba ya uzalishaji wa umeme. Tunaongeza matumizi ya umeme kwa kupeleka umeme zaidi vijijini na maeneo ya migodi, lakini umeme huu hautaweza kuongezeka.

Mfano halisi ni mahitaji ya umeme wa upepo, umeme wa geothermal na umeme wa makaa ya mawe. Mnatumia miaka mingapi kujadiliana hii mikataba? Ni kwanini hamharakishi kupitisha hii mikataba? Mnakimbilia kwenda kuidhinisha mikataba ya mambo ambayo hayana manufaa makubwa kwa nchi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatutaweza kutumia gesi hii kuwanufaisha wananchi kwa kuweka viwanda vingi zaidi. Hakuna manufaa ya gesi dunia nzima kama hatutaweza kuweka viwanda. Sasa kwanini hatuharakishi matumizi ya gesi yaweze kunufaisha viwanda vyetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mawili; la kwanza ni eneo la Njia Nne. TPDC wahakikishe wanaenda kulipa fidia ya wananchi ambao wanadai kwa ajili ya upitishaji wa bomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine napongeza sana kampuni ambayo ilibuni na kuanzisha utaratibu wa ununuzi wa umeme kupitia mitandao; kampuni ya Selcom. Hilo tunawapongeza sana. Lakini kwenye ununuzi huu kuna matatizo. Ninao ushahidi kwamba nilinunua umeme mimi mwenyewe binafsi tangu tarehe 03 ya mwezi wa Tano kupitia Tigo Pesa, lakini mpaka leo umeme huo sijapata token. Sasa ni wananchi wangapi ambao wanapoteza fedha zao na inakuwa ni gharama kubwa kufuatilia kwenye makampuni haya? Ni kwanini hatuweki mfumo mzuri ambao wananchi hawatapoteza fedha zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na msongamano mkubwa sana katika upakuaji wa mafuta, lakini niwapongeze sana Serikali kwa kukubaliana na ushauri wa Kamati ya Nishati na Madini na taasisi nyingine kukubalia kuanza kushusha mafuta katika eneo la Tanga. Kubwa zaidi ni lazima zile depots ambazo zimejengwa ziwe zinakidhi mahitaji na ikiwezekana mtenge maeneo ambayo yataainishwa ili wawekezaji ambao watakuwa wako tayari kuwekeza wajenge maghala mapya ya uhifadhi wa mafuta na tuweze kurahisisha utoaji wa mafuta katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho. Kumekuwa na mradi wa umeme wa Kilwa Energy. Nia ni njema na wawekezaji hawa ni wa ndani. Kwanini Serikali haitoi fedha kuunga mkono kwa kiasi kinachotakikana ili huu mradi uweze kuendelea na kuanza? Wananchi wengi sana kuanzia Somanga mpaka unafika Dar es Salaam wamekaa kipindi kirefu wanahitaji kulipwa fidia zao. Serikali imekaa kimya, hamtaki kutoa tamko ni nini ambacho kinatakikana kufanyika. Ni lazima Serikali ichukue wajibu kuwaelimisha wananchi na kuwapa taarifa zinazotakikana.

Kama mradi huu hautaanza na hamko tayari kushirikiana na mradi huu, basi wananchi waendelee kufanya shughuli zao katika maeneo hayo. Lakini kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitatu, wananchi wamekaa hawahudumii mashamba yale, mikorosho inakufa, minazi imeanguka, sehemu nyingine watu walikuwa wanalima mpunga na shughuli nyingine wameacha kuafanya shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubaliane, kama mradi huu unasita, basi usite...

(Kengele ya pili illilia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Devotha Likokola! Wajiandae Mheshimiwa Lembeli na Mheshimiwa Riziki Lulida.

MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuunga mkono hoja hii na kupongeza sana kazi ambayo imefanyika na Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Mtanzania ambaye hataeleza ukweli huu. Kazi ambayo imefanywa na Wizara ya Nishati na Madini ni kubwa hasa kwa upande wa REA. Vijiji vingi vimepata umeme; na hii ni utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana kwanza, Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri. Tumeona katika Wizara hii Naibu Mawaziri wanapishana huku na huku kuhakikisha utekelezaji wa suala zima la kupeleka umeme vijiji linafanya kikamilifu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia maeneo matatu. Eneo la kwanza ni fedha za REA, eneo la pili nitachangia kuhusiana na wachimbaji wadogo wadogo wa madini nchini kwetu na eneo la tatu nitachangia mradi wa kupeleka umeme unaotoka Makambako kwenda Songea. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na agenda ya REA. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote, kama kweli tunataka maendeleo ya nchi yetu, suala la REA kupata fedha zake tuweke kipaumbele namba moja. Nawaomba Wabunge wote, leo ndiyo leo na bajeti hii isipite kama REA haijaongezewa fedha. Ni lazima tushirikiane REA wapate fedha, vijiji vyetu vipate umeme na wananchi wapate maendeleo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, Bunge limefanya kazi nzuri sana. Nakumbuka mwaka 2014 Bunge hili liliazimia kabisa fedha za REA ziongezeke. Lakini tuliongeza katika bajeti. Kwa masikitiko makubwa, Wizara hii imepata fedha kidogo, ni asilimia 35 tu mpaka leo! Kwa hiyo, naomba agenda hii ya REA, hakika Serikali ikae makini kuangalia suala zima la REA. Haiwezekani REA ina fedha zinazodaiwa na Wakandarasi, lakini vilevile REA wametengeneza bajeti nzuri sana kuonesha ni kiasi gani wanadaiwa na ni kiasi gani wanaweza kutekeleza miradi ya maendeleo. Lakini taasisi hii upatikanaji wa fedha umekuwa ni mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama Serikali itakuwa makini, ikiwalipa wale Wakandarasi wa REA, hakika umeme utaendelezwa katika vijiji vyetu vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwazungumzie wachimbaji wadogo wadogo wa nchi hii ya Tanzania. Kwanza kabisa ni jambo la kushangaza sana, mchango wa Sekta ya Madini ni asilimia tatu tu kwa Taifa kubwa kama hili na kwa madini yote tunayoambiwa tunayo katika nchi yetu, lakini katika pato la Taifa (GDP) mchango wa Sekta ya Madini ni asilimia tatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie, kwanini mchango umekuwa ni asilimia tatu tu? Ni kwa sababu shughuli zinazofanywa na wachimbaji wadogo wadogo hazijajumlishwa katika mahesabu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wachimbaji wadogo wadogo wanahangaika. Mimi nimeshuhudia katika Kamati yetu tu wamekuja zaidi ya mara tatu au nne. Naiomba Serikali, wakati umefika Wachimbaji wadogo wadogo wavezeshwe. Wafanyiwe mafunzo, wapewe vifaa, waweze kuchimba madini ya nchi yao na wajivunie madini ya nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali; iliweka ruzuku na mikopo, lakini mikopo ile wachimbaji hawakuweza kuchukua kwa sababu walikuwa hawajawezeshwa kimafunzo.

Kwa hiyo, naiomba Serikali na hapa napenda niwapongeze sana Kampuni ya Anglo Gold Ashanti kwa kuanzisha mpango wa kuwawezesha Wachimbaji Wadogo Wadogo. Lakini niwaambie Anglo Gold Ashanti na Acacia kwamba mpango ule waupeleke nchi nzima. Mchango wa madini ni kwa nchi nzima! Wasianze tu na Geita na Tarime. Songea kuna

Wachimbaji, Namtumbo kuna Wachimbaji, Tunduru kuna Wachimbaji na Mbinga kuna Wachimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Anglo Gold nitakuja niwaone na lazima tupeleke mpango huu kwenye mikoa yote. Iringa wako Wachimbaji, Dodoma wako, Singida wako, hivyo ni lazima tufanye kazi nzuri kwa nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie watu ambao wanatakiwa kutekeleza mradi wa umeme wa Makambako, Songea. Mradi huu umekuwa ni wimbo wa Taifa. Kila siku tukisimama hapa imekuwa ni Makambako, Songea! Makambako, Songea! Leo nimefurahi Waziri amesema kwamba, fidia kwa wananchi zimelipwa; Mkoa wa Njombe wamelipwa; Mkoa wa Ruvuma wamelipwa wananchi 767 na kwamba mradi huu sasa utaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Waziri ninataka katika majibu yako lazima ueleze mradi huu utaanza lini, kwa tarehe. Ninyi ni wataalam lazima mtuambie tarehe ili sisi tuwe pale tunashuhudia mradi wa Makambako, Songea unaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Njombe na Songea wanataka kuona mradi huu. Kifanya watu wanataka kuona mradi huu! Mikoa ile ya Kusini tumekuwa wavumilivu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie, kwa mfano, Mkoa wa Ruvuma, tumejiwekea strategic plan yetu kwamba sisi ni walishaji wakubwa, kwa hiyo, tunahitaji umeme mwangi ili sasa tufanye viwanda vikubwa vikubwa, viwanda mama ili tuweze kuleta maendeleo. Ule mkoa ni wa wazalishaji, kwa hiyo, ni lazima wapate umeme mwangi ili tuendelee na uzalishaji. Sisi hatuna longo longo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lembeli! Jiandae Mheshimiwa Lulida.

MBUNGE FULANI: Nakushukuru kunipa point.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Kwa namna ya pekee kabisa naomba niitumie nafasi hii hili likiwa Bunge la mwisho kabla ya uchaguzi niwashukuru wananchi wote wa Jimbo la Kahama kwa ushirikiano na mshikamano mkubwa ambao wamenipa hadi tukafikia mafanikio makubwa katika suala zima la mapato yanayotokana na migodi. Nasema hili kwa sababu Wilaya ya Kahama ina migodi mikubwa miwili; na katika Jimbo la Kahama, tuna mgodi wa Buzwagi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirejee, kwa zaidi ya miaka nane kila mara nimesimama kuchangia bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, sijaunga mkono. Safari hii naunga mkono kwa sababu ya mambo makubwa ambayo yamefanyika, lakini yote haya yanatokana na jitihada za pamoja baina ya Mbunge na wananchi wa Jimbo la Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mambo makubwa na kihistoria ambayo yametekelawa katika kipindi kifupi sana katika Jimbo la Kahama ni pamoja na barabara ya zaidi ya kilomita sita katika Mji wa Kahama ambayo imetokana na fedha iliyotolewa na Mgodi wa Buzwagi. Hapa sina budi kuwapongeza viongozi wa Acacia na Meneja wa Buzwagi hususan Bwana Filbert Rweyemamu, ambaye tangu ameingia Buzwagi kumekuwa na ushirikiano mkubwa zaidi na wananchi na matunda yake yanaonekana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limefanyika katika kipindi kifupi ni ujenzi wa Kituo cha Afya cha kisasa kabisa, katika Kata ya Mwenda Kulima, ujenzi wa Ofisi ya Kata Mwenda Kulima, Shule za Chapulwa na Mwime zimefanyiwa matengenezo makubwa na nyumba za Walimu zijengwa.

Zaidi ya hapo, kwa mara ya kwanza kabisa, taasisi hii au kampuni hii imeweza kulipa ile asilimia 0.3 kwa Halmashauri ya Mji wa Kahama ambayo ilipokea zaidi ya Shilingi milioni 843. Yote haya ni matokeo ya jitihada za pamoja baina ya wananchi na mgodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo moja, yote haya yasingewenza kufikiwa kama Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na hususan Mkuu wa Wilaya mwenyewe Bwana Benson Mpesya maarufu kama Baba Askofu asingekuwa na mshikamano na viongozi wenzake, lakini pamoja na Mbunge.

Hivyo hivyo, kwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Bwana Ruhunga amesaidia sana katika kurekebisha hali hii. Ikumbukwe kabisa kwamba kwa muda wote mimi nilikuwa nimekataa kabisa kupata huduma ya Mgodi wa Buzwagi ikiwa ni pamoja na ndege yao. Leo hii nitakuwa tayari kupanda ndege kutoka Dar es Salaam kwenda Kahama kwasababu wametekeleza yale ambayo wananchi wa Kahama wangependa kuyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwa upande wa REA. Kwa heshima kabisa napenda kuipongeza Serikali kwa kuleta mradi huu katika Jimbo la Kahama. Umeme Kahama mara nydingi umekuwa pale Mjini na kwa mara ya kwanza kabisa umeme umeelekezwa katika Jimbo la Kahama na Kata ambazo zitanufaika na mradi huu ni pamoja na Kata ya Zongomela, Nyandekwa, Mpunze, Saba Sabini hadi Bulungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa naomba ni kwamba ndani ya Bunge hili kwa mbwembwe kubwa zaidi tuliambiwa kwamba ifikapo mwezi wa Tatu, umeme katika Jimbo la Kahama utakuwa umeshawashwa. Leo hii ni mwezi wa Sita na hakuna dalili za kuwashwa kwa umeme na kazi ya kutandika nyaya bado inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumwombwa Mheshimiwa Waziri aniambie ni lini hasa ile ahadi iliyotolewa humu Bungeni kwa mbwembwe itatekelezwa? Pia ningependa kujua awamu ya pili ya REA katika Jimbo la Kahama hapa nikimaanisha Kata za Ukune, Kisuke, Uyogo, Ushetu, Ulowa hadi Bugomba awamu hii itaanza lini ili wananchi ambao wana matumaini makubwa sana na Serikali yao waweza kuijweka tayari kupokea mradi huu.

Mwisho, napenda kujua ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga mtambo wa kupoza umeme pale Kahama Mjini ku-tape umeme unaokuja Mgodini ili uweze kutumika kwa matumizi ya kawaida ya wananchi wa Mji wa Kahama? Kwasababu kukatika kwa umeme katika Mji wa Kahama ni jambo la kawaida na wananchi wamechoshwa sana na tabia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni kwamba wananchi wa Kahama wanapenda maendeleo, lakini kuunganishwa umeme katika maeneo ya makazi yao limekuwa ni tatizo sugu.

Nataka kujua, hivi tatizo ni nini? Mboma katika Wilaya nyingine, katika Miji mingine, watu wanaunganishiwa umeme bila ya kujali hali zao kwa maana ya wenye vipato na ambao hawana vipato? Hili jambo ambalo ningependa sasa hivi wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha, ameshafika Kahama, tatizo hili analifahamu; nini tatizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali, naunga mkono hoja hii kwasababu imekuwa ni ya manufaa kwa wananchi wa Jimbo la Kahama. Ahsante. (Makof)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Lulida, na Mheshimiwa Bukwimba ajiandae.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Namshukuru Mwenyezi Mungu zaidi kwa kunijalia kuwa na afya njema nami niweze kuchangia katika hoja iliyoko mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tuko katika kipindi chetu cha mwisho na tunakwenda katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani, nawatakiae Waislamu wenzangu waende katika kipindi cha Mfungo na Mwenyezi Mungu awajalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri Simbachawene. Nikiwa katika Kamati nilimwambia kuna maeneo ambayo bado umeme wa REA haujafika ikiwemo Mtama, Nyangamara, Naukauka, Mandwanga na Lindwandwali, kote nguzo zilikuwa hazijawekwa na ilikuwa haijawekewa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kutoka Nangurukuru mpaka Mbwemkulu, nashukuru zimetengwa Shilingi bilioni 48 kwa maeneo ya Nangurukuru Kilanjelanje Mandawa, Nanjilinji kote umeme utafika. Sasa hivi katika Mkoa wa Lindi suala la Umeme ni kuchelete. Tumtakie heri, mabadiliko haya anayoyafanya na mazingira haya anayotuletea katika Mkoa wa Lindi kwa kutuletea umeme, akishirikiana na Waziri wake. Basi nasema ahsante sana kwa hili, Mungu awawezesha, (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila tu naiomba Wizara ya Fedha ahadi yake iliyotoa iwafanye hawa watu waweze kufanya kazi. Bila kupata fedha ya ziada, watashindwa kutimiza malengo yao kwa vile bado fedha hazijakwenda katika Wizara ya Nishati na Madini. Kwa hili, napenda niwapongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia wachimbaji wadogo wadogo ambao wataweza kuliongeza pato la Taifa katika nchi hii hasa katika Sekta ya Madini. Mikoa ya Lindi, Mtwara Ruvuma mpaka Mkoa wa Rukwa inaongoza sasa hivi kwa kuwa madini. Lakini je, tumewaandaaje hao wachimbaji wadogo na wao waweze kukuza uchumi wa nchi? Kinachofanyika, wao wameanzisha maeneo yao, wakija wachimbaji wakubwa na wawekezaji wakubwa wanatolewa. Hii haitaleta tija kwa watu masikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kuwafanya watu masikini kuwa masikini zaidi wao waje wapate faida. Neno linalotumika sasa hivi, wanakwambia una mihogo kiasi gani, una miembe kiasi gani? Unatolewa, unapata Shilingi milioni tano, anakuja mwevezaji anapata trilioni za fedha. Hii ni dhuluma kwa Watanzania. Tufanye kila njia wananchi hawa waandaliwe Wanasheria ambao watawasimamia katika maeneo yao ili haki zao zisipotezwe.

Kila siku ninazungumza kwamba Watanzania tuwe Wazalendo. Umasikini hauna hatimiliki wala hakuna aliyepewa hatimiliki kuwa wewe utakuwa tajiri na wewe utakuwa masikini. Huyu sungura ni kwa Watanzania wote. Sasa hivi kumeingia udalali mkubwa wa ardhi, watu wanachukua ardhi maeneo ambayo wanakuwa wameyapatia taarifa kwamba yatakuwa na madini, hivyo wao ndiyo watakaoidhulumu nchi hii na kuifanya nchi hii iwe mufilisi kwasababu hati zao wanazifanyi udalali katika nchi mbalimbali huko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachukua hizi hati, wanachukua maeneo makubwa kama ekari 20,000 au 100,000 wanakwenda katika Stock Exchange kufanya udalali mkubwa na kuiacha nchi ikiwa inaning'nia, chini haipo, juu haipo; itakuwa kama mkungu wa ndizi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana niwapongeze baadhi ya wataalamu wa jiolojia ambao wako Tanzania. Hawa wataalamu watengenezewa mazingira ili wawe watu wa kutusaidia katika taaluma ya jiolojia. Tuna upungufu mkubwa wa wataalamu. Hivyo, akina Dkt. Kafumu, akina Profesa Mhongo na kundi lingine la Majiolojia wajunge watengeneze consultation Unit ambayo itawasaidia Watanzania tujiondoe katika mazingira magumu maana wenzetu wamesoma, sisi hatukusoma; wenzetu wana utaalamu, sisi hatuna utalaamu. Hawa wataalamu wetu tusiwaache wakiwa hawana mahali pa kwenda. Tuwatengenezee mazingira waje kuinusuru nchi katika sekta hii ambayo ni ngeni na kwetu imekuwa ni kitu kipyta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya wanavijiji wetu sasa hivi ni ngumu. Maeneo yote ambayo yametambulika kuwa yana uchumi wa gesi na mafuta, tayari wako katika hekaheka ya kutolewa na wanatolewa katika hela ndogo sana ikiwemo Sh. 400,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, awe makini wakishirikiana na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, maana ndani ya maeneo yetu ya hifadhi kuna madini. Kuna game reserves kuna madini ambayo yanachimbwa sasa hivi. Je, uchumi huu tutausimamiaje? Hali ni tete, Serikali iwe makini.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bukwimba; na Mheshimiwa Kombo Khamis ajiandae.

MHE. LOLESTIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hoja hii katika bajeti ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Manaibu Waziri wote wawili kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya ndani ya Wizara ya Nishati na Madini. Nachukua fursa hii pia kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Busanda kwa kunipa ushirikiano mkubwa kwa kipindi chote cha kuweza kuwatumikia ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe kwamba kuanzia wiki ijayo tunaanza kujandikisha katika Daftari la Kudumu, naomba wajitokeze kwa wingi katika kujandikisha. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuiomba Serikali rasmi, ni kwa kipindi cha miaka mitano; kuanzia mwaka nilioingia hapa Bungeni, ni miaka mitano sasa, lakini jambo ambalo kila mwaka nalizungumzia, habari ya wachimbaji wadogo wa madini. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kusema kwamba wananchi wa Nyarugusu wamenituma tena kwa mara nyingine, lile eneo ambalo Mheshimiwa Rais katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi aliahidi yeye mwenyewe, akasema atawapa eneo la uchimbaji wa madini katika eneo la Nyarugusu, maeneo ambayo ni ya STAMICO; vilevile kuna wananchi wa Buziba ambao pia wanahitaji maeneo ya uchimbaji wa madini. Mheshimiwa Rais yote hayo aliweza kuwaahidi wachimbaji wadogo wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naiomba Serikali itamke jambo kwa ajili ya wananchi hawa. Sasa hivi wanasubiri tamko la Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya wananchi hawa kuweza kupewa maeneo hayo ya uchimbaji. Nazungumza hivi, ni kipindi kirefu sasa, ni miaka mitano. Najiuliza kwamba Wizara inafanyaje kazi namna hii? Kwa kipindi chote hiki wananchi wanasubiri na

Mheshimiwa Rais amesema wapewe, lakini watumishi wa Wizara wamekuwa na kigugumizi gani kuweza kulifuatilia suala hili ili wananchi waweze kupewa maeneo haya? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwasababu katika Mkoa wa Geita na maeneo hayo ambayo nimeyataja kwa kweli uchumi wetu unategemea sana shughuli za uchimbaji wa madini na Serikali isipowajali wachimbaji wadogo wa madini maana yake ni kwamba uchumi wetu unakuwa hauendelei, kwasababu wachimbaji hawa kutokana na shughuli zao za uchimbaji wanaongeza kipato na pao la Taifa kwa ujumla kwa ajili ya shughuli hizi za wachimbaji wadogo.

Kwa hiyo, naiomba Serikali kama kweli tuna nia ya dhati kwamba wananchi wa Tanzania wajijiri wenyewe, tujijekeze basi kwa wachimbaji hawa wadogo kwa kuwapa mitaji, vilevile kwa kuwawezesha kuwapa maeneo ya uchimbaji ili tuweze kumiliki shughuli za uzalishaji ndani ya nchi yetu na wananchi wenyewe wahusika wawe na utayari wa kuweza kujishughulisha katika shughuli hizi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ilichukue jambo hili kwa uzito mkubwa ili wananchi wanufaika na shughuli hizi za uchimbaji wa madini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nzungumzie wananchi wa Rwanagasa amba Serikali ilichukua maeneo yao na kuwapa wawekezaji wa Barcliff. Ni kipindi kirefu sasa ambapo wameshafanyiwa tathmini, lakini mpaka sasa ni miaka miwili imepita, hakuna chochote kinachoendelea.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, wakati wa majumuisho nipate maelezo ya kutosha kwamba ni lini wananchi hawa wanalipwa fidia? La sivyo, wapewe maelekezo mengine zaidi ili waendelee na shughuli zao ili waweze kujipatia vipato kuititia ardhi hii ambayo wanayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la umeme naishukuru Serikali kwa kazi kubwa ambayo inaendelea kuifanya, lakini usambazaji wa umeme unaenda taratibu sana, naomba tuongeze kasi ya usambazaji wa umeme, tukizingatia pia katika taasisi muhimu kama Shule za Sekondari, Zahanati na Vituo na vya Afya. Tunahitaji umeme huu ili uweze kuwanufaisha Watanzania. Siyo tu unapita juu kwa juu, vijiji vyote ambavyo vimepitiwa na nguzo za umeme kwa juu, naimba Serikali itoe tamko kwamba ni lini vijiji hivi vitawenza kupatiwa umeme? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwasababu kuna vijiji vingi tu ambavyo vimepitiwa umeme; kuna Nyaruyeye, Buziba na vijiji vingi ambavyo vinahitaji umeme huu. Naomba Serikali iangalie uwezekano, vijiji vinavyopitiwa na nguzo yaani kwa juu, ihakikishe umeme huu unafika kwa wananchi walioko katika maeneo husika. Vilevile Mheshimiwa Kitwanga alikuja Geita, alijionea mwenyewe. (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kombo! Jiandae Mheshimiwa Kitandula na Mheshimiwa Kayombo!

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nashukuru kwa kupata nafasi hii, lakini kwanza nataka kusema kwamba Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi ilioa kauli kwamba ifikapo Juni 30th mradi wa umeme utokanao na REA utakuwa umeshasambazwa vijijini kote. Juni 30th 2015!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kimoja, kusema ni kitu kimoja na kutekeleza ni kitu kingine. REA hawapewi fedha za kuendeleza umeme hali ya kuwa wananchi wanachangia fedha hizi kupitia tozo za mafuta na umeme. Sasa kutoka kwenye tozo za mafuta, mtu anachangia kila lita Sh. 50/=. Tujuilize, pesa hizi zinazochangiwa zitokanazo na mafuta, zinakwenda wapi baada ya kufikishwa REA? Kwa hiyo, ile kauli ya kusema kwamba tutawafikisha Watanzania kwenye Uchumi wa kati, ni kauli ambazo tunazisema kwenye majukwaa, ni kauli ambazo hazitekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, niende kwenye madini. Watanzania wanavumbua madini kutoka maeneo mbalimbali nchini, lakini nataka niseme kwamba madini haya hayawafaidishi Watanzania. Kulikuwa kuna haja sasa ya Serikali kuangalia upya ni namna gani Tanzania inaweza kufaidika na madini. Kwa mfano, tuna madini ya Tanzanite madini ya Tanzanite yamevumbuliwa na Watanzania, lakini leo tuangalie Tanzania inapata kiasi gani katika madini haya? Wawekezaji kutoka nje ndio wanaofaidika wao na nchi zao. Kwa mfano, Tanzania inapata Shilingi milioni 36 Dola za Kimarekani, lakini Kenya wanapata Dola milioni 100 zitokanazo na Tanzanite ambayo inachimbwa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afrika ya Kusini wanapata Dola milioni 200; India wanapata Dola milioni 300 zitokanazo na Tanzanite inayotoka Tanzania. Leo Jaipur, India wana wafanyakazi 250,000 wanaochakata madini ya Tanzanite inayotoaka Tanzania, lakini Tanzania hatufiki wafanyakazi 10,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipeleka wapi Tanzania na tunawapeleka wapi Watanzania? CCM mkiambiwa kwamba wakati wenu wa kuondoka madarakani umefika, msichukie! Nawaambie kuwa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na baraka za Mtume, Inshalaah mtaondoka madarakani kutokana na mnayowafanyiwa Watanzania. (Makofi)

Leo mtu anakuja hapa, ananyayuka, anakuja juu kwa kasi, analaumu Upinzani halafu anakula matapishi, analaumu Serikali yake. Si kujihanihi wenyewe?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kombo, hebu futa hilo neno lako!

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme; je, si kujidharaulisha? (Kicheko)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa Mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha, kaa.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami nichangie kwenye bajeti ya Wizara ya Nishati. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye kila siku anazidi kutupa Baraka zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme ni kichocheo muhimu sana kwa maendeleo. Umeme na maendeleo ni watoto pacha. Ukitaka kuondokana na umaskini, lazima utoe kipaumbele kwenye upatikanaji wa uhakika wa umeme. Nachukua fursa hii kuipongiza sana Wizara hii kwa jitihada inazozifanya kupitia Serikali kuhakikisha kwamba umeme unapelekwa kwa kasi kwenye maeneo yetu ya Vijijini. (Makofi)

Nakala ya Mlando (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa REA, jitihada ni kubwa katika nchi yetu na Mkinga nayo haikusahaulika. Ipo miradi kule Mwanza Kata ya Gombero, Mapatano, Bwiti, Mabinduro, Bosha, Daluni na Kilongoi. Naomba kasi ya kutekeleza miradi hii iongezeke. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto ndogo ambazo bado yapo maeneo ambayo yameshahaulika, yamerukwa; na ni maeneo ya kimkakati.

Katika Kata ya Gombero tuna mradi mkubwa wa maji pale ambapo tunatumia pump ya diesel. Nafikiri kwa sababu umeme unapita kwenye eneo lile, ni vizuri tukaelekeza nguvu kuhakikisha tunapeleka umeme kwenye chanzo kile cha maji. (Makofij)

Vilevile kwenye eneo hilo hilo, kwenye Kijiji cha Jirihini, umeme umepita pale, unagusa Vitongoji kadhaa lakini eneo la Jirihini limerukwa. Nawasihi sana, eneo hili likumbukwe. Pia Kata ya Kigongoi. Kata nzima ile haina umeme, mradi huu unaelekea kule. Naomba kasi iongezeke ili wananchi wale waweze kupata umeme. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia yapo maeneo katika Kata ya Mkinga ambayo bado hayajapatiwa umeme. Nimewasilisha orodha ya Vijiji, Halmashauri imenorodhesha maeneo yale, tumewasilisha tena taarifa hiyo. Naomba Wizara ichukulie kwa umuhimu mkubwa kuweza kutupatia umeme katika maeneo haya. Nakusihi sana Ndugu yangu Mheshimiwa Mwijage, ile ahadi yako kwamba kabla Bunge hili halijaisha tutapiga kambi pale Mkinga, basi usiisahau. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nayasema haya, nayasema nikielewa kwamba katika mwaka huu uliokwisha, Wizara hii imepata asilimia 35 tu ya bajeti. Hii ni changamoto kubwa! Nawasihi sana Serikali tujitahidi kuhakikisha fedha zile zilizobaki zinapatikana ndani ya kipindi cha mwaka wa fedha huu unaokwisha ili miradi ile iweze kukamilika. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kuimarisha COPEC na GASPO, ni hatua nzuri. Tuendelee kuwaongeza nguvu ili makampuni haya yaweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa jitihada inazokuja nazo za kuleta sheria ya uzalishaji, uvezeshaji na usambazaji. Sheria hizi ni muhimu sana. Sheria zilizopo sasa zimepitwa na wakati. Tuhakikishe sheria hizi tunazileta haraka sana ili tusije kuathirika na rasilimali zetu kupo rwa na kutokuwa na usimamizi madhubuti. Nawasihi sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu sheria hizi zitakapokuja tuzipitishe, kwa sababu ndiyo kitu pekee ambacho kitalinda rasilimali za Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napitia kitabu hiki, nimeona wamegusia juu ya miradi ya joto ardhi, lakini bado naona kasi yetu siyo kubwa sana. Naomba tuongeze kasi katika miradi ile ya joto ardhi katika kuzalisha umeme.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa Mzungumzaji)*

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Ya kwanza hiyo?

MWENYEKITI: Ya pili Mheshimiwa! Ahsante. Mheshimiwa Kayombo!

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, na ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku mbili zilizopita kule Mbanga iliokea ajali kubwa sana na Padri mmoja alifariki na wanafunzi wengine sita. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kuwapa pole na kuwashukuru sana wananchi wa Kigonsera kwa kazi nzuri waliyofanya katika kuwasaidia na kuokoa vifo vile visitokee vingi zaidi. Nampa pole sana Mheshimiwa Baba Askofu ambaye ndiye mwenye shule ile ya Kigonsera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja iliyoko mbele yetu. Tulipokuwa tunazungumzia habari ya Wizara ya Maji, tulikuwa na bahati nzuri kwamba Waziri wa Fedha alikuwepo. Leo Naibu Waziri wa Fedha yupo. Naye Mheshimiwa Waziri jana alikuwa anatupa *comfort* ya kututhibitishia kwamba zile hela zilizobaki katika Wizara ya Maji zingweza kutolewa kabla ya mwisho wa mwezi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti natarajia na ninategemea kwamba pengine Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha atatupa *comfort* ile ile ya kutuhakikishia kwamba fedha ambazo REA inazidai ili kukamilisha miradi ambayo ipo katika Majimbo yetu, zitatoka. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri utampa nafasi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha aweze kufanya hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipokuja Mheshimiwa Rais tarehe 19, mwezi wa Saba 2014, aliongozana pia na aliyejewa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Mhongo; na aliahidi kuipatia Mbanga umeme Vijiji 80. Mpaka sasa zipo nguzo katika baadhi ya Vijiji na katika Vijiji vile kama Matiri, Lukalasi, Mikaranga, Kambarage na ile barabara inayokwenda Rwanda, hakuna nguzo hata moja. Nategemea kwamba program hiyo bado ipo na inaendelea na kwamba hizo nguzo zitawekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Kindimba katika Kata ya Myangayanga, kina mradi wa umeme wa maji. Kijiji hiki kwakweli kimeishaidia REA na naomba kumshukuru Mtendaji Mkuu na wenzake kwa kusaidia Kijiji hicho. Lakini ule msada haujafika mwisho, maana yake ule umeme uliwashwa tu katika Sekondari, Shule ya Msingi, Kanisani na kwenye Zahanati. Tunataka kupeleka kwa wananchi na Halmashauri imechangia katika ununuzi wa nguzo. Kazi hii inahitaji kama Shilingi milioni 170, lakini tukipewa hata Shilingi milioni arobaini, tungeweza tukaanza kazi ya kuweka zile nguzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea na Mheshimiwa Waziri na Naibu wake Mheshimiwa Mwjjage. Naomba sana mtusaidie katika kazi ili wale watu wasikate tamaa. Zile nguzo zimenunuliwa miaka miwili iliyopita, zipo pale, zisioze! Tutapoteza nguvu! Tumepata ufadhili kutoka Ujerumani; vifaa vingi sana viro pale. Nafikiri Serikali ingeweza kuunga mkono kwa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie kuhusu umeme wa makaa ya mawe. Nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri na nimesikiliza. Nimeona STAMICO watafua umeme Megawatt 200 na wanatafuta wabia; lakini Tancoal ambao wanataka kufua umeme sasa, mmewakataza. Mmesema mnatangaza tenda. Kwanini unapofika kwenye Tancoal mkatae, mnafikira kwenye STAMICO mwaruhusu? Kwanini tuwe na double standard katika nchi hiyo hiyo? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii inahitaji umeme sasa na haraka. Kwanini watu wanapotaka kuzalisha umeme huu, mwakatalie?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mmeshandaa hizo bei, kwa nini msiwape hao wakatengeneza? Tancoal ni kampuni tanzu pia ya Serikali. Serikali ina share kubwa sana pale! Masikitiko yangu ni kwamba mradi huu wa makaa ya mawe ya Ngaka hata katika speech ya

Waziri haukutajwa, ingawa mara zote wanajibu maswali yangu. Mheshimiwa Waziri kulikoni hapa? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo makaa mengi sana tunayaiza sehemu mbalimbali, lakini lengo la mradi huu kwa kweli ilikuwa ni kutengeneza umeme ili kuleta unaafuu. Kwa hiyo, naomba mnisaidie hilo. Lakini pia katika makaa ya mawe sasa mmeruhusu makampuni mengi sana yanaagiza mkaa kutoka nje ya nchi. Hao ndugu zetu wa *Tancoal* wanakosa soko. Sasa hivi wameniambia juzi wamenunua tani 300, sasa wanafikiria kufunga ule mradi. Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba mradi huu unaendele tuweze kutumia mkaa wa kwetu hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Wilaya ya Nyasa ni Wilaya ambayo ilianzishwa hivi karibuni na Wilaya nyininge ambazo mmezitaja humu ndani, zimepashapata umeme. Kwanini Wilaya ya Nyasa mpaka sasa haijapata umeme? Mnakumbuka kwamba tumempoteza Mheshimiwa Kapt. Komba; kila mtu anaposimama, anatoa pole kwa familia, anatoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Mbinga Mgharibi; sasa kwanini hatumwenzi kwa kumpatia umeme katika Wilaya yake. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Malima, dakika saba.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hoja hii ya Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze sana Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Kitwanga na Mheshimiwa Mwijage kwa kazi nzuri walinayoifanya katika kusimamia sekta hii ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu, katika mengi ambayo yamesemwa, mimi nataka nizungumzie suala la REA kwa sababu nalijua vizuri. Wakati REA inaanza mwaka 2007, bajeti ya kwanza 2007/2008 nimeifanya kazi mimi nikiwa Naibu wa Waziri wa wakati ule Mheshimiwa Ngeleja, na wakati wa bajeti ya REA sikumbuki kama tulipata zaidi ya Shilingi bilioni nne. Humo kulikuwa na pesa za SIDA na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namna moja ya kufanya kazi ya REA, jambo la kwanza unalofanya ni kwamba huwezi ku-address issue ya Wakala wa Nishati Vijijini, bila ya kuhakikisha kwamba tunatafuta vyanzo vya kupeleka pesa kwa ajili ya miradi mbalimbali iliyokuwepo kwa ajili ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule nakumbuka mwaka 2008/2009, kuna Mbunge mmoja humu aliwahi kusimama, akasema kwamba ukienda Rwanda nchi nzima maeneo yote yana umeme, Tanzania sisi hatuna umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rwanda ni ndogo kuliko Wilaya ya Chunya. Katika mambo ambayo lazima tuambizane ukweli, maana hapa tumekaa tunazungumza mambo mengine ambayo hayatusaidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa tunapeleka baadhi ya miradi ya umeme kwa wananchi, kuna miradi ya umeme unapeleka Shilingi bilioni mbili unaenda kuunganisha watu 30, kwa watu wanaotumia Sh. 15,000/= kwa mwezi. *Four hundred and fifty thousand per month!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema hii miradi itakwenda kutuumiza. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa nchi hii, ninamshukuru, ninampongeza na ndiyo wa kuinuliwa; yeze amesema kwamba miradi hii iende kwa wananchi kwa namna yoyote ile. Kwa sababu miradi hii imeacha kuwa ni miradi ya uwekezaji, imekuwa sasa ni miradi ya huduma kwa jamii.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nihesabie hizo dakika zangu.

TAARIFA

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kafulila!

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mzungumzaji, Mheshimiwa Malima, alipotoa mfano wa kwamba Rwanda ni ndogo kuliko Tanzania ndiyo sababu ni rahisi kuiendeleza. Yeye ni mtaalamu wa uchumi. Ni kweli kwamba Rwanda ni ndogo, lakini nilitaka kumpa taarifa kwamba ukubwa wa Tanzania, kuwa nchi yenye dhahabu nyingi Afrika, kuwa nchi yenye Mito mingi; ya 11 duniani; ukubwa wa Tanzania kuwa na Tanzanite peke yake, ulitosha kufanya nchi hii iendeleee. Ukubwa huu CCM ilipashwa kuifanya kuwa tija.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kafulila ameshakuelewa. Mheshimiwa Malima!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, namsamehe bure. Kwa sababu nililokuwa nasema na analogema yeze ni vitu viwili tofauti. Ninachokwambia ni kwamba huo mradi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Malima, zungumza na Kiti.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuelekeza wewe sasa! Huo mradi mmoja anaosema ambao unaweza ukatengenezwa kwa Shilingi bilioni tano ama sita ukajaza watu chungu mzima, kwa Tanzania unatengeneza mradi kama huo unapeleka umeme kwa watu 2000. Hii nchi ina *nine hundred and forty thousand square kilometers*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba nimepata bahati kwa dhamana niliyopewa ya kupitia miradi na naijua. Muulize Mheshimiwa Blandes kule kwake Nyaishozi kama umeme ulikuwa unafika kama siyo REA! Muulize Mheshimiwa Herbert Mtangi, nimekwenda Muheza, muulize kama kulikuwa hakuna REA! Tunduru kule kwa Mheshimiwa Abdallah Mtutura!

Sasa mnachosimama hapa mnasema Serikali ya CCM inafanya kiini macho, inawahadaa wananchi, *Lailah ainallah!* Basi mkizungumza, zungumzeni muwe wa kweli kidogo. Mimi naijua, nimekwenda. Nilikwenda wakati wa kiza na sasa hivi hawa wanaofanya kazi hii wanafanya kazi nzuri na miradi mingi inaendelea. Miradi ile haikuwa na kigezo cha uwekezaji wa kiuchumi, ilikuwa ni huduma kwa jamii ili wananchi wa Tanzania wapate umeme ambao utawasaidia kujikwamua kiuchumi. Sasa kama hamlijui, basi usilolijua ni usiku wa kiza. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, pesa zinazochangia kwenye REA zina vyanzo vinne. Ina ruzuku ya Serikali, inatozwa kutoka kwenye mafuta, inatozwa asilimia tatu ya TANESCO na kuna pesa nyingine ambazo Serikali inakopa kwa ajili ya kukamilisha miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maana hiyo, vyanzo hivi unavipangia bajeti, lakini kama ukusanyaji haukwenda sambamba au matumizi ya mafuta hayakwenda sambamba na mipango iliyokadiriwa, mtakusanya ndoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichofanya ni nini? Jambo moja kubwa ambalo limesemwa na Kamati na tumekiri kwamba ni tatizo, ni kwamba pesa ziliwu zinatoka TRA zikishakusanya kwenye mafuta, zinakwenda Wizara ya Fedha, zikarekodiwe; zinakwenda Benki Kuu zikishatoka Benki Kuu ziende REA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekubaliana kwa ushauri wa Kamati za Bunge kwamba pesa za TRA zinazokusanya kwenye tozo za mafuta ziende moja kwa moja REA.

Kwa maana hiyo, hakuna kelele. Kichokusanya ndicho kinachokwenda. Ikitoka pale, sisi tunaletewa karatasi. TRA tumekusanya kiasi fulani tumepeleka REA moja kwa moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika miezi mitatu, minne, ufumbuzi tuliuopata ni huo na tunaenda kulifanya kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu huo sasa, matarajio yetu ni kwamba pesa zile ambazo zimekusanya zitakwenda moja kwa moja. Pesa nyininge ambazo zinategemea kwenye bajeti na mikopo ya Serikali na vyanzo vingine, lakini kwa kiasi kikubwa, pesa hizi ni zile ambazo tunakusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, kuna fikra moja amezungumza pale Mheshimiwa Kombo maskini, zinazokusanya kwa Watanzania ni dhuluma nakadhalika. Hajui kwamba hata hiyo tozo unakusanya labda Shilingi bilioni 150. Kile kinachokusanya kutokana na tozo ya mafuta, labda kinakidhi mahitaji ya asilimia 30 ama 35 ya miradi yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine linalozungumzwa ambalo kwa bahati mbaya sana natarajia Mawaziri wenzangu watanisaidia hapa, ni kwamba tulifanya maamuzi ya makusudi.

Mwaka 2008 Wakandarasi walikuwa wawili tu kwenye miradi ya REA; Rousant na Symbion. Tukaleta Wakandarasi wengine, local contractors ili kuongeza wigo wa utekelezaji wa miradi. Kuna baadhi ya wakandarasi wengine utendaji wao siyo mzuri; wengine wapo hata Jimboni kwangu Mkurunga. Juzi tumekwenda tumetembelea miradi ya REA, pesa imekwenda nakadhalika, lakini unakuta watu hawajalipwa na tumetembea Wilaya nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lazima tuwe wakweli. Jambo la Ngoswe, mtupie Ngoswe. Kuna maeneo mengine ambayo REA imefanya vizuri, inasimamia vizuri, akina Dkt. Mwakahese na nani, pesa zinakwenda kwa Wakandarasi. Wakandarasi wenyewe ndio wana matatizo! Kwa hiyo, jambo moja ambalo tumekubaliana na tumewaomba TANESCO na tunaiomba Wizara ya Nishati na Madini kwamba tunapotoa pesa zile tuhakikishe kwamba kama Mkandarasi ambaye yupo certified na TANESCO kufanya kazi hiyo, kama inamshinda hiyo kazi tuwaondoe. Kwa sababu vinginevyo, hata ile pesa Serikali unayoipeleka pale inakuwa haipati ufanisi ule unaotakiwa. Matokeo yake wanapatikana watu wa kusema maneno kidogo ambayo hayafanani na ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba tatizo linaweza likawepo lakini kuna hatua mbalimbali. Pesa za Serikali tumezitoa, nimeambiwa pale na Mheshimiwa Kayombo, naomba nikuahidi Mheshimiwa Kayombo kwamba kwa utaratibu tunaokwenda nao sasa hivi, pesa zote zinazotokana na tozo, zitakwenda moja kwa moja. Zinazotokana na utaratibu wa

bajeti, bado hizo zinategemea na vyanzo vingine. Kwa hiyo, kama tumekusanya fedha, kile kilichomo kwenye bajeti; zile za tozo ni direct, hizi nyingine zinategemeana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana (*Makofii*)

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo!

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mimi nikisimama wewe unakaa, ndiyo utaratibu!

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini uone sasa!

MWENYEKITI: Kaa basi.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Eeeh!

MWENYEKITI: Mwenyekiti Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mpina, anaomba kuitangazia Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kwamba leo tarehe 6, mara baada ya kuahirisha kikao cha Bunge, kutakuwa na kikao cha Kamati katika ukumbi wa Pius Msekwa.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kuhusiana na jambo limejitokeza hivi karibuni, kufuatia mimi kunyimwa nafasi ya kuchangia ilihali nilikufahamisha tangu asubuhi kwamba nimeomba.

Lakini pili, NCCR Mageuzi kama ilivyo utaratibu wa Mheshimiwa Spika, kwamba kuna idadi ya NCCR, idadi ya CHADEMA, idadi ya CUF na kuna idadi ya CCM. NCCR Mageuzi haikupata hata mchangiaji mmoja, lakini zaidi ya yote katika jambo ambalo naona kwamba kuna mashaka na kuna mkakati wa kuzuia baadhi ya hoja kuja mezani hapa, ni wakati nawasiliana na wewe Kiti chako hapo kinawasiliana na Wizara. Yaani Wizara inapanga mtu wa kuzungumza huku Bungeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kuhusu uhuru wa kiti chako, naona kabisa kuna kila dalili kwamba....

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kafulila, kaa chini. Kwanza Mheshimiwa Kafulila, Kiti hakina nafasi yoyote ya kupanga majina. Subiri tena usitake kunijibu wakati nasema, *behave yourself*.

Mheshimiwa Kafulila, napewa orodha ya majina na Vyama vyenu, tatizo liliopo hapa huo UKAWA wenu ni wa nadharia tu. No, no, no!

*(Hapa Mheshimiwa David Z. Kafulila alikuwa
akibishana na Mwenyekiti kuonesha kutoridhishwa
na maelezo yanayotolewa)*

MWENYEKITI: Subiri Mheshimiwa Kafulila, kama una uthibitisho Kiti kinapanga majina lete. Hilo la kwanza, wewe huzungumzi na mimi.

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Hapa Mheshimiwa Kafulila aliendelea kubishana na Mwenyekiti kuonesha kutoridhishwa na maelezo yanayotolewa)

MWENYEKITI: Usinijibu sasa kwanza. Kwanza usinijibu acha niseme.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Lazima nikujibu.

MWENYEKITI: Usinijibu! Huna nafasi ya kunijibu, acha niseme.

Waheshimiwa Wabunge, CCM wameleta majina 11, CHADEMA majina Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Gervas Mbassa; CUF Mheshimiwa Suleiman Bungala, Mheshimiwa Kombo Khamis, ndiyo majina yaliyoletwa hapa, wanne kwa 12.

(Hapa Mheshimiwa Cheyo alikuwa akibishana na Kiti)

MWENYEKITI: Mzee kaa kimya, wewe kama haupo UKAWA subiri utajunga UKAWA baadaye. Kuna muda ambaa umepangwa hapa, leo ni Jumamosi hatuendani na ratiba za siku zingine zote, hilo moja. Pili, Kiti hakina nafasi kabisa ya kumdhulumu mtu. Nimekujibu barua yako na nikakwambia nitakupa nafasi kwenye mshahara, ni dakika tano, una dakika tano, una dakika ya kutoa hela ukapata dakika tano zingine, kaa chini.

Mheshimiwa Naibu Waziril

(Hapa Mheshimiwa David Z. Kafulila aliendelea
kubishana na Kiti kuonesha kutoridhishwa
na maamuzi yaliyotolewa)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kafulila behave yourself ndani ya Bunge. Hakuna mtu anayeogopa. Sikiliza, jipangeni wenye huko kwenye Vyama vyenu, napata orodha hapa.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Kila chama kimeleta!

MWENYEKITI: Basi kaa chini, nafasi umekosa, kaa chini.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia uhai na nguvu ili nichangie hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini ya Bajeti ya 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Spika binafsi, namshukuru Naibu Spika, Kamati ya Bunge na bwana.....

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunataka order ndani ya Bunge.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu ulindwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Spika yeye binafsi, Naibu Spika, Katibu wa Bunge na Watalaam wa Bunge kwa kunipatia fursa mimi kushiriki kwenye Kamati ya Nishati tangu naingia katika Bunge hili. Uamuzi huo umenipatia fursa ya kutumia taaluma yangu kwani leo ninapozungumza nimefikisha miaka 31 tangu niingie kwenye sekta hii. Niliingia kwenye sekta ya mafuta nikiwa nasimamia valve, navaa magwanda ya kaki, leo nasimamia sekta ya nishati nikiwa Naibu Waziri wa Nishati ninayesimamia mambo ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwamba anapohitrimisha Awamu yake ya Nne dakika za mwisho kabisa aliona ni bora anipatie fursa ili kusudi niweze kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi. Watanzania wataamua, wana-CCM mtaamua kama nimeitendea haki hii fursa niliyopewa.

Mheshimiwa Spika, wakati nachangia hotuba ya bajeti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa ushirikiano na mahusiano tuliojenga. Mheshimiwa Simbachawene ni rafiki yangu wa kwanza nilipoingia katika Bunge, tulikuwa tukichakata mijadala yote pamoja, lakini namshukuru Classmate wangu Mheshimiwa Kitwanga tumetoka wote Tosamaganga, tumekuwa wote shule na sasa tupo Wizara moja. Nawashukuru Watendaji wa Wizara na taasisi zote, ushirikiano mnaonipa umeiwezeka kazi hii iende kwa kasi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu naishukuru familia yangu hasa kitinda mimba change, Nyangireki, kijana huyu ananipa moyo katika kazi zangu. Nawashukuru wana-Muleba na wana-Kagera na Watanzania wote na watu wote amba wanantia moyo katika kazi hii, wakiwepo traders wa Kimataifa amba nimefanyakazi nao katika shughuli za mafuta. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, naomba nianze kwa kuwaasa Watanzania wenzangu, uwepo wa rasilimali gesi na baadaye tukipata mafuta haitakuwa laana kwetu. Naomba nirudie, uwepo wa rasilimali gesi na baadaye tukipata mafuta haitakuwa laana kwetu. Tuelimishane, tushauriane, tuwe na subira na tutulie ili tuvune rasilimali hii kwa manufaa ya kizazi hiki na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nzungumzie kwa ufupi sekta ninazosisimamia. Tunasimamia vizuri sekta ya mafuta. Mafuta yamekuwa yakiingia nchini yaliposhuka bei wananchi mlipata pungozo la bei sawia. Shughuli za utafutaji na uchimbaji wa gesi zinaendelea. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge kuna shughuli za uchimbaji zinaendelea Tanga, kuna shughuli za utafutaji zinaendelea Ruvu, Chalinze, nendeni mfike pale muone shughuli ya uchorongaji kama anavyosema Mheshimiwa Mangungu kwamba utafutaji na uchimbaji wa mafuta siyo kama kuchimba viazi, kwa hiyo tutumie fursa hii, twende kwenye maeneo tujuje hatarisho ambalo wanalipata wale wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawajibu Wabunge waliochangia katika ajenda zilizopita. Imekuwepo hoja ya kwamba tuhakikishe mafuta yanaingia nchini kwa uhakika, tumeamua na Mheshimiwa Waziri atawaambia tena. Tunapitisha mafuta Tanga. Hifadhi za Tanga zitakazojengwa zitaondoa upungufu wote wa hifadhi ya Dar es Salaam, upungufu wote uliopo Dar es Salaam utaondolewa. Tutaweza kuhakiki mafuta yanapoingia ndani ya matenki kwa kutumia electronic lakini tutakuwa na bonded warehouses tunaweza ku-backload na kufanya trading, tutaweza pale kufanya kitu kinaitwa bunkering. Kwa hiyo, Tanga kumekucha na nimshukuru Mzee Nundu kwa kutuunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala la umeme. Kuna watu amba wanaindeza TANESCO, namshukuru Mjomba wangu Mheshimiwa Malima. TANESCO wanafanya kazi kubwa, unasafirisha umeme kilomita 120 unakwenda kupata mteja mmoja, economics ziko wapi? Hata hivyo, Mheshimiwa Dkt. Kikwete alituambia siyo kwamba mnakwenda kuiangazia Taifa, bali mpeleke umeme kule ambako watu hawatarajii, ndicho tunachofanya. Tunapeleka umeme ambako hatutarajii, nichukue nafasi hii kumshukuru Mbunge wa Sikonge, ameamua kuanzisha business center ambako magogo yatachakatwa Sikonge na hakuna gogo litatoka Sikonge kuja mjini, tutataka fenicha zitengenezwe kule mjini, ndiyo namna ya kumuenzi Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumze suala la *mini-grid*, tunaandaa mpango wa kuwa na *mini-grid*, msiwe na wasiwasi Watanzania, sehemu za Delta kwa Mzee Kaombwa, sehemu za Visiwa ikiwemo visiwa vya Goziba na Bumbile, sehemu za Mbuga za wanyama tutatengeneza *mini-grid* na terehe 6 Julai, Waheshimiwa Wabunge tukiwa hapa, wanakuja watalaam kutoka Marekani kuleta mitambo bure *it is a grant*. Wanakuja kuniona, nawaalika mje hapa, wanakuja kuhakikisha kwamba mambo yanapendeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirukie kwenye hoja za Wapinzani. Naomba Wapinzani mnisikilize, wakati nazungumza, nahestimu taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Silinde. Hoja aliyoitoa Mheshimiwa Silinde inatengua ukurasa wa 23 na ukurasa wa 24. Ukurasa wa 23 na 24 wa Upinzani Mheshimiwa Silinde ameutengua, ni Mjumbe mwenzangu wa Kamati ya Nishati, namheshimu. Naendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa nane imeelezwa kuhusu Artumas, Kambi ya Upinzani inasema Artumas alikuja akachuma gesi, baada ya kuchuma gesi akaondoka, siyo gesi! Hatujawahi kuvuna gesi na Artumas. Kuvuna gesi inahitaji bomba, kuvuna gesi inahitaji *LNG Plant* alitumia *LNG Plant* gani? Huo ni upotoshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende ukurasa wa nane pale pale, Serikali imetenga miradi yenye thamani ya kiasi gani. Mheshimiwa Waziri atarudia tena kueleza namna watu wa Mtwara watakavyofaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lulida amesema bilioni 48 tunaweka ziada kutengeneza. TPDC nimewaelekeza namna ya kushughulika na Mkusa mmoja mzima wa gesi. Zaidi ya hapo, ukurasa wa kumi, Msemaji wa Upinzani amezungumzia Bulk Procurement kwamba ina faida gani, ndiyo ina faida. Kutokana na saving kwenye demurrage, tulikuwa tuna-suffer demurrage ya dola hamsini mpaka sitini kwa tani, through bulk procurement demurrage ni 1.5 per tone, tume-serve bilioni 365 kwa kuchukulia mafuta tunayo-import kwa mwaka, hiyo ndiyo serving.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa kumi anazungumzia COPEC, namshukuru Mdogo wangu Kitandula anajua anaelewa kwamba COPEC iko njiani inakuja na tunaendelea kuiimarisha COPEC, nilikuwa naisemea, Mheshimiwa Mntangi Mkuu wangu wa kazi alikuwa anaisemea, sasa nimepewa jukumu la kuhakikisha kwamba COPEC inasimama na GASCO inasimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala la REA, kuna ukweli ndani ya REA, inauma mtu anapopotosha. Katika taarifa ya Msemaji wa Upinzani anazungumza kwamba tulianza kutoza tozo Januari 2011 siyo kweli. Tulianza Julai, 2013. Anazungumza bilioni 400 siyo kweli, mzungumze hoja za ukweli ili kusudi huyo tunayemwomba mwenye chungu, tunayemtaka aweze kutupa kile kinachostahili. Takwimu zilizotumika za EWURA siyo sahihi, mafuta yanayoingia nchini ngoja nikueleze, that is my job. Mafuta yanayoingia nchini KOJ 9, kuna transit product, kuna Jet A1, kuna HFO hayatozwi tozo, kwa hiyo mzungumze uhakika. Hiyo siisomi ni uzoefu wangu ambao nimefanya kazi nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Kamati ya Nishati, michango yenu Kamati ya Nishati nakubaliana nanyi, mapendekezo yenu kuhusu pesa na nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge aliyesema kwamba kwa sababu mahitaji ni makubwa kila sehemu wanataka umeme, tukubaliane tuongeze tozo. Ni juu yetu sisi Wabunge. Ametueleza Mheshimiwa Malima kwamba tozo zote haziwezi kuzidi bilioni 150, kama tunatambua wananchi wetu wanataka umeme basi tuongeze zaidi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la umeme kwamba wengine wanabaguliwa na wengine wanacheleweshwa. Tumelitatu hilo, tumeanza kitu kinaitwa *modal purchasing*, *power purchasing agreement*. Mheshimiwa Kayombo tumeanzisha MPPA kwa hiyo utakuja utapewa *modeling* ya *power purchasing agreement* utajiondoa mwenyewe. Hata hivyo, ngoja niwaambie, ubaguzi ulikuwepo na kwa nini ulikuwepo, ulikuwa ni wa makusudi, kuna watu walidhani nchi hii ni shamba la bibi, wakawa wanakuja na *tariff* za juu walikuwa wanakataliwa na wataendelea kukataliwa. Uje na bei ndogo utaruhusiwa kuzalisha umeme, ukija na bei kubwa hili siyo shamba la bibi. Kama ni watoto wa marehemu wamekua sasa wanadhibiti mali yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hoja za Wabunge, sina muda, lakini katika ukurasa wa 20 wa Wapinzani msisahau mpitie suala la TANESCO, zabuni iliyotajwa PA 106 namba yake halisi ni PA 030 mradi huu unatekelezwa kwa awamu. Awamu ya kwanza ni mwaka 2013 ulitengewa shilingi za Kitanzania milioni 400, katika mwaka 2014 mradi ulitengewa shilingi za Kitanzania bilioni tatu, hivyo mradi huu haujakiuka sheria za manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maneno ni njama za kuonesha kwamba TANESCO haifai. TANESCO ndio general electric ya Tanzania, kama una matatizo na mtu, mtu aondoke lakini TANESCO ndio general electric ya kwetu. Kwa hiyo, anayeandika awe na habari za kina na hatuna uhasama, njoo uniilize, ndio dhamana niliyopewa. Kama unataka kujua TANESCO uje uniilize. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi kabambe wa kusambaza umeme vijiji (REA-Phase II na III). Niwaeleze Wabunge wenzangu tunakwenda REA III, tunawaomba ili twende vizuri Mheshimiwa Waziri ameleekeza, hoja zenu zote tuzipeleke Wilayani. TANESCO wachakate, vijiji vilivyorukwa tumeshaainisha tutaleta transforma 4000, tutadondosha umeme lakini inategemea na upatikanaji wa pesa. Baada ya kuainisha tunasema shule zote zitapata, wigo mdogo utaongezewa, lakini yote mapenzi yetu yanategemea na rasilimali ambazo sisi tutaweza kuzikusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda siyo rafiki nizungumzie hoja za Wabunge. Nimshukuru Mheshimiwa Seleman Zedi na Mheshimiwa Badwel wamezungumzia miradi, miradi yenu yote itatekelezwa. Kuna kasi ndogo ya usambazaji wa umeme, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amezungumza, pesa zitapatikana na tutasukumana kwenda kupeleka umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, langu binafsi napigana umeme uende Momba, tumeandika Waziri wa Maliasili amekubali kuruhusu msitu ufyekwe umeme uende Momba, kwa hiyo suala la Momba halina matatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la ukatikaji wa umeme. Ukatikaji wa umeme, Biharamulo Mheshimiwa Mbassa naona ameondoka, Biharamulo niliwaambia tarehe 4 mwezi wa Sita nawasha umeme, nimeshawasha. Mpanda kuna suluhisho linakuja na Ngara kuna suluhisho linakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine hayatoshi...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Ahsante, Naibu Waziri mwininge!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu, vile vile nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunipa nafasi katika hii Awamu ya Nne, nilianzia Sayansi na Teknolojia, nikajifunza, nikaenda Ofisi ya Makamu wa Rais nikafahamu Zanzibar, nikafahamu maeneo yote yanayohusu mazingira na sasa hivi nipo Wizara ya Nishati, nimeanzia Nishati na sasa hivi nipo Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana vile vile wapiga kura wangu katika Jimbo langu la Misungwi tunaendelea, sisi hatuna Mpinzani tunaendelea mbele, wanaojifanya wanakuja UKAWA tutaonana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru vile vile familia yangu kwa ushirikiano ambao wameendelea kunipa, lakini kwa sababu ya muda niende haraka haraka katika kujibu hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa. Nianze na North Mara kwa sababu imekuwa ni wimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria iko wazi kama ilivyo sheria ya barabara, barabara ukiifuata hulipwi, barabara ikikufta unalipwa, hivyo hivyo kwa mgodi, ukiifuata mgodi hulipwi, mgodi ukikufta utalipwa. Kwa hiyo, tunafuata sheria na sheria iko wazi kabisa. Kwa hiyo, ndugu zangu wa kule North Mara nilisema hivi na upotoshaji katika hotuba ya Upinzani imesema kwamba tunafanya ubaguzi wa Wazawa. Hatujasema Wazawa wala nini, tumesema kwamba wananchi wote ambao mgodi uliwakuta pale North Mara watalipwa na watapata compensation na wale waliofanyiwa tathmini na walikutwa na mgodi watalipwa. Kufanya tathmini maana yake siyo kulipwa watu wote, kwa sababu huyu Mwekezaji alipokuwa anafanya tathmini alikuta wengine waliokuja kutegesha, kuna neno linaitwa kutegesha kwa Kiingereza wanasema speculation.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anakuja akishasikia kwamba hapa watachimba anakuja anajenga, anapojenga anataka alipwe, lakini amekuja kujenga wakati tayari mwenye mgodi kwa Sheria ya Madini ya mwaka 2010 tayari haruhusiwi kujenga pale. Sasa huyu ameufuata mgodi, huyu hatalipwa na ndivyo tulivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho kimezungumzwa cha kupotoshwa kabisa, ni kwamba, vikao halali vilikaa. Nitoe taarifa tu ambayo vile vile Mheshimiwa Msomaji wa Taarifa ya Waziri Kivuli ambaye hayupo, inanishangaza kabisa ndiyo sababu nasema kwamba hawa wenzetu bado mno. Wewe ni Waziri Kivuli, siku ya kusoma Wizara yako haupo una-delegate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu cha kushangaza zaidi hotuba ya wenzetu mwanzo mpaka mwisho ni mipasho, kitabu chote hakina alternative budget, leo hii tukiondoka watafanya nini?

WABUNGE FULANI: Ondokeni.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Ndiyo sababu hatuondoki na hamtatutoa kwa sababu *you are not an alternative*. Kwa sababu, *alternative* wanaweka bajeti *alternative*, hamna bajeti mbadala, yote hapa yaliyosemwa ni kuzungumza yale ambayo Watanzania tunawaeleza kuwafanya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ongea na kiti utapata taabu kuanza kujibu watu, wewe jibu hapa wananchi wakusikilize. Una jukumu la kuelimisha Bunge na wananchi, asiyetaka kusikiliza mwache asisikilize.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hili tunalosema kwamba, walibaguliwa; mkutano walikaa, walipokaa wananchi ambao wametegesha wakaja wakashawishi, wakaandika muhtasari ambao ukapelekwa kwa Mkuu wa Wilaya. Wananchi wanaostahili kulipwa walikuwa wananchi 290 nao wakaandika muhtasari; niko tayari kuleta mihtasari yote miwili hapa, waliotegesha wameandika muhtasari na hawa wengine wameandika muhtasari, niko tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliambie tu Bunge lako Tukufu na wananchi watambue, kuanzia Aprili mwaka 2012 mpaka Machi mwaka huu North Mara imelipa fidia katika eneo lile ya jumla ya shilingi bilioni 60 na hizi ziko hapa, niko tayari kuweka. Hata hivyo, ukiangalia kwa mfano, kitongoji kimoja kimelipwa fidia ya bilioni 28. Kitongoji kingine, sehemu moja imelipwa bilioni nne, lakini nyine imelipwa bilioni saba, lakini hii iliyolipwa bilioni saba, kitongoji jirani yake kinaomba na chenyewe bilioni 29, kwa sababu ya kitu kinaitwa kutegesha (*Speculation*)!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili jambo tuungane tu na Mheshimiwa Esther Matiko ambaye siku zote tumekuwa tukienda naye kule, tuhakikishe kwamba, wale ambao mgodi umewakuta watalipwa kwa sababu, ni haki yao na ndivyo Sheria inavyosema. Uzuri wa Sheria ya Ardhi inasema watalipwa kwa *the current value* ya ardhi; watalipwa kwa *the current value* ya ardhi. Ukiangalia baada ya mimi kuongea na watu wa North Mara, wanalipa mara tano ya value ili kuwashawishi. Sasa ukiangalia hata *per square kilometre on average, cost per square hectare* ni shilingi milioni 454 na milioni 300 *per square hectare*, hekta moja wanacholipa hawa watu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, haya mambo yanaletwa zaidi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, hivi unampenda mtu kule? Zungumza na mimi! (Kicheko)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuzungumzie suala la mita 200. Hili la sasa hivi analolizungumza mita 200 wanazosema, nitoe mfano mmoja tu; wanachofanya, kuna mfanyakibashara mmoja alilipwa shilingi milioni 300, lakini kule kule kijiji baada ya kuwa ameshalipwa, mgodi umeshaanza katika eneo hilo, akaenda kujenga mita 25 hostel ya vyumba 87, mimi mwenyewe nimekwenda siku hiyo nikashuhudia ujenzi unaendelea! Sasa mambo kama haya yanalamikiwa, lakini huu ndio ukweli. Kwa hivyo, sisi tutashirikiana Serikali za Vijiji, Serikali...

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther hebu vumilia. Umezungumza... No! No! No! kuna Kipindi kita... Hebu kaa chini Mheshimiwa Esther!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie atulie kwa sababu, nitasema mengine ambayo hayastahili kusemwa hapa.

WABUNGE FULANI: Sema yote!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Mwenyekiti, maana asubuhi hii nimeongea na Mheshimiwa, baada ya yeze kumpigia Mheshimiwa DC na akamweleza na akaniambia jamani nakwenda kugombea, acha nitetee watu wangu! Si mnasema niseme! Sasa hayo mengine ngoja tuyaache hapo, waache wagombee huko, lakini wasitumie wananchi kuwadanganya. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la wachimbaji wadogo. Suala la wachimbaji wadogo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana wakati wa Hotuba ya Waziri Mkuu na leo hii. Kwa mfano, Mheshimiwa Bukwimba suala lake tumelifanyia kazi, watu wa Nyarugusu, mimi mwenyewe nimefika kule, nimetembelea, tumezungumza na mwekezaji na mwekezaji amekubali kutoa sehemu ya eneo hilo. Sasa hivi tunachofanya ni kuhakikisha kwamba, taratibu zote za Kisheria zinafuatwa ili tuweze kuhakikisha kwamba, hawa wachimbaji wadogo wadogo katika eneo la Nyarugusu wanapatiwa sehemu za kuweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili vile vile limezungumziwa na Mheshimiwa Vicky Kamata na leo hii tena Mheshimiwa Bukwimba amesisitiza. Maeneo mengine vilevile tunaendelea kutenga, sio tu kutenga maeneo, lakini vile vile kuwawezesha hawa wachimbaji wadogowadogo; mwaka huu tulitangaza utoaji wa ruzuku, kabla ya hapo tulikuwa tuktoa mikopo, lakini kinachofanyika kwa sasa hivi ni kuhakikisha kwamba, wachimbaji wetu wadogo ambao walikuwa wanashindwa kuandika Busines Plan, tumetengeneza fomu rahisi ambayo anaijaza, anapoanza kujaza hatua ya kwanza mpaka anapofika mwisho, inakuwa ni Busines Plan, lakini watu wote wajaze halafu Kamati kwa uwazi kabisa itakaa, itachuja, itaona nani anayefaa kupewa mkopo na nani ambaye asubiri kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo kwa wachimbaji wa North Mara na Geita peke yake, ni kwa wachimbaji wadogo wote wa nchi nzima na sio kwa dhahabu peke yake, ni kwa aina zote za madini na vito. Kwa hivyo, wananchi waendelee kuwa na subira na katika bajeti yetu mwaka huu, kama mtakuwa mmeona, tumeongeza kidogo tuone ni kwa namna gani mwaka huu tena tunaweza tukaendelea kutoa ruzuku kwa wachimbaji wetu; mwanzoni ilikuwa ni mikopo, sasa hivi tunatoa ruzuku. Ruzuku hii inapotolewa tunafanya ufuatiliaji kuona kwa namna gani hawa wachimbaji wadogo wanakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia duniani 60% mpaka 70% ya dhahabu inayopatikana, hupatikana kutokana na wachimbaji wadogo na wachimbaji wa kat. Research iliyofanyika kwa Tanzania wachimbaji wadogo ndiyo wanaozalisha dhahabu nyingi zaidi. Japokuwa tuna tatizo la kuhakikisha kwamba, hawa wachimbaji wadogo ambao tunawatetea vile vile wafuate Sheria, waweze kulipa tozo, waweze kulipa mrabaha, waweze kulipa kodi zote ambazo zinatakiwa za Serikali, ili mchango wa madini katika pato letu uweze kuwa mkubwa zaidi.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mto Hoja!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza niwashukuru sana wachangiaji karibu 19 tuliowapata, waliochangia katika Wizara yangu ya Nishati na

Madini. Aidha, nianze kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa mchango wao ambao umesomwa na Mwenyekiti mwenyewe, Mheshimiwa Ndassa, ambao ulikuwa unatuongoza vizuri na kutushauri vizuri, ili tuweze kumalizia ngwe yetu na kumalizia kazi tulizoahidi kuwafanya wananchi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, nimshukuru sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika Wizara hii kwa hotuba yake ambayo, imesomwa na Mheshimiwa Esther Matiko, kwa yale yote ambayo wameyasema mazuri, tutayachukua na tutaya fanya kazi na yale mengine ya vijembe ni siasa, hatuna cha kufanya nayo chochote. Pia, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla kwa michango yao mizuri ambayo kwa hakika imejikita katika kutusaidia, ili muda huu mdogo uliobakia tuweze kumalizia kazi zetu na twende tukawaombe wananchi kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki ni vizuri sana ukiwa Mbunge makini unayejua maana hasa ya kazi yako ya Ubunge, unasema yale uliyoafanya katika kipindi cha miaka mitano ulipoingia madarakani, bila kujali wewe ni Mbunge wa upande gani. Kwa sababu, wananchi hawatakuchagua kwa umahiri wako wa kukandia yaliyofanyika! Wananchi watakuchagua kwa kazi ulizozifanya. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wa Kambi zote, wale walioishukuru Serikali kwa kazi walizozifanya kwa miaka mitano katika Majimbo yao. Nawashukuru sana. Kwa wale ambao wanaendelea kunung'unika maana yake ni kwamba, wameshindwa kuwawakilisha wananchi, hawastahili kuchaguliwa maana hakuna kilichofanyika kwenye Majimbo yao. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya REA inayofanyika katika nchi nzima ni miradi iliyoaamsha uchumi wa Taifa letu. Ni miradi iliyoaamsha wananchi wetu kutaka maisha bora na ndiyo maana katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi tumewaa hidi Maisha Bora Kwa Kila Tanzania tulimaanisha mambo haya. Katika kipindi cha miaka 10 ya Awamu ya Nne ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kama Rais wa nchi, tumetoa kutoka kwenye 10% ya Watanzania waliokuwa wanapata umeme mijini na vijijini hadi 36%. Haya ni mafanikio makubwa sana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2010 – 2015, tuliahidi kupeleka umeme mijini na vijijini kwa 30%, tumezidi lengo hilo tumefanya kwa 36%. Kwa hiyo, tumetekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi zaidi ya pale tulipokuwa tumejipangia. Haya ni mafanikio makubwa na wananchi lazima muone na ninyi ndiyo mnaoshuhudia yanayofanyika katika Vijiji vyenu, katika Kata zenu, katika Tarafa zenu na mambo makubwa mengi yamefanyika na wananchi ni mashahidi. Katika hili wala si suala la propaganda, wananchi mnajua kilichofanyika na mtu akisema hakuna kilichofanyika, nyie ndiyo mnaofahamu na majibu yake mtamwonesha maana yeche si sehemu ya mafanikio haya. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, kama nilivyoileza, unatokana na msingi wa mahitaji ya Watanzania. Sisi tutaendelea kama Chama cha Mapinduzi na Serikali yake kupeleka umeme vijijini na wale ambao wananchi waendelee kunung'unika kwa sababu, inakatisha tamaa pale ambapo Hotuba ya Upinzani Ukurasa wa 25 inasema:-

"Kinachofanyika sasa katika kupeleka umeme vijijini ni kuwatapeli wananchi kwa kusambaza nguzo tu na sehemu zingine kuzisimika tu na sehemu zingine wanaunganisha nguzo tatu au nne kwa waya, ili wananchi waamini kuwa umeme unaletwa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hakuna ubishi katika hili, wananchi wanajua, wanaona, umeme unawashwa, lakini usitegemee mtu asiyekupenda kukusifia na usitegemee mtu asiyekupenda kukupa ushauri. Wahenga walisema ukiona mtu ambaye hakupendi, unajua ni adui yako, akikupa ushauri, huo ushauri kataa. Kwa hiyo, nasema hatutarajii kusifiwa katika hili na tunaamini kabisa kwamba, tuliyoyafanya Watanzania ndiyo watakaotuhukumu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa miradi ya umeme sehemu kubwa ni ukusanyaji wa vifaa na kuvipeleka katika eneo la kazi. Nguzo huwezi kuzifungia kwenye stoo, ni lazima ukizitoa bandarini uzipeleke sehemu utakakojenga, Watanzania ipigieni makofi Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu, tunatoa vitu bandarini tunaweka kwenye maeneo yenu na ninyi mnaona. Kazi nyine ukishamaliza hapo ni kuanza kuifanya, sasa umeshapeleka vitu kwenye eneo la kazi ni kuanza kuifanya; ndiyo maana wananchi tumewaambia walinde vitu hivi, washirikiane na Wakandarasi kuhakikisha kwamba, kazi hii inatekelezwa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi inayofuatia sasa ni kujenga maeneo hayo na tumeshaanza kujenga. Kwa sasa niseme tu kama taarifa, juzi nimewaita Wakandarasi wanaofanya miradi yote nchini; Makandarasi wako 35, makampuni 35 yamezagaa nchi nzima wanajenga miradi ya umeme. Katika tathmini tulioifanya, malipo tuliyoyafanya ni 48%, ukifanya average ya kazi zilizofanyika ni chini ya 48% maana yake ni kwamba, tumelipa vizuri isipokuwa kazi tu-push zaidi, ili Wakandarasi watekeleze kazi yao. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tunalifanya na tutaendelea kulifanya, ili kuhakikisha kwamba, wananchi wanapata umeme. Jambo ambalo nataka niwasih sana Waheshimiwa Wabunge wale amba mnaridhika na mnafurahia kazi hii iliyofanyika ni kwamba, kweli wananchi wamehamasika na karibu maeneo yote wanataka umeme, lakini siyo rahisi kwa mara moja tukapeleka umeme katika nchi nzima, siyo rahisi, lazima tutakwenda kwa awamu. Hivi sasa Waheshimiwa Wabunge tunaandaa awamu ya tatu ya utekelezaji wa Miradi ya REA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana wale wananchi amba wanahitaji umeme, viongozi amba mnawasimamia wananchi wenu vizuri, kupeleka maombi haya kwenye Ofisi zetu za TANESCO za Wilaya na Mikoa, ili tuanze kutengeneza awamu ya tatu. Niwatoe mashaka Waheshimiwa Wabunge mnaorudi kwenda kusema maeneo ambako mmeweka umeme, yale maeneo ambayo bado naomba sana wananchi wetu mnaokwenda kutuchagua, msiwahukumu Waheshimiwa Wabunge kwa sababu, hapa tukiweka kesho yake haturudii hapo, tunaendelea mbele. Kwa hiyo, kama bado Kijiji chenu hakijapatiwa umeme siku zijazo, kwenye awamu hii ya tatu inayokuja, mtapatiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakandarasi waliopo kazini sasa wanaendelea kukamilisha miradi ya awamu hii ambayo bado katika vile viji ambavyo havijajengwa tunahakikisha vinajengwa na deadline ni Juni tarehe 30. Kama watakuwa bado hawajamaliza kulingana na mikataba ya utekelezaji wa kazi, tutaongeza muda kidogo kama wa siku 60, ili waweze kumalizia, lakini awamu ya tatu anzeni Waheshimiwa Wabunge sasa kwenda kwenye Wilaya, ili kuweza kupeleka maombi yale, ili muwaeleweshe wananchi wasije wakatuhukumu. Kwa wale waliopata wanafurahia, amba hawajapata wanakuwa wanajisikia vibaya, lakini haya yote ni maendeleo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimependa niliseme tu hilo na kwamba, kwa kweli tumefanya kazi kubwa, karibu kilometra 15,000 za usambazaji wa umeme tunesambaza katika nchi nzima. Kilometra 15,000 ni sawasawa na kwenda South Africa na kurudi mara nane, lakini imejengwa kwa muda wa mwaka mmoja! Ni jambo kubwa, tupongezeni tu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamesemwa mambo mengi na hili nimelisema kwa sababu, limekuswa na karibu wasemaji wote waliozungumza na kasi yake itakwenda hivyo. Mheshimiwa Deo Sanga amezungumzia mradi wa Makambako Songea; nimhakikishie kwamba, hatua zote sasa zimekamilika, mchakato uliopo sasa ni Mkandarasi. Mazungumzo yote no objection tayari na naomba, mradi ule wa Makambako - Songea una package mbili; una package ya transmission na package nyingine ni ile ya usambazaji. Kazi za usambazaji zitaanza mapema zaidi ndani ya mwezi huu wa Sita na kazi za usafirishaji wa umeme hizo ndiyo zitachukua muda kwa sababu, ukandarasi wake ndiyo uko kwenye mchakato katika kupatikana. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbassa amezungumzia masuala ya ORIO; ORIO Mheshimiwa Mbassa tumeikamilisha na sasa ni utekelezaji, fedha ile itatolewa na Serikali. Nimekubaliana na Waziri wa Fedha amesema hela hiyo itatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Susan Kiwanga amezungumzia masuala ya Kilombero, kuna mradi kule wa Low Cost. Nimhakikishie Mheshimiwa Kiwanga, changamoto zilizokuwepo katika miradi hii ya msaada mara nyingi huwa ina matatizo, lakini hata hivyo tumekubaliana na mambo yamekwisha na utekelezaji wa mradi huu utaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zabein Mhita amezungumzia miradi ya Jimboni kwake. Nichukue nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Zabein kwamba, katika maeneo yale yote ambayo ameyasema, kama ambavyo Mkandarasi anaendelea, tutaendelea na tutakamilisha kabla ya mwezi wa Saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mansour amepongeza sana EWURA, lakini pia, akataka kubadilisha Kanuni na vitu vingine. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mansour kwamba, template hizi tutazismamia na jana nimeonana na Mwakilishi wa wamiliki wa Makampuni ya Mafuta, tumeongea naye, tutajitahidi kuondoa hii kasoro, ili industry hii isije ikatetereka katika kipindi hiki ambacho tunaelekea kwenye uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Kafumu amezungumzia suala la yale maamuzi yaliyofanywa ya kuongeza tozo katika vitalu vya migodi ya madini. Sababu kubwa ya kuongeza tozo hii, ilikuwa ni kwamba, speculators walikuwa wameshika maeneo mengi sana. Hata hii jitihada yetu ya kupata maeneo kwa ajili ya kuwasaidia wachimbaji wadogo imefanikiwa tu pale ambapo hawa waliokuwa wamehodhi haya maeneo wameanza kuyaachia kwa sababu, sasa wanashindwa kuyaendeleza, lakini wameyahodhi. Iwapo kama walioyashika maeneo hayo wanayaendeleza, sisi Serikali hatuwanyang'anyi na wala hatufanyi hivyo na wala tozo ile si tatizo kwao kwa sababu, wakiwa wanayaendeleza hawapati matatizo kama aliyoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutaendelea kushirikiana na kushauriana zaidi na Dkt. Kafumu ni mtaalam katika eneo hili, tuone pengine alichokisema kilikuwa kinamaanisha nini, lakini la msingi hapa ni suala la VAT ambalo ameshauri kwamba, katika vifaa vya ufanyaji utafiti wa madini nini vizuri tukaondoa kodi ya VAT. Hili tutalichukua na tutaendelea kulitafakari kuona namna gani tunaweza kulatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gesi na Mafuta na Kampuni ya Taifa ya Mafuta niseme tu kwamba, ni vizuri sana na hili amelisema pia Mheshimiwa Kitandula na Mheshimiwa Lulida na Mheshimiwa Lembeli ingawa alisema katika madini zaidi na Mheshimiwa Mangungu na Mheshimiwa Bukwimba amelisema. Lazima kama Taifa wakati huu wakati ambapo tunapata rasilimali hizi Mwenyezi Mungu anatujalia tuendelee kushikamana sana na kupeana mawazo na maoni ambayo si kwa sababu tu ya siasa za leo, iwe ni kwa sababu ya mustakabali wa maisha ya watu wetu na nchi yetu baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu leo hii imegundua gesi katika kiwango kikubwa sana, TCF trillion cubic fit za ujazo trillioni 55.08, ni kiasi kikubwa kweli na tunaendelea kugundua. Rasilimali hii haiwezi ikajengwa katika msingi wa mabishanobishano ya aina ya kiwango tunachozungumza wakati rasilimali hii Mataifa ya nje yanaitamani sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kitandula amesema jambo hapa kwamba, hizi sheria zinazokuja ambazo tunataka tuzilete ni muhimu sana katika kipindi hiki. Tunaleta sheria ya uwazi na uwajibikaji katika masuala ya uchimbaji wa rasilimali hizi na tunaleta sheria inayoweza kubana watakaokuwa wanaingia mikataba kama ilivyokuwa siku za nyuma kuzingatia sheria zaidi kuliko mawazo yao na utaalam wao tu. Tunataka tuwabane katika sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika sheria hizi zote tatu zitakazokuja, zikija Waheshimiwa Wabunge, inazungumzia uwazi, inayozungumzia ushiriki wa Tanzania na Watanzania, ni vizuri tukaiweka katika sheria na siyo kama ilivyokuwa katika matamko mbalimbali na kutoa mwanya mkubwa kwa wanaokaa kwenye meza ku-negotiate na hao wanaowekeza amba ni makampuni makubwa. Mnakaa kwenye meza una-negotiate, uchumi au vitibu vya kampuni moja tu ya ExxonMobil ni sawasawa na uchumi wetu wa Tanzania mara tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakaa na mtu kama huyo una-negotiate, umempeleka afisa wako amemaliza degree yake sijui Chuo Kikuu au sijui wapiwapi hapo, haiwezekani! Tukaeni hapa tutunge sheria, tutakapoleta hizi sheria na tukazitunga, zitabana zitaweka wigo mdogo sana wa mapato na hivyo maslahi ya Taifa yanaweza yakapatikana. Niwaombe tushirikiane katika jambo hili, Mheshimiwa Kitandula nakushukuru sana kwa kutukumbusha. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bungara rafiki yangu amesema mengi, lakini nimhakikishie kabisa kabisa tunatekeleza miradi katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Tumetenga hela ya nyongeza shilingi bilioni 48 itakayopatikana katika mwaka huu wa fedha na siyo unaokuja, katika huu mwaka amba kabla ya kuisha wakandarasi wawe wameanza kusambaza umeme katika mikoa hii. Maeneo yote ambako wire umepita juu, tushushe umeme chini lakini vijiji vyote vinavyokwenda na mkuza wa bomba vyote tutavipelekea umeme kabla ya mwaka, yaani siyo kwa bajeti hii tunayoiaandaa sasa, kwa bajeti hii iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kuchukua chukua katika maeneo mbalimbali na kujibana bana, tunataka tutekeleze miradi hii ili wenzetu ambako rasilimali hizi zinatoka na wenyewe wajisikie sehemu ya mafanikio yanayopatikana. Hili ni jambo tulishalimaliza limekaa vizuri na Waheshimiwa Wabunge wa maeneo hayo wanalfahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimetolewa pia hoja mbalimbali zinazohusiana na miradi ya madini na hasa masuala ya fidia kwa migodi. Niwaombe sana viongozi, kama kweli tunawapenda wananchi wetu na hasa Mgodi wa Nyamongo ambaa kinachotokea kule ni tegesha, inaitwa tegesha, wakisikia katika eneo linalozunguka mgodi, kampuni inataka kwenda kupeleka shughuli zake katika upande fulani, wanawahi kule wanazunguka wanajenga vijumbajumba wanasema tunahitaji fidia. Wakiendewa wakifanyiwa assessment pale, wale wakaacha pale wakienda sehemu nyingine na wenyewe wanakwenda kule. Kwa hiyo, fedha zilitengwa, fedha za kampuni zimetengwa kwa ajili ya fidia, lakini wachache tu waliochukua na wengine wote wameendelea kuongezeka kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani, si kwamba kweli tunawasaidia wananchi, si kwamba kweli tunawapenda wananchi kwa sababu kama zile fedha zingekuwa zimelipwa na wananchi wamepata fidia, leo hii maisha ya watu wanaozunguka mgodi ule yangekuwa yamebadilika

sana, lakini sisi viongozi tumewajaza wananchi hasira, tumewajaza expectation na sasa hata rasilimali ile ambayo walitarajia kuipata wanashindwa kuipata mapema ili waweze kuitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo limesemwa sana na Waheshimiwa Wabunge wengi ni kuhusiana na Mgodi wa Ngaka. Hapa amesema Mheshimiwa Kayombo, amezungumza masuala mengi lakini niseme tu, *Tancoal* haijakatazwa na Wizara wala Serikali kwa ujumla. *Tancoal* ni Kampuni ya Serikali, *Tancoal* ilikuwa na tatizo na mbia mwenzie. Kwa hivyo, hatukuwahi na mpaka sasa hivi tumesaidia *Tancoal*, sasa angalau mradi huu unaanza kupata mwanga, tunachotafuta tu ni kwamba fedha itapatikana wapi ya kutekeleza mradi kwa sababu yule mbia wao wa mwanzo amejitoa. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, katika maeneo na wananchi wa maeneo yanayozunguka eneo hilo, sisi tutajitahidi kama Serikali kutafuta namna mbadala za kuendeleza miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuzalishe umeme wetu kutokana na vyanzo mbalimbali. Vyanzo tulivyojaliwa na Mwenyezi Mungu Tanzania vya kuzalisha umeme ni vingi sana. Kama Serikali tumejipanga na nichukue nafasi hii kuwaeleza Kamati ya Nishati na Madini katika eneo walilosema hofu ya shida ya umeme katika kipindi kifupi kijacho katika mwaka huu ambapo hatuna maji ya kutosha. Serikali imejipanga na kwamba mradi wa Kinyerezi One utaanza wakati wowote, kuanza majaribio mwezi wa Saba na unaweza ukaingia kwenye *full operation* kabla ya mwezi wa Tisa. Naamini megawatt 150 tukiingiza kwenye *grid* ya Taifa zitatusaidia sana katika kupunguza deficit ya umeme ambayo ingeweza kuwepo kutokana na vyanzo vingine vya maji kutokuwa vinatoa umeme wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumejipanga kwamba, hata katika ile mitambo ya TANESCO ambayo iko pale Jacobson One, Jacobson Two ambayo inamiliikiwa na TANESCO ambayo ina megawatts karibu mia mbili na ushee, lakini pia tunaongezea mtambo mwingine ambao una megawatts karibu mia kumi na tano. Kwa hiyo, tutakuwa na megawatts karibu mia tatu ambazo zilikuwa hazina gesi, gesi hii itakapoingia sasa tutapeleka pale. Ukiijumuisha na hii mia moja hamisini tuna karibu megawatts mia nne na ushee ambazo zitakuwa zimeongezeka kwenye *grid* kutokana na gesi peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hofu hii ya tatizo la umeme naomba kabisa tusiwe nayo, tuombe Mungu tu kusitokee balaa lolote, mradi wetu wa bomba la gesi uweze kupampu gesi ije Kinyerezi na tuwashe ule mtambo na hatimaye tuunganishe na maeneo mengine yakiwemo ya Tegeta ambako kuna mitambo mingine. Hili limesemwa na Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali itoke kwenye mitambo ya kuzalisha umeme kwa bei kubwa na kuja kwenye mitambo hii ambayo ni ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli TANESCO kwa sasa wanamiliki uwezo wa karibu nusu ya uzalishaji wa umeme mitambo ni ya TANESCO kwa hivyo hatuna mashaka kabisa, hapo hakuna capacity charge wala energy charge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, kama ambavyo nimejibu hoja hizi ambazo kwa kweli siyo rahisi kuzijibu zote na tutaendelea kuzijibu humu ndani, lakini tutaendelea kutoa majibu kwa Waheshimiwa Wabunge hata baada ya leo kwa majibu ambayo ni mazuri ili wawakilishi wa wananchi waweze kurudi kuwa na majibu ya Serikali kwa namna ambayo tutandaa schedule maalum na kuwapa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo basi, niombi radhi tu kwa wale ambao sikuweza kuwajibu, kwa sababu ya muda niwashukuru sana wote kwa michango yenu, niwashukuru sana kuunga mkono Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (Makof)

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MWENYEKITI: Ahsante hoja imeungwa mkono. Katibu!

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

FUNGU 58 - WIZARA YA NISHATI NA MADINI

Kif. 1001 - Administration and Human
Resources Management... ... Sh. 10,017,257,000/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, wala msiwe na papara majina yako hapa. Maana naona Kafulila alikuwa anataka kusimama, majina ninayo jamani kwa hiyo suburini. Kila jina linaloletwa litapata nafasi yake, taratibu zilizokuwepo ndiyo kazi ya Bunge, haogopwi mtu wala haiogopwi hoja hapa, majibu yote yapo.

Waheshimiwa tunaanza na Mheshimiwa Missanga!

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu toka enzi za Muhongo, amekuja Mheshimiwa Waziri huyu Simbachawene nimekuwa nikifuatilia ubaguzi uliofanywa katika Jimbo langu kwa maana ya kwamba, mpango huu wa REA, namba mbili Majimbo yote katika Mkoa wa Singida wamepata umeme au wanaendelea kupata umeme kupitia REA namba mbili, kasoro Jimbo moja tu la Singida Magharibi ambalo mimi ndiyo mwakilishi wake.

Sasa najiuliza ubaguzi huu wa nini? Kama Mkandarasi yupo ameteuliwa kwa ajili ya Mkoa wa Singida na Jimbo la Singida Magharibi liko katika Mkoa wa Singida. Majimbo yote, mengine yote yamepata umeme, lakini Jimbo langu limebaguliwa. Sasa najiuliza hii philosophy ya ubaguzi imetoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejiuliza mara nyingi sana, jibu sipati ingawa mwisho nikaja kupata jibu, lakini sina hakika kama ni jibu sahihi. Kwa hiyo, nataka kujua, huu ubaguzi uliofanywa wa kutokupeleka umeme katika vijiji ambavyo vimeainishwa, vijiji ambavyo Mheshimiwa. Katibu Mkuu wa CCM Mheshimiwa Kinana alikuja na orodha yake anatamba kwamba kijiji hiki na hiki ifikapo tarehe 30 mwezi wa Sita mtakuwa mmeputa umeme. Watu wakamshangilia sana, lakini mpaka sasa hata kijiji kimoja. Huku si kumdhailisha Katibu Mkuu wa watu? (Makof)

Sasa kama mtu anafikiri hujuma kwa Missanga, hapana, ni hujuma kwa CCM. Mimi kuwa Mbunge jambo lingine, lakini CCM ndiyo inastahili hasa kupata Wabunge. Ningependa kujua ni kwa nini ubaguzi umefanywa, Majimbo yote yamepata umeme kasoro Jimbo langu mimi la Singida Magharibi? Vinginevyo kama sikupata...

MWENYEKITI: Mheshimiwa umechelewa kaa chini, Mheshimiwa Waziri...

MHE. MOHAMED HAMISI MISSANGA: Nitatoka na shilingi yangu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Missanga umeshachelewa. Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa concern ya Mheshimiwa Missanga. Katika miradi ya kujenga umeme Tanzania kuna miradi ambayo imejengwa moja kwa moja na TANESCO, kuna miradi imejengwa chini ya Mfuko huu wa REA, kuna miradi ambayo imejengwa kwa kutegemea wahisani akiwemo MCC na kuna miradi ambayo inajengwa kwa kutumia hizi *investments* kwenye Mkuba wa Backbone. Sehemu anayoizungumzia Mheshimiwa Missanga ikiwemo na sehemu ya baadhi ya Mkoa ya Songea, Ruvuma na Njombe zimekuwa zikitegemea kutumia MCC au hii miradi ya backbone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme wazi ruzuku au pesa kuitia MCC imekwenda taratibu na Mheshimiwa Waziri alizungumza kwamba, mtoto tunayeweza kumtegemea anayekwenda kasi ni mtoto wetu wa kuzaa na mtoto wetu wa kuzaa ni REA. Mheshimiwa Missanga nimeshaelekezwa na Mheshimiwa Waziri kurekebisha maeneo hayo yote na ndiyo kazi yangu niliyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi nimeelekezwa nisikae ofisini na hapa nimekuja tu na eneo ninalolishughulikia ni sehemu yako ikiwemo Bahi, sehemu za Songea nimeelekezwa kwenda huko. Mheshimiwa Missanga nimsihi, anisikilize mimi, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amenieleza juzi wamemalizana na MCC, MCC anaanza kazi, watu wa Backbone utaona mkongo mkubwa unajengwa, kuna towers kubwa zinajengwa za *volts 400 pale wanapopita* tumewaelekeza kwamba washushe umeme ndiyo kile kitu nilichokiita *underline*, watakuwa wanapita pale wanashusha umeme na Jimbo lako ni sehemu ya eneo itakayofaidika. Naomba rudisha shilingi ya mkuu wangu wa kazi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Missanga!

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka niweke record sawasawa. Si kweli kwamba vijiji vya Jimbo langu viko chini ya MCC, siyo kweli! Kama nilivyosema vijiji ambavyo viko kwenye Jimbo langu viko kwenye REA kama vilivyo vijiji vingine vya Majimbo yote ya Mkoa wa Singida na Mkandarasi ni Spencon. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri inawezekana amepewa taarifa potofu, lakini ndiyo ninachojua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimezungumza na Dkt. Mwakahesya akaniambia kuna utaratibu wanafanya, lakini nataka hayo aliyonieleza Dkt. Mwakahesya utaratibu wanaofanya nipate *commitment* ya Mheshimiwa Waziri, kama sikupata *commitment* ya Mheshimiwa Waziri, bado naendelea kushikilia shilingi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri *commitment*!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa akinagiza, mimi ndiyo namwagiza Commissioner wa Umeme na Commissioner wa umeme ndiyo anamwagiza Mwakahesya na ndiyo maana tumesema, mwende TANESCO, TANESCO iwalete Wizarani, naagizwa na Mheshimiwa Waziri, namwagiza Commissioner anamweleza, nimepewa maelekezo kwamba nishughulikie. Eneo la Mheshimiwa

Mbunge linashughulikiwa, Bahi inashughulikiwa, liko chini yangu, hao wengine ni wafanyakazi, Mheshimiwa Missanga tutakushughulikia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri mpe agizo. Mpe agizo mbele ya Bunge!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nimeshamwagiza Mheshimiwa Naibu Waziri.

MWENYEKITI: Nakushukuru. Mheshimiwa Missanga agizo lilishatoka na Bunge limeshuhudia. Mheshimiwa Missanga!

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nasubiri kuona utekelezaji. (Makofij)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Barwany!

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nishukuru kwa kazi kubwa ambayo imefanywa na Wizara hii, lakini nataka kufahamu tu kupitia Waziri kwamba, hii miradi ya REA katika maeneo mengi ambayo inapita kuna athari kubwa ambayo inapatikana kutokana na uharibifu wa baadhi ya mazao ambayo nguzo za umeme zinapita katika maeneo yale. Hatuamini kabisa kwamba kama kutakuwa na mradi wowote wa Serikali ambao hautalipwa fidia kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini pia kwamba, miradi yote ya maendeleo ambayo ipo imetengenezwa na wananchi na mingine imeletwa na Serikali, lakini tunaamini pia kuwa kwamba miradi ambayo inaletwa na Serikali isiatirii miradi mingine ambayo wananchi wanajipatia maisha yao ya kila siku. Kwa maana hiyo, katika maeneo mengi hususan katika Jimbo langu la Lindi Mjini, minazi zaidi ya 3,000 imekatwa katika njia ambayo umeme unapita, lakini bado REA haijatamka na haijatuthibitisha kwamba ni namna gani wananchi wale watalipwa fidia mpaka leo, inafikia mahali mpaka wananchi wanakwenda Mahakamani bado Wizara ya Nishati haijatoa majibu rasmi kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa shilingi kama bado Serikali haijathibitisha namna gani inaweza kuwalipa wananchi wale fidia kwa maeneo ambayo minazi yao imekatwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri fidia!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wale ambao miradi hii inatekelezwa katika maeneo yao, lakini zaidi sana niwashukuru wananchi wa maeneo ambako mradi hii inatekelezwa. Tunapata *feeling* tofauti, baadhi ya maeneo wananchi wanajitolea hata kuchimba mashimo, baadhi ya maeneo wananchi wanabeba mpaka nguzo na kuwasaidia Wakandarasi hata kuwachinjia mbuzi, kuku na maeneo mengine ng'ombe. Pia maeneo mengine wananchi wanadai kwamba maeneo yao yameathiriwa kwa maana ya mazao yao kama anavyosema Mheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa Lindi na Mtwara hivi karibuni na miongoni mwa mambo ambayo niliyashughulikia kweli ni pamoja na hili lilipungua kidogo. Sasa niombe tu, kwa sababu masuala haya ni kama vile tunasaidiana. Wananchi hawa hawa wanahitaji umeme sana, wananchi hawa hawa pia katika kufanya maendeleo yao mengine hatutakiwi kuathiri maisha yao, ni kweli, lakini miradi ya umeme hii inafanywa na Serikali kwa fedha ya Serikali na kwa maana hiyo basi haikuwa na element ya fidia. Sasa nitajaribu kuonana na Mheshimiwa Barwany, ni rafiki yangu, tuweze kuona madhara hayo ni makubwa kiasi gani na yameathiri kiasi

gani na pengine kuwashirikisha wananchi wenyewe kama ni bora umeme wapate au tuache kabisa kuelekea huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona tutashirikiana yeye na niko tayari kuongea naye hata baada ya hapa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Barwany!

MHE. SALUM K. BARWANY:- Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, kuna maeneo mengine yameathirika kwa kiasi kikubwa. Kwa kule kwetu Lindi, zao la mnazi ni zao muhimu ambalo tayari linasomesha watoto, linatoa huduma muhimu za maendeleo kwa wananchi wake. Kwa taarifa rasmi ni kwamba zao la mnazi linatoa mazao mara nne kwa mwaka, hakuna zao lolote lingine katika nchi hii ambalo linatoa kipato kikubwa kwa wananchi. Leo minazi ile kwa kiasi kikubwa imepotea, lakini pia zao la mnazi linetoka malighafi kwa ajili ya viwanda ambao ungesaidia umeme huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo unapopeleka umeme, malighafi ambazo tunazitarajia kwa ajili ya kuboresha viwanda, vinyavyotokana na umeme huo, mazao yale yanaondolewa, bado hatuwezi kumsaidia mwananchi wa kawaida. Nakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba tutakutana ili tuone ni namna gani wananchi wale wanapatiwa fidia kwa maeneo ambayo minazi yao imekatwa. Ahsante.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana kwa kukubali kushawishi wananchi. Mheshimiwa Cheyo!

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru. Pia natumia nafasi hii kuiomba Wizara au Mheshimiwa Waziri amsukume zaidi yule Mkandarasi anayepeleka umeme kutoka Mwamapalala na vijiji vyote vilivyo njiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nililosimamia hapa ni jambo la Kitaifa. Ningependa kupata kama kisera, kwanza Bunge hili lilezwe, ni fedha kiasi gani imetumika katika kuleta bomba kutoka Mtwara, mpaka Dar es Salaam na pia tufahamishwe, kama limekamilika asilimia 95, hiyo gesi iko wapi? Imeshatayarishwa au mwelekeo ule ule, tutasubiri tena mpaka gesi itoke kwenye bahari kuu na ukiangalia issue ya bahari kuu, tunajua katika mikataba iliyopo, kuna kitu kinaitwa cost gas yaani gharama na gharama hizi tunaelewa ni karibu dola milioni 1.5 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ni kutengeneza mradi na kupata hiyo gesi, itachukua takribani miaka 10, je kutakuwa kweli kumebakia na chochote katika gesi ambayo tunategemea ndiyo iinue uchumi wa Taifa hili, ndiyo tuwe na Mfuko wa kujenga shule yetu, ndiyo tuwe na Mfuko hata wa kusambaza umeme zaidi kwa matumizi zaidi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nipate jibu katika sehemu hiyo, ili wote tuelewe, kwa sababu gesi ni mali ya Watanzania na kwa hiyo, kama kuna gesi inatoka na inauzwa na hili nitakuja kulizungumza kwenye Wizara ya Fedha, tunataka kuona senti hiyo hata kama ni moja, inaonekana kwenye budget frame, kwamba katika mwaka huu gesi hii itatoka kiasi fulani, lakini siyo tunatengeneza tu kampuni 'A', kampuni 'B' na vitu kama hivyo. Naomba majibu na sitaki kutoa shilingi ni rafiki yangu, atueleze tu na najua ana uwezo wa kutoa maelezo hayo. Ahsante sana.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na hisia kidogo ya tofauti juu ya bomba na gharama yake. Mabomba haya yako duniani, sehemu nydingi ambako

gesi imegunduliwa na Tanzania si ya kwanza na ili kufanya ulinganifu, gharama yake inapatikana kwa kuangalia kipenyo cha lile bomba, halafu unagawanya na urefu wake, kwa maana ya kilomita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti yake na sisi Tanzania, ni kwamba bomba letu sisi tulilitaja kwa umoja wake, kwamba mradi ule mzima unagharimu kiasi cha dola bilioni 1.26. Sasa mle ndani yake mle, kuna processing plant, lakini kuna nyumba zilizojengwa kama kambi kwa ajili ya wasimamiaji wa mradi ule. Pia tuna Kinyerezi, ile receiving station, lakini pia tumeweka na vipuri vya kulinda mradi huo utakapoanza kwa miaka karibu mitatu, lakini pia tumeweka huko ndani na training kwa ajili ya kujenga uwezo wa Watanzania watakaoshughulikia bomba hilo, wakati tunaanza na hata baadaye kuendelea kwa sababu ya sustainability. Gharama zote hizo, tutaziweka pamoja na ndiyo maana akija mtu akigawanya, anaona kama hapana, lakini ukiantaliza, tofauti ya bomba moja na lingine ni vile vitu viliviyowekwa katika ule mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabomba haya yako sehemu nyingi, lakini sisi Serikali, Wizara ya Nishati na Madini, tuko tayari kutoa elimu maalum kwa muda maalum utakaopangwa na Spika, ili tuweze kutoa presentation na kulinganisha mabomba mengine duniani, yalivyofanywa na viliviyofanyika ili hii doubt iweze kutoka tuendelee kusonga mbele katika kuifanya gesi yetu iweze kusaidia uchumi wa Tanzania. (Makof)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Philipo Mulugo!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna issue ya gesi inatoka wapi....

MWENYEKITI: Hii naruhusu kwa heshima ya mzee Cheyo, unatakiwa ujibu specific issue moja, jibu moja, lakini nakuruhusu ujibu, sababu hili lina importance yake.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo gesi pale Msimbati, Mnazibay ya kiasi ambacho tumeshaongea, tumekwishapatana, tuna masharti fulani fulani tunayatekeleza na wabia wenzetu amba ni kati ya Serikali, maana kile kitalu cha pale Mnazibay, basically ni mali ya Serikali, wale Maurel et Prom waliingga kuendeleza. Kwa hiyo, tuna kauli kubwa, tofauti na maeneo ya deep sea na wapi.

Kwa hivyo, mazungumzo yamekwenda vizuri na gesi ipo ya kutosha kuanza nayo katika kuzalisha umeme wa megawatt 150 na baadaye gesi hiyo kwanza kabisa, hata megawatt 150 zimekamilika, imedhihirika kwamba ni nyingi, hatuwezi kui-pump, mpaka tukamilishe na viungio na ndiyo maana tumeomba kwenye bajeti hii bilioni 45 kwa ajili ya kutengeneza viungio vya kuleta Ubungo pale kwenye mitambo yetu miwili ile, lakini pia kupeleka Tegeta kwenye mtambo wetu wa kule ili uki-pump gesi itumike yote, huwezi uka-pump gesi ile ni nyingi, halafu ikoja kutumia trail moja kuzalishia umeme wa megawatts 150. Kwa hiyo, niwahakikishie, niwahakikishie Mheshimiwa Cheyo na Watanzania kwa ujumla, tusiwe na hofu tunakwenda vizuri na gesi itakuwa na ipo, kutoka kule Msimbati na kutoka Songosongo.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mulugo!

MHE. PHILIP A. MULUGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Suala langu ni moja tu lakini ni zito. Mheshimiwa Waziri, alipokuwa Naibu Waziri Wizara hiyo, mwaka 2012, alitembelea Jimbo langu, tulikuwa pamoja na wananchi wa Songwe wakamvisha na nguo maalum kama Chief wa Songwe.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa sasa, rafiki yangu Mwijage, mwezi uliopita alikuwa Jimbo la Songwe, amefika Kijiji cha Kanga na amefanya mukutano wa hadhara na yaliyosemwa nayanukuu hapa. Mheshimiwa Waziri alipokuwa Jimboni na Naibu Waziri na wote ni rafiki zangu, kwamba; nililalamika mara ya kwanza, kwamba Wilaya ya Chunya, katika distribution yake, awamu ya kwanza umeme wa REA haukwenda kwenye Jimbo langu, sikuwa Mbunge wakati huo, awamu wa pili nikaomba vijiji 12; Vijiji vya Magamba, Totowe, Illembu, Garula, Ilasiro, Kanga, Tete, Ifenkenya, Mbala, Isechi, Ifuko, Mbuyuni na Chang'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka hivi ninavyosema, Mkandarasi yuko site, SINOTECH, Mheshimiwa Mwijage mlikuwa naye pale, mchini. Umeme ambao umekwenda kule umepita barabarani kutoka Mbalizi unakwenda Mkwajuni na vijiji vilivyoafaidika ni Vijiji vitatu tu, Kanga, Mbala na Isechi, full stop. Katika vijiji vingine vyote 12. Kwa hiyo, vijiji tisa wananchi walishajiandaa na yule Mkandarasi alishawaambia wachimbe mashimo na ramani ipo, kila kitu kinaendelea na mashimo yalishachimbwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mpaka sasa ukimwambia yule Mkandarasi anakwambia bado REA hawajani pa fedha ili niweze kuendeleza vijiji vingine. Nguzo Galula ziko pale, lakini hakuna kinachoendelea. Naomba mnihakikishie, ni lini hivi vijiji vingine tisa na kwa sababu tayari nilishakuwa yatima toka huko kwamba, maana yake Jimbo la Songwe awamu ya pili ndio vimeenda na awamu ya tatu nadhani nitawaomba tena, ni lini sasa vijiji vile Mheshimiwa Mwijage ulivyoviahidi, umeme utapelekwa na Mkandarasi ataanza kazi? Kwa sababu yuko tayari lakini hana fedha. Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (CHARLES J. P. MWIJAGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu swali la Mheshimiwa Mulugo kama ifuatavyo:-

Kweli nilifika Kanga, tulifanya shughuli nydingi na nilikagua ukubwa wa Jimbo lako, ni mionganoni mwa Majimbo makubwa katika nchi hii. Kutoka kijiji mpaka kijiji kingine ni kilomita 20 na hiyo ni sehemu mojawapo ya maeneo yanayotupa changamoto. Baada ya kuona changamoto hiyo, nilimwambia Mbalamwezi, Engineer wa TANESCO, Mbeya niliyekuwa naye, kwamba aandike andiko maalum, alipeleke makao makuu, makao makuu wawaeleze REA kuhusu hiyo abnormality nilioionna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijiji kimoja mpaka kingine, kilomita 30, bwana Mulugo, awe na imani na mimi, awe na imani na Waziri wangu, bado nipo kazini, nakwenda kulishughulikia. Mkandarasi hawezi kufanya lolote, mpaka apate approval kutoka REA, lakini faida aliyonayo, vifaa vyote vya SINOTECH viko site, anachosubiri ni ruhusa, lakini ruhusa haiwezi kutoka mpaka procedures zote mzijue. Kuna taratibu ambazo tumejiwekea, lazima zifuatwe, uhakiki ufanyike na nakuhakikishia, awe na imani na mimi hatujakutana hapa, tumetoka mbali, amenifaa na mimi siwezi kumtupa.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katika mchango wangu wa maandishi, niliomba Serikali kwa maana ya Mheshimiwa Waziri, awajulishe tu wananchi wa Jimbo la Arumeru Magharibi, kwamba, katika maeneo ambayo wao walijitolea kwamba wasilipwe fidia, wakafyeka mazao yao ili umeme uweze kupita. Mkandarasi alipopima maeneo ambayo nguzo zitawekwa, wakasema sisi tutajitolea kuchimba, bila kulipwa, lakini hadi leo maeneo hayajajengwa na maeneo mengine ambayo umeme umepita, umekwenda, last mile ndio wamepata umeme, hawa ambao wamejitokea mashamba yao, wakafyeka mazao na miti ili umeme upite, hawajapatiwa, wameachwa nguzo zinapita juu ya mashamba yao. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeomba tu Mheshimiwa Waziri atujulishe, ni lini maeneo hayo, ikiwemo eneo la Kiserian, Midawe, Kimelok, Saitabau, Tarakwa, Natema, Siwandeti, Losikito, Mwandeti, Musa, Oldonyowas, Ilikein, Lovilukuny pamoja na Lemugur, watapatiwa lini umeme huo? (Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri umeme lini?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (CHARLES J. P. MWIJAGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, njibuu swali la Mheshimiwa Ole-Medeye. Hili ndilo alilolizungumza Mheshimiwa Waziri wangu, mkuu wangu wa kazi. Hayo ndiyo ya Arumeru Magharibi, ndiyo ya Arumeru yote, sikiliza alivyozungumza kuhusu Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu walifyeka mazao kweli, lakini kiutaratibu, inapotoka wigo wa kazi, wanaita scope, unakuwa umeidhinishwa na Bodi ya REA. Wananchi kwa mwamko wa Arumeru waliamua kusafisha njia na wakachimba mashimo wenye na kule *trail* ni mbaya, kuna milima, watu wakabeba nguzo, nimekwenda mwenyewe nimeona. Kuna Arumeru nyagine ile ya Mashariki nilipofika kule nilitangazwa kuwa Mangi wa umeme, nikavikwa na nguo kabisa ninayo, Mangi wa umeme, nilibeba nguzo mimi mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya wananchi kwenda nje ya scope tunayashughulikia na nimemwagiza Meneja wa Arusha, kwamba hawa watu waliokwenda nje ya scope, bila approval, tuwape kipaumbele inapokuja REA namba tatu. Tunajua Wabunge wote tulivyo na constrain ya fedha, fedha hamna, mtu anahamasika anakwenda zaidi, lazima tukubali tufuate utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuwa aggressive, nataka kuwardhisha Waheshimiwa Wabunge, lakini nikienda REA, nikienda TANESCO wanabanwa na sheria. Mheshimiwa Ole-Medeye, nimezungumza naye na nimemwambia, nimeshaamrishwa na bosi wangu, nikitoka hapa nitakwenda Arumeru Magharibi, nikitoka hapo, nakwenda Same, nikitoka hapo nakwenda kwa mdogo wangu Kitandula. Kwa hiyo, ndiyo kazi nimeshapangwi na wakati nakwenda nyumbani nikitoka hapa, napita kwa Mzee Cheyo, ndiyo kazi niliyopewa, mimi ni mtu wa barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuendelee.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Silinde!

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia fursa hii. Nina jambo moja la Kitaifa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mitano, Kambi ya Upinzani Bungeni, tumekuwa na hoja moja ya kuitaka Serikali, iyaelekeze au iyaagize makampuni yote makubwa ya madini, kujisajili ama kujiorodhesha katika soko la hisa la ndani. Lengo la Kambi ya Upinzani, ni kwamba tunataka tujue mwenendo wa makampuni, tunataka mitaji ile, wananchi wa Tanzania washiriki kwenye umiliki wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa ni miaka mitano, makampuni hayajajisajili kwenye soko la ndani na ikumbukwe kabisa kwamba na najua Serikali inafahamu, Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, inataka makampuni yajiorodheshe. Isipokuwa kitu ambacho kimefanyika mpaka sasa hivi, kuna cross list ya amejasajili London, siyo katika soko la ndani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka Serikali itueleze ni kwa nini mpaka sasa hivi jambo hilo halijafanyika, kwa miaka mitano, wanakwenda kinyume cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010. (Makofii)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri kabla hujanini, anachokisema Mbunge ni kweli, Marekani mwaka 2010 wametunga sheria, Dodd-Frank Act, ambayo makampuni yote ya Kimataifa, ambayo yanafanya kazi nje ya nchi hizo, wanatakiwa ku-disclose activities zao huko Marekani. (Makofii)

Huu ni mwanya sasa, sababu kule hawawezi kupeleka ripoti ya uongo, wanaweza, inawezekana wakatoa taarifa tofauti na wanazotoa kule. Kwa hiyo, hiyo ndiyo njia sasa ya kusaidia Mbunge na Taifa. Disclosure wanazozifanya kule, ziwe disclosed hapa ili Serikali iweze kupata benefit na revenue watakayoipata. Mheshimiwa Waziri jibu mwenyewe!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Silinde, huo ndiyo Ubunge, unasema kitu chenye sense, kitu kinachosaidia Taifa. Ni kweli tulipitisha sheria, lakini katika sheria kupitisha, kulikuwa kuna mambo mengi hayajakaa vizuri na kufikiri unakumbuka habari ya corporate tax na vitu vingine, lakini mrahaba, tumetoka asilimia tatu mpaka nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya mambo tayari tulikwishaingia mikataba, hatukuwa tume-foresee hayo, lakini, mambo haya yote sasa, yanayohusu ushiriki wa Watanzania na ushiriki wa Tanzania, yanakuja na Miswada tunaouleta wa *Tanzania Extractive industries Transparency Initiative*, ambapo tunataka kuweka masuala ya uwazi na uwajibikaji na ushiriki wa Watanzania. Hii Miswada miwili ya local content na huu mwingine wa uwazi na uwajibikaji, ikija hii miwili hapa Waheshimiwa Wabunge, hapo ndiko sasa tusimike ili tuweze kuitekeleza Sheria ya mwaka 2010 ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili unalolisema ni kweli kabisa, nikubaliane na wewe, kwamba haiwezekani na sisi kama Serikali tunasema, tuko tayari kushirikiana na Bunge na Wabunge wanaolewa mambo kama Silinde, ili tuweze kuisaidia nchi yetu kupata ushiriki mzuri kwa ajili ya kuongeza uchumi wa nchi, lakini uchumi wa watu wetu. Kwa hiyo, hili tunalichukua kama wazo zuri sana. (Makofii)

MWENYEKITI: Amesema lini! Maana yake isichukue muda mwingi. Alichosema Mbunge na meza inakubali...

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Sheria...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, subiri, kaa tu pumzika kwanza. Hatusemi muifute mikataba, tunataka mui-refine, iendane basi na hayo maneno mazuri uliyoyasema kwa sasa na naamini, kwa wewe you can do it. When do you think will be the possible, siku ya karibu kabisa.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilishukuru Bunge lako kupitia kwako na kwa Mheshimiwa Spika, kwamba mmekubali kuongeza muda wa Bunge na sababu kubwa ni pamoja na Miswada hii ambayo inakuja. Kama kuna jambo zuri mtakalotusaidia Waheshimiwa Wabunge, ukiondoa hii mimi kusema kwamba kesho au kesho kutwa, that does not mean anything anyway. Kinachomanisha hapa, ni zana zipi mnatupa Serikali za kwenda kufanya hiki mnachotaka tukifanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu, baada ya sheria kupitishwa hapa, hizi ambazo tutazileta, ambazo zinazeleza haya mambo waliyosema kwa uwazi na zaidi ya kiasi hicho, naamini ni silaha nzuri sisi wenzeni kwenda kutusaidia katika kubadilisha mikataba ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya maeneo tumefanya jithada kubwa na tumebadilisha, hata hii corporate tax na yenyele ilikuwa kidogo shida, lakini sasa tunaanza kulipa. Pia silaha muhimu zaidi ni hii itakayotungwa na Bunge na kuweka utaratibu mzima wa mambo yote haya namna tutakavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la lini, ni baada ya kupitishwa kwa sheria hizi ndipo tutakapokuwa tunaweza kufanya kazi hii na inaweza ikafanyika ndani ya muda mfupi tu kwa sababu sheria itakuwepo.

TAARIFA

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Bukwimba, taarifa.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa taarifa kwa umuhimu tu kwamba, hili ni Bunge na ni chombo kikubwa sana chenye heshima katika nchi. Hili jambo ambalo Mheshimiwa Silinde analizungumza la *listing* asili yake ni ripoti ya Bomani ya 2008 na utaratibu wa kutunga sheria, sheria ikishatungwa kinachofuata ni kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza mara kadhaa kwamba ni lini kanuni za kutekeleza sheria hiyo zitaundwa? Powers za kuandika kanuni ni power za Waziri, haya majibu anayoyatoa ya kuleta sheria nyine juu ya sheria wakati sheria ya kwanza kanuni zake bado. Haya majibu ni ya ujanja ujanja, tunahitaji majibu *smart yanayopimika* ambayo yako focused kwamba ni lini mtatengeneza kanuni za kufanya sheria hii itekelezeke. Kwa sababu sasa hivi hakuna kanuni na umuhimu wa jambo hili ni huu amba Mheshimiwa Silinde amezungumza, kwamba ukienda Zambia wananchi zaidi ya 1,500,000 wanashiriki uchumi wa madini kwa sababu tu kampuni kule ziko *listed*, kwa hiyo hata Walimu, hata watu wa kawaida wanaweza wakashiriki kwenye uchumi wa madini. Sisi hapa kitu hicho kimeshindikana kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni mdau, si tu kwenye madini hata kwenye simu, miaka mitano hiyo issue ya *listing* bado...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kafulila inatosha, no, no, no, umetoa taarifa Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima yangu kwa Mheshimiwa Kafulila siwezi kusema siipokei kwa sababu anazungumza kitu ambacho *the context* ni nzuri, lakini tunazungumzia kutekeleza sheria. Mimi ni Mwanasheria, mwenzangu labda amesomea vitu vingine. Sheria peke yake haiwezi kukujengea msingi wa kutengeneza kanuni tu ambazo yenyele tu kwanza, ile provision ya sheria zenyele inaanza kuleta tatizo kwa sababu ya kitu kinaitwa *retrospectivity*. Sasa kwa sababu tulitunga sheria, lakini pia kuna mikataba iliyokwishaingwa nyuma huwezi ukatunga sheria ukairudisha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimkumbushe tu, tulipokuwa tunataka kutunga *Telecommunication Act* iliyokuwa inataku kulazimisha Makampuni ya Simu yaweze ku-register kwenye soko la hisa la ndani ya nchi tulikwamia kwenye Kamati, wakati ule mimi nilikuwa Mwenyekiti wa kikao na Mheshimiwa Attorney General aliyeondoka alikuwa anawakilisha kama Attorney General. Tulikwamishwa kwenye kikao kwamba, *the law will be retrospective and it's*

against the Constitution. Sasa ndiyo maana tulifika hapa tukasema hapana, this time hebu twende tumejiandaa zaidi, hebu tutunge na sheria nyingine ili tuwabane kote kote. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Kafulila, Mheshimiwa Silinde nawaombeni tusaidieni tutunge sheria kesho kutwa ya uwazi na uwajibikaji na local content, itamaliza habari zote hizi.

MWENYEKITI: Hapana, Mheshimiwa Kafulila kaa, Mheshimiwa Bukwimba!

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi...

MWENYEKITI: Waheshimiwa kutokana na *hot debate*, normally Jumamosi mwisho ni saa nane, naongeza nusu saa.

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu katika mchango wangu, kwanza nakusudia kutoa Shilingi kama sitapata majibu ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mitano nimezungumzia habari ya wananchi kupewa maeneo ya uchimbaji, hasa pale Rwanagara eneo la STAMICO. Suala hili pia liko ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010 - 2015, lakini kwa kipindi chote hiki sijaweza kupata majibu sahihi juu ya suala hili. Leo sasa nimesimama hapa kuomba commitment ya Serikali kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri aliyosema kwamba sasa wanlishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanlishughulikia kwa muda wote huo, kwa sababu alikuja Geita mwezi wa Nne akasema kwamba nipe mwezi mmoja tu, leo hii ni miezi miwili. Kwa hiyo, nataka kusikia commitment ya Serikali juu ya suala hili kwamba, waniambie ni lini sasa wananchi hawa wataweza kupewa maeneo haya ya uchimbaji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri commitment!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru sana Mheshimiwa Bukwimba kwa ku-tolerate pamoja na wananchi wa eneo la Nyarugusu, lakini tutambue tu kwamba kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwenye jibu la Mheshimiwa Silinde. Mkishakuwa na mkataba inachukua muda mrefu sana kumshawishi yule ambaye tayari ameshapewa leseni. Huyu mtu tayari ana leseni na sheria inavyosema, ukishampa leseni sasa ni ushawishi wako kumshawishi ambaye ameshapewa leseni aweze kukubali kuliachia eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninacheweza kusema tu na nafurahi kumweleza Mheshimiwa Bukwimba kwamba, tayari huyu mwekezaji tumezungumza naye na amekubali. Kilichobaki sasa ni ile procedure (taratibu) za kuweza, wao wakae katika Bodi yao, watengeneze Board resolution watuletee ili tuweze kuona namna ambavyo tunaweza kuwagawia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumwombe na tumsihi tena, nimsihi ndugu yangu ambaye kwa kweli amekuwa akilifuatilia jambo hili mara kwa mara na nilipotembelea katika eneo lake alionesha uchungu na niliona mimi mwenyewe. Mimi mwenyewe natoka eneo hilo, nafahamu watu wa sehemu hiyo jinsi ambavyo wana shauku ya kuweza kupatiwa. Nimwombe tu na nimsihi kwamba, kwa sababu tayari tumeshachuna huyu ng'ombe, sasa tunakaribia kuanza kuchukua ile nyama kuipeleka jikoni, atupe muda huu mchache tuweze kukamilisha hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshakamilisha na namhakikishia kabisa jambo hili sasa hivi linawezekana kwa sababu...

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bukwimba!

MHE. LOESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijaridhika. Ninachotaka kujua sasa kwamba ni lini, kwa sababu gani, taratibu kama hizi tulifanyiwa kule Nyakagwe haikuchukua muda, wakati huo Mheshimiwa Kafumu ndiye alikuwa Kamishna. Kwa hiyo, ningependa kupata commitment hapa ni lini, kwa sababu ni suala la siku nyngi sana na term karibu inakwisha sasa, mwezi huu wa Saba Bunge linakwisha, lakini kabla ya kwisha kwa Bunge ningependa kujua ni lini ili wananchi na wenyewe waweze kujua hasa kwamba ni lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hayo maneno ya Mheshimiwa Waziri nahitaji aje kule Nyarugusu awaeleze ye ye mwenyewe moja kwa moja ili wananchi waweze kusikia jambo hili.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, lini? Kuna uchaguzi huko mbele yake.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bukwimba ni Mbunge anayeongea taratibu lakini kwa kweli anaafutilia na nawapongeza sana wananchi wa Jimbo lake kwa kumchagua Mbunge makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubali, jambo hili ni la muda mrefu, tumemaliza mazungumzo kwa eneo la Buziba na anayemiliki eneo lile amekubali, mchakato unaendelea. Nyarugusu, lile eneo liko chini ya STAMICO na STAMICO iko chini yangu. Nataka nikuhakikishie kabla ya mwezi huu kwisha nakwenda pale kwenda kuwapa maeneo haya wananchi. (Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bukwimba, umeridhika?

MHE. LOESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naomba utekelezaji sasa.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama, kama ambavyo unafahamu, bajeti siku zote huwa tunazungumzia mapato na matumizi na moja ya mambo ambayo ni ya muhimu sana kwenye matumizi ni namna gani ambavyo utatumia sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunalalamika hapa kuhusu miradi ya umeme. Mimi mwenyewe Jimboni kwangu mradi wa REA mpaka sasa hakuna ambacho kimeendelea na Mheshimiwa Waziri amesema vizuri hapa kwamba amekutana na Wakandarasi wote wa REA. Nafahamu unafahamu kwamba kwenye Jimbo la Kafulila Wakandasi wa REA wame-stuck, hakuna kazi ambayo inaendelea. Zaidi ya hapo Mheshimiwa Waziri unafahamu kwamba, eneo la Tarafa ya Nguruka ambalo ye ye alikuja na Waziri Mkuu lina watu wengi kiasi ambacho ni aibu kukosa umeme. Mpaka sasa uamuzi wa TANESCO kupeleka station ya umeme mpaka sasa haujatekelezeka na haujatekelezeka kwa sababu ya pesa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati Serikali, Wizara inalia kwamba haina pesa kwa ajili ya kutekeleza miradi kama hii, wakati huo huo Wizara hii hii inakiuka maazimio ya Bunge ya kuendelea kumlipa Singa Singa, Singh Sethi bilioni tano kila mwezi, wakati Bunge limeshaazimia kwamba malipo yale ya-stop, malipo yale yaki-stop tunaweza tukaokoa miradi mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nipate majibu ya Serikali katika jambo hili, hivi ni kwa nini Wizara inaendelea kukiuka, kukaidi maazimio ya Bunge ya kutaka malipo ya capacity charge ambayo analipwa mmiliki wa *IPTL*, Singh Sethi mpaka leo yanaendelea kulipwa, bilioni tano, Dola milioni 2.6 ni bilioni tano kila mwezi, halafu wakati huo huo Serikali inasema haina pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimeona niseme hili kwa sababu linahusu heshima ya Bunge na ni bahati mbaya tu kwamba, kitu chenyewe siku hizi kama kinayumba. Tulikubaliana kwamba kabla ya mwisho wa Bunge hili, taarifa iletwe kuhusu utekelezaji wa maazimio kuhusu *ESCROW*. Spika nilishamwambia mara mbili haeleweki, nakwambia tena na wewe, kwamba tunahitaji kuokoa fedha katika jambo hili ili kusudi miradi hii iweze kutekelezeka, bila hivyo haiwezekani.

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana kwa kiti chako wewe, lakini pia kwa Serikali, kwa Wizara ya Nishati *in specific* kwa sababu kuna mambo mengine ni ya Wizara ya Fedha, lakini Wizara ya Nishati *in specific*, ni lini mtasitisha malipo ya capacity charge ya Dola milioni 2.6 ya kila mwezi, ili muoneshe kwamba mnaheshimu Bunge lenu, lakini pia mnaheshimu maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo na kama sipati majibu ya kuridhisha, nitatoa Shilingi kama kawaida.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mdogo wangu Kafulila, Mheshimiwa Mbunge tunazungumza naye sana, alikuwa rafiki yangu kidogo zamani, lakini jambo hili ni la kisheria sana kuliko siasa. Naomba mnisikilize kwa makini sana, ni la kisheria sana kuliko siasa. Ukiweka kisiasa unaweza ukalitumia kwa namna unavyotaka ukampiga ye yule, ukampiga huyu sawa, kapigwa Spika, kapigwa Mwenyekiti wa Bunge, vyovvye vile, tena linanoga maana linafurahisha kweli. Ukiwaambia Watanzania *ESCROW* wanaelewa, lakini, suala hili ni la kisheria. Mkataba uliopo ni Mkataba kati ya *TANESCO* na *IPTL*, haujafa, upo na hakuna Mahakama imewahi kuufuta mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Singh Sethi simjui, ninachojua ni mahusiano y *IPTL* na *TANESCO*. *IPTL* na *TANESCO* wana mkataba wa kuuziana umeme. Swali, umeme unazalishwa, ndiyo; swali, mkataba ule umekwisha muda wake bado. Sasa unajuliza tunafutaje mkataba, ni vigumu, unaufutaje? Kisheria, Sheria ya Makampuni, a company is a person, *IPTL* is a person, huyo mwingine anayetajwa naye is a person.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu person anayeitwa *IPTL* hawezi akaathiriwa hivi hivi tu, tutashtakiwa kama Taifa totalipa gharama kubwa kuliko hata hizi tunazolipa. Mifano mnaifahamu, tumepoteza gharama nyngi katika kulipa kutokana na maamuzi mabaya. Sasa naomba, Bunge lituambie tutekelezeje. Bunge liseme hivi, sasa ninyi katika hili, kwa sababu kuna mkataba, nendeni mkafanye hivi, ili yakitokea huko tusije kuulizwa hapa. Kwa sababu watakuwa wametuambia, kwa hiyo, hatutaulizwa, maana tunaona tukitaka kutekeleza hili lina magumu yake, lakini hebu twende nalo taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, Mheshimiwa Kafulila amekuwa akisikika akisema, mara nyngi, kwamba iliagizwa tusimamishe capacity charge; maazimio manane haya hapa, mimi nilikuwa mjumbe wa Kamati iliyoweka maazimio haya. Mimi na Tundu Lissu tulikuwa wajumbe ndiyo tulio-coach *this*. Hilo azimio analolisema Kafulila kila siku halimo humu, labda

Spika kama mnalo ninyi mtupe, lakini maazimio nane, hakuna linalosema tusimamishe malipo ya capacity charges kwa IPTL. (Makof)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kafulila!

Waheshimiwa Wabunge, niwape tahadhari, Mheshimiwa Kafulila kaa kwanza. Issue hii bado iko Mahakamani na Bunge limeingia kwenye mgogoro na Mahakama kwa mambo kama haya. Najua concern ya Kafulila ni very burning, lakini kuna masuala ya kisheria. Nikiwa kama referee, nafuata taratibu zilizowekwa katika kuendesha Bunge kwa mujibu wa Katiba. Naielewa vizuri sana hoja yako Mheshimiwa Kafulila ndiyo unayo siku zote na Waziri amejaribu kukujibu, nimeiacha at least upate comfort.

Vile vile kiti hakitaweza kukubali mjadala huu sasa uibuke wakati mambo haya tulishayafanya maamuzi na kwa mujibu wa kanuni zetu jambo lolote tulifofanya maamuzi 53(8) haliwezi kurudiwa tena. Nimekupa tu hiyo *comfort, benefit of doubt*, lakini majibu ya Serikali aliyojatoa Mheshimiwa Waziri ya Serikali ndiyo majibu sahihi. Mheshimiwa Kafulila, tukizungumza jambo lolote lingine tutai-pre-empty Mahakama. Katiba ya nchi yetu, chombo kinachotoa haki katika nchi yetu ni Mahakama na hiki kitu kiko Mahakamani.

Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Kafulila, nakurudishia ili ufunge hoja yako kwa sababu ndiyo mujibu wa kanuni zetu zinavyosema. Mheshimiwa Kafulila!

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo umuhimu wa kwamba tulikubaliana Bungeni, Serikali kabla ya mwisho wa uhai wa Bunge hili tuletewe taarifa ya utekelezaji. Kwenye taarifa ya utekelezaji ndipo hayo mambo ya Mahakama tungeelezwa, kwenye taarifa utekelezaji ndiyo mambo ya kisheria tungeelezwa, kwenye taarifa ya utekelezaji ndiyo mambo yote, madudu yote tungearambiwa hapa tukajadiliana, tukafunga mjadala. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa sababu kuna mambo mengi ambayo kwenye jambo hili yako pending na yanavunja credibility ya Bunge na hata Serikali yenyewe. Kwa mfano, leo watu wanasema kwamba mmiliki wa kampuni ile ambayo ina asilimia 50 za IPTL mpaka sasa, Simba Trust wamiliki wake wana mahusiano ya karibu na ikulu, jambo hilo haliwezi kufutika kama mjadala haujafa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kafulila...

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo haliwezi kufutika kama jambo hilo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kafulila hebu kaa chini, hebu kaa. Waheshimiwa Wabunge, jamanii ku-politicize vitu ambavyo hamna uthibitisho navyo, sasa, subiri basi Kafulila. Unajua unaweza ukaja na hoja vizuri, halafu baadaye unaondoka unaondoka kwenye mstari mwenyewe. Unapoanza ku-implicate watu wengine, Bunge linaweza kukwambia utele uthibitisho, wewe mwenyewe unasema hiyo Simba Trust haifahamiki, mara unasema ina mahusiano na watu fulani. Hatuna muda wa hear say ndani ya Bunge hili.

(Hapa Mheshimiwa David Z. Kafulila alibishana na Mwenyekiti kuonesha kutokubaliana na maelezo yanayotolewa)

MWENYEKITI: Subiri sasa, mimi nikisema wewe unatulia. Umesikia Mheshimiwa Waziri, kama una majibu jibu, halafu tumrudishie tuendelee na Bunge.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sina majibu ya zaidi ya hapo kwa sababu kwanza jambo lenyewe kwa sehemu liko Mahakamani, kwa sehemu limeamuliwa, ziko amri za Mahakama. Kuna mambo mengi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nasema...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kaa. Kutokana na kauli uliyosema mwanzo issue iko Mahakamani nafunga mjadala wa Mheshimiwa Kafulila.

Mheshimiwa Lembeli, halafu ajiandae Mheshimiwa Mrema!

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tofauti na miaka mingine nasimama si kutoa Shilingi kwa Mheshimiwa Waziri, bali kupata ufanuzi kwa jambo ambalo nimelizungumza katika mchango wangu wa kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya kupata umeme kwa kila Mtanzania ni ya msingi sana. Sasa wakati nachangia nilisema kuna tatizo la kukatika umeme mara kwa Kahama mara kwa mara na kwamba Serikali kwa zaidi ya miaka mitano imekuwa ikiahidi ndani ya Bunge hili kwamba itajenga mtambo wa kupoza umeme unaokuja Buzwagi ili uweze kuondoa hilo tatizo la umeme kukatika. Mheshimiwa Waziri katika majibu yake hajazungumzia jambo hilo na Mheshimiwa Mwijage anapita Kahama kila siku na yeye anazimikiwa umeme huo. Sasa nataka ufanuzi na aseme hapa lini atakuja Kahama wakati anakwenda kwake, aone hili tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la substation kwa ajili ya ku-stabilize umeme katika Mji wa Kahama limekuwepo na mpango wa kwanza ulikuwa ni kwamba tujenge au tutumie substation ya Mgodi wa Bulyankhulu ili uweze ku-supply umeme pale kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunajenga *line* kubwa ya umeme kutoka Iringa ya 400 na mwisho wake utakuwa Shinyanga. Katika mpango huu pamoja na mahitaji ya mgodi wa Buzwagi pale Tinde tutatengeneza, nadhani atakuwa ameshaona, tutatengeneza *line* nydingine kubwa kidogo ambayo ita-supply umeme katika Mji wa Kahama pamoja na kuongeza nguvu ya umeme katika mradi wa Buzwagi. Mradi wa Buzwagi wanatarajia kwamba kama watapata umeme wa TANESCO, maisha ya ule mgodi hayatakuwa miaka mitano zaidi, wanaweza kuongeza muda mrefu. Kwa hiyo, tumwombe Mheshimiwa Lembeli kwamba, ashukuru mradi huu utakapokamilika ambao tayari upo katika ujenzi, umeme utapatikana katika mji wake.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mrema!

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Waziri nimeona ratiba ya kusambaza huu umeme wa REA kule Vunjo. Kwa hiyo, kwanza ni miradi itakayoanza tarehe 1 Juni, 2015, nimeona Vijiji vya Upendo, Njiapanda I, Njiapanda II, Karesia Kitovo, Mareale, Mawanjeni, Madukani, Mawanjeni Kati, Mawanjeni B, Mawanjeni Kanisa na KKKT na Yam Juu na Yam Chini, nashukuru sana. Pia, nimeona miradi ambayo itakamilika tarehe 30 Juni, 2015; Neema, Kilototoni I, Kilototoni II, Wona VTC, Lotima I, Lotima II, Lotima III, Matala, Mauru, Miwaleni, Kisangesangeni na Mkonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba, nimeona bajeti ya usambazaji wa umeme ni *3.2 billion shillings*, hilo la kwanza nataka kujua. Kweli hizo fedha zinaweza kupatikana ili tuwe na matumaini mema kwamba huu umeme utapatikana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kwamba, kule Lotima nimeambiwa Lotoma I, Lotima II na Lotima III, ule umeme hauendi kwenye vitongoji vyote, sasa kuna kitongoji kimoja cha Kifula ambacho watu wanalia kwamba je, umeme utarudia njiani au na wenyewe utafika pale? Je, hiyo sera yenu ya kusambaza umeme kwenye Kijiji, ni kwenye vitongoji vyote au ni mradi tu uonekane?

Mheshimiwa Mwenyekiti, langu ndiyo hilo, wala simtolei shilingi Mheshimiwa rafiki yangu, aendeleee kudunda kama anavyofanya. (Makof)

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimjibu Mheshimiwa Lyatonga Mrema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu letu ni kuisimamia hiyo mipango ni kuisimamia na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, tulikuwa na Wakandarasi ambaa tumewahimiza wafanye kazi kama alivyosema Naibu Waziri wa Fedha kwamba kuna fedha zinatolewa. Utaratibu wa ujenzi wa umeme siyo kwamba Mkandarasi anapewa fedha zote zilizopangwa, akisha-mobilize vifaa na wale Wakandarasi wote wana uwezo, shida yangu ni kuhakikisha kwamba wananchi wako wote wanapata umeme kwenye muda uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitongoji, mpango na utaratibu wetu ni kupeleka umeme vijijini, ndiyo mpango wa nchi nzima, lakini Mzee Mrema yeye ni Mzee wangu, ninapopita kwenda Arumeru nitapita kwa mama kunywa chai, nitaangalia hivi vitongoji vipo sehemu gani.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 - Finance and Accounts... Sh. 2,462,995,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ole-Medeye na Mheshimiwa Machali. Mheshimiwa Medeye kwanza!

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nipo kwenye Kasma 221100 *Travel Out of Country*, katika kasma hii kuna shilingi milioni 208, lakini nimepiga hesabu kwa Wizara nzima...

MWENYEKITI: Samahani, 211100?

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: 221100!

MWENYEKITI: No, hiyo ni *Travel Out of Country*, ni shilingi milioni 111 lakini shilingi milioni 208, ni *Travel in Country* kwa sababu tunafuutilia hapa unachokisema.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, nimekosea figure ni sh milioni 111.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepiga hesabu kwa Wizara nzima gharama ya travel out of country kwa Wizara nzima ni sh. 4,830,000,000/. Sasa hizi ni fedha nyngi sana kwa kasma moja na ukiangalia maelezo kwenye randama, moja ya gharama ambazo inasemekana itagharamiwa kwa kasma hii ni mafunzo wakati kuna kasma ya mafunzo ndani ya nchi na kuna kasma ya mafunzo nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafikiri pengine Wizara hajajipanga vizuri kwamba hii kasma inatumikaje na Hazina imepitisha hivyo hivyo. Naomba kushauri kwamba kama kazi ambazo zimepangwa ni hizo za mafunzo ambazo tayari zimegharamiwa kwenye kasma zinazohusika fedha zipunguzwe katika kasma hii ili zipelekwe kwenye miradi ya maendeleo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe maelezo ya nyongeza Mheshimiwa Ole-Medeye. Shida yake au hoja yake anayoizungumza kulingana na ukubwa wa fedha zilizotengwa. Hii ni Wizara ya Nishati na Madini, tunashughulikia mambo ya gesi, mafuta na umeme, ninapozungumza sasa hivi kuna wafanyakazi wa shirika zaidi ya 10 wako nje ya nchi wanazunguka, wawekezaji na mitambo yote inanunuliwa nje, hizi fedha kimsingi hazitoshi kukabili kazi za kwenda, inabidi watu wengine wafanye kazi hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu letu ni kubwa, mimi nilikuwa na ufahamu na Wizara hii, lakini nimefika pale nimeshtuka, kumbe nilikuwa na ufahamu kidogo, hizi fedha hazitoshi. Kuna watu wanakwenda nchi za nje kuchenjua mawe, wanachukua sample nchini, wanakwenda kuzi-analyze kule, hiyo ni travel, unapokwenda ku-analyze una-travel, lakini ukifika kule unapoangalia wenzako wana-analyze una-learn na una-train. Kwa hiyo, kuna vitu ambavyo vina-cost pesa nyngi, ni kwa nia njema ya kuivusha nchi hii kuipeleka kwenye uchumi wa gesi na uchumi wa kati.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Machali!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Najielekeza kwenye kasma 221400, *Hospitality Supplies and Services*, ukiangalia pale pesa zimeongezeka sana kutoka shilingi milioni 46 ya mwaka jana ambayo itaishia tarehe 30 Juni na mwaka juzi ilikuwa shilingi milioni 37 plus, imekwenda kwenye shilingi milioni 83 kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo ni kwamba, ukiangalia kwenye subvote nyininge kumekuwa na trend ya kuongezeka kwa fedha hizi, wakati huo huo tukiangalia bajeti ya miradi ya maendeleo ni kidogo. Huko vijiji kuna miradi mingi imekwama kwa mfano REA Phase I maeneo yote hamkutekeleza kama ambavyo Profesa Muhongo alituaminisha Waheshimiwa Wabunge kwamba twende kifua mbele, miradi itatekelezwa, matokeo yake Wabunge tunaonekana ni waongo kwenye Majimbo yetu, lakini hizi fedha za *Hospitality* kwenye maeneo mengi, Wizara imeongenza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli ya Serikali, ni sababu gani ambazo zinawafanya waongeze fedha kwa ajili ya matumizi ya kununua chai, sambusa, maji na kadhalika maana yake niliwapa compliment Wizara ya Katiba na Sheria, walionesha spirit ya kuzipunguza pesa

hizi, lakini ninyi ni mionganoni mwa Wizara ambazo zimeongeza fedha hizi kwa mwaka huu wa fedha. Sababu ni nini? Kwa nini msibane matumizi ya kawaida mkazi peleka kwa ajili ya miradi ya maendeleo, huko miradi imekwama, Wakandarasi wamekwama site hawawezi kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli ambayo ina ithibati za kisayansi, ni kwa nini mnaongeza fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida msipeleke kwenye miradi ya maendeeo ili wananchi wapate umeme vijiji na mijini? Naomba statement ya Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Mwenyekiti, imeandikwa *Hospitality Supplies and Services*, hivi chai ni services? Hiyo ni portion kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, randama ilivyoandikwa...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hebu subirini kidogo, Mheshimiwa Machali umesema yeye kakusikiliza, Mheshimiwa Esther kaa kimya, tulia! Endelea Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya randama imeandikwa vizuri tu, pamoja na vitu kama chai vile vile kuna stationery, akumbuke kwamba tulikuwa na kanda chache, lakini sasa hivi tumeongeza Kanda kule Mara, Songea na tumeongeza Kanda karibu sita ambazo si kama tulivyokuwa zamani. Kwa hiyo, mahitaji ya stationery na services lazima tuhakikishe kwamba tunakwenda sawasawa.

Mheshimiwa Machali akiangalia ataona tu pamoja...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther kaa kimya, wewe vipi? Sasa sikiliza, utasimama nitakapokuruhusu mimi, hata nyumbani kwako huwezi ukanyanya tu.

(Hapa Mheshimiwa Esther Matiko alikuwa akibishana na Kiti kuonesha kutokubaliana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri)

MWENYEKITI: No! Mimi ndiye nitakaye amua kwamba anapotosha au hapotoshi na siyo wewe, wewe nitakupa nafasi ya kusema kwa muda wako, nyamaza!

Mheshimiwa Waziri, randama unayo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo.

MWENYEKITI: Hebu soma randama!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Kifungu hiki kitatumika kugharamia huduma zitakazotolewa kwa wageni wa Idara ya Madini na hasa wageni wa Kamishna wa Madini watakaokuja kwa ajili ya shughuli za kikazi na vikao vitakavyosimamiwa na Kamishna wa Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nielezee tu kwamba, Kamishna wa Madini amekuja ana wageni, anataka kwenda kwenye Kanda moja au nyingine anahitaji huduma, stationery...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, hebu kaa kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, mmeuliza swalı mwachenı ajibu mnakuwa kama sasa mnamchanganya ili asijibu na siyo *fair*, akisema stationery hata kama haikuandikwa stationery inaweza kuwa accommodated ndani ya kasma vile vile.

Mheshimiwa Waziri, jibu tu za matumizi ya kawaida, nипитиshe kifungu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za Kamishna siyo chai tu, ana wageni kutoka nje, ana mikutano, wanakwenda site na kadhalika, services zote zitakazotolewa kwa yeye kwenda kule zitatumia kifungu hiki.

MWENYEKITI: Ahsante!

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 - Policy and Planning... Sh. 2,992,806,000/=
Kif. 1004 - Internal Audit... Sh. 1,358,256,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1005 - Legal Services... Sh. 5,901,738,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Matiko!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, subvote 1005 - Legal Services, lakini nakwenda kwenye kasma ya 220100 - Office and General Suppliers and Services. Kwa mwaka 2014/2015 ilikuwa ni shilingi milioni 50, kwa mwaka huu 2015/2016 ni sh. 107,400,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba, ongezeko ni kubwa, lakini Mawaziri watujibu kulingana jinsi tunavyowauliza. Mheshimiwa Machali aliuliza kuhusu Hospitality vitafunwa, akajibu kuhusu stationery, stationery ina kifungu chake...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther subiri, kaa chini, hapa hatupo kwenye club. Mheshimiwa Esther sikiliza, nyamaza, kama jambo tumeshafanya maamuzi hatuwezi kurudia tena hapa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliendelea kubishana
na Mwenyekiti kuonesha kutokubaliana
na maamuzi yake)

MWENYEKITI: Tulia wewe!

Kif. 1006...

Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Hapa Mheshimiwa Moses J. Machali aliendelea kulalamika kuonesha kutokubaliana na maamuzi ya Mwenyekiti wa Bunge)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, sikiliza! Hebu jamani tuheshimu Bunge. Mheshimiwa Machali subiri kwanza, kama maamuzi ya kifungu yameshapitishwa huwezi kuhoji jambo hilo, kama una tatizo...

(Hapa Mheshimiwa Esther N. Matiko aliendelea kubishana na Mwenyekiti wakati akiendelea kutoa ufanuzi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther, mimi nasema na wewe vipi? Wewe ni mtu namna gani?

Kama kifungu kimeshapitishwa, kimehojiwa, kama una hoja nacho kimeshapitishwa wala huna nafasi nyingine. Kama una matatizo ya uendeshaji wa Kiti au Serikali basi tumia kanuni ya 5(4) *simple as that*. Mnakaa mnajishaua tu mnapiga makelele bila sababu yoyote, *for no reason at all*, Mheshimiwa Halima kaa chini tunataka kwenda kuzika, kaa chini!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumia lugha za staha.

MWENYEKITI: Maana wakati mwininge itabidi tuendeshe Bunge Kidar es Salaam, kaa chini!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumia lugha za staha usitutukane, tunaendesha Bunge, watu wanatuji kihunihuni halafu unatetea upuuzi.

MWENYEKITI: Mnajua wakati mwininge mnataka kutoa Serikali kwenye *the right path*, sababu mengi yamefanywa mmeshindwa kujenga hoja, sasa mnaanza kuweweseka, tulia! (Makofii)

Tuendelee! Habari ndiyo hiyo, mambo ya Dar es Salaam yatakuja hapa! (Makofii)

Kif. 1006 - Government Communication

Unit... Sh. 2,741,103,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther, tena uwahi kusimama ukichelewa mimi nakunini tu.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Si ndiyo kawaida, tumeshazoea hata ukipitisha hamna shida.

MWENYEKITI: Na mtazoea miaka yote hivyo hivyo!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasoma sub vote 1006 - Government Communication Unit na nataka majibu ya kina, sitaki ngonjera na kujibu kifungu tofauti.

MWENYEKITI: Soma kifungu!

MHE. ESTHER N. MATIKO: 220300, wameandika Fuel, Oil and Lubricants, kwa mwaka uliopita ilikuwa ni sh. 87,905,000 kwa mwaka huu wameweka shilingi milioni 200. Kwenye randama wanatuambia ni magari mawili ya kitengo. Sasa nahoji, ni kwa nini imeongezeka sh. 120,195,000 kwa magari mawili; moja linatumika ndani na lingine mmesema linakwenda kwenye matangazo. Hii fedha ni kubwa sana unapojibu usianze kusema ni vipuri vya fungu lingine, jibu kulingana na kitu ulichoulizwa. (Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyofundishwa namna ya kujibu inatutia wasiwasi.

MWENYEKITI: Wewe jibu tu!

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA): Mheshimiwa Mwenyekiti, haya magari ni kwa ajili ya communication yaani kutoa mafunzo, kuelekeza wananchi katika maeneo mbalimbali. Hayo ni magari maalum ambayo yatatumika mara kwa mara kuhakikisha kwamba tunafika kila eneo kutoa mafunzo na matangazo na haya magari kama utayaona yamekuwa well equipped, yana vifaa vya kutolea huduma na haya yatatumika mara kwa mara na kitakachotumika ni pamoja na mafuta yatakayotumika kuhakikisha kwamba tunafika kila mahali.

MWENYEKITI: Ahsante!

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaingia kwenye guillotine.

Kif. 1007 - Procurement Management

Unit... Sh.1,357,803,000/=

Kif. 1008 - Environment Management

Unit... Sh. 750,546,000/=

Kif. 1009 - Management Information

System... Sh. 1,678,940,000/=

Kif. 2001 - Minerals... Sh. 40,710,399,800/=

Kif. 2002 - Madini Institute... Sh. 6,625,366,000/=

Kif. 2004 - Tanzania Diamond Sorting

Agency (TANSORT) Sh. 1,718,263,000/=

Kif. 2005 - Eastern Zone... Sh. 2,318,904,000/=

Kif. 2006 - Western Zone... Sh. 1,568,287,000/=

Kif. 2007 - Lake Zone... Sh. 1,852,895,000/=

Kif. 2008 - Northern Zone Sh. 1,906,202,000/=

Kif. 2009 - Southern Zone Sh. 1,080,454,000/=

Kif. 2010 - Central Western Zone... Sh. 1,495,712,000/=

Kif. 2011 - Central Zone... Sh. 1,469,481,000/=

Kif. 2012 - Southern Western Zone... Sh. 1,238,573,000/=

Kif. 2013 - Lake Victoria Eastern Zone... ... Sh. 1,691,238,000/=

Kif. 2014 - Lake Nyasa Zone... Sh. 1,510,126,000/=

Kif. 3001 - Energy and Petroleum... Sh. 77,166,153,200/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 58 – WIZARA YA NISHATI NA MADINI

Kif. 2001 - Minerals... Sh. 25,918,045,000/=

Kif. 2002 - Madini Institute... Sh. 1,500,000,000/=

Kif. 2003 - Research and Laboratory Services... Sh. 0/=

Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kif. 3001 - Energy and Petroleum... ... Sh. 337,928,893,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Mtoha hoja, Taarifa!

TAARIFA

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia makadirio ya matumizi ya fedha za Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2015/2016, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (Makofii)

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka
wa Fedha 2015/2016 Yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu wako na Watendaji wako. Kwa kweli mnafanya kazi nzuri sana na haya maneno mnayopigwapigwa humu ndani ni tabia ya kibinadamu tu kushikwa na donge kwa kuwa chama kitarudi tena mwakani. Kwa hiyo, tunaelewa! (Makofii)

Kipindi hiki ambacho tunamaliza Bunge hatutafanya adhabu yoyote ya kuwaadhibu humu ndani ili msije mkaharibikiwa makwenu huko, tutawapa fursa mseme, majibu yaktoka yatawaingia vizuri na mkiondoka, mtaondoka vizuri na majibu huko mnakokwenda. (Makofii)

Mmefanya kazi nzuri nawapongeza pamoja na watendaji a job well done, mnastahili pongezi na pesa kidogo mlizopipata bado mmeweza ku-deliver. Sasa hivi nchi nafikiri baada ya miaka nitatu inayokuja itakuwa yote inang'aa. Isipokuwa moja, TMAA, TMAA wanafanya kazi nzuri sana ya ku-audit migodi, lakini ni lazima kuwa na networking ya TRA. TMAA wanapokuja na audit zao wenye mamlaka kisheria ni TRA kwenda kutekeleza maagizo ya TMAA. Naomba Wizara na TRA, m-network pamoja ili mapato ya nchi yapatikane pale yanapostahili kupatikana. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, nawakumbusha kesho kuna Bunge kama kawaida na litaanza saa tano na litakwisha saa tisa mchana.

Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tano asubuhi.

(Saa 8.24 Mchana Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumapili,
Tarehe 7 Juni, 2015, Saa Tano Asubuhi)

